

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Saba – Tarehe 7 Februari, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

MHE. PROF. NORMAN A. S. KING – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

MHE. DOTO M. BITEKO -MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kipindi cha kuanzia Januari 2016 hadi Januari 2017.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Katibu!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali, Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 69

Tatizo la Ulevi

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA aliuliza:-

Ulevi wa kupita kiasi hasa wa pombe za kienyeji umekuwa na athari kubwa za kiafya na kiakili kwa Watanzania wenyewe tabia ya ulevi wa kukithiri:-

Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na tatizo hilo hasa ikizingatiwa kuwa Sheria ya Vileo ya mwaka 1969 ni ya zamani sana kiasi kwamba inawezekana kabisa haikidhi mabadiliko ya hali halisi ya vileo kwa wakati huu.

NAIBUWAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pombe za kienyeji zimeainishwa katika Kifungu cha pili (2) cha tafsiri katika Sheria ya Vileo, Sura ya 77. Kwa mujibu wa sheria hiyo, wafanyabiashara wote wanatakiwa kuwa na leseni ambayo inatolewa na Halmashauri. Aidha, biashara hiyo hairuhusiwi kufanyika katika muda wa kazi. Muda unaoruhusiwa Kisheria ni kuanzia saa 12 jioni hadi saa tano usiku kwa siku za Jumatatu hadi ljumlahaa na kuanzia saa tano asubuhi hadi saa sita usiku kwa siku za Jumamosi, Jumapili na siku za sikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, unywaji wa pombe kupita kiasi ni tabia ya mtu ambayo inawezekana kabisa haitokani na upungufu wa kisheria. Wakuu wa Mikoa na Wilaya wameagizwa kusimamia taratibu za uendeshaji wa biashara za vileo na kuchukua hatua kwa watumiaji na wafanyabiashara wanaobainika kukiuka Sheria hiyo. Hata hivyo, endapo kuna haja ya kuifanya marekebisho sheria hiyo ya vimeo, Serikali itakuwa tayari kupokea mapendekezo yenyewe upungufu ili yaweeze kufanyiwa marekebisho kupitia Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa wito kwa Watanzania wote kutumia muda wao kufanya kazi kwa bidii ili kujilettea maendeleo kwa ustawi wa Taifa zima. Serikali haitasita kuchukua hatua kwa wanywaji wa pombe wasiozingatia utaratibu pamoja na wazururaji wakati wa kazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Murtaza Giga, swali la nyongeza.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, bado nina swali moja la nyongeza ambalo linahusiana na hawa watoto wadogo chini ya umri wa miaka 18 kutumia huu ulevi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile nilisema sheria hii ya mwaka 1969 ni ya muda mrefu sasa ni lini Serikali itaweza kujipanga na kuleta ili tuweze kufanya marekebisho sheria hii ili tuwabane na hawa watoto wadogo walio chini ya umri wa miaka 18 kutumia ulevi? (Makofij)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBUWAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli. Sasa hivi kuna tabia kwenye baadhi ya Mikoa, utakuta watoto wadogo asubuhi au wakati wa weekend wananyweshwa

pombe. Jambo hili kwanza kimsingi ni ukiukwaji wa haki za kibinadamu kwanza na haki za watoto ambapo mtoto mdogo anatakiwa kuendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tuchukue huu ushauri kwa sababu sheria hii ni ya muda mrefu sana na kutokana na maoni ya wadau mbalimbali tutaangalia jinsi gani tutafanya turekebishe, lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba Taifa letu linakuwa Taifa imara kwa sababu lazima tuwalee hawa watoto kwa kizazi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tuchukue ushauri. Itakapoonekana pale ina haja, basi wadau mbalimbali wataleta maoni yao na sisi Wabunge ni mionganini mwa wadau wa kutengeneza hizo sheria. Kwa hiyo, hili nadhani tutalifanyia kazi vema tuweze kulifanikisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa katika swali la msingi linazungumzia pombe za kienyeji na pombe za kienyeji katika Taifa letu ni nyingi ikiwemo mbege, kimpumu, ulanzi na pombe nyinginezo. Ni lini sasa hawa watu wa viwango vyta kuandika kilevi kilichoko kwenye pombe ikiwemo TBS wataingia katika maeneo husika ili kuweza kujua kwamba ni kiwango gani cha ulevi kinachoruhusiwa katika pombe za kienyeji?

NAIBU SPIKA: Nilidhani Waziri wa Viwanda atatujibia TBS hapa. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu. (Kicheko)

NAIBUWAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna pombe mbalimbali. Kuna mbege, kuna ulanzi na nyinginezo, bahati mbaya pombe hizi hazijawekwa katika viwango stahiki na ndiyo maana maeneo mengine utakuta kuna kesi mbalimbali zimejitokeza. Baadhi ya watu saa nyingine wamekunywa pombe, pombe ile imewadhuru na matukio haya tumeona kwamba yametokea maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwa sababu sasa hivi tuna Wizara ambayo inafanya kazi vizuri zaidi na hususan suala zima la viwanda na naamini wenzetu sasa wa TBS watachukua jukumu lao katika maeneo mbalimbali kuhakikisha ni jinsi gani tunafanya kurekebisha utaratibu mzuri hasa katika hivi vikundi vidogovidogo vinavyojihusisha na pombe za kienyeji, lengo kubwa ni kumlinda Mtanzania anywe kitu kinachordhisha maisha yake lakini na afya yake ya msingi vilevile.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Engelbert Ndugulile.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa, ulevi wa pombe hizi za kienyeji sasa hivi kumekuwa na ongezeko la matumizi makubwa sana ya pombe aina ya viroba ambavyo vifungashio vyake na bei yake imekuwa ni nafuu sana ambapo imepelekea hata watoto wa shule wanaweza kumudu kati ya shilingi 300 mpaka 500 kuzinunua. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kupiga marufuku pombe za viroba ili kunusuru Taifa hili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika sasa ni utaratibu, lakini ukweli ulio wazi ni kwamba viroba vitapigwa marufuku na tutaanzisha packaging ya pombe kali kwenye ujazo ambaa itakuwa ni vigumu kwa mtu kuficha. Watoto wa shule kwa sababu ni rahisi wanawenza kuficha. Tutaweka kwenye chupa ya glass, ujazo utakuwa mkubwa kiasi kwamba mtoto ashindwe kununua lakini hata dereva wa daladala ashindwe kuficha. Ni suala la muda na Waziri wa Mambo ya Mazingira alizungumzia jana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, swali la nyongeza.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Sehemu ya swali langu imeshajibwa lakini naomba niulize. Kwa kuwa sasa hizi pombe zinatumwa sana na watu wengi, ni kwa nini Serikali sasa isifikirie kujenga kiwanda cha kuzisafisha na kuziwekea viwango kama Uganda wanavyofanya na kile kinywaji cha ‘Uganda Waragi’?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji majibu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Serikali ni kuweka mazingira ya uwezeshaji, wanaowekeza ni Sekta Binafsi. Nichukue fursa hii shangazi, tujasirie kusudi tuweze kukusanya ile konyagi ya nyumbani, tuiweke kwenye ubora tuweze kuuza. Kila mtu atafute fursa kwake kusudi aweze kuboresha vile vinywaji ambavyo havina viwango viingie kwenye viwango, tupate pesa, tutengeneze ajira lakini mwisho wa siku tulipe kodi. (Kicheko)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako sasa aulize swali lake.

Na. 70

Ujenzi wa Vyuo vya VETA Katika Kila Wilaya Nchini

MHE. DEO K. SANGA aliuliza:-

Serikali iliahidi kujenga Vyuo vya VETA kwa kila Wilaya ili kuwasaidia vijana kujifunza stadi za kazi mbalimbali:-

- (a) Je, hadi sasa ni Vyuo vingapi vya VETA vimeshajengwa katika nchi nzima?
- (b) Je, ni lini Chuo cha VETA kitajengwa katika Wilaya ya Njombe?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi VETA imeshajenga na kumiliki vyuo 29 vya ufundu stadi vya ngazi ya Mkoa, Wilaya na vyuo maalum vya ufundu. Vyuo hivyo orodha yake ni Mikoa ni Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara, Moshi, Manyara, Dodoma, Kigoma, Mbeya, Iringa, Mwanza, Kihonda na Tabora. Vyuo vya Wilaya ni Dakawa, Mikumi, Singida, Songea, Mpanda, Shinyanga, Kagera, Mara, Makete, Ulyankulu na Arusha ambapo vyuo maalum vya ufundu ni pamoja na Chuo cha Ualimu wa Ufundu Stadi Morogoro, Chuo cha Mafunzo ya TEHAMA Kipawa na Chuo cha Mafunzo ya Hoteli na Utalii -Njiro.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sasa haina mpango wa kujenga chuo cha ufundu stadi katika Wilaya ya Njombe, badala yake itaviboresha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - Njombe na Ulembwe na kuvijengea uwezo ili viweze kutoa mafunzo ya ufundu stadi sanjari na mafunzo ya maendeleo ya wananchi. Aidha, Mkandarasi wa ujenzi wa Chuo cha VETA cha Mkoa wa Njombe ameshapatikana ambaye anaitwa *Herkin Builders Limited* na yupo katika eneo la kazi, Kijiji cha Shaurimoyo Wilaya ya Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo hicho kinajengwa katika eneo hilo kimkakati kutokana na miradi ya chuma na makaa ya mawe ya Mchuchuma na Liganga. Vilevile, Wizara kupitia bajeti ya mwaka 2016/2017 imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 450 kwa ajili ya kujenga bweni katika chuo cha VETA Makete ili kuongeza udahili kwa wanafunzi wanaotoka maeneo ya mbali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Sanga, swalii la nyongeza.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kwa kuwa lengo la Serikali ilikuwa ni kujenga VETA kila Wilaya ili vijana wetu waweze kupata mafunzo, vijana ambaao wanakuwa wameshindwa kuendelea na vyuo vikuu na kadhalika. Je, sasa Serikali imejipangaje kuhakikisha inakamilisha azma yake iliyopanga ya kujenga chuo cha VETA kila Wilaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, pamoja na majibu mazuri kama nilivyosema ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali kwa majibu yake imesema kule Njombe tuna Chuo cha Ulembwe pale ambacho kinamilikiwa na Wilaya yetu ya Njombe. Je, Serikali sasa kwa majibu haya imejipangaje kuhakikisha chuo hiki kinaboresha kama walivyosema ili wananchi wa Wilaya ya Njombe hususan pamoja na Jimbo la Makambako, vijana hawa waweze kwenda kusoma chuo hiki cha VETA ambacho kiko pale Ulembwe?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali imeendelea na hiyo mikakati, lakini niseme tu kwamba kujenga chuo kimoja cha VETA ni gharama. Kwa hiyo, kwa kutumia fursa hii kwamba Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC's) navyo sasa hivi vimerudishwa katika Wizara yetu. Tunaangalia katika Wilaya ile ambayo ina chuo cha aina hiyo basi kiweze kuboreshwa na kiweze kuchukua nafasi ya mafunzo ambayo yatakuwa yanatolewa yanayowahusu wale wananchi wote bila kujali sifa zao ili mradi wana akili timamu lakini hali kadhalika kwa wale ambao wanahitaji mafunzo yale yanayofanana na yanayotolewa katika VETA yaweze kupatikana, tayari tumeshaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika Mkoa wa Kagera, chuo cha Gera tayari sasa hivi kimeshafanyiwa ukarabati, lakini pia Rubondo tumeshaanza kufanya ukarabati, kuna Kibondo, Kasulu na maeneo mengine. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa upande wa Ulembwe tutahakikisha kwamba chuo hicho kinaboreshwa. Niwafahamishe tu kwamba ili tusifanye kazi ambazo hazina tija, tayari Wizara imeshapanga kukutana na Wakuu wa Vyuo vyote vya FDC's ili kuweza kukaa pamoja na kufahamu kwa undani changamoto zilizowakabili kabla hatujatoa fedha za kwenda kukamilisha au kuanza uboreshaji wa vyuo hivyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dunstan Kitandula, swali la nyongeza.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali iliwha kutoa orodha ya Wilaya za kipaumbele za ujenzi wa vyuo vya VETA na katika orodha ile Wilaya ya Mkinga ilikuwa ni mionganini mwa Wilaya hizo. Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga chuo kile kule Mkinga?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali inatambua hilo na hata tunapojibu maswali ya VETA tunajua tutapambana nna swali la Mkinga. Nimfahamishe tu kwamba katika vipaumbele vya Serikali bado Mkinga iko pale pale. Tukipata fedha tunaamini kwamba tutatekeleza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anthony Komu, swali la nyongeza.

MHE. ANTHONY C. KOMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa, wananchi wa Moshi Vijijini kule Tarafa ya Kibosho katika Kata sita, Kata ya Kirima, Kibosho Kati, Okaoni, Kibosho Magharibi na Kibosho Mashariki wameshaitikia huu wito na kujenga chuo ambacho kwa kweli kina hadhi kubwa sana na kinawenza hata kubeba Wilaya kama mbili, tatu. Waziri atakuwa tayari kwenda na mimi kule kwenda kuona hiki chuo na kukiwekea utaratibu mzuri, maana naamini akienda kule atawenza kukiwekea utaratibu mzuri wa kukipa ruzuku kama Walimu na kadhalika?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza wananchi kwa kutambua umuhimu wa stadi za kazi kwa wanafunzi wa vyuo hivyo. Niseme tu kwamba nitakuwa tayari ili mradi siku hiyo muimbe pia na nyimbo zile za ki...

NAIBU SPIKA: Hatujasikia ni nyimbo gani ulikuwa unazisema Mheshimiwa umemalizia katikati. Mheshimiwa Maige, swali la nyongeza.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tatizo la uhaba wa vyuo vya ufundu na ahadi imekuwa ni ya muda mrefu na tatizo ni la muda mrefu. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala tumekwishaanza juhudzi za kufanya au kutekeleza jambo hili. Kwa bahati nzuri kwa mazingira yetu tuna mgodi wa Bulyanhulu ambao vijana wengi sana wanakosa fursa za kufanya kazi pale kwa sababu ya kukosa elimu fulani ya ufundu na mgodi umeonesha nia ya kushirikiana na Serikali kuutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumwomba au kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri kwamba anaonaje akitusaidia katika kutia chachu mazungumzo kati ya Halmashauri ya mgodi ili kuweza kutekeleza mradi huu kwa yeye mwenyewe kufika na kukaa na watu wa mgodi ili kuona namna gani tunaweza tukatekeleza mradi ambao tayari eneo lilishapatikana muda mrefu kwenye Kijiji cha Bugarama?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Niseme tu kwamba kwanza nawapongeza hao wadau wa madini kwenye migodi wanavyotu- support katika masuala ya elimu kwa Mkoa wa Shinyanga na Msalala nadhani ikiwa ni wanufaika wamojawapo. Kwa hiyo, kama kuna jitihada za aina hiyo Wizara pia tuko tayari. Hata hivyo, niseme tu kwamba Msalala mtakuwa hamjapungukiwa sana kwa sababu tayari kuna chuo cha VETA kiko Shinyanga ambacho pia kinajihuisha na masuala ya madini. Vilevile tunategemea kujenga chuo ambacho kitakuwa ni cha Mkoa katika Mkoa wa Geita ambapo pia ni jirani zenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hizo jitihada nitakuwa tayari kushirikiana nanyi kuweza kuomba kama kuna huo uwezekano.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 71

Kuwasaidia Wakulima na Wafugaji wa Same

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza:-

Kumekuwa na mgogoro kati ya wafugaji na wakulima wa Jimbo la Same Mashariki dhidi ya TANAPA:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia wafugaji hao shamba darasa kupitia hekta 346,000 zinazofaa kwa ufugaji?

(b) Ili kutatua tatizo la maji na malisho kwa wafugaji wa Same Mashariki: Je, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi haioni umuhimu wa kuanzisha mradi wa kuvuna maji ya mvua ambazo hunyesha mara kwa mara?

(c) Je, Waziri yuko yatari kuambatana na wataalam wake kutembelea Jimbo la Same Mashariki ili kuona ni jinsi gani anaweza kuwasaidia wafugaji kuanzisha mitambo ya Biogas kwenye mazizi yao pamoja na kuwaelimisha matumizi bora ya mbolea ya samadi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki, lenye sehemu (a) (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Shamba darasa la unenepeshaji mifugo limeanzishwa katika Kijiji cha Ruvu mferejini, Kata ya Ruvu kati ya hekta 2,754 zimepimwa kutokana na hekta 346,000 zilizoainishwa na vijiji mbalimbali katika Wilaya kwa ajili ya ufugaji. Uainishaji wa maeneo umefanyika katika Kata zote zinazopakana na mbuga za Mkomazi na upimaji utafanyika kulingana na upatikananji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaona umuhimu wa kuvuna maji ya mvua ili kutatua tatizo la maji kwa mifugo katika Jimbo la Same Mashariki; ambapo kwa kushirikiana na taasisi binafsi ya Women and Youth Empowerment, Enviro Care and Gender Trust Fund (WOYOGE) na TANAPA, imewezesha ujenzi wa birika la maji katika Kijiji cha Muheza katika Kata ya Maole na maji yanaingia katika birika hilo kutokana na chanzo cha maji kutoka Milima ya Mbaga. Aidha, uvunaji wa maji ya mvua unatarajiwa kutekelezwa kwa ufadhilli wa Shirika la United Nations Capital Development Fund (UNCDF) kwa kukarabati bwawa katika Kata ya Kalemawe kwa matumizi ya maji kwa kilimo, mifugo, uoteshaji wa miti na ufugaji wa samaki ambaa utasaidia upatikanaji wa maji kwa kipindi cha mwaka mzima utakapokuwa umetekelvezwa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia CAMARTEC ikishirikiana na sekta binafsi ya Tanzania Domestic Biogas Program imeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi ya biogas katika Jimbo la Same Mashariki ambapo jumla ya mitambo 106 ya biogas imejengwa katika Vijiji vya Bwambo, Goha, Kirangare, Bendera, Kihurio, Mtii, Vuje, Njagu, Ndungu, Myombo, Mjema, Maore, Mvaa na Mpirani. Aidha, Serikali imekwishaanza kutoa uhamasishaji wa matumizi ya biogas na mbolea ya samadi. Hata hivyo, kukiwa na uhitaji kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi na kwa sababu inahusu nishati na Waziri wa Nishati na Madini wanawenza kuambatana na wataalam wao kutembelea Jimbo la Same Mashariki.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka swali la nyongeza.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kabla ya swali langu la nyongeza, nataka nieleze masikitiko yangu makubwa kwa jinsi aliyempa Mheshimiwa Waziri taarifa hii alivyoipotosha. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi namheshimu sana na inabidi kueleza ukweli kwamba upotoshaji huu, itabidi huyu aliyempa hizi taarifa za uwongo

amchukulie hatua. Kwa mfano, hapa ilipoandikwa kwamba, TANAPA wakishirikiana na WOYOGE Trust Fund wameshajenga birika ni uwongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na-declare interest, hii WOYOGETrust fund mimi ndiyo Mwenyekiti wake. Huu mradi mwaka jana nilimuuliza Waziri wa Maliasili na Utalii, kwamba wanyama wale wameharibu sana miundombinu ambayo nilikuwa nimewasaidia wananchi kule kwa ufadhilli wa Ubalozi wa Japan na Waziri akakubali kwamba watarekebisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kaboyoka ni maswali ya nyongeza ukitoa maelezo mrefu labda kama ukishamaliza kutoa maelezo utataka Serikali ikujibu huko baadaye. Otherwise muda wetu unakimbia sana.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, basi nimwambie tu kwamba, Waziri amepotoshwa maana TANAPA hawajaja kujenga chochote kwanza ndiyo naambiwa mradi umeenda kwenye Bodi na kwamba hata haujapitishwa. Wamempotosha sana.

Swali langu la nyongeza ni kwamba je, Waziri haoni kuna umuhimu wa kuweka kituo cha *artificial insemination*, kwa kuzingatia kwamba madume yanayopelekwa kusaidia wafugaji yanakufa, maana wafugaji wanayawaga nayo yale yanataka yafanyiwe zero grazing? Naomba ajibu swalii hilo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu taarifa tulizotoa kupishana na taarifa aliyonayo yeye, niko tayari kukaa naye kuangalia kwa nini yeye ana taarifa tofauti na ile ambayo tunayo kama Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *artificial insemination* ningependa kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari huduma za *artificial insemination* zinatolewa karibu kabisa na Jimboni kwake akifika tu kituo cha Tengeru, huduma hizi zinaweza kupatikana vilevile niko tayari kukaa naye na kumwelekeza zaidi namna ya wafugaji wake watakavyoweza kunufaika na huduma hii.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yussuf swalii la nyongeza.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Jimbo la Same Mashariki ni Jimbo ambalo lina ardhi nzuri kwa kilimo cha tangawizi: Je, Mheshimiwa Waziri kwa nini huoni sababu wataalam wake kushirikiana na wataalam wa TANAPA kuwapa elimu wananchi wa eneo hili wakalima kilimo cha tangawizi ambacho hakidhuriwi na mifugo, tukaondokana na mzozo wa wakalima na wafugaji? (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kama alivyosema kwamba eneo la Same kutokana na hali ya hewa

na aina ya udongo inafaa sana kwa zao la tangawizi, tayari Wakulima wa Same ni wakulima mahiri wa zao la tangawizi, na tayari Serikali kwa kushirikiana kwa karibu sana na aliyekuwa Mbunge wa Same Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, ambaye tunashukuru amerudi kwenye Bunge hili walishajenga kiwanda kwa ajili ya kuchakata tangawizi kama njia ya kuwaongezae wakulima faida zaidi. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, sasa aulize swali lake.

Na. 72

Kuiwezesha MSD Kuwa na Fungu Maalum Hazina

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Jukumu la MSD ni kununua na kusambaza dawa na vifaa tiba; na MSD inakabiliwa na tatizo kubwa la fedha za kununua dawa na vifaa tiba:-

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ipo haja kubwa ya MSD kuwezesha kuwa na Fungu (Vote) maalum kutoka Hazina?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la MSD kuwa na Fungu (Vote) lilishaanza kushughulikiwa tangu mwezi Desemba, 2015. Hatua hii ilichukuliwa kufuatia ushauri uliotolewa na iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii. Wizara iliwasilisha ombi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambayo ndio yenze mamlaka na majukumu ya utoaji wa mafungu (Votes).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia maombi hayo walishauri kwamba, MSD ipewe *line item* ndani ya kifungu (*sub vote*) chini ya Fungu la Wizara yaani Fungu Na. 52. Ushauri huu ulitolewa kwa kuzingatia utaratibu uliopo Serikalini kwamba, Fungu hutolewa kwa taasisi za Serikali Kuu peke yake ikiwa ni maana ya Wizara na Ofisi za Wakuu wa Mikoa. Baada ya kupokea ushauri huu, Wizara iliwasilisha ombi kwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya MSD kupatiwa *line item*.

Mheshimiwa Naibu Spika, MSD wameshapatiwa *line item* ndani ya Kifungu 2005 chini ya kitengo cha Huduma za Dawa (*Pharmaceutical Services Unit*) pale Wizara ya Afya. Baada ya kupatiwa *line item* ndani ya kifungu hicho yaani kifungu 2005 itahitajika kutenga bajeti, mwaka ujao wa fedha 2017/2018 inayokidhi mahitaji ya msingi kwa ajili ya MSD kutekeleza majukumu yake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lubeleje swali la nyongeza.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu maswali hayo. Sasa nina maswali mawili.

Kwa kuwa, MSD imetengewa fedha shilingi bilioni 251 kwa ajili ya kununua madawa, kwa kuwa kuna upungufu mkubwa sana wa madawa katika hospitali zetu wagonjwa wakienda hospitalini wanaandikiwa vyeti na Madaktari wanawaambiwa mkanunue dawa maduka binafsi. Je, kwa nini hizo fedha bilioni 251 zisipelekwe moja kwa moja MSD badala ya kukaa Hazina na wanapelekewa kidogo kidogo?

Swali la pili, kwa kuwa, katika Jimbo langu la Mpwapwa kuna Vituo vya Afya, vya Mima, Mbori, Berege, Mkanana pamoja na Zahanati za Chamanda, Igoji Kusini, Kibojane Lupeta, Makutupa, Majami, Nana, Mgoma havijakamilika hadi sasa na ujenzi huu sasa umechukua zaidi ya miaka kumi. Je, Serikali ina maelezo gani kwa wanachi wa vijiji hivyo, kwa sababu wananchi wa vijiji hivyo hufuata tiba zaidi ya kilomita 15?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa fursa hii. Swali lake la kwanza kuhusu kwa nini Serikali isipeleke pesa moja kwa moja kutoka Hazina kwenda MSD moja kwa moja tayari nilikwishatoa maelezo ya msingi, kwenye jibu la msingi; kwamba Idara za Serikali zinazopewa vifungu ni Serikali Kuu tu na Ofisi za Wakuu wa Mikoa na pamoja na Wizara. Kwa hivyo, MSD hawezi kupewa pesa moja kwa moja kutoka Hazina ambapo ni Serikali Kuu na bila kupitia Wizara ya Afya, kwenye kifungu kile ambacho sasa tumepeewa kinaitwa kifungu 2005 chini ya Mfamasia Mkuu wa Serikali. Kwa hivyo, utaratibu huo ni lazima uzingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kukanusha kauli yake ya kwanza aliyoisema kwamba kuna upungufu mkubwa wa dawa, hapana, hakuna upungufu mkubwa wa dawa nchini. Kwa taarifa tulizonazo sisi na ukweli ni kwamba upatikanaji wa dawa (*Drug availability*) kwa sasa ni wa kiwango cha asilimia 84 kwa mujibu wa taarifa za wiki iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili lina maelezo yake sipendi kupoteza muda wako, naomba nisiyatoe hapa lakini huo ndiyo ukweli. Serikali katika Awamu hii ya Tano imewekeza sana kwenye dawa na ndiyo maana tumepeewa bilioni 251.5 ukilinganisha na bilioni 31 kwenye mwaka wa fedha kabla ya huu. Bilioni hizo mpaka sasa tunavyozungumza kufikia Desemba tulikuwa tumeshapokea bilioni 84 kutoka Hazina kwa ajili ya manunuzi ya dawa. Kwa hivyo upatikanaji wa dawa ni wa kutosha pengine hizo anazozisema Mheshimiwa George Malima Lubeleje ni hadithi za zamani kidogo anapaswa kufanya utafiti wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuhusu kukamilisha zahanati na vituo vya afya kwenye jimbo lake, naomba nitoe rai kwake yeye mwenyewe, Halmashauri yake pamoja na kwa Wabunge wengine wote na Halmashauri zote nchini kuzingatia ukweli kwamba, ukamilishaji wa majengo ya zahanati na vituo vya afya inapaswa kuwa kipaumbele cha Halmashauri husika. Kwa sababu

miradi hii ya maendeleo kama ambavyo imewekwa kwenye llani ya Uchaguzi kwamba tutajenga zahanati kila kijiji, kituo cha afya, kila kata hatuwezi kusema sasa tunapewa pesa na Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ili tujenge hapana. Sisi sote tuna wajibu wa kutimiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima katika Halmashauri zetu tuweke kipaumbele kwenye kukamilisha miradi ya zahanati ambayo imeanzishwa na wananchi kwa kujitoa sana kwenye Halmashauri tukakamilishe zahanati hizo ili ziweze kuanza kufanya kazi. Wala tusitarajie kwamba sasa Wizara ya Afya itatuletea pesa ili tukamilishe. Pesa ile inapaswa kutoka kwenye ownsources za Halmashauri na maamuzi ya kufanya hivyo wanayo Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani kwenye Halmashauri zao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima swali la nyongeza!

MHE. HALIMA ALI MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Kwa kuwa, kwa mujibu wa taarifa ya CAG ya mwaka ulioshia Juni 2015, inaonesha kwamba kuna bohari ambazo hazina viwango. Sasa, je, Serikali inasema nini kuhusiana na hatari ya afya za wananchi wetu? (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa bohari za dawa hazina viwango, japo kuuwa swali hili linaweza kuwa hali endani na la msingi, lakini nadhani unaweza ukalijibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwanza naomba nikanushe vikali sana kwamba kuna bohari za dawa zisizo na viwango. Kwa sababu, hiyo ni ripoti ya CAG, sasa hii ni taarifa ya Serikali. Kwa hivyo naongea kama Serikali kwa mamlaka kamili niliyopewa. Kwamba bohari tulizonazo pale MSD ni bohari zenye viwango vya hali ya juu. Viwango hivi vimethibitishwa kwa ISO standards na standards hizi zinakaguliwa kila baada ya miaka mitano ili kuthibitisha viability yake na kwa msingi huo hatuwezi kutunza dawa kwenye bohari zisizo na viwango kwa sababu zitaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifahamike kwamba dawa ni *high value items*, hatuwezi kuzitunza hovyo hovyo kwa sababu tunazinunua kwa gharama kubwa na ndio maana kuanzia utenzaji kwenda kwenye usambazaji mpaka kwenye storage kwenye kituo cha afya kijijini kuna mnyororo uliokamilika unaozingatia viwango vya ubora. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa Mbunge ameuliza taarifa zinazotokana na ripoti ya CAG, Serikali iangalie kwenye hiyo ripoti kunasema nini kama alichosema Mbunge kiko sawasawa ama hakiko sawasawa. Kama anachokisema kimeandikwa kwenye ripoti ya CAG naomba Wizara ya Afya mliangalie jambo hili. Mheshimiwa Waziri wa Afya naona unataka kuongeza majibu. (Makofii)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake lakini pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, niseme tumepokea swali na tutalifanyia kazi na tutaleta majibu Bungeni. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea Waheshimiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Dua William Nkurua, Mbunge wa Nanyumbu sasa aulize swali lake.

Na. 73

Kuweka Mnara wa Simu – Nanyumbu

MHE. DUA W. NKURUA aliuliza:-

Kuna tatizo la usikivu wa simu za mkononi katika Kata za Napacho na baadhi ya maeneo ya Kata ya Maratani na Kata ya Mnauje:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti na hatimaye kuweka minara ya simu katika maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dua William Nkurua, Mbunge wa Nanyumbu kama ifuatavyo:-

Vijiji vyote katika Kata za Napacho, Maratani na Mnauje viliingizwa katika awamu ya pili na awamu ya tatu ya utekelezaji wa mradi wa mawasiliano vijiji ni wa kampuni ya simu ya Vietel(Halotel). Mpaka sasa Vijiji vya Kazamoyo na Nakopi Kata ya Napacho na Kijiji cha Mchangani Kata ya Maratani vimekwishapatiwa huduma ya mawasiliano kupitia kampuni ya Vietel(Halotel). Aidha, vijiji viliwyobaki vitafikishiwa huduma ya mawasiliano kupitia utekelezaji wa mradi awamu ya tatu ambao unatarajiwa kukamilika ifikapo Novemba, 2017.

MHE. DUA W. NKURUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu, lakini nataka nifanye marekebisho kidogo siyo Kata ya Mnauje ni Kata ya Mnanje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu yake mazuri, nina swali dogo la nyongeza. Katika Kijiji cha Marumba, Kata ya Mkonona kulijengwa mnara wa TTCL na mnara ule uliwashwa, lakini utendaji kazi wa mnara huu siyo mzuri. Kijiji hiki kipo mpakani kabisa mwa Tanzania na Msumbiji na sote tunafahamu umuhimu wa mawasiliano mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, kijiji hiki kinahudumia mpakani na mnara huu haufanyi kazi vizuri. Je, Serikali itafanya nini kuhakikisha kwamba, mnara huu unafanya kazi haraka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea taarifa yake na nitatafuta muda nizungukie huo mpaka ili tuone vijiji vyote vya mpakani hali ikoje, ikiwa ni pamoja na hiyo Kata ya Mkonona.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Tatizo la mawasiliano ni kubwa sana kwenye Visiwa vya Ukerewe, hususan kwenye maeneo ya Bwasa, Kata ya Igala na maeneo ya Bukiko, Kata ya Bukiko. Sasa je, Serikali iko tayari kutumia wataalam wake kufanya utafiti na kusaidia upatikanaji wa mawasiliano kwenye maeneo haya ya visiwa vya Ukerewe? (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko tayari. Naomba tu nitoe kauli kwamba Mfuko wetu wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) waifanye kazi hiyo haraka iwezekanavyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niipongeze Wizara hii imekuwa ni siku sana. Katika Jimbo la Mlalo karibu Kata zote sasa mawasiliano yapo, isipokuwa katika Kata ya Rangwi na Kata ya Malindi hasa eneo la Makose. Je, ni lini sasa katika hii Kata ya Rangwi na Malindi mawasiliano ya simu za mkononi yatapatikana?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rashid Shangazi kwa namna anavyofuatilia mambo mbalimbali, hususan barabara pamoja na mawasiliano katika Jimbo lake. Nimhakikishie, kama ambavyo nimekuwa nikimweleza wakati anakuja ofisini kufuatilia shughuli za wananchi wake kwamba, haya maeneo machache ya hizi Kata mbili za Malindi, Rangwi, Serikali itaangalia uwezekano wa kuyafikia na hasa kwa kushirikiana na wadau wetu kwa maana ya makampuni ya mawasiliano ya simu. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Matatizo yaliyopo ya usikivu wa simu Jimbo la Nanyumbu ni sawa na yaliyopo Wilaya ya Ngara katika Kata ya Mganza, Nyakisasa, Keza, Kabanga na Rusumo, ambayo yanaingiliana na nchi jirani za Rwanda na Burundi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha usikivu wa simu katika Kata hizi? (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia na vilevile nilimsikia Mbunge wa Jimbo ameeleza kwa muda mrefu sana matatizo ya Jimbo hilo. Namwona pale nimhakikishie na nimhakikishie Mheshimiwa Semuguruka kwamba, upacha wao ni lazima uzae

matunda katika miaka hii mitano na tutafuatilia maeneo hayo ili hatimaye mawasiliano yapatikane ya uhakika. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lako.

Na. 74

Upanuzi Uwanja wa Ndege – Sumbawanga

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA aliuliza:-

Serikali ilipanga kujenga na kupanua Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga Mjini.

Je, ni lini ujenzi huo utakamilika pamoja na kuwalipa fidia wananchi wanaozunguka uwanja huo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa.....

Nani anajibu swali sioni mtu akisimama, Mheshimiwa Naibu Waziri ameelekeea wapi? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kujenga Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga kwa kiwango cha lami pamoja na jengo jipya la abiria (*Terminal Building*). Kiwanja hiki ni mionganini mwa viwanja vinne ambavyo vitajengwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Rasilimali ya Ulaya (*European Investment Bank*). Viwanja vingine vitakavyojengwa kwa mkopo kutoka European Investment Bank katika kundi hili ni Viwanja vya Shinyanga, Kigoma na Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi zilitangazwa mwezi Agosti, 2016 na kufunguliwa mwezi Oktoba, 2016 ambapo Mkataba na Mkandarasi wa kujenga kiwanja hiki utasainiwa baada ya kupata idhini (*no objection*) kuhusu taarifa ya uchambuzi wa zabuni ambayo watu wa EIB (*European Investment Bank*) tunatarajia kuipata. Aidha, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa zoezi la uhakiki wa mali za wananchi ambao wataathirika na mradi huo lipo katika hatua za mwisho.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, wananchi wale walifanyiwa tathmini ya nyumba zao muda mrefu na kwa kuwa, pesa inapanda thamani kila kukicha. Je, Serikali ipo tayari kuwafanya tathmini upya na kuwalipa kwa wakati?

Swali la pili; kwa kuwa, wananchi hawa wamepoteza imani na matumaini ya kulipwa fidia zao kwa wakati na kwa kuwa, jitihada za Mbunge wa Jimbo Mheshimiwa Aeshi Hilaly, amekuwa akifanya juhudhi muda mrefu. Je, Mheshimiwa Waizri yupo tayari kuongozana nami mpaka kwa wananchi ili akajionee mwenyewe nyumba zinavyobomoka? Ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilieleza katika jibu la swali la msingi kwamba hivi tunavyoongea suala la uhakiki wa mali za wananchi ambao wataathirika na mradi huu lipo katika hatua za mwisho. Kwa maana hiyo, taarifa kamili ya nani na nini watalipwa inatarajiwa kupatikana hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwenda kujionea madhara ambayo wananchi wale waliosimamishwa muda mrefu kuendeleza nyumba zao, naomba sana uwasiliane na Mheshimiwa Aeshi ili Mheshimiwa Aeshi aniruhusu niongozane naye. Kwa sababu, nina uhakika Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata na Mheshimiwa Aeshi wanafanya kazi moja ya kuwatetea wana Sumbawanga, nimhakikishie tu kwamba nitakuwa tayari kuongozana na yeye akiwa na Mheshimiwa Aeshi. (Makofi)

WABUNGE FULANI: Aaah!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri kama unatoa ahadi ya kwenda utaenda na aliyeuliza swali. Kama Mheshimiwa Aeshi ataambatana na wewe huo ni uchaguzi wake. (Makofi/Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Aida Khenan swali la nyongeza!

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa, tathmini imefanyika toka mwaka 2009 mpaka leo hakuna kitu kinachoendelea. Wananchi wa Sumbawanga wanataka majibu ya uhakika ni lini watalipwa pesa zao, kwa sababu ahadi zimekuwa za kila siku?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba mara baada ya uhakiki unaofanyika kukamilika, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuwalipa wananchi hao fidia zao. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu lako la msingi lilisema mmeshamaliza uhakiki, kwa hiyo, naomba tafadhali, bajeti ijayo muwatengue watu fedha zao. (Makofij)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Saul Henry Amon, Mbunge wa Rungwe, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete.

Na. 75

Mradi wa Masoko Group Water Scheme

MHE. FREDY A. MWAKIBETE (K.n.y. MHE. SAUL H. AMON) aliuliza:-

Mradi wa Masoko Group Water Scheme umeshughulikiwa kidogo na miundombinu tayari imeshaharibika.

Je, ni lini mradi huu utamaliziwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saul Henry Amon, Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Masoko Wilayani Rungwe unatarajiwa kuhudumia jumla ya vijiji 15. Mradi huu ni mionganini mwa miradi inayojengwa chini ya programu ya maendeleo ya sekta ya maji kwa fedha za ndani. Mradi huu ulisimama baada ya Halmashauri kuvunja mkataba na Mkandarasi ajulikanaye kwa jina la Osaka Store.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu kwa sasa umeanza tena kutekelezwa na Mkandarasi Multi Professional Limited, aliyeanza kazi mwezi Februari, 2016 ambapo awamu ya kwanza inahusisha ujenzi wa chanzo cha Mbaka, ujenzi wa tenki la kuhifadhi maji Kijiji cha Lufumbi, kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 12.6 na kujenga vituo vitano vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe tayari mwezi Disemba, 2016 ilitangaza zabuni ya kuwapata wakandarasi watakaotekeliza ujenzi wa awamu ya pili utakaohusisha ulazaji wa bomba kilomita 92.1 na ujenzi wa vituo 135 vya kuchotea maji. Mradi huu ukikamilika utagharimu jumla ya shilingi bilioni 5.3 na utawanufaisha wananchi wapatao 19,624 katika Vijiji vya Bulongwe, Ngaseke, Igembe, Ntandabala, Lupando, Bujesi, Lufumbi, Nsaya, Ikama, Itagata, Busiya, Mbaka, Isabula, Lwifa na Nsanga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fredy Mwakibete, swali la nyongeza.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo wameushughulikia mradi huu wa masoko na miradi mingine iliyo ndani ya Wilaya ya Rungwe. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza; kwa kuwa, mradi huu wa maji umechukua muda mrefu na Mkandarasi aliyekuwa amepewa

kazi hiyo Osaka, baada ya kutangazwa tenda ya mara ya pili anaondolewa. Tungependa kufahamu ni sababu gani zimesababisha Mkandarasi huyu wa mara ya kwanza ashindwane na Halmashauri?

Swali la pili; kwa kuwa, miradi hii ya maji ni ya thamani kubwa, zaidi ya bilioni tano tungependa tumwombe Mheshimiwa Naibu Waziri aweze kuitembelea hii miradi pamoja na ya Mwakaleli One pamoja na Kapondelo ikiwemo na hii ya Masoko. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji swali ni moja halafu lingine nadhani ni ombi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ameuliza sababu zilizofanya Mkandarasi asimamishwe kuendelea na kazi, sababu ziko kimkataba. Kwa hiyo, sababu za kimkataba hatuwezi kuzijadili sisi Waheshimiwa Wabunge, lakini la kuelewa tu ni kwamba, alishindwa ku-perform vile ilivyokuwa imetakiwa kimkataba ndiyo maana Halmashauri kwa kutumia vifungu vya mkataba ikamsimamisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Rungwe. Kwa mara ya kwanza ameleta bajeti ya miaka mitano na nimefurahi sana. Ameweka mpango wa miaka mitano na bajeti inayotakiwa akaweka na kifungu cha matengenezo ya miradi atakayokuwa ameitekeleza ili kuhakikisha kwamba miradi tunayojenga basi inakuwa ni ya kudumu na mabomba yanaendelea kutoa maji mwaka mzima. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, na mimi nina swali la nyongeza kwenye hili. Mheshimiwa Mwakasaka! (Makofi)

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nauliza swali ambalo kama ilivyo Rungwe ule mradi wa Masoko, Tabora Mjini ule mradi wa Ziwa Victoria, kuna vijiji ambavyo niliviorodhesha kwenye swali Na. 57 liliojibiwa hapa Bungeni ambavyo ni Vijiji vya Itetemla, Uyui, Ntalikwa, Kabilia, Mtendeni, Itonjanda na baadhi ya maeneo ambayo ni ya Kata za Tumbi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji hivi na hizi Kata havijaorodhesha kwenye huu mradi wa Ziwa Victoria na vina shida sana ya maji. Sijui vitapitiwa lini na mradi huu wa Ziwa Victoria? Naomba swali langu lipatiwe majibu. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, japokuwa swali siyo la nyongeza hilo ni la msingi kama ilivyo, lakini naona upo tayari kulijibu majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa Tabora Mjini kuna mradi mkubwa wa maji ambaa umekamilika kutoka bwawa la Igombe na kwamba maji yanayozalishwa ni lita milioni 30 kwa siku wakati mahitaji ni lita milioni 24. Kwa hiyo, kwa maana ya Tabora Mjini tayari imeshakamilisha huduma maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tupo na mradi ambaa sasa hivi upo kwenye zabuni ambaa utatoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Nzega, Tabora na

Igunga. Kwa hiyo, nina hakika kabisa kwamba sasa Tabora itakuwa na maji mengi na ndiyo maana tunataka hayo maji yakishafika tuyaelekeze yaende mpaka eneo la Sikonge. Kwa hiyo, Vijiji vyote Mheshimiwa Mbunge ambavyo havina maji nje ya Manispaa ya Tabora kuitia mradi huo tutakuwa na maji ya uhakika kuhakikisha sasa kata na vijiji vyote vinapata maji ikiwemo na sehemu ya eneo la Uyui. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rhoda Kunchela, swali la nyongeza.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Katika Mkoa wa Katavi kumekuwa na changamoto kubwa ya miradi ya maji kuendelea kususua kwisha. Je, ni lini sasa Serikali itasema mikakati ya kujenga hii miradi ili iishe kwa wakati, kwa sababu pesa nyingi zimekuwa zikutumika mfano, kwenye Kata ya Ugala ambako kuna mradi mpaka sasa ni miezi sita, mradi umesimama. Sasa, ni lini Serikali itamaliza kujenga hii miundombinu ya umwagiliaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa Mkoa wa Katavi, eneo la Mpanda linahitaji lita milioni 11 kwa siku, lakini sasa hivi maji yanayozalishwa ni lita milioni 3.5. Tayari tumeshakamilisha mradi wa Ikolongo na wananchi wanaendelea kupata huduma; lakini tuna miradi miwili ambayo tunasaini mwezi huu kwa ajili ya kuleta maji Mji wa Mpanda. Kwa upande wa eneo la Ugala kwanza lina bwawa moja kubwa ambalo linaweza kuhudumia ule Mji wa Ugala. Sasa hivi kuitia kwenye Halmashauri tunayo miradi ambayo inaendelea kuhakikisha kwamba wananchi wa Ugala wanapata huduma ya maji.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea wakati nikiuliza swali langu la nyongeza ambalo si lazima nijibewe leo. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ni lini mradi wa Masoko utakamilika? Ndiyo swali lilikuwa hilo, lini mchakato utaendelea, lakini lini utaje kabisa, siyo leo, utanijibu nikisharudi kwenye Kiti wakati mwagine, kwa sababu siruhusiwi kuuliza maswali ya nyongeza. (Makofii)

WAheshimiwa Wabunge tunaendelea, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Azza Hamad.

Na. 76

Kusimama kwa Miradi ya Maji ya World Bank - Solwa

MHE. AZZA H. HAMAD (K.n.y. MHE. AHMED ALLY SALUM) aliuliza:-

Miradi ya maji ya World Bank katika Jimbo la Solwa imesimama kwa sababu ya Wakandarasi kutokulipwa fedha zao kwa muda mrefu sasa:-

Je, ni lini Serikali itawalipa Wakandarasi fedha zao ili miradi hiyo ikamiliike.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Jimbo la Solwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli miradi mingi ya maji ikiwemo miradi ya Jimbo la Solwa ilisimama kutokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha. Serikali kuitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji mpaka sasa imeshatuma fedha kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kiasi cha shilingi bilioni 1.17 kwa ajili ya kuwalipa Wakandarasi kulingana na hati zao za madai walizowasilisha. Kwa sasa wakandarasi wote wanaojenga miradi ya maji katika Halmashauri ya Shinyanga Jimbo la Solwa wanaendelea na kazi katika Vijiji vya Mendo, Nyashimbi, Mwanamadilana na Mwakitolyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutuma fedha katika Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Shinyanga kwa kadri fedha zitakavyopatikana ili kuhakikisha miradi yote inakamilika kama ilivyokusudiwa. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Azza Hamad, swalii la nyongeza.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji nina maswali mawili ya nyongeza. Naibu Waziri amekiri miradi hii imechukua muda mrefu kutoka 2012 mpaka leo hii haijakamilika; Je, Wizara haionti sasa ni muda muafaka wanapokuwa wamepelekewa certificate waweze kulipa malipo haya kwa muda muafaka kwa sababu wanawachelewesha wakandarasi. (Makofii)

Swali la pili; miradi hii imechukua muda mrefu sana mpaka muda huu imefikia asilimia 70 ya utekelezaji. Mheshimiwa Naibu Waziri haoni ni muda muafaka sasa wa kuanza kutafuta fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi hii? (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza amesema Serikali ione haja ya kulipa haraka certificate, tunafanya hivyo Mheshimiwa Mbunge kwamba certificate ikishawasilishwa kwenye Wizara yetu na Halmashauri yoyote, kitu cha kwanza lazima tuihakiki, hatuwezi kulipa moja kwa moja bila kuhakiki kwa sababu imetokea huko nyuma tulipotoka, mtu analeta certificate unatoa hela, halafu hela inakwenda kukaa kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati mwiningine ucheleweshaji wa kulipwa unatokana na ule uhakiki ili kujiridhisha kwamba kweli kazi imefanyika na kwamba hela ile ikifika ni moja kwa moja inakwenda kwa mkandarasi mhusika ili kazi iweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili kwamba Serikali sasa haionti kwamba ni wakati muafaka wa kutafuta fedha. Kwa bahati nzuri Waheshimiwa Wabunge katika bajeti iliyopita ambayo sasa hivi tunaitekeleza mlipitisha ninyi wenywewe fedha za Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika Bunge hili amesema mpaka sasa tayari tumeshapokea zaidi ya bilioni 71 ambazo zimetokana na Mfuko wa Maji na fedha hizi mpaka hapa ninapoongea Waheshimiwa Wabunge kwamba tayari tuna fedha kwenye Wizara, kwa hiyo, wakati wowote certificate ikifika tunailipa. Kwa hiyo, Serikali tayari inakusanya fedha kuhakikisha kwamba miradi mingi ambayo ilikuwa imekwama inaendelea na utekelezaji wake ili iweze kukamilika. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Haule, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Miundombinu ya mradi wa umwagiliaji wa Bwawa la Dachi lililopo katika Kata ya Malolo liligharimu takribani sh. 600,000,000 ambazo zilifadhiwa na Shirika la JICA la Japan lakini miundombinu hiyo imeharibika vibaya na imejengwa chini ya kiwango.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwashughulikia wale wote waliofanya ubadhilifu huu na inachukua hatua gani ya kuokoa mradi huu ambao sasa Mto Mwega umejaa mchanga na kuharibika na wananchi wakiwa wanategemea sana bwawa hili kwa ajili ya umwagiliaji pale Malolo? (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haule swali la nyongeza huwa ni moja, Mheshimiwa Naibu Waziri ujibu swali moja, majibu mafupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa taarifa kwamba kuna mradi wa umwagiliaji umejengwa eneo la Malolo na kwamba mradi huo pengine umepata shida kutokana na mafuriko au pengine kutokana na usanifu haukuwa sawasawa au ujenzi haukufanyika vile inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kitu tutakachofanya tutakwenda kuchunguza kuona ni nini kilichopo na tukishachunguza kitu cha kwanza ni kuhakikisha tunaboresha mradi huo ili uendelee kufanya kazi iliyotarajiwa. Baada ya kufanya uchunguzi kama kuna tatizo lolote ambalo tutaliona kwamba lipo, basi litashughulikiwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, Mbunge wa Segerea sasa aulize swali lake.

Na. 77

Kurudishwa kwa Wananchi "Msitu wa Nyuki"

MHE. BONNAH M. KALUWA aliuliza:-

Katika maeneo ya Kata mpya ya Bonyokwa Jimboni Segerea kuna msitu unaoitwa "Msitu wa Nyuki" ambao kwa muda mrefu umekuwa kichaka cha kujifchia majambazi; na wapo wananchi ndani ya Jimbo hilo waliokumbwa na tatizo la bomoa bomoa katika Kata za Buguruni Mnyamani, Tabata Liwiti, Vingunguti na Kipawa wanaozunguka bonde la Mto Msimbazi ambao hawana pa kwenda:-

Je, Serikali haioni kuwa ni busara kurudisha Msitu huu kwa wananchi hao waliokumbwa na tatizo la bomoabomoa ili waweze kuweka makazi yao eneo hilo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Moses Kaluwa, Mbunge wa Segerea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Msitu wa Kinyerezi wenye ukubwa wa hekta 4.4 ulipimwa mwaka 1997 ukiwa chini ya usimamizi wa Serikali Kuu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Msitu huu ambaa ndio msitu pekee uliopo ndani ya Jiji la Dar es Salaam ukiacha misitu ya mikoko, kwa sasa unatumika kama Ukanda wa Kijani (Green belt), hifadhi ya ardhi kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo ambaa unatishia kutokea katika maeneo yanayozunguka msitu na kituo kwa ajili ya mafunzo ya elimu ya misitu na upandaji miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa msitu huu ndani ya Jiji ni fursa adimu inayoweza kuendelezwa na kutumika kama sehemu muhimu ya kutembelea kwa utalii katika Jiji la Dar es Salaam. Serikali ina mpango kabambe wa kufanya msitu huu kuwa forest park ili kufanya shughuli za utalii wa kiikoloja (eco-tourism) kwa kuwa katika msitu huo pamoja na sifa nyingine kuna aina za miti zilizo hatarini kutoka duniani ukiwemo mpingo. Hivyo, Serikali inahamasisha uhifadhi shirikishi kwenye rasilimali hiyo kwa manufaa ya wananchi waishio jirani na msitu huo na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la wananchi waliokumbwa na zoezi la bomoa bomoa katika Kata za Buguruni Mnyamani, Tabata Liwiti, Vingunguti na Kipawa wanaozunguka bonde la Mto Msimbazi na kukosa makazi, Wizara yangu inawashauri wachukue hatua sahihi kwa kushirikiana na taasisi na mamlaka husika za Serikali ili kupata elimu na taratibu za mipango miji zitakazowezesha upatikanaji wa suluhisho endelevu la changamoto walizonazo kuhusu makazi bila kuathiri dhana nzima ya uhifadhi endelevu wa misitu. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, swali la nyongeza.

MHE. BONNAH M. KALUWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Kwa kuwa, Wizara ya Maliasili imelitelekeza hili eneo kwa muda mrefu na hili eneo limekuwa ni eneo hatarishi na lipo katikati ya makazi ya watu, watu wamekuwa wakipita hapo wanavamiwa na wengine wameumizwa. Je, Wizara haioni sasa umefikia wakati muafaka kulirudisha hili eneo Manispaa ya Ilala ili liweze kutumika kwa maendeleo ya Watanzania wote. (Makofii)

Swali la pili; Jimbo la Segerea lina wakazi wengi lakini ndio Jimbo mpaka sasa hivi halina kituo cha afya, halina soko, halina viwanda vidogovidogo ambavyo wananchi au vijana wanaweza wakajiendezea. Je, Wizara ya Maliasili haioni kwamba umefikia wakati ilirudishe hili eneo kwa wananchi wa Jimbo la Segerea ili sisi tuweze kujenga kituo cha afya na mimi Mbunge wa Jimbo la

Segerea nitatoa milioni 50 katika Mfuko wa Mbunge ili tuweze kuanzisha kujenga kituo cha afya. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalii lake la kwanza Wizara hajijatelekeza eneo la Msitu wa Kinyerezi na badala yake mionganii mwa maeneo ambayo tayari yana maboya kwenye mipaka na ambayo yana mabango na usimamizi wake unaendelea kwa kufuata mipaka hiyo niliyoitaja ambayo imeshawekwa alama kama nilivyotangulia kusema eneo la msitu huu ni mojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyo sema eneo hili ni la hekta 4.4 tu. Eneo la hekta 4.4 ni dogo sana, tunapata changamoto kubwa sana kama Taifa ya kwamba Miji inaonekana kama vile ili uone mahali kuna mji ni sawasawa kwamba panatakiwa pawe mahali palipo wazi kabisa hapatakiwi kuwa na miti hata kidogo. Hii ni dhana ambayo tunapaswa kuondokana nayo twende katika mwelekeo ambaao Miji yetu itakuwa pamoja na majengo na vitu vingine unavyoweza kuviona kama miundombinu, misitu iwe ni sehemu mojawapo. Tuwe na miti, bustani ndiyo tunaweza kuwa na miji ambayo itakuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalii la pili la mahitaji ya eneo; nimesema kwenye swalii la msingi, llala ina eneo kubwa bado kwa mujibu wa sensa iliyopo ina jumla ya hekta 21,000. Kwa hiyo, hakuna uhaba wa ardhi, tuna changamoto ya matumizi bora ya ardhi. Haya mambo mawili ni tofauti. Kukosa ardhi au kuwa na uhaba wa ardhi na kukosa mbinu za matumizi bora ya ardhi ni mambo mawili tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu narudia tena Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Baraza la Madiwani na Halmashauri ya Wilaya inayohusika, waende wakakae wajaribu kuangalia llala kwa ukubwa wake na eneo lake lote, miundombinu iliyopo na fursa zingine zilizopo za matumizi ya ardhi, wafanye mpango bora wa matumizi ya ardhi ili waweze kupata maeneo ya kuweza kujenga miundombinu alioizungumzia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa John Mnyika, swalii la nyongeza.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Wakati likijibowiwa swalii juu ya Msitu wa Nyuki, Serikali imeeleza kwamba inakusudia kuendeleza msitu huu kuwa sehemu ya vivutio vya utalii Dar es Salaam. Kwa miaka mingi Serikali imekuwa ikitoa ahadi juu ya kuugeuza msitu wa akiba wa Pande (Pande Forest Reserve) kuwa kivutio cha utalii, ikafikia hatua mpaka Serikali ikatangaza tenda.

Sasa kama msitu huu mpaka leo haujakamilika kuwa kivutio cha utalii ni miujiza gani ambayo Serikali inayo ili kuharakisha kwamba haya mapori ya Dar es Salaam yageuzwe kuwa sehemu za utalii na kuingiza kipato kwa Dar es Salaam badala ya kuyaacha kama yalivyo na hatimaye kugeuka kuwa misitu ya mauaji kama ilivyokuwa pori la akiba la Mabwepande. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze kwa mtazamo ambao ni chanya wa kwamba, kwanza anakubaliana na dhana nzima ya matumizi bora ya maeneo ya misitu; hapingani na dhana nzima ya Serikali kuhusiana na kuifanya misitu iwe ni rasilimali ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya maslahi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwamba kuna ucheleweshaji kama ambavyo amesema; nataka nimtoe wasiwasi kwamba historia ni nzuri, inatukumbusha tulipotoka, mahali tulipo na inatuwezesha kuona kule ambako tunakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Mheshimiwa Mnyika akubaliane tu na rai yangu kwamba tumetoka huko tulikotoka, mipango imekuwepo lakini sasa awamu hii mipango hii ninayoizungumza ni uhakika na kwamba nataka anipe muda wa mwaka mmoja tu, halafu aweze kuona katika eneo hili tunafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. matatizo yaliyopo huko Segerea yapo pia katika Jimbo langu la Manyoni Magharibi katika Halmashauri ya Itigi kuna msitu unaitwa Chaya Open Area, ni kitalu cha uwindaji ambacho muda mrefu hakina Mwekezaji. Sasa Serikali inataka kuondoa wananchi ambao wamekaa pale kwa ajili ya kulima na wanafuga vizuri sana. Je, Serikali inaweza ikaona umuhimu wa wananchi wale kuendelea kutumia Chaya Open Area ambapo ni eneo ambalo halina kabisa faida kwa ajili ya uwindaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, anazungumzia eneo la Chaya na anatoa maoni kwamba pengine Serikali ilioe sasa eneo hili kwa ajili ya matumizi ya kibinadamu kwa wananchi wa eneo hilo na wanaozunguka eneo hilo. Tumejibu swali hili mara nyingi kama Serikali kwamba tunayo changamoto kama Taifa ya kwamba katika maeneo kadhaa wananchi wamepata au wameonekana kuwa na uhitaji wa maeneo kwa ajili ya matumizi ya kibinadamu yakiwemo makazi, kilimo pamoja na ufugaji. Kama Serikali tumekwishesema kwamba jambo hili linatakiwa lishughulikiwe kisayansi na kitaalam. Huwezi kuzungumzia juu ya uhaba wa ardhi jujuuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wakati huu tunavyoendelea tayari Serikali imekwishaunda Kamati ya Kitaifa inayohusisha Wizara nne ambayo inapita katika maeneo yote ya nchi hii kuangalia kwa uhalisia kabisa wapi kweli kuna uhaba wa ardhi na wapi kweli ardhi tungeweza kuitumia kwa namna bora zaidi. Kamati hii itasaidia baadaye Serikali iweze kuja kusema kwamba eneo hili ni kweli linaweza likabadiishwa matumizi na eneo lingine liendelee kubakia kutumika kwa namna ambayo sote tutakubaliana tukiwa tunaongozwa na Serikali kwamba matumizi hayo ya hivi sasa ni matumizi ambayo yana tija zaidi kwa Taifa.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Na. 78

Gharama ya Ukaguzi wa Filamu

MHE. COSATO D. CHUMI aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapunguzia wasanii gharama za ukaguzi wa filamu ambapo kwa hivi sasa gharama hizo ni shilingi elfu moja kwa dakika?

(b) Je, Bodi ya Filamu imejipanga kwa kiasi gani kuhakikisha huduma zake zinatambulika nchi nzima tofauti na sasa ambapo ni wasanii wachache wa filamu ndio wanafahamu wajibu na majukumu wa Bodi hiyo ambayo hata ofisi zake hazijulikani ipasavyo sehemu zilipo Jijini Dar es Salaam?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ada za uhakiki kwa nchi yetu zipo kwa mujibu wa sheria na kanuni. Gharama hizi hulipwa kwa nakala mama tu (*master*) baada ya hapo mtayarishaji huzalisha nakala kwa idadi anayohitaji. Nchi yetu hutoza ada ambazo ni rafiki ukililinganisha na nchi nyingine. Kwa mfano, Nigeria ambayo ni nchi iliyopiga hatua kubwa kwa upande wa filamu hutoza filamu yenye urefu wa dakika 60 ambayo ni filamu ya lugha ya asili kwa naira 30,000 sawa na zaidi ya dola 150 ambayo ni sawa na Sh. 337,950 kwa viwango vya ubadilishaji vya Sh. 2,253 kwa dola na Kenya ni sawa na Sh.190,000 za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hutoza filamu za Kitanzania zenye urefu wa dakika 60 kwa Sh.60,000 sawa na Sh.1,000 kwa dakika. Gharama hizi ni asilimia 18 ya zile za Nigeria na asilimia 32 ya zile za Kenya. Kwa maana hiyo, ni wazi kwamba Tanzania hutoza ada ambayo ni nafuu na rafiki.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Filamu imeendelea kujitangaza kwa wadau kupitia shughuli mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa. Mfano kushiriki katika Maonesho ya Sabasaba, Nanenane, Wiki ya Vijana na Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru na Jumuiya ya Afrika Mashariki Utamaduni Festivals. Vilevile Bodi inatumia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo TBC1, E-FM, Clouds Media, Gazeti la Mtanzania na kadhalika. Pia Bodi imekuwa ikifanya warsha za kuwajengea wadau weledi katika masuala ya filamu sehemu mbalimbali ikiwemo mikoa na wilaya ambapo ni sehemu ya kujitangaza. Aidha, Bodi inakamilisha tovuti yake ambayo itasaidia kujitangaza na itaendelea kutumia vyombo vya habari, machapisho na warsha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Bodi za Mikoa na Wilaya ambazo zinafanya majukumu ya Bodi katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Wizara kwa

kushirikiana na TAMISEMI itaendelea kuimarisha Bodi za Mikoa na Wilaya ili ziweze kutoa huduma kwa wigo mpana zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi za Bodi awali ziliwa Barabara ya Morogoro, Jengo la *Textile* ambapo hapakuwa rafiki kwa wadau. Mwaka 2012, Wizara ilihamisha ofisi za Bodi kwenda Mtaa wa Samora, Jengo la Shirika la Nyumba, Plot No. 2271/32 ambapo zipo Ofisi za Habari Maelezo mkabala na Tawi la Benki ya NMB, ghorofa ya kwanza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cosato Chumi, swali la nyongeza.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nieleze masikitiko yangu kwamba yaani kumbe mpaka leo Bodi haina tovuti, 2017, *this is very bad, ni jambo la kusikitisha. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niende kwenye swali langu la kwanza la nyongeza, nimeona muainisho wa hizo gharama, wasanii wanapokwenda kusajili, pamoja na hizo gharama lakini wanalazimika kwenda kupata huduma hii Dar es Salaam tu haitolewi katika maeneo mengine. Wakishapata hii huduma ya kutoka BASATA kusajili COSOTA na Bodi ya Filamu, kuna huduma nyingine kwenda TRA ili wapate stika ambayo ni mapato na stika zinatolewa tu Makao Makuu ya TRA Dar es Salaam. Je, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba angalau Ofisi hizi za BASATA, COSOTA na Bodi ya Filamu zinakuwepo hata katika ngazi ya mikoa ili kuwarahisishia wasanii na kuwapunguzia gharama? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuna hizi filamu za kutoka nje maarufu sana kwa jina la mazagazaga kwa sababu unakuta wametandika chini zimezagaazagaa, gharama yake *maximum* kwa CD moja ni Sh.1,200 lakini hazitozwi gharama zozote za usajili wala hakuna mapato yoyote ambayo Serikali inapata. Kwa kulinda kazi za ndani za wasanii wetu wa filamu wa ndani ambao CD zao sasa zimeshuka thamani hadi Sh. 2,000 halafu wanashindana na za nje za Sh.1,200 na Serikali inakosa mapato, je, inasemaji katika kudhibiti filamu hizi za kutoka nje, imeshindwa kabisa? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza anataka kujua kama kuna utaratibu wowote ambao Serikali imefanya ili wasanii waweze kupata vibali kutoka mikoani. Ninachoweza kusemea ni kuhusiana na Bodi ya Filamu, kama nilivyosema awali, Bodi ya Filamu tayari inazo ofisi katika Wilaya na Mikoa na kule kuna Bodi za Filamu za Mikoa na Wilaya ambapo RAS kwa upande wa Mkoa ndiye Mwenyekiti na Afisa Utamaduni ndiye Katibu na kwa upande wa Wilaya DAS ni Mwenyekiti na Afisa Utamaduni wa Wilaya ni Katibu na kuna wajumbe wengine katika Bodi hizi. Kwa hiyo, vibali vinatoka pia katika wilaya na mikoa na siyo lazima wafuate huduma hizi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa TRA zipo ofisi za mikoa lakini upande wa COSOTA sina uhakika sana. Hata hivyo, tunafanya mazungumzo na vyombo vyote hivi ambavyo vinadhibiti wizi wa kazi za wasanii na wajumbe wake wote ni wajumbe wa Kamati ya Urasimishaji na hivyo basi, tunafanya kila jithada ili tuweze kuona tunamkombo msanii kuanzia ngazi za wilaya, mkoa na hata makao makuu Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa BASATA, mpaka sasa tunataka kufanya utaratibu wa usajili kwa njia ya mtandao pamoja na Bodi ya Filamu. Hivyo, niwahakikishie wasanii kwamba huduma hizi zitafikishwa kwa na watakuwa hawapati usumbufu sana kufika Dar es Salaam kwa sababu tunawatachia mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa filamu za nje, nadhani wengi tumekuwa mashahidi kwamba Serikali inafanya kila jithada. Zoezi la urasimishaji lilianza tangu mwaka 2009 ambapo kazi za wasanii zilianza kuwekewa ushuru wa stempu tangu mwaka 2013 kwa Sheria ya Ushuru wa Stempu. Kwa zile kazi ambazo zinatoka nje na hazifuati utaratibu zimekuwa zikikamatwa na wahusika kuchukuliwa hatua. Napenda kuwatangazia kwamba zoezi hili ni endelevu, tumekuwa tukifanya msako au opereshenitangu 2014 hadi 2016 na tunaendelea. Hivyo, nawaoomba wote ambao wanauza kazi za wasanii nje ya utaratibu wafuate utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini pamoja na majibu yake mazuri, naomba kuongeza kwenye sehemu ya pili ya swali la Mheshimiwa Cosota Chumi. Ni kweli tatizo la kazi za sanaa kutoka nje katika nchi yetu ni kubwa na baya na linaua kwa kiasi kikubwa kazi za sanaa za ndani. Ili kushughulika na tatizo hili kuna sheria za vyombo zaidi ya vitano zinahusika. Kuna Sheria za TRA, BASATA, Bodi ya Filamu, COSOTA, ukizijumlisha zote kwa pamoja ndiyo at least unaweza kushughulika na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapitia upya sheria hizi na kuangalia upungufu uliopo, turekebishe na tuzi-harmonise kwa pamoja ili tuweze kulimaliza tatizo hili. Kwa sheria zilizopo, namna ya kushughulika na tatizo hili bado ni ngumu sana. Kwa hiyo, tunachoweza kuahidi hapa ni kwamba tunazipitia na tuko mahali pazuri na tukilikamilisha zoezi hilo kazi hii itakuwa imekwenda vizuri na kwa hiyo tutapambana na tatizo hili la piracy kwenye nchi yetu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Richard Ndassa, swali la nyongeza.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Wizara hii inashughulika na habari, utamaduni, sanaa na michezo. Kwa idhini yako, naomba uniruhusu niulize swali la michezo. Timu yetu ya vijana under 17 imebahatika kwenda kwenye fainali itakayofanyika Gabon Aprili, ni mwezi mmoja tu sasa umebaki. Je, Serikali pamoja na TFF tunajiandaa namna gani ili timu yetu hii isiende kushiriki bali iende kushindana na kuleta ushindi katika nchi yetu? (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, hilo ni swali jipya lakini naona uko tayari kulijibu. Mheshimiwa Waziri wa Habari, majibu.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serengeti Boys wamefanya vizuri sana katika mchezo wa mpira wa miguu katika nchi yetu na kuiletea heshima nchi yetu. Nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa moyo wao wa dhati ambapo wamejitahidi kupambana na kwa kweli wanafanya vizuri. Kama Serikali, kwanza nilihakikishie Bunge lako kwamba tumeshiriki kikamilifu kwa wao Serengeti Boys kufanikiwa kufika pale walipofika ikiwemo kutafuta rasilimali kwa wadau. Niwashukuru sana wadau wa sekta binafsi ambao wamekuwa wakijitolea kuhakikisha timu yetu hii inafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwa kushirikiana na TFF tumejipanga kwamba Serengeti Boys watakwenda kupiga kambi ya mwezi mzima kabla ya kwenda kwenye fainali za mashindano haya. Serikali ikishirikiana na wadau wa sekta binafsi, tutahakikisha zinapatikana rasilimali za kutosha kuhakikisha vijana hawa wanapiga kambi yao, lakini pia wanakwenda kuchukua kombe na siyo kushiriki. Kila tukiangalia uwezekano wa kushinda, ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa pamoja tuungane pamoja kwa dua zetu na rasilimali zetu kuhakikisha kwamba Serengeti Boys wanakwenda na wanarudi na ushindi hapa nchini. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Fedha na Mipango. Mheshimiwa Suzana Mgonokulima sasa aulize swali lake.

MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba yafanyike masahisho kwenye jina langu, naitwa Mgonukulima sio Mmono.

Na. 79

Serikali Kupeleka Fedha za Miradi kwa Wakati

MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA aliuliza:-

Miradi mingi ya maendeleo inashindwa kumalizika kwa wakati kutokana na Serikali Kuu kutokuleta fedha za miradi kwa wakati:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa wakati kwenye Halmashauri ili miradi ya maendeleo itekelezwe kwa kipindi kilichopangwa?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suzana Chogisasi Mgonukulima, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa kutumia fedha za makusanyo ya ndani, mikopo ya ndani na nje, misaada kutoka

kwa washirika wa maendeleo pamoja na makusanyo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato ya fedha za ndani (*tax revenues and non tax revenues*) hupelekwa katika Wizara, taasisi na idara mbalimbali za Serikali pamoja na Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kulingana na upatikanaji wa fedha kutoka katika kila chanzo. Aidha, asilimia 60 ya makusanyo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa hubakishwa katika Halmashauri husika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miradi inayotekelawa kwa kutumia fedha za mikopo ya ndani au nje, pamoja na fedha za washirika wa maendeleo, fedha hizo hupelekwa kwenye Halmashauri zetu mara tu zinapopatikana. Hivyo basi, uhakika wa mtiririko wa fedha kutoka vyanzo vyote vya mapato ndiyo msingi wa kupeleka fedha kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wetu Waheshimiwa Wabunge kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani katika Halmashauri zetu kupanga mipango stahiki, kuainisha vyanzo vya mapato na kusimamia ukusanyaji na matumizi ya mapato hayo ipasavyo ili kuziwezesha Halmashauri zetu kujenga uwezo wa kifedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hivyo kupunguza utegemezi kutoka Serikali Kuu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suzana Mgonukulima, swali la nyongeza.

MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na majibu ya Waziri, Manispaa ya Iringa ina miradi mikubwa ya Machinjio ya Kisasa ya Ngelewala, Soko la Ngome, Sekondari ya Mivjeni, Nyumba za Waganga na Waugazi wa Zahanati ya Njiapanda na Nduli. Katika Baraza la Madiwani, kuititia bajeti ya mwaka 2016/2017, Manispaa ya Iringa ilikadiria kukusanya mapato ya ndani Sh. 4,532,000,000 ili kuweza kumalizia miradi midogo iliyokuwa inaikabili Manispaa hiyo. Manispaa ya Iringa, vyanzo vikuu vya mapato vinatokana na kodi ya majengo, Serikali ikaamua kodi hizi za majengo zikusanywe na TRA, je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kupeleka hela za miradi hii kwa wakati ili kuweza kumalizia miradi ambayo haijamalizika hadi sasa? (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inaona umuhimu wa miradi yote ya maendeleo kama ilivyopitishwa katika bajeti yetu mwezi Juni. Hivyo, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kinachopelekea kupeleka fedha hizi ni upatikanaji wa fedha hizi. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameongelea kuhusu kodi ya majengo, naomba nimwambie kwamba TRA imekusanya kodi ya majengo mwezi wa Kumi, baada ya quarter ya kwanza kupewa Halmashauri zenyewe kukusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge, anapuhudhuria Baraza la Madiwani aweze kusimamia mapato yaliyopatikana ili

yawezo kutumika katika miradi aliyoitaja. Serikali yetu baada ya kukusanya kuanzia mwezi wa Kumi, fedha zote tulizoahidi zitarejeshwa katika Halmashauri husika kutohana na bajeti zilizopitishwa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda tutamalizia swali la mwisho.

Na. 80

Matumizi Holela ya Dola Nchini

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU aliliza:-

Je, ni kwa nini Serikali isidhibiti matumizi holela ya dola nchini ili kupunguza utakatishaji wa fedha na kuimarisha ukuaji wa uchumi kama zinavyofanya nchi nyingi duniani?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kudhibiti matumizi holela ya fedha za kigeni, Benki Kuu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania imeongeza usimamizi katika maduka ya kubadilisha fedha za kigeni ambapo taarifa za kila muamala wa fedha za kigeni unaofanywa zinapaswa kuoneshwa. Hatua zimechukuliwa pia kuhakikisha kuwa miamala ya fedha za kigeni inayofanywa na mabenki ni ile inayohusu shughuli za kiuchumi tu ili kulinda thamani ya shilingi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tamko na mwongozo uliotolewa na Serikali mwaka 2007, ulieleza kuwa bidhaa na huduma zinazowalenga watalii au wateja wasio wakazi wa Tanzania, bei zake zinaweza kunukuliwa kwa sarafu mbili yaani shilingi ya kitanzania na sarafu ya kigeni na malipo kufanyika kwa sarafu ambayo mlipaji atakuwa nayo. Pia, mkazi ye yeyote wa Tanzania asilazimishwe kulipia bidhaa au huduma yoyote hapa nchini kwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa kuruhusu soko huru la fedha za kigeni hapa nchini ni hatua ya makusudi ambayo ilichukuliwa na Serikali yetu ili kuiwezesha nchi kuondokana na hali ya kuadimika kwa fedha za kigeni. Mfano, kufikia Desemba, 2015 akiba ya fedha za kigeni ili kuwa dola za Kimarekani milioni 4,093.7 wakati amana za fedha za kigeni za wakazi wa Tanzania zili kuwa dola za Kimarekani milioni 2,933.1 na rasilimali za fedha za kigeni za mabenki zili kuwa kiasi cha dola za Kimarekani milioni 1,021.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, utulivu wa urari wa biashara ya nje umetokana na sera huru ya fedha za kigeni ambayo imechangia kuimarisha uchumi kwa zaidi ya miaka 10 iliyopita. Wastani wa ukuaji wa uchumi wa Taifa letu katika kipindi cha miaka 10 iliyopita ulikuwa ni asilimia saba ikiwa ni wastani wa juu sana ikilinganishwa na nchi zingine duniani. Mfano, wastani wa ukuaji wa uchumi wa

Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ni asilimia 5.4 katika kipindi hicho, wakati ule wa nchi zinazoibukia kiuchumi ulikuwa ni asilimia 5.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia zinazotumika kutakatisha fedha ni pamoja na kuziingiza fedha haramu kwenye taasisi za fedha na kuziwekeza katika rasilimali halali kama ardhi na nyumba. Baadhi ya mambo yanayowapatia wahalifu fedha haramu ni pamoja na biashara ya dawa za kulevyta, rushwa, ujangili, ujambazi, ukwepajji kodi na kadhalika. Fedha zinazotokana na shughuli za kihalifu zinaweza kuwa shilingi za Kitanzania, dola za Kimarekani au fedha nyingine yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko kanuni ambazo zinafuatwa na vyombo vya fedha ili kuzuia utakatishaji wa fedha zote zilizopatikana kutoka vyanzo haramu na siyo dola tu. Benki Kuu kupitia jukumu la usimamizi wa taasisi za fedha hufuafilia mabenki ili kuhakikisha kuwa kanuni hizo zinafuatwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dokta Dalaly Peter Kafumu, swali la nyongeza.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo hayatoshelezi kwa sababu niliwahi kuuliza swali hili lakini nimepata majibu yale yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la msingi, ni kwa nini tuendelee kutumia dola katika kununua, siyo uhuru wa soko. Sasa swali la kwanza, kwa nini Tanzania isitumie utaratibu wa nchi zingine kama Zambia, South Africa, Ghana, Dubai na Ulaya? Wote tumesafiri tumeona ukifika tu kwenye nchi hizo unaachana na matumizi ya dola lazima ubadilishe na ukalipe kwa hela yao. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa nini au ni lini Serikali sasa itakagua haya maduka ya fedha ambayo kwa kweli kuna taarifa za ki-intelijensia zinasema wanatumika kutorosha fedha zetu? Wakaguliwe, mapato yao yajulikane na ijulikane pia ni jinsi gani wanazitumia hizi fedha na kuziweka kwenye soko letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi Sheria yetu ya Benki Kuu ya mwaka 2006, Sehemu ya Tatu, kipengele cha 26 kimeweka wazi kabisa kwamba fedha halali kutumika ndani ya nchi yetu ni shilingi ya Kitanzania. Pia Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Kigeni ya mwaka 1992 inaruhusu mtu ye yeyote kupokea na nimeeleza kwa nini Serikali yetu imepitisha sheria zote mbili, dhamira ikiwa ni kukuza uchumi wetu na kuwa na fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwambie tu Dokta Kafumu kwamba nchi nyingine hufuata utaratibu kutokana na mazingira ya nchi yao. Kwa nchi yetu hatujaona athari kubwa ya kuruhusu wageni wetu kutumia fedha hizo ndani ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni lini Serikali itakagua, naomba nimwambie kwamba, Serikali yetu inakagua siku hadi siku. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi Serikali yetu haijalala, Benki Kuu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato zinakagua siku hadi siku na sasa miamala yote ya maduka haya ya kubadilishia fedha yanakuwa monitored na Benki Kuu kupitia TRA. Pia tunaendelea kuimarisha mifumo yetu ili kuhakikisha fedha na uchumi wetu uko salama kabisa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda tutaishia hapo kwenye kipindi chetu cha maswali na majibu. Nitaleta matangazo tuliyonayo mezani leo. Tunayo makundi mawili ya wageni waliotufikia.

Kundi la kwanza ni wageni walioko Jukwaa la Spika, wageni 10 wa Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na Spika wa Baraza, Mheshimiwa Zubeir Ally Maulid. Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi ameambata na Naibu Spika wa Baraza hilo, Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Katibu wa Baraza, Ndugu Raya Issa Mselem na watendaji wengine wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, Zanzibar. Karibuni sana. (Makofii)

Kundi lingine ni wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Karibuni sana wageni wetu, hili ndio Bunge lenu. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, ninayo pia matangazo ya kazi. Tangazo la kwanza linatoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaye ni Mwenyekiti wa ibada, anawatangazia kwamba leo tarehe 7 Februari, 2017 Waheshimiwa Wabunge wote wanaombwa kuhudhuria ibada katika Chapel iliyopo Jengo la Pius Msekwa, ghorofa ya pili mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana. Aidha, Wana maombi wa Mkoa wa Dodoma watahudhuria ibada hiyo. Kwa hivyo, Wabunge wote mnakaribishwa.

Tangazo la pili ni la semina. Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba leo Jumanne, tarehe 7 Februari, 2017 kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu changamoto zinazokabili huduma za uzazi salama hapa Tanzania. Semina hiyo itatolewa na Muungano wa Utepe Mweupe wa Uzazi Salama (*The White Ribbon Alliance for Safe Motherhood Tanzania*) katika ukumbi wa Bunge kuanzia saa saba mchana. Sasa tangazo hili linamaanisha mtabaki humu ndani ili mwendelee na semina.

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa William Mganga Ngeleje ambaye ni Mwenyekiti wa BungeSports Club na ni tangazo linalohusu pongezi kwa SerengetiBoys. BungeSports club kwa niaba ya Mheshimiwa Spika na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla tunaungana na Watanzania wapenda soka kuipongeza kwa dhati kabisa timu yetu ya Taifa ya Vijana walio chini ya umri wa miaka 17 (under 17), Serengeti Boys kwa kufanikiwa kutinga fainali ya michuano ya Mataifa ya Afrika kwa vijana inayotarajiwa kufanyika nchini Gabon mwaka huu.

Endapo kwenye fainali hizo za Gabon, Serengeti Boys itafanikiwa kuingia hatua ya nusu fainali, basi timu yetu hii itafuzu kucheza michezo ya michuano ya Kombe la Dunia inayoratibiwa na Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) baadaye mwaka huu nchini India. Bunge Sports Club tunaamini kwamba timu yetu hii ya vijana ikiendelea kuimarishwa vizuri, ndio msingi wa kuiwezesha Tanzania kufikia

hatua ya fainali zijazo za AFCON na hata Kombe la Dunia kwa timu yetu ya TaifaStars. Bunge Sports Club inawaomba wadau wote wa soka na Watanzania kwa ujumla tuunganishe nguvu kuisaidia timu yetu hii ya Serengeti Boys katika maandalizi yake. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, hayo ni matangazo yaliyotufikia, kwa hiyo, tunaendelea. (Makofi)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. HALIMA J.MDEE: Mwongozo wa Spika.

MHE. JOHN W. HECHE: Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Mwongozo, Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa jambo lilitokea mapema jana. Jana Mheshimiwa Lissu baada ya kutoka kwenye Ukumbi wa Bunge na kuwa kwenye viunga vya Bunge alipofika karibu na getini alikamatwa na Polisi na tunaambiwa alisafirishwa jana usiku kuelekea Dar es Salaam. Nimeliuliza hili kwa sababu kilichotokea jana kwa Mheshimiwa Lissu ndicho kilichotokea kwa Mheshimiwa Lema miezi kadhaa iliyopita na tunavyozungumza Mheshimiwa Lema bado yupo ndani licha ya kwamba kosa lake ni dogo tu ambalo linaweza likapewa dhamana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa sababu ninyi ni viongozi wa Bunge na Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge inatoa ulinzi kwa Wabunge pale ambapo tumehudhuria vikao vya Bunge na tuko kwenye viunga vya Bunge. Tukiruhusu utaratibu unaoendelea wa Jeshi la Polisi kudhalilisha Wabunge wakiwa kwenye majukumu yao ya Kibunge wakati wana fursa nyingine ya kuweza kuwakamata kama kuna kosa lolote ambalo limefanyika, mhimili huu unapata udhalilisho wa hali ya juu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba mwongozo wako kama kiongozi wa Bunge hili, naamini kilichotokea jana ofisi ya Spika haijui na ustaarabu wa kawaida unasema, kama kuna shida na tuko kwenye shughuli za Bunge basi uongozi wa Spika uweze kujua ili tujue nini ambacho kinatoka kwa viongozi hawa. Naomba mwongozo wa Kiti chako, mnadhani ni sahihi kwa vitendo vinavyofanywa na Jeshi la Polisi ambao sijui wanapewa na nani kiburi cha kudhalilisha Wabunge wakiwa katika majukumu yao ya kila siku ya Bunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimesimama kwa Kanuni ya 47, kwanza nikiomba kusitisha shughuli za Bunge ili tujadili jambo la dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisikia watu wanauana Tarime vita za koo ni kwa sababu ya ardhi. Tarime ardhi ni pungufu kiasi kwamba ukienda kwenye Kata ya Nyanungu kwa mfano watu wanalima upande wa Kenya yaani hakuna eneo lolote wanaloeweza kulima upande wa huku kwetu inabidi wavuke upande wa pili walime halafu mazao yao yakikomaa wanavuna wanaleta huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu juzi kumetokea tukio ambapo DC anatembea na watu ambao anawaita wawekezaji, ameandika barua kwa kuwatumia watendaji kuzuia watu wa maeneo ya Kata ya Manga, Vijiji vya Mrito na Wegita kulima kwenye maeneo yao na amewaandikia barua hii kupitia VEO kuwazuia wasipande hata mazao kwamba hilo eneo linataka kupewa mwekezaji ambapo mimi Mbunge sina taarifa yake, Mwenyekiti wa Halmashauri ambaye ndiye kiongozi wa Halmashauri yetu hana hiyo taarifa na kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, DC hana mamlaka yoyote ya kugawa ardhi na maeneo haya watu wanayatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri wewe ni mwanasheria unajua, sheria yetu inaruhusu kama eneo limetumiwa na mtu kwa miaka 12 consecutive bila kuingiliwa wala kuzuiwa na kitu chochote hilo eneo linakuwa miliki yake. Pia ili ardhi igawanywe kwenye kijiji, Mkutano Mkuu wa Kijiji ndiyo unaruhusiwa kugawa ardhi kwa maana ya heka 50 mwisho, lakini DC anatembea na hawa watu ambao amewaweka mfukoni na jana nimemuuliza Waziri wa Viwanda anasema hiyo taarifa hana, watu wa TIC ambao ni *Tanzania Investment Centre* hawana hiyo taarifa. DC huyu anataka kuchukua ardhi kwa mabavu, wamemkamata Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya yuko ndani alipokwenda kutembelea eneo hilo, wamemkamata Katibu wangu yuko ndani na wamekamata wanavijiji wako ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali iko humu na jambo hili linawenza kusababisha tatizo, Tarime najua na mimi natoka hapa naenda huko mtayasikia yatakayotokea. Nimeomba ili tujadili kabla halijaleta balaa kwa sababu kutaka kucheza na ardhi ya watu wa Tarime ni kutaka kuchochaea machafuko. Kwa hiyo, nimeomba hili jambo kwa hekima yako na busara uruhusu lizungumzwe humu na Serikali itoe majibu ili tuokoe hali inayoweza kujitokeza kule Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. (Makofii)

WABUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Cosato Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Nitaenda moja kwa moja kwenye Kanuni ya 46 kuhusiana na swali langu kwamba Waziri au Wizara inapaswa ijibu vile ambavyo swali limeulizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitika sana kusikia kwamba kuna Bodi za Mikoa na Wilaya ambazo zinatekeleza majukumu ya Bodi, *this is not true, nothing is existing*. Ndiyo maana tunapopigia kelele jambo hili siyo tu kwa wasanii wa filamu lakini pia tunazungumzia mapato ya Serikali. Kama shughuli hizi zitarahisishwa wengi watajisajili na Serikali itapata mapato mengi. Sasa hizo Kamati ambazo ziko chini ya Ma-RAS na Ma-DAS na Makatibu ambao ni Maafisa

Utamaduni hata mama yangu Mheshimiwa Martha Mlata Msanii wa siku nyingi anajua hakuna kitu cha namna hiyo. Humu ndani kuna watu wameshakuwa Ma-DC wawe wakweli, kuna Kamati ya namna hiyo ambayo inafanya kazi ya Bodii? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapouliza maswali maana yake ni kwamba Serikali ikafanye utafiti ili itoe majibu siyo kwa kujifurahisha, hapana! Je, hicho kitu kipo, kinarahisisha na utekelezaji wake ukoje? Waziri anasema sheria ziko nyingi, lakini pia hakuna sera inayo-govern mambo haya, utaendaje kwenye sheria huna sera?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) kuhusiana na jambo lilijitokeza jana wakati wa mjadala wa Bunge kwa bahati mbaya hatukupata nafasi. Kwa busara yako naomba mwongozo ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme mimi binafsi naunga mkono jitihada za kukamata wauza madawa ya kulevyia, lakini dalili ya kwanza ya kuanza kumhisi mtu kama anajishughulisha na biashara ambazo hazieleweki, moja, ni mienendo ya mtu yeyote, siyo Mbunge wala nani kama Mheshimiwa Rais alivyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, RC wa Dar es Salaam mwaka 2015 alikuwa anakaa kwa Membe. Amekuwa RC kwa mwaka mmoja, RC wa Dar es Salaam anatumia lexus ya petrol ya zaidi ya milioni 400. Kama hiyo haitoshi, ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam imekarabatiwa kwa zaidi ya shilingi milioni 400 bila kufuata utaratibu wa manunuzi ya Serikali. Pia ana ma-V8 na Mwanza amejenga maghorofa kwa mwaka mmoja, ni akina nani hasa wanaotakiwa kujadiliwa na kufanyiwa uchunguzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa Mawaziri tulionao humu kwa nini mmepigwa ganzi? Utawala Bora, Mambo ya Ndani, Waziri wa Sheria, kwa nini mmepigwa ganzi mnalifanya suala hili ni la Rais kuanza kuhangaika na Mkuu wa Mkoa. Hata kama anachangiwa na wahisani, Sheria ya Maadili inatutaka anayetuchangia tumtangaze, lini amewatangaza wanaomchangia pesa? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kama wengine wanaweza kufanya mambo ya hovyo halafu akawa ana kinga na Mawaziri wakapigwa ganzi humu ndani hawawezi kufuatilia, utuelekeze, tunataka RC wa Dar es Salaam achunguzwe mali zake alizonazo. Kwa mwaka mmoja huwezi ukamiliki V8, ukaenda Marekani, ukajenga Mwanza na ukununua viwanja! Wala siyo suala la kuogopa. Ninachosema, niko tayari kuwasaidia Mawaziri na vyombo vyaya usalama tuwaoneshe, tunataka kumaliza wauza madawa, tuanze na mizizi, tusishike matawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. (Makofi)

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mwongozo wa mwisho utatoka kwa Mheshimiwa Mipata.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba mwongozo kwa Kanuni 68(7) kwa jambo lililotokea kwenye Jimbo langu. Hivi karibuni mwezi Desemba, Serikali imeamua kuifuta Shule ya Milundikwa Sekondari ambayo imejengwa na wananchi kwa miaka 17. Wazazi maskini, wamekusanya nguvu zao kwa muda wa miaka 17 wametengeneza shule nzuri, shule ya kata ambayo sasa hivi ni mionganoni mwa shule bora kabisa katika wilaya yangu. Shule hii ina matokeo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ina form one mpaka form six, watoto wa kike wako pale wa kidato cha tano na cha sita na tuna mabweni ya kutosha. Wananchi waliamua wenyewe kufanya shule nzima yenyewe watoto zaidi ya 384 kuwa ya bweni na tunachanga chakula. Ni shule inayofanya vizuri kitaaluma katika Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa agizo la Serikali kuanzia Desemba mwaka huu shule hiyo imefutwa na watoto wametawanywa. Watoto wa kidato cha tano na cha sita wameathirika. Watoto wa kike maskini ya Mungu wamepelekwa kwenye shule mbalimbali na watoto zaidi ya mia mbili na kitu wa kidato cha kwanza mpaka cha nne wamepelekwa kwenye shule ya Kasu ambayo ujenzi haujamalizika, miundombinu haijatosheleza, hakuna madarasa ya kutosha, hakuna vyoo vya kutosha na kwa kweli ni usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye shule hii wananchi wamewekeza vya kutosha kiasi cha zaidi ya shilingi milioni 871 kwa mujibu wa Mthamini wa Serikali. Serikali inalionaje jambo hili, haioni kwamba imewatendea dhambi wananchi ambaa wamehimizwa kujenga shule na wamejenga kwa mikono yao, lakini Serikali inawapoka kwa mabavu makubwa ya kutumia jeshi na jeshi wamesharipoti tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge. Wabunge wanne wameomba mwongozo wa Spika, mmoja ameleta jambo la dharura analoomba lijadiliwe. Tutaanza na mwongozo alioomba Mheshimiwa Halima Mdee kuhusu Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba alikamatwa jana jioni ama usiku na kusafirishwa mpaka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Halima Mdee wakati akieleza jambo hili amelilinganisha na jambo lililotokea Mheshimiwa Godbless Lema ambaye naye alikamatwa na mpaka sasa yupo chini ya uangalizi wa dola kwa maana ya kwamba bado yuko rumande. Ametoa hoja yake kwa kueleza kwamba huu ni udhalilishaji wa Wabunge lakini pia ni udhalilishaji wa mhimili. Pia ameleeza kwamba yeze anaamini kilichotokea jana Ofisi ya Spika itakuwa haina taarifa lakini pia ametoa maelezo kwa kirefu kuhusu vitendo vya polisi kwamba vinawadhalilisha Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Halima Mdee ametoa maelezo hayo ambayo nimeyarudia kwa kifupi kwa ufasaha zaidi lakini ameeleza jambo zuri kwamba hata Ofisi ya Spika hajui. Hata hivyo, Kanuni yetu ya 68(7) ambayo inaeleza kuhusu Mbunge yeote kuomba Mwongozo wa Spika, inataka Mwongozo wa Spika uombwe kwenye jambo ambalo limetokea Bungeni mapema. Niseme wazi si kwamba viunga vya Bunge siyo sehemu ya Bunge, ni sehemu ya Bunge lakini liwe limetokea mapema na tulishapewa tafsiri ya mapema maana yake nini.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo, kwa kuwa hili jambo limetokea jana namshauri Mheshimiwa Halima Mdee...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Atumie utaratibu unaotakiwa ili kuweza kushughulika na jambo hili na siyo kwa kuomba mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 68 (7).

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine limetoka kwa Mheshimiwa John Heche. Mheshimiwa John Heche ameenda kwenye Kanuni ya 47 akielezea jambo la dharura. Maelezo aliyoyatoa kwa kirefu yanahusu ugomvi ambao huwa unatokea kati ya koo mbalimbali katika Jimbo lake lakini pia na maeneo yote ya Tarime. Pia ametoa maelezo kwamba wakulima kwa namna ambavyo eneo haliwatashi wanalima nchi ya jirani na ameitaja Kenya kwamba badala ya kulima nchini Tanzania wanalima Kenya halafu wanaenda kuvuna.

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia ametoa maelezo kumhusu Mkuu wa Wilaya ambaye kwa maelezo ya Mheshimiwa Heche anasema anazunguka na wawekezaji na anawazuia wananchi wasilime na kwa hivyo hawataweza kupanda na kuvuna chochote. Pia ametoa maelezo kwamba yeye kama Mbunge wa eneo hilo hajui hizo taarifa za wawekezaji lakini pia Mwenyekiti wa Halmashauri hajui. Amemalizia kwa kusema yeye anajua kabisa sheria zinasema ugawaji wa maeneo ya vijiji ni Mkutano Mkuu wa Kijiji ndiyo unaogawa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu amelileta jambo lake chini ya Kanuni ya 47 na Kanuni ya 47 na vifungu vyake vidogo kwa mujibu wa namna alivyoitao hoja hii anataka ijadiliwe kama ni jambo la dharura. Jambo hili kwa mujibu wa Kanuni ya 47 ikisomwa na masharti yaliyoko katika Kanuni ya 48 linaweza kushughulikiwa na utaratibu uliopo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Heche na Serikali ipo hapa ndani imekwisha kumsikia na yeye afuate utaratibu mwagine ili kuhakikisha vijiji hivi kama haviko tayari kumpokea huyu mwekezaji basi vinajua utaratibu. Kama hawajonesha eneo, DC hawezi kwenda kuonesha eneo kwa maana Mkuu wa Wilaya hana eneo kwenye hivyo vijiji, kwa hiyo, vijiji havitaweza kumruhusu. Kwa hiyo, utaratibu uko wa kawaida na hatuna sababu kama Bunge ya kulijadili jambo hilo kama la dharura.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia mwongozo na Mheshimiwa Cosato Chumi kwa kutumia Kanuni ya 68(7), lakini akatoa maelezo chini ya Kanuni ya 46 ambayo inataka Serikali kujibu maswali kwa ukamilifu. Mheshimiwa Cosato Chumi kwa maelezo marefu aliyoyatoa anasema Serikali wakati ikijibu swali lake lililohusu tasnia ya sanaa na namna ambavyo wasanii wanapata tabu

mpaka waende Dar es Salaam kwa ajili ya sticker za mapato lakini pia kwa ajili ya kutafuta ofisi ambazo wanahusika nazo. Mheshimiwa Waziri wakati akijibu swali hili alielezea kuhusu ofisi hizi kuwepo ngazi ya mkoa lakini pia ngazi ya wilaya. Mwongozo wa Mheshimiwa Cosato Chumi anasema ofisi hizi katika wilaya wala mkoa hazipo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu majibu haya yametolewa hapa na Serikali na mwongozo umeombwa na Mheshimiwa Cosato Chumi, nitautoa baadaye kwa maana ya kwamba nataka kujiridisha kama hizo ofisi zipo mkoani ama wilayani ama hazipo ili niweze kuiagiza Serikali kama ikalete maelezo ya ziada kwa sababu Mheshimiwa Waziri alitaja kabisa ni akina nani wanaohusika huko. Alitaja ma-DAS, kwa sehemu ya wilaya na nadhani ni ma-RAS kwa upande wa mkoa. Kwa hivyo, tutafuatilia jambo hilo halafu huu mwongozo utatolewa hapo baadaye ili tuweze kusema kama Serikali inatakiwa ilete maelezo ya ziada ama hapana.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo mwingine nimeombwa na Mheshimiwa Joseph Musukuma ambaye ametoa maelezo kuhusu jambo lililotokea jana. Ametoa maelezo marefu sana na kwa Kanuni zetu zilivyo nisingependa kuyarudia hapa kwa sababu ni kama nitakuwa naweka msisitizo jambo ambalo kanuni zetu zinakataza. Zinakataza kwa maana ya kwamba mambo aliyoyataja Mheshimiwa Musukuma, yule mtu aliyekuwa akimtaja na wengine wanaohusika kwa mujibu wa Kanuni hizi kama jambo alilolisema Mheshimiwa Musukuma haliko sawasawa wana uwezo wa kuja Bungeni.

Sasa mimi kama msimamizi wa shughuli hizo leo sitayarudia maelezo ambayo mmeshayasikia, lakini kwa sababu nimeombwa mwongozo, Kanuni ya 68(7) kama nilivyoeleza kwenye mwongozo wa kwanza zinataka niombwe mwongozo kwa mambo yaliyotokea Bungeni mapema. Kwa hivyo, kwa sababu jambo hilo limetokea jana Mheshimiwa Musukuma, naomba utumie Kanuni yingine ambayo unaweza kuleta hoja yako hiyo ili Bunge iweze kuiangalia.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo mwingine nimeombwa na Mheshimiwa Mipata kuhusu jambo ambalo limetokea jimboni kwake. Mheshimiwa Mipata anatoa maelezo kwamba shule ya Milundikwa imefutwa na Serikali na hili Jambo limeleta usumbufu sana kwa sababu wananchi wameijenga shule hii kwa miaka 17. Pia ameeleza kwamba watoto wa kike wameathirika kwa kufutwa shule hiyo kwa sababu wamepelekwa katika shule mbalimbali ambazo hazina uwezo wa kuwachukua wote lakini pia hazina vifaa vyta kuweza kuwafundishia yaani zina upungufu. Ametoa maelezo kwamba uwekezaji katika shule hii ambayo ilijengwa na wanajamii ni shilingi milioni 8.71.

Waheshimiwa Wabunge, jambo hili pia limetokea Bungeni na kama nilivyosema kwa miongozo miwili iliyotangulia kwa kuwa jambo hili Imetokea Bungeni, namshauri Mheshimiwa Mipata atumie Kanuni mahsusizi zinazoweza kumfanya yeye alete hoja hii hapa Bungeni ama kama ataona inafaa anaweza akaiuliza Serikali kama swali ili aweze kupatiwa majibu mahsusizi kwa nini Serikali imefuta shule hii. Kwa kuwa Serikali imesikia na Mbunge yuko hapa wanaweza wakaamua kulishughulikia jambo hilo kabla hajachukua hatua nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo tunaendelea, Katibu!

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linalohusu Haki za Bunge.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa Kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linalohusu Haki za Bunge.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zitto, shughuli zetu za leo ni nyingi na kwa hivyo zitatumchukua muda kwa sababu...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 51 naomba uiangalie.

NAIBU SPIKA: Naomba tusikilizane kidogo. Wakati nikiruhusu wale watu watano, sikuwa nimewataja mwanzo nilikuwa naangalia watu waliosimama. Watu waliokuwa wamesimama walikuwa ni hao ambao nimewaruhusu kutoa miongozo. Mheshimiwa Zitto, wakati ule nilikuwa na huo muda ambao nimetoa kwa sasa hivi naomba tuendelee na shughuli zilizoko mbele yetu.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu siyo kuhusu mwongozo.

NAIBU SPIKA: Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. (Makofii)

MHE. PROF. NORMAN A.S. KING – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mungu mwingi wa rehema aliyetupa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii leo. Naomba taarifa hii niisome kwa ufupi lakini yote iingie kwenye Hansard kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Kanuni ya 117(15), Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtiririko wa taarifa hii umegawanyika katika maeneo makubwa manne yafuatayo:

Sehemu ya kwanza, maelezo ya jumla yaani utangulizi. Sehemu ya pili ni uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Sehemu ya tatu ni maoni, mapendekezo na ushauri wa Kamati na sehemu ya nne ni hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ina wajumbe 27, kama wanavyooneshwa kwenye vitabu ambavyo mmegawiwa au mtagawiwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, majukumu ya Kamati ni pamoja na:-

- (a) Kushughulikia bajeti ya Wizara inayoismamia;
- (b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara husika;
- (c) Kufuatilia Utendaji wa Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara inayoismamia;
- (d) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara husika; na
- (e) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zilizofanyika kwa kipindi cha mwaka 2016/2017. Kiambatisho namba moja (1) kinaonesha mchanganuo wa majukumu yote yaliyotekelizwa na Kamati katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017. Aidha, jedwali hilo linabainisha shughuli zilizofanywa kwa njia mbalimbali ikiwepo vikao, ziara na semina.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua utekelezaji wa miradi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na mapendekezo na makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Hata hivyo, Kamati ilibaini changamoto kubwa ni Serikali kutokupeleka fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano iliidhinishiwa shilingi trilioni 4.2 ambayo ni sawa na 16.7% ya bajeti yote ya Serikali. Kamati imebaini kuwa mwenendo wa bajeti hii si mzuri kwani taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa nusu ya mwaka wa fedha (Julai- Desemba 2016) inaonesha miradi mingi bado haijapatiwa fedha. Fedha zilizopelekwa ni Ujenzi 38.3%, Uchukuzi 34.3%, na Mawasiliano ni 24%.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya uchukuzi. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania - TPA. Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazoikabili Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA zikiwemo:-

- (a) Kuzorota kwa huduma za reli nchini;
- (b) Uwezo mdogo wa Bandari ya Dar es Salaam kuhudumia meli kubwa; na

(c) Uchakavu wa miundombinu na uwepo wa bandari bubu na ushindani wa Bandari zingine kama vile Beira-Msumbiji, Mombasa-Kenya na Durban-Afrika Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hairidhishwi na hali ya bandari nchini kwani shehena zimeendelea kushuka ukilinganisha na mwaka uliopita. Mfano, Bandari ya Dar es Salaam katika mwaka 2014/2015 kulikuwa na upungufu wa asilimia 5.2 ukilinganisha na mwaka 2015/2016. Katika kipindi cha nusu mwaka cha 2015/2016 na 2016/2017 kumekuwa na upungufu wa shehena wa asilimia 0.1. Bandari ambazo zimeathirika na kushuka kwa shehena ni pamoja na Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Tanga, Bandari ya Mwanza, Bandari ya Kigoma na Bandari ya Itungi-Kyela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bandari ya Dar es Salaam, hii ni bandari mama na bandari kubwa kuliko zote Tanzania ambayo inahudumia nchi ambazo hazina bandari kama vile Rwanda, Burundi, DR Congo, Uganda, Zambia na Malawi. Hata hivyo, katika kuboresha na kuongeza ufanisi wa bandari ya Dar es Salaam, ni muda sasa tangu kumekuwepo na mipango mbalimbali ya kuboresha na kuendeleza bandari hii ili iweze kuhudumia meli kubwa na kuweza kuhudumia ongezeko kubwa la shehena linalotarajiwa kwa miaka ijayo. Kamati imejulishwa kuwa mipango hiyo imefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Kuhusu uboreshaji na uongezaji wa kina katika gati namba moja hadi saba na ujenzi wa gati mpya ya kushushia magari eneo la Gerezani Creek, zabuni kwa hatua ya pili na ya mwisho kwa ajili ya kupata mkandarasi na hatua za ujenzi zimepelekwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kuridhia ili zitolewe kwa makampuni na wakandarasi yaliyopita katika hatua ya kwanza ya mchujo. Zabuni zilitolewa mwezi Februari, 2016 na kufungwa Julai, 2016. Kampuni ya M/S Inros Lackner ya Ujerumani ndiyo iliyoteuliwa kuwa msimamizi wa kazi ya ujenzi;

(b) Kuhusu uchimbaji wa lango la kuingilia meli na sehemu ya kugeuzia hadi kina cha mita 15.5 pamoja na kupanua lango. Mkataba wa Mshauri Mwelekezi wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu ulisainiwa mwezi Disemba, 2015 na kazi ilianza tarehe 20 Januari, 2016 na inatarajiwa kukamilika ifikapo Februari, 2017; na

(c) Kuhusu ujenzi wa gati namba 13 na 14, Serikali inaendelea na kushauriana na wafadhili kuboresha Bandari ya Dar es Salaam. Mwezi Oktoba 2015, ilikubalika kujumuisha magati yote ya bandari kwenye mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ambapo unatarajiwa kuanza rasmi mwaka 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi kabisa bandari ya Mwanzambali na changamoto zilizoorodheshwa katika hotuba hii, bandari ya Mwanza inakabiliwa na changamoto zifuatizo:-

(a) Ujenzi wa vituo vya kuegesha meli ambavyo ni vya watu binafsi na na ambavyo siyo rasmi;

(b) Mgogoro wa mipaka kati ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Bandari; na

(c) Ushindani mkubwa kutoka kwa bandari bubu pamoja na kuharibika mara kwa mara kwa meli ya MV Serengeti na MV Victoria ambazo zimekuwa ndio tegemeo kubwa la usafiri wa mwambao wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ya Tanga. Licha ya changamoto mbalimbali zinazoikabili bandari ya Tanga, bandari hii imekuwa ikiijidesha kwa hasara tangu mwaka 2013 hivyo kuwa mzigo kwa Mamlaka ya Bandari nchini. Pamoja na kuijidesha kwa hasara, miradi mbalimbali ya maendeleo imekuwa ikiendelea kutekelezwa kama vile ujenzi wa bandari ya Mwambani, kuimarisha gati namba mbili na ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kati ya Uganda na Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa bandari ya Mwambani-Tanga. Baada ya upembuzi yakinifu kukamilika Agosti, 2012 hatua zilizofikiwa ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kumilikishwa eneo la ardhi lenye ukubwa wa hekta 92 ambalo ni kwa awamu ya kwanza pamoja na kulipa fidia kwa Halmashauri ya Jiji la Tanga kiasi cha shilingi bilioni 2.59 kwa ajili ya wananchi waliokuwa wakiishi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Huduma ya Meli (MSCL). Changamoto kubwa imekuwa ni uchakavu wa meli kutokana na kutokufanyiwa matengenezo makubwa kwa wakati na hivyo kusababisha gharama kubwa za uendeshaji. Mfano, MV Butiama ambayo haifanyi kazi tangu mwaka 2010, MV Victoria nayo haifanyi kazi toka mwaka 2014 na MV Liemba ambayo inafanya kazi lakini kwa kusuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutatua changamoto hizo, mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga shilingi bilioni 50.5 kwa ajili ya malipo ya asilimia 50 ya ujenzi wa meli mpya ya Ziwa Victoria, ukarabati wa MV Victoria, ukarabati wa MV Liemba na MV Butiama. Kamati ilijulishwa kuwa kazi hii ipo kwenye uchambuzi wa zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa reli ya kati. Suala la ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha standard gauge ni muhimu sana. Kamati katika hotuba yake ya mwaka wa fedha wa 2016/2017 iliishauri Serikali kuwa kampuni ya reli ya Serikali ya China iliyojenga kipande cha reli ya mfano kwa ajili ya uzinduzi pale Soga-Kibaha, kwa ubora uleule iendelee. Kamati ilitoa angalizo la kuharakisha uamuaji na ujengaji wa reli ya kati kwa kuwa kukamilisha haraka ujenzi wa reli hiyo ndio faida kwa uchumi unaotokana na mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kuwa fedha za ujenzi wa reli ya kati yaani dola bilioni 7.6 zitatoleta kama mkopo wenyewe masharti nafuu na Serikali ya China kupitia China Exim Bank na kwamba hii ilipelekea kutengwa kwa shilingi trilioni moja kama sehemu ya asilimia 15 ya mchango wa Serikali kwa ajili ya ujenzi wa reli hiyo. Kwenye hotuba ya Kamati tuliangaliza kuwa mzigo unaotegemewa na Tanzania pia unategemewa na nchi jirani. Kwa mantiki hiyo, kukamilisha ujenzi wa reli ya kati haraka ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya ujenzi wa reli ya kati yalianza kipindi kilekile na ujenzi wa reli ya kutoka Mombasa kwenda Nairobi, nchini Kenya. Wenzetu wamemaliza sisi bado. Maana kama mtandao wa reli wa nchi jirani utakuwa umekamilika kabla sisi hatujakamilisha reli yetu, upo uwezekano mkubwa reli yetu itakuwa ya abiria zaidi kuliko mizigo, wakati huo huo mizigo

unategemewa ambao kimsingi ndiyo nguvu yetu ya kujenga reli yaani ongezeko tarajiwa la mzigo kutoka tani milioni tano za sasa mpaka tani milioni 17 reli itakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati tunalazimika kuelezea juhudzi zinazofanywa upande mwingine wa nchi jirani kwa kuwa Tanzania si kisiwa na miundombinu ya reli inategemea sana mzigo wa nchi jirani. Kamati inatambua kuwa yapo makubaliano ya ujenzi wa reli kwa mfano kutoka Mombasa, Kampala mpaka Kigali na nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua pia kumekuwepo na makubaliano ya Tanzania na Burundi ya kuharakisha ujenzi wa tawi la kutoka Uvinza kwenda Msongati kwa ajili ya kuchukua chuma na pia makubaliano ya Serikali ya Tanzania na DRC Congo ya kuchukua mzigo wa kutoka Congo kuititia bandari ya Kalemi kwenye Ziwa Tanganyika. Makubaliano hayo bila shaka ni moja ya kichocheo cha ujenzi wa reli ya katika kwa kiwango cha standard gauge kwa kuwa mzigo tuna hakika nao. Ikiwa mtandao wa reli wa nchi jirani utakamilika kabla yetu, ni wazi tutakuwa na kazi kubwa ya kufanya ili reli ya katika iweze kuwa ya manufaa kiuchumi na maendeleo ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua kuwa kwenye anga za kimataifa kila msaada unaopewa na nchi yoyote unajipambanua na nchi hiyo. Pia Kamati inatambua kuwa Kampuni ya Serikali ya China ambayo ndiyo iliyojenga kipande cha reli cha mfano pale Soga Kibaha ni mali ya Serikali ya China ambayo ilianzishwa mara baada ya kukamilisha ujenzi wa reli ya TAZARA.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kukawa na upungufu wa utekelezaji wa mradi huo katika Serikali ya Awamu ya Nne, narudia, inawezekana kukawa na upungufu wa utekelezaji wa mradi huo katika Serikali ya Awamu ya Nne kutegemea nani anatazama upungufu huo na kwa nia gani, lakini ni muhimu Serikali kuhakikisha kuwa upungufu wa mtu au watu kama upo, unarekebishwa ili mradi Serikali isipoteze lengo la msingi la ujenzi wa reli ya katika kuititia makubaliano yaliyopo. Serikali inaweza kusahihisha ama kurekebisha makubaliano yoyote inayotilia shaka maadam iendelee kuenzi diplomasia za kimataifa na hasa nchi zile ambazo zimejipambanua kuwa rafiki zetu awamu zote tano za Serikali ya Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua kuwa uchumi wa kimataifa na mipango ya maendeleo mikubwa hasa ujenzi wa reli, viwanja vikubwa vya ndege, ujenzi wa bandari, uchimbaji wa mafuta na gesi na miradi kama hiyo inahitaji kutokupoteza lengo maana chochote kinaweza kufanyika ili mradi kusicheleweshwe katika kukamilisha miradi hiyo. Kwa mfano, pale ambapo una hifadhi ya mafuta ardhini, unaweza kuambiwa mafuta huna, utafiti uendelee. Pale ambapo unatakiwa kukamisha *terminal* ya uwanja wa ndege, unaweza ukaambiwa fedha zimechelewa kuitishwa/kusainiwa ama kuruhusiwa hivyo subiri. Pale ambapo unatakiwa ujenge gati ya bandari ya kina kirefu au bandari mpya, unaweza ukaambiwa Bodi ya Benki ya Dunia haijapitisha mkopo mpaka kikao cha mwaka unaofuata. Ni wazi maendeleo ni vita lazima tuwe makini. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ya sasa uchumi wake unategemeana sana. Ukiboresha reli ya katika maana yake pia umeboresha utoaji huduma wa

Bandari ya Dar es Salaam. Kwa kufanya hivyo, unahatarisha bandari za nchi zingine kwa kuwa mizigo na wateja ni walewale. Hivyo, chochote kinaweza kufanya ili nchi ishughulikie vitu ambavyo havisaidii kujenga reli ya katni na kwa kufanya hivyo, tunabaki kusema hiki hakikuwatwa au kilikuwatwa na mwisho hatujengi au tukachelewa kujenga reli yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu kwa kusaini mkataba na Kampuni ya Uturuki pamoja na Ureno wa kujenga reli kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro. Narudia, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kusaini mkataba na Kampuni ya Uturuki pamoja na Ureno wa kujenga reli kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro. Ujenzi wa reli hiyo yenye kasi ya kilomita 160 kwa saa itasaidia sana kurahisisha usafiri hasa wa abiria kutoka Morogoro hadi Dar es Salaam. Ni vyema Serikali ikakamilisha pia sehemu ya reli ya katni iliyobaki na matawi yake yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati imefarijika kuona kwamba kiwanja cha Mwanza kimetengewa shilingi bilioni 30 ambapo mpaka mwezi Januari, 2017 zilizotolewa ni shilingi bilioni 7.6 tu. Ni dhahiri kuwa fedha hizi zikitolewa kwa wakati zitaharakisha ujenzi wa kiwanja hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere. Kuhusu ujenzi wa jengo la tatu la abiria (*terminal III*) katika kiwanja hiki, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 mradi ultengewa shilingi bilioni 26 ambazo Kamati imejulishwa hadi Desemba, 2016 fedha hizo hazikuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa uwanja wa Songwe. Mradi huu kwa bajeti ya mwaka 2015/2016 ultengewa kiasi cha shilingi bilioni tano ambazo hadi kufikia Aprili, 2016 hazikuwa zimetolewa. Vivyo hivyo, katika mwaka wa fedha 2016/2017, mradi huu ultengewa shilingi bilioni saba, lakini hadi kufikia Desemba, 2016, hakuna fedha iliyokuwa imetolewa kwa ajili ya uwanja huu wa Songwe. Kamati haionti sababu za msingi za kutokulizia kiwanja hiki ukizingatia kuwa ili mradi huu ukamilike unahitaji jumla ya shilingi bilioni 16 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Ndege Tanzania (ATCL). Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kuonesha nia ya dhati na jitihada za kulikwamua Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ambapo bajeti yake ya mwaka wa fedha 2016/2017, ilitenga shilingi bilioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa ndege. Sote tunajua ndege hizo zimenunuliwa na zingine ziko katika mpango wa kununuliwa. Kamati inaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa ATCL inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- (a) Uhaba wa rasilimali fedha;
- (b) Upungufu wa wataalam hasa marubani na wahandisi ambapo wengi wao wamefikisha umri wa kustaafu;
- (c) Kuchelewa kurejea katika Chama cha Mashirika ya Ndege Duniani (IATA);

(d) Kushindwa kuanza baadhi ya safari kwa wakati kwenye baadhi ya mikoa kama vile Mpanda kutokana na upungufu katika viwanja hivyo; na

(e) Ukosefu wa gari la zima moto katika viwanja kwa mfano cha Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizi zinapaswa kutafutiwa ufumbuzi kama inavyoolekezwa katika mapendekezo ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania-TMA. Changamoto nyingi ambazo zipo TMA ni pamoja na hizi:-

(a) Kukosekana kwa jengo la kudumu la Makao Makuu na Kituo Kikuu cha Utabiri wa Hali ya Hewa hivyo kuathiri taratibu za kuweka mitambo ya kisasa;

(b) Uchache wa wataalam wa hali ya hewa;

(c) Upungufu na uchakavu wa vituo na vifaa vyia kupimia hali ya hewa;

(d) Mabadiliko ya mara kwa mara ya hali ya hewa duniani yanayosababisha changamoto katika utabiri wa hali ya hewa; na

(e) Gharama kubwa za kununua na kuendesha mitambo ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*). Kuhusu usafiri wa barabara, pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na *SUMATRA*, Kamati imebaini kuendelea kuwepo kwa changamoto mbalimbali zifuatazo:-

(a) Kuendelea kuwepo kwa baadhi ya vyombo vyia usafiri vibovu ambavyo si salama;

(b) Baadhi ya vyombo vyia usafiri kama *NOAH* ambavyo vimepewa leseni ya kusafirisha abiria chini ya Kilomita hamsini tu. Jambo hilli limekuwa likilalamikiwa na wananchi hasa kwenye maeneo yale ambayo usafiri ni mgumu;

(c) Baadhi ya wamiliki wa mabasi kutoza nauli tofauti na zilizopangwa na *SUMATRA*; na

(d) Mwendo kasi wa baadhi ya vyombo vyia usafiri hasa wakati wa jioni au usiku hivyo kuhatarisha usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na tafiti zilizofanyika, asilimia 85 za ajali zinazotokea zinasababishwa na makosa ya kibinadamu kama vile kutokuzingatia alama za barabarani, kutokuwa na elimu ya kutosha katika fani ya udereva, umakini wakati wa kupita gari lingine (*overtake*), ulevi, uchovu na matumizi ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaona bado kuna haja ya vyombo vinavyohusika kama Wizara ya Mambo ya Ndani; Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na

Mawasiliano; Wizara ya Katiba na Sheria; Wakala wa Barabara Tanzania; Chama cha Wamiliki wa Mabasi; na Chama cha Madereva kukaa pamoja na kuona namna nzuri itakavyoweza kufanyika kupunguza changamoto hizi na kuweka mazingira salama kwa wasafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika,Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROAD*). Hadi kufikia Desemba, 2016, utekelezaji wa matengenezo ya barabara kuu na zile za mikoa pamoja na madaraja ulifikia asilimia 30 ambapo kazi zilizofanyika zilijumuisha kilometra 6,852 za matengenezo ya kawaida pamoja na kilometra 1,151 za matengenezo ya muda na kilometra 274 za matengenezo ya sehemu korofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo Wakala wa Barabara unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

- (a) Kutokutolewa kwa wakati fedha za miradi ya maendeleo hali inayosababisha kazi zilizopangwa kwa baadhi ya miradi kutokukamilika;
- (b) Msongamano wa magari barabarani hasa Jiji la Dar es Salaam;
- (c) Baadhi ya wasafirishaji kuendelea kuzidisha uzito wa mizigo kwenye magari na kusababisha uharibifu wa barabara;
- (d) Uwezo mdogo wa baadhi ya wakandarasi hasa wa ndani wanapokuwa wamepewa miradi ya ujenzi; na
- (e) Kuendelea kuwepo uvamizi wa maeneo ya hifadhi za barabara ambapo wananchi wamekuwa wakijenga katika maeneo ya hifadhi za barabara bila kujali Sheria ya Barabara Na.13 ya Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika,kuhusu matuta barabarani, licha ya Wakala wa Barabara (*TANROADS*) kuahidi kuendelea kurekebisha matuta makubwa ili kuyaweka katika viwango vilivyoainishwa katika mwongozo wa Wizara mpaka sasa bado kuna barabara ambazo matuta hayo hayajarekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Jiji la Dar es Salaam. Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudhi mbalimbali zinazofanywa katika kuhakikisha Jiji la Dar es Salaam linakuwa halina msongamano mkubwa wa magari. Juhudi mbalimbali zinazoendelea ni pamoja na:-

- (a) Ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo kasi (*BRT*);
- (b) Kujenga barabara za juu (*flyovers*) katika eneo la TAZARA;
- (c) Maaandalizi ya ujenzi wa barabara za juu (*Interchange*) katika eneo la Ubungo;
- (d) Maandalizi ya ujenzi na upanuzi wa daraja la Selander ambalo litaanzia eneo la Coco Beach hadi eneo la Aga Khan; na
- (e) Kukamilisha barabara zingine za kupunguza msongamano Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na miradi hii ya kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam kuwa mingi na yote kuhitajika kwa haraka, Kamati inaona ipo haja ya kuhusisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi hii ili iweze kukamilika kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika,mizani za barabarani.Licha ya kuwepo kwa vituo vingi vya mizani bado barabara zimekuwa zikiharibika. Suala hili lisipotafutiwa ufumbuzi wa kudumu mapema, Taifa hili litakuwa linaendelea kutenga fedha nyingi kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa barabara kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali na hasa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kwa kuendelea kutekeleza ushauri uliotolewa na Kamati kwa kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017 na hatimaye kuweza kufanikisha yote yaliyoorodheshwa katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa postal code na *Symbol* za Posta. Kamati ilielezwa kuwa mfumo huu uko tayari katika nchi nzima, kinachosubiriwa ni Serikali za Miji na Mitaa kutekeleza katika maeneo husika. Mamlaka imeweka *postal code* ya maeneo mbalimbali mfano Jiji la Arusha, Dodoma na Dar es Salaam ambapo imeweka namba za nyumba na majina ya mitaa. Hata hivyo, changamoto kubwa imekuwa kutokuwa na mipango miji na ujenzi holela. Pia, upatikanaji wa majina ya mitaa na kutohana na mabishano juu ya majina katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake na hatimaye kuanza kulipa deni ambapo mpaka sasa Serikali imelipa kiasi cha shilingi bilioni 1.7. Kufuatia hali mbaya ya kifedha ya Shirika la Posta Tanzania, shirika limeshindwa kulipa madeni ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilikamata akaunti za shirika mara tatu katika vipindi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF), Kamati imejulishwa kuwa, kumekuwepo na mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma ya mawasiliano vijiji ambapo katika kipindi cha miezi sita ya kwanza mwaka 2016/2017, Mfuko wa Mawasiliano ulifikisha huduma za mawasiliano katika Kata 138 zenye jumla ya vijiji 557.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuzingatia ukubwa wa nchi yetu, ni muda muafaka sasa toka kuanzhishwa, Kamati bado hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kuhakikisha kwamba inatenga fedha nyingi ili kuwezesha mfuko huu kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ni Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuendeleza miundombinu nchini ambapo kwa mara ya kwanza Sekta ya Miundombinu katika Bajeti ya mwaka 2016/2017 imetengewa asilimia 16.7 ya bajeti yote ya Serikali. Hata hivyo, Kamati inasitisiza Serikali kutoa fedha kwa wakati, kuharakisha miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uchukuzi, kwa kuwa, Bandari ya Dar es Salaam ni kiungo kikubwa cha nchi yetu na nchi jirani; na kwa kuwa bandari hii

ikiimarishwa itaweza kuingizia nchi yetu mapato mengi zaidi na hasa kukuza uchumi; Kamati inaishauri Serikali kuboresha mazingira ya Bandari ya Dar es Salaam kwa kuongeza kina katika gati namba 1- 7, upanuzi wa lango la kuingilia meli, kujenga gati namba 13 & 14 pamoja na kuimarisha usafiri wa njia ya reli kutoka bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Kamati inaishauri changamoto zifuatazo zifanyiwe kazi: Hofu ya wateja kutohana na kuanzishwa kwa Sheria ya Value Added Tax kwa huduma zitolewazo na Mawakala kwenye mizigo ya jirani (VAT on transit goods); pia, mgongano wa tozo za hifadhi ya mizigo (Customs Warehouse Rent) inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Storage Charges zinazotozwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo haya yanafanana isipokuwa yametofautiana majina tu, hivyo wafanyabiashara wanaona kuwa wanalipa mara mbili ilhali mizigo ni ile ile. Tozo ya barabara ambapo hutozwa Dola ya Kimarekani 16 kwa Kilomita ukilinganisha na Dola za Kimarekani nane kwa Kilomita zinazotozwa kwenye bandari shindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine wa Kamati ni kama ulivyoorodheshwa kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bandari Kavu (ICD's), Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri wa kujenga bandari kavu inayotegemewa kumilikiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mionganoni mwa kero za wafanyabiashara wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam ni kutokuwepo kwa maegesho ya magari yanayoingiza na kutoa mizigo bandarini; Kamati inaishauri Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Temeke kushirikiana na kuhakikisha eneo linatengwa kwa ajili ya maegesho ya wafanyabiashara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kuwa na mchakato wa ununuzi wa flow meter mpya kuendelea, Kamati inasisitiza kuwa suala hili lipewe kipaumbele ili mchakato huo uweze kukamilika haraka kwani ni muhimu kufahamu kiasi cha mafuta kinachoingia na kutoka ili kuweza kutoza kodi stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha standard gauge; kwa kuwa Serikali imeonesha nia ya kutaka kuifufua reli ya kati na kujenga katika kiwango cha kisasa kwa kutenga bajeti yake ya mwaka 2016/2017 shilingi trilioni moja, Kamati inaiomba Serikali...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, muda wako umekwisha naomba umalizie!

MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA KING – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kamati inaiomba Serikali kuharakisha ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kampuni...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, hiyo ripoti yako itaingia kwenye Hansard na Wajumbe wanazo hizo ripoti. Kwa hiyo, wewe malizia.

MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA KING – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ikiwa ni pamoja na reli, barabara, viwanja vya ndege, bandari na mawasiliano ni nguzo ya Taifa lolote na kwa kweli ndiyo vichochezi vya maendeleo ya sekta nyingine. Hivyo, ni lazima tutambue kuwa maendeleo ni vita na lazima tupange mipango yetu kama tupangavyo vita yoyote ile.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa naomba utoe hoja tafadhalii.

MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA KING – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelizwa, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017 pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Wajumbe, hamjasimama kuunga mkono hoja. (Kicheko)

MHE. BHAGWANJI M. MEISURIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante na hoja imeungwa mkono.

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2016 HADI JANUARI, 2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1:0 MAELEZO YA JUMLA

Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 117 (15), Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017.

Mheshimiwa Spika, mtiririko wa Taarifa hii umegawanyika katika maeneo makubwa manne yafuatayo:-

- a. Sehemu ya I- Maelezo ya Jumla (Utangulizi);
- b. Sehemu ya II- Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati;
- c. Sehemu ya III- Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati; na
- d. Sehemu ya IV- Hitimisho

Wajumbe wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

- | | |
|-----------------------------------------------|-----------------|
| 1. Mhe .Prof. Norman Adamson Sigalla King, Mb | - Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb | - M/ Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb | - Mjumbe |
| 4. Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb | " |
| 5. Mhe. Mizar Bakari Haji, Mb | " |
| 6. Mhe. James Francis Mbatia, Mb | " |
| 7. Mhe. Mansoor Shanif Hirani, Mb | " |
| 8. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb | " |
| 9. Mhe. Saul Henry Amon, Mb | " |
| 10. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb | " |
| 11. Mhe. Quambalo Willy Qulwi, Mb | " |
| 12. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb | " |
| 13. Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb | " |
| 14. Mhe.Dkt. Chuachua Mohamed Rashid, Mb | " |
| 15. Mhe. Mary Deo Muro, Mb | " |
| 16. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb | " |
| 17. Mhe. Khadija Salum Ally Al-Qassym, Mb | " |
| 18. Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb | " |
| 19. Mhe. Dua William Nkurua, Mb | " |
| 20. Mhe. Musa Rashid Ntimizi, Mb | " |
| 21. Mhe. Lathifah Hassan Chande, Mb | " |
| 22. Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb | " |
| 23. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb | " |
| 24. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibajuka, Mb | " |
| 25. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb | " |
| 26. Mhe. Charles Kitwanga, Mb | " |
| 27. Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka, Mb | " |

Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 6(8), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imepewa jukumu la kusimamia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Katika kusimamia Wizara hiyo, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Aprili, 2016 imeainisha majukumu ya Kamati kama ifuatavyo:-

- Kushughulikia Bajeti ya Wizara inayoismamia;
- Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara husika;
- Kufuatilia Utendaji wa Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara inayoismamia;
- Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara husika; na
- Kufuatilia Utekelezaji unaofanywa na Wizara kwa Mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba.

Shughuli zilizofanyika kwa Kipindi cha Mwaka 2016/2017

Mheshimiwa Spika, kiambatisho namba 1 kinaonesha mchanganuo wa majukumu yote yaliyotekelze wa na Kamati katika kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017. Aidha, jedwali hilo limebainisha shughuli zilizofanyika, njia mbali mbali zilizotumika ikiwepo vikao, ziara na semina.

SEHEMU YA PILI

UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Mapendekezo na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Hata hivyo, Kamati ilibaini changamoto kubwa ni Serikali kutokupeleka fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imeidhinishiwa shilingi trilioni 4.2 (4,229,408,685,900.00) ambayo ni sawa na asilimia 16.7 ya Bajeti yote ya Serikali. Kamati imebaini kuwa mwenendo wa Bajeti hii si mzuri kwani taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa nusu ya mwaka wa fedha (Julai- Desemba 2016) inaonesha miradi mingi bado haijapatiwa fedha. Fedha zilizopelekwa ni Ujenzi asilimia 38.3; Uchukuzi asilimia 34.3; na Mawasiliano asilimia 24.

Sekta ya Uchukuzi

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazoikabili Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA zikiwemo:-

- a. Kuzorota kwa huduma za reli nchini jambo linalosababisha usafirishaji wa mizigo kutegemea barabara pekee;
- b. Uwezo mdogo wa Bandari ya Dar es Salaam kuhudumia meli kubwa na kina kifupi katika bandari ya Dar es Salaam pamoja na Tanga;
- c. Uchakavu wa miundombinu ya bandari nchini;
- d. Uwepo wa bandari bubu na ushindani wa Bandari zingine kama vile Beira- Msumbiji, Mombasa-Kenya na Durban-Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi kabisa na hali ya bandari nchini kwani shehena zimeendelea kushuka ukilinganisha na mwaka uliopita. Mfano; katika Bandari ya Dar es Salaam katika mwaka 2014/15 kulikuwa na upungufu wa asilimia 5.2 ukilinganisha na mwaka 2015/16 na katika kipindi cha nusu mwaka 2015/16 na 2016/17 kumekuwa na upungufu wa shehena asilimia 0.1. Bandari ambazo zimeathirika na kushuka kwa shehena ni pamoja na Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Tanga, Bandari ya Mwanza, Bandari ya Kigoma na Bandari ya Itungi-Kyela.

a) Bandari ya Dar es Salaam

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari ya Dar es Salaam; hii ndio bandari mama na bandari kubwa kuliko zote Tanzania ambayo inahudumia nchi jirani ambazo hazina bandari kama vile Rwanda, Burundi, DR Congo, Uganda, Zambia na Malawi. Hata hivyo, pamoja na kuwa katika nafasi nzuri ya kijirografia bado bandari hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za miundombinu inayounganisha bandari kama vile reli na barabara na kutokuwepo kwa maegesho kwa ajili ya magari yanayoenda kupakia mizigo bandarini hivyo kuathiri uondoshaji wa mizigo kutoka bandarini. Kwa ujumla changamoto hizi zinasababisha nchi kupoteza wateja wengi waliokuwa wakitumia bandari ya Dar es Salaam na kwa sasa kuhamia katika bandari zingine shindani za Mombasa- Kenya, Beira- Msumbiji, Durban- Afrika Kusini na Walvis Bay-Namibia ambazo zimeweka mazingira rafiki na wafanyabiashara na kuvutia wengi kukimbilia huko.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha na kuongeza ufanisi wa bandari ya Dar es Salaam, ni muda sasa tangu kumekuwepo mipango mbalimbali ya kuboresha na kuendeleza bandari hii ili iweze kuhudumia meli kubwa na kuweza kuhudumia ongezeko kubwa la shehena linalotarajiwa kwa miaka ijayo. Kamati imejulishwa kuwa mipango hiyo imefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

- i) Kuhusu uboreshaji na uongezaji wa kina katika gati namba 1 hadi 7 na ujenzi wa gati mpya yakushushia magari eneo la Gerezani Creek. Zabuni kwa hatua ya pili na ya mwisho kwa ajili ya kupata mkandarasi wa kazi za ujenzi zimepelekwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kuridhia ili zitolewe kwa makampuni na wakandarasi yaliopita katika hatua ya kwanza ya mchujo. Zabuni zilitolewa mwezi Februari 2016 na kufungwa Julai 2016. Kampuni ya M/S Inros Lackner Ag ya Ujerumani ndio iliyoteuliwa kuwa msimamizi wa kazi ya ujenzi;
- ii) Kuhusu uchimbaji wa lango la kuingilia meli na sehemu ya kugeuzia hadi kina cha mita 15.5 pamoja na kupanua lango. Mkataba na Mshauri Mwelekezo wa kufanya kazi ya Upembuzi yakinifu ulisainiwa mwezi Disemba 2015 na kazi zilinza tarehe 20 Januari 2016 na inatarajiwa kukamilika ifikapo Februari 2017;
- iii) Kuhusu ujenzi wa gati namba 13 na 14, baada ya Serikali kushauriana na wafadhili wa kuboresha Bandari ya Dar es Salaam mwezi Oktoba 2015, ilikubalika kujumuisha magati yote ya bandari kwenye mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ambapo unatarajiwa kuanza rasmi mwaka 2018 baada ya kukamilika kwa uhamishaji wa gati la mafuta la Kurasini Oil Jet (KOJ) na mabomba yake.

b) Bandari ya Mwanza

Mheshimiwa Spika, mbali na changamoto zilizotajwa awali zinazorotesha bandari nchini, bandari ya Mwanza inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- i) Ujenzi wa vituo vya kuegesha meli ambavyo ni vya watu binafsi na baadhi siyo rasmi. Vituo kadhaa vimejengwa karibu sana na bandari ambapo pamoja na kuinyima mapato Serikali pia vinatishia usalama na utaratibu wa uendeshaji wa meli katika Maziwa;
- ii) Mgogoro kati ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Bandari Mwanza kuhusu mipaka ya bandari pamoja na tozo mbalimbali za ushuru kwa magari yanayoingia na kutoka bandarini jambo linalosababisha gharama kwa wafanyabiashara na hivyo kuona usumbufu na kuamua kutumia bandari nyingine; na
- iii) Ushindani mkubwa kutoka kwa bandari bubu pamoja na kuharibika mara kwa mara kwa meli ya MV Serengeti na MV Victoria ambazo zimekuwa ndiyo tegemeo kubwa la usafiri wa mwambao wa Ziwa Victoria.

c) Bandari ya Tanga

Mheshimiwa Spika, licha ya changamoto mbalimbali zinazoikabili bandari ya Tanga, bandari hii imekuwa ikijijendesa kwa hasara tangu mwaka 2013 hivyo kuwa mzigoto kwa Mamlaka ya Bandari nchini. Pamoja na kujijendesa kwa hasara, miradi mbalimbali ya maendeleo imekuwa ikiendelea ikitekelezwa kama vile ujenzi wa bandari ya Mwambani, kuimarisha gati namba mbili (2) na ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kati ya Uganda na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa ujenzi wa bandari ya Mwambani-Tanga, baada ya upembuzi yakinifu kukamilika Agosti 2012 hatua zilizofikiwa ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kumilikishwa eneo la ardhi lenye ukubwa wa hekta 92 ambalo ni kwa awamu ya kwanza pamoja na kulipa fidia kwa Halmashauri ya jiji la Tanga kiasi cha shilingi bilioni 2.59 kwa ajili ya wananchi waliokuwa wakiishi katika eneo la mradi. Taratibu za umilikishwaji wa eneo jingine la ardhi lenye hekta 82 zinaendelea. Hata hivyo, Kamati ilishangazwa kuona kuwa jiwe la msingi liliwekwa mnamo mwaka 1975 hata hivyo wananchi waliendelea kujenga na kuishi katika eneo hilo na baadae kudai kulipwa fidia.

Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa imekuwa ni uchakavu wa Meli kutokana na kutokufanyiwa matengenezo makubwa kwa wakati na hivyo kusababisha gharama kubwa za uendeshaji. Mfano, MV Butiama ambayo haifanyi kazi tangu mwaka 2010, MV Victoria nayo haifanyi kazi toka mwaka 2014 na MV Liemba ambayo inafanya kazi lakini kwa kusuasua. Katika kutatua changamoto hizo, mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga **shilingi bilioni 50.5 (50,500,000,000)** kwa ajili ya malipo ya asilimia 50 ya ujenzi wa meli mpya ya Ziwa Victoria, ukarabati wa MV Victoria (MSCL), ukarabati wa MV Liemba na MV Butiama. Kamati imejulishwa kuwa kazi hii ipo kwenye uchambuzi wa zabuni.

Ujenzi wa Reli ya Kati

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha standard gauge ni muhimu sana. Kamati katika hotuba yake ya mwaka wa fedha wa 2016/17 iliishauri Serikali kuwa kampuni ya reli ya Serikali ya China iliyojenga kipande cha Reli ya mfano kwa ajili ya uzinduzi pale Soga-Kibaha, kwa ubora uleule iendelee. Na kamati ilitoa angalizo la kuharakisha uamuaji na ujengaji wa reli ya kati kwa kukamilisha haraka ujenzi wa reli hiyo ndiyo faida kwa uchumi unaotokana na mzigoto.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa fedha za ujenzi wa reli ya kati yaani **dola 7.6 bilioni** zitatolewa kama mkopo wenye masharti nafuu na Serikali ya China kupitia China Exim bank. Na kwamba hii ilipelekea kutengwa kwa **shilingi triliioni 1** kama sehemu ya **asilimia 15** ya mchango wa Serikali kwa ajili ya ujenzi wa reli hiyo. Kwenye hotuba ya kamati tuliangaliza kuwa mzigoto unaotegemewa na Tanzania pia unategemewa na nchi jirani. Kwa maantiki hiyo kukamilisha ujenzi wa reli ya kati haraka ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya ujenzi wa reli ya kati yalianza kipindi kilekile na ujenzi wa reli ya kutoka Mombasa kwenda Nairobi, nchini Kenya. Wenzetu wamemaliza, sisi bado. Maana kama mtandao wa reli wa nchi jirani utakuwa umekamilika kabla sisi hatujakamilisha reli yetu, upo uwezekano mkubwa reli yetu itakuwa ya abiria zaidi kuliko mzigoto, wakati huo huo mzigoto unategemewa ambao kimsingi ndiyo nguvu yetu ya kujenga reli yaani ongezeko tarajiwala mzigoto kutoka tani milioni 5 za sasa mpaka tani milioni 17 reli ikikamilika haitawezekana.

Mheshimiwa Spika, Kamati tunalazimika kuelezea juhudzi zinazofanywa upande mwiningine wa nchi jirani kwa kuwa Tanzania si kisiwa na Miundombinu ya reli inategemea sana mzigo wa nchi jirani. Kamati inatambua kuwa yapo makubaliano ya ujenzi wa reli kutoka Mombasa, Kampala mpaka Kigali.

Mheshimiwa spika, Kamati inatambua pia kuwa kumekuwepo na makubaliano ya Tanzania na Burundi ya kuharakisha ujenzi wa tawi la kutoka Uvinza kwenda Msongati kwa ajili ya kuchukua Chuma, na pia makubaliano ya Serikali ya Tanzania na DRC Congo ya kuchukua mzigo wa kutoka Congo kupitia bandari ya Kalemi kwenye Ziwa Tanganyika. Makubaliano hayo bila shaka ni moja ya kichocheo cha ujenzi wa reli ya katika kiwango cha Standard gauge kwa kuwa mzigo tunahakika nao. Ikiwa mtandao wa reli wa nchi jirani utakamilika kabla yetu, ni wazi tutakuwa na kazi kubwa ya kufanya ili reli ya katika iweze kuwa ya manufaa kiuchumi na maendeleo ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa kwenye anga za kimataifa kila msaada unaopewa na nchi yoyote unajipambanua na nchi hiyo. Na pia Kamati inatambua kuwa kampuni ya serikali ya China ambayo ndiyo iliyojenga kipande cha reli ya mfano pale Soga Kibaha ni mali ya serikali ya China ambayo ilianzishwa mara baada ya kukamilisha ujenzi wa reli ya Tazara. Inawezekana kukawa na mapungufu ya utekelezaji wa mradi huo katika serikali ya awamu ya nne, kutegemea nani anatazama upungufu huo na kwa nia gani, lakini ni muhimu Serikali kuhakikisha kuwa upungufu wa mtu au watu kama upo, unarekebishwa ilimradi serikali isipoteze lengo la msingi la ujenzi wa reli ya katika kupitia makubaliano yaliyopo. Serikali inaweza kusahihisha ama kurekebisha makubaliano yoyote inayotilia shaka maadam iendelee kuenzi diplomasia za kimataifa na hasa nchi zile ambazo zimejipambanua kuwa rafiki zetu awamu zote tano za serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa uchumi wa Kimataifa na mipango ya maendeleo mikubwa hasa ujenzi wa reli, viwanja vikubwa vya Ndege, ujenzi wa bandari, uchimbaji wa mafuta na gesi na miradi kama hiyo inahitaji kutokupoteza lengo maana chochote kinaweza kufanyika ili mradi tucheleweshwe katika kukamilisha miradi hiyo. Kwa mfano, pale ambapo unahifadhi ya mafuta ardhini, unaweza kuambiwa mafuta huna, utafiti uendelee; pale ambapo unatakiwa kukamisha terminal ya 3 ya uwanja wa Ndege, unaweza ukaambiwa fedha zimechelewa kupitishwa/kusainiwa/kuruhusiwa kwa hiyo subiri; pale ambapo unatakiwa ujenge gati ya bandari ya kina kirefu au bandari mpya, unaweza ukaambiwa bodi ya benki ya dunia haijapitisha mkopo mpaka kikao cha mwaka unaofuata. Ni wazi maendeleo ni vita lazima tuwe makini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ya sasa uchumi wake unategemeana sana. Ukiboresha reli ya katika, maana yake pia umeboresha utoaji huduma wa Bandari ya Dar es Salaam; na kwa kufanya hivyo unahatarisha bandari ya nchi zingine kwa kuwa mizigo na wateja ni walewale. Hivyo, chochote kinaweza kufanyika ili nchi ishughulikie vitu ambavyo havisaiddii kujenga reli ya katika na kwa kufanya hivyo, tunabaki kusema hiki hakikuwatwa au kilifuatwa na mwisho hatujengi au tunachelewa kujenga reli yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusaini mkataba na Kampuni ya Uturuki pamoja na Ureno wa kujenga reli kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro. Ujenzi wa reli hiyo yenye kasi ya km 160 kwa saa itasaidia sana kurahisisha usafiri hasa wa abiria kutoka Morogoro hadi Dar es Salaam. Ni vyema Serikali ikakamilisha pia sehemu ya reli ya katika iliyobaki na matawi yake yote.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini kwani imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege nchini licha ya changamoto kubwa zilizopo za upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege nchini. Kutopelekwa kwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa wakati kumekuwa kikwazo kikubwa cha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mfano, hadi kufikia mwezi Machi 2016, hakuna fedha zozote zilizokuwa zimetolewa kwa viwanja vya ndege isipokuwa shilingi bilioni 5 (5,000,000,000.00) tu, ambazo zilitolewa kwa ajili ya Kiwanja cha Ndege cha Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi na utolewaji wa fedha za miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege ukizingati kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inakusanya fedha nyingi zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

a) Kiwanja cha Ndege cha Mwanza

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na nia ya kukiendeleza Kiwanja cha ndege cha Mwanza kwa kukipanua ili kiweze kukidhi mahitaji mengi ya sasa ya wakazi wa Kanda ya Ziwa hatimae kutua ndege kubwa za Kimataifa. Hata hivyo ujenzi wa mradi huu umekumbwa na changamoto ya kutotolewa kwa fedha kwa wakati hivyo kusababisha kasi ya utekelezaji wa mradi kuwa ndogo. Mfano halisi ni katika mwaka wa fedha 2015/2016, Kiwanja hiki kiliidhinishiwa **shilingi bilioni 10.7 (10,777,975,000.00)** ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2016 kilikuwa kimepewa **shilingi bilioni 5 tu (5,000,000,000.00)**.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati imefarijika kuona kiwanja hiki kimetengewa **shilingi bilioni 30.1 (30,150,000,000.00)** ambapo mpaka mwezi Januari, 2017 zimetolewa **shilingi bilioni 7.6**. Ni dhahiri kuwa fedha hizi zikitolewa kwa wakati zitaharakisha ujenzi wa kiwanja hiki.

b) Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere Dar es Salaam

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona ni muhimu sasa kiwanja hiki kikafanyiwa ukarabati kwani majengo na miundombinu yake yamechakaa na inahitaji ukarabati mkubwa. Kuendelea kubaki katika hali ya uchakavu ni aibu kwa nchi yetu hasa ukizingatia wageni wengi wanaotembelea nchi yetu hutumia kiwanja hiki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa jengo la tatu la abiria (*terminal III*) katika Kiwanja hiki, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 mradi ultengewa **shilingi bilioni 26** ambazo Kamati imejulishwa hadi Desemba 2016 fedha hizo hazikuwa zimetolewa.

c) Kiwanja cha Ndege cha Songwe

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwanja hiki umekuwa ukisusua kutoptera na changamoto ya upatikanaji wa fedha jambo linalokwamisha kukamilika kwa baadhi ya maeneo yanayojengwa kama vile jengo jipya la abiria. Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/2016 mradi huu ultengewa kiasi cha **shilingi bilioni 5** ambazo hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 hazikuwa zimetolewa. Vivo hivyo, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 mradi huu umetengewa **shilingi bilioni 7** lakini hadi kufikia Desemba 2016 hakuna fedha iliyotolewa kwa ajili ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati haioni sababu za msingi za kutoptera Kiwanja hiki ukizingatia kuwa ili mradi huu ukamilike unahitaji fedha kiasi cha **shilingi bilioni 16.154 tu (16,154,239,492.14)**.

Shirika la Ndege Tanzania-ATCL

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuonesha nia ya dhati na jitihada za kulikwamua Shirika la Ndege Tanzania- ATCL ambapo katika Bajeti yake ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 ilitenga shilingi bilioni 500 (500,000,000,000.00) kwa ajili ya ununuzi wa ndege. Mwezi Oktoba 2016 utekelezaji ulanza ambapo ndege mbili mpya aina ya Dash 8 Q400 zenyet uwezo wa kubeba abiria sabini na sita (76) ambapo abiria sita (6) ni wa daraja la kibashara ziliwasili nchini na kufanya shirika hili sasa kumiliki ndege tatu (3) ambapo moja ni aina ya Dash 8 Q300. Hata hivyo, Kamati imejulishwa kuwa Serikali inaendelea na mpango wa ununuzi wa ndege nyingine mbili zenyet uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 155.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa ATCL imeandaa orodha ya ulipaji wa baadhi ya madeni ambapo orodha imehusisha wadeni muhimu ambao hutoa huduma kwa ATCL kwa ajili ya uuzaaji wa tiketi za ndege na ukusanyaji na udhibiti wa mapato. IATA Clearing House-(ukusanyaji na udhibiti wa mapato), SITA Reservation System-(huduma ya mfumo wa mauzo ya tiketi), Kampuni ya Simu Tanzania-TTCL – (huduma za mitandao ya kuunganisha vitengo mbalimbali) ni kati ya wadeni waliopewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ATCL inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa rasilimali fedha, upungufu wa wataalam hasa marubani na waaandisi ambapo wengi wao wamefikisha umri wa kustaafu, Kucheleva kurejea katika chama cha mashirika ya ndege duniani (IATA), Kushindwa kuanza baadhi ya safari kwa wakati kwenye baadhi ya mikoa kama vile Mpanda kutokana na mapungufu katika viwanja hivyo mfano, ukosefu wa gari la zima moto. Changamoto hizi zinapaswa kutafutiwa ufumbuzi kama inavyoelekezwa katika mapendekezo ya Taarifa hii.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania – TMA

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa katika sekta ya hali ya hewa nchini, Mamlaka hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- a. Kukosekana kwa jengo la kudumu la Makao Makuu na Kituo Kikuu cha Utabiri wa Hali ya Hewa hivyo kuathiri taratibu za kuweka mitambo ya kisasa ya utabiri;
- b. Uchache wa wataalam wa hali ya hewa ili kukidhi matakwa ya Shirika la Hali ya Hewa Duniani ambapo linataka taasisi ya hali ya hewa kutumia wataalam wenye shahada ya kwanza kwa ajili ya kutoa huduma za hali ya hewa katika viwanja vya ndeg ifikapo Desemba 2016;
- c. Upungufu na uchakavu wa vituo na vifaa vya kupimia hali ya hewa;
- d. Mabadiliko ya mara kwa mara ya hali ya hewa Duniani yanayosababisha changamoto katika utabiri wa hali ya hewa; na
- e. Gharama kubwa za kununua na kuendesha mitambo ya hali ya hewa ambapo sehemu kubwa ya huduma hutolewa bila malipo.

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) ilianzishwa kwa Sheria Na. 9 ya Mwaka 2001 ili kudhibiti usafiri katika sekta za reli, barabara, bandari na usafiri wa majini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa barabara, pamoja na jitihada mbalimbali za udhibiti zinazofanywa na SUMATRA, Kamati imebaini kuendelea kuwepo kwa changamoto mbali mbali zifuatazo:-

- a. Kuendelea kuwepo kwa baadhi ya vyombo vya usafiri vibovu na ambavyo si salama kwa kusafirisha abiria;
- b. Baadhi ya vyombo vya usafiri kama NOAH ambavyo vimepewa leseni ya kusafirisha abiria chini ya Kilomita hamsini (km 50). Jambo hili limekuwa likilalamikiwa na wananchi kwani vyombo hivi vilikuwa na msaada mkubwa hasa maeneo ambayo ya uhaba wa usafiri;
- c. Baadhi ya wamiliki wa mabasi kutoza nauli tofauti na zilizopangwa na SUMATRA; na
- d. Mwendo kasi wa baadhi ya vyombo vya usafiri hasa wakati wa jioni au usiku na kuhatarisha maisha ya abiria.

Mheshimiwa Spika, kulingana na tafiti zilizofanyika, asilimia 85 za ajali zinazotokea zinasababishwa na makosa ya kibinadamu kama vile kutokuzingatia alama za barabarani, kutokuwa na elimu ya kutosha katika fani ya udereva, umakini wakati kupita gari jingine (Overtake) , ulevi, uchovu na matumizi ya simu za mkononi. Kamati inaona bado kuna haja ya vyombo vinavyohusika kama Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Wizara ya Katiba na Sheria, Wakala wa Barabara Tanzania, Chama cha Wamiliki wa Mabasi, Chama cha Madereva kukaa pamoja na kuona namna nzuri itakayoweza kupunguza changamoto hizi na kuweka mazingira salama kwa wasafiri.

Sekta ya Ujenzi

Wakala wa Barabara Tanzania- TANROAD

Mheshimiwa Spika, Wakala wa barabara ulianzishwa kwa taarifa ya Serikali iliyotolewa kwenye Gazeti la Serikali Na. 293 mwaka 2000 chini ya kifungu 3(1) cha Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997. Jukumu kubwa la wakala huu ni kuhudumia mtandao wa barabara ambao unakadirwa kuwa na urefu wa jumla ya kilometra 35,000 ambapo kati ya hizo kilomita 12,786 ni barabara kuu na kilometra 22,214 ni barabara za Mikoa. Lengo ni kuwezesha barabara zetu ziweze kupitika kwa urahisi na hatimaye kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi kama ilivyofafanuliwa katika Mpango na Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Kisekta.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa katika kipindi cha Julai- Disemba 2016, jumla ya Kilometra 392.48 za barabara kuu zimejengwa na kilometra 39 zimekarabatiwa kwa kiwango cha lami pamoja na kukamilisha ujenzi wa madaraja matatu (3). Aidha, Kamati imejulishwa kuwa kwa upande wa barabara za mikoa jumla ya kilometra 19 zilijengwa kwa kiwango cha lami na kilometra 122.22 zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Desemba 2016, utekelezaji wa matengenezo ya barabara kuu na zile za mikoa pamoja na madaraja ulifika asilimia 30 ambapo kazi zilizofanyika zilijumuisha kilometra 6,852 za matengenezo ya kawaida (*routine and recurrent maintenance*), kilometra 1,151 za matengenezo ya muda (*periodic maintenance*), kilometra 274 za matengenezo ya sehemu korofi (*spot improvement*). Vile vile madaraja 870 yalifanyiwa matengenezo ya kawaida na madaraja 71 yalifanyiwa matengenezo makubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo Wakala wa Barabara unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

- a. Kutokutolewa kwa wakati fedha za miradi ya maendeleo hali inayosababisha kazi zilizopangwa kwa baadhi ya miradi kutotekelzwa ama kutekelzwa kwa kiasi kidogo;
- b. Msongamano wa magari barabarani hasa jiji la Dar es Salaam, na miji mingine inayokuwa kwa kasi kama Mbeya, Mwanza na Arusha;
- c. Baadhi ya wasafirishaji kuendelea kuzidisha uzito wa mizigo kwenye magari na kusababisha uharibifu wa barabara;
- d. Uwezo mdogo wa Makandarasi wa ndani katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara kutokana na kukosa mitaji ya kutosha pamoja na mitambo ya kisasa; na
- e. Ongezeko la gharama za ujenzi ambazo ni kikwazo kwa ujenzi wa nyumba za kutosha za gharama nafuu kwa ajili ya makazi ya watumishi wa umma.

f.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na migogoro na mvutano kutoka kwa wananchi mbalimbali unaotokana na wasiwasi wa kutolipwa fidia au kulipwa fidia kwa kiasi kidogo ambacho hakiendani na hali ya uchumi wa sasa jambo linalopelekea wananchi kugoma kuondoka katika maeneo ya miradi na kusababisha kuchelewa kuanza kwa miradi.

Aidha, kumeendelea kuwepo uvamizi wa maeneo ya hifadhi za barabara ambapo wananchi wamekuwa wakijenga katika maeneo ya hifadhi za barabara bila kujali Sheria ya barabara Namba 13 ya Mwaka 2007, hii inaleta usumbu na gharama kubwa katika ujenzi wa barabara. Ni rai ya Kamati kwamba, vyombo vyya usimamizi wa Sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa na kubomolewa mapema kuliko kuacha na kusababisha msuguano baadae.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matuta barabarani, licha ya Wakala wa Barabara (TANROADS) kuahidi kuendelea kurekebisha matuta makubwa ili kuyaweka katika kiwango viliuyoainishwa katika mwongozo wa Wizara kuhusu usanifu wa barabara wa mwaka 2011 (*Road Geometric Design MANUAL, 2011*) bado kumeendelea kuwepo matuta makubwa hasa katika barabara kuu ambapo yamekuwa chanzo cha uharibifu wa barabara kwani magari yenye mizigo hulazimika kwenda mwendo mdogo hivyo uzito kuwa mkubwa na kusababisha barabara kutitia. Aidha, matuta barabarani yamekuwa yakisababisha mizigo kuhama na kuelemea upande mmoja jambo ambalo wakati mwengine limekuwa chanzo cha ajali kwa magari mengi ya mizigo.

a) Barabara za Jiji la Dar es Salaam

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa Jiji la Dar es Salaam limekuwa likikabiliwa na msongamano mkubwa wa magari unaotokana na sababu mbalimbali zikiwemo ofisi nydingi za umma kujengwa sehemu moja na kupelekeea wakazi wa jiji kuwa na uelekeo mmoja, ubovu wa barabara za mlisho (feeder roads), utegemezi usafiri wa barabara kwa kiasi kikubwa, uduni wa huduma za usafiri wa umma na ongezeko kubwa la idadi ya magari ikilinganishwa na uwezo wa barabara. Msongamano huu wa magari unaathari nydingi za kiuchumi, kijamii na kimazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi mbalimbali zinazofanywa katika kuhakikisha jiji la Dar es Salaam linakuwa halina msongamano mkubwa wa magari. Juhudi mbalimbali zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo kasi (BRT), kujenga barabara za juu (flyovers) katika eneo la TAZARA na maaandalizi ya ujenzi wa barabara za juu (Interchange) katika eneo la Ubungo. Vilevile maandalizi ya ujenzi na upanuzi wa daraja la Selander ambalo litaanzaia eneo la Coco Beach hadi eneo la Aga Khan pamoja na kukamilisha barabara zingine za kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam.

b) Mizani za Barabarani

Mheshimiwa Spika, moja kati ya majukumu ya TANROADS ni ujenzi na utunzaji wa barabara, kudhibiti uzito wa magari ili kuhakikisha barabara zinadumu kwa muda mrefu. Hata hivyo, pamoja na jukumu hilo bado changamoto imekuwa ni uharibifu wa barabara unaosababishwa na magari kubeba mizigo yenyе uzito mkubwa. Mfano, magari mengi ya aina ya fuso kwa wastani yanatakiwa kubeba mizigo usiozidi tani 3.5 lakini mengi yanazidisha na kubeba mizigo hadi tani 8. Hali hii ni hatari sana kwani mara nydingi yamekuwa yakisababisha ajali pamoja na uharibifu wa barabara kwani matairi yake ni membamba na huchimba barabara na kusababisha mabonde.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya magari yanayobeba mizigo kupita kiasi yanachostaili, mizani ndicho chombo muhimu sana katika udhibiti uzito wa magari ambayo hupelekeea uharibifu wa barabara. Kwa sasa nchini kazi ya udhibiti wa uzito wa magari zinaendelea kwa kutumia mizani 38 ya kudumu, mizani 22 inayohamishika, na mizani mitatu (3) incayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion Weighbridge-WIM).

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwepo kwa vituo vingi vya mizani bado barabara zimekuwa zikiharibika. Suala hili lisipotafutiwa ufumbuzi wa kudumu mapema, Taifa hili litakuwa linaendelea kutenga fedha nydingi kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa barabara zile zile kila mwaka.

Aidha, ili kupunguza msongamano wa magari katika vituo vya mizani, ni vyema sasa katika maeneo ambayo mizani zinakuwa na msongamano mkubwa wa magari kufungwe mizani ya kisasa unaopima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion Weighbridge-WIM) kama ule uliopo Vigwaza mkoani Pwani ambapo kuwepo kwa mzani huu kumesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamano mkubwa wa magari uliokuwapo katika mzani wa Kibaha kwani na kupunguza malalamiko hasa ya wafanyabiashara.

Sekta ya Mawasiliano

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Mheshimiwa spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA ilianzishwa chini ya Sheria Na. 12 ya Mwaka 2003 ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania baada ya kuunganishwa kwa iliyokuwa Tume ya Utangazaji Tanzania na Tume ya Mawasiliano Tanzania-TCC. Dhumuni la kuanzishwa kwa Mamlaka hii ni kusimamia Makampuni ya Mawasiliano nchini ikiwemo Makampuni yanayotoa huduma za Simu, Utangazaji, Intaneti, Posta na Usafirishaji wa Vifurushi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kuendelea kutekeleza ushauri unaotolewa na Kamati katika kipindi cha Januari 2016/2017 na hatimae kuweza kufanikisha yafuatayo:-

- a. Kuhakiki mawasiliano ya simu za ndani ambapo takwimu za mawasiliano ya ndani yaliyofanyika baina ya watoa huduma za ndani (mwingiliano wa mawasiliano kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine (off-net) kwa mujibu wa Kanuni za Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta za mwaka 2011. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imekamilisha mfumo wa *on-net traffic monitoring* mnamo mwezi Septemba, 2016 ambapo vifaa vilifungwa kwenye makampuni nane (8) ambayo ni Vodacom, TIGO, Airtel.ZANTEL, HALOTEL, TTCL SMART na SMILE na kuunganishwa na mfumo wa usimamizi uliofungwa katika ofisi za TCRA. Aidha, kumbukumbu za mawasiliano ya simu za ndani ya mtandao mmoja (*on-net*) zilichukuliwa;
- b. Kuhamishwa kwa sehemu ya Miundombinu au uendeshaji wa Mitandao ya mawasiliano nje ya nchi ambapo mara baada ya kulibaini hili makampuni matatu ya simu yaligundulika kukiuka Sheria ya Kieletroniki na Posta ya Mwaka 2011. Makampuni hayo yalitakiwa kulipa faini ya **shilingi milioni mia moja (100,000,000.00)** kila moja na kufanya jumla ya faini iliylipwa kuwa **shilingi milioni mia tatu (300,000,000.00)**;
- c. Mfumo wa kubaini simu za ulaghai (Antifraud Management System), ambapo simu hizo zimeendelea kutambuliwa na kufungiwa kwani zimekuwa zikiingiza mawasiliano ya simu za kimataifa kwa ulaghai na kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali; na
- d. Kufanya utafiti ili kubaini ukiukwaji wa masharti ya usajili laini za simu za mkononi ambapo makampuni sita yaliyukwaji yamekiuka masharti hayo hivyo kupewa adhabu ya faini kulingana na makosa yao ambapo jumla ya shilingi milioni miatano tisini na moja (**591,000,000.00**) zililipwa.

Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta

Mheshimiwa spika, mradi wa anuani za makazi unalenga kuanzisha mfumo mpya wa anuani nchini utakaowezesha kuwapo kwa utambulisho wa makazi ya watu na makampuni kwa kutumia anuani za makazi ujulikanao kama postikodi. Mradi huu ni muhimu sana kwani utarahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchimi na kisiasa. Miongoni mwa huduma zitakazorahisishwa na kuwapo kwa mfumo huu ni pamoja na huduma za umeme, gesi, maji, mabenki, ulinzi na usalama, huduma za dharura kama zima moto ,magari ya wagonjwa, pamoja na wasambazaji wa vifurushi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa mfumo huu uko tayari nchi nzima kinachosubiliwa ni serikali za miji na mitaa kutekeleza katika maeneo husika. Mamlaka imeweka postikodi maeneo ya mfano katika jiji la Arusha, Dodoma na Dar Salaam ambapo imeweka namba za nyumba na majina ya mitaa. Hata hivyo, changamoto kubwa imekuwa kutokuwa na mipango miji na ujenzi holela, na pia upatikanaji wa majina ya mitaa, kutowana na mabishano juu ya majina katika ngazi ya Halmashauri husika.

Vilevile, changamoto nyingine zinazoukabili mradi huu ni kutokuwa na fedha za kutosha, kutokuwepo kwa takwimu halisi za idadi ya barabara/mitaa katika kata, kutokuwepo kwa takwimu na taarifa halisi za makazi na wakazi katika Kata na uharibifu wa miundombinu kama vile nguzo za majina ya mitaa na vibao vya namba za nyumba hata sehemu zilizopangwa.

Mheshimiwa spika, kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi huu ukilinganisha na umuhimu wake kwa Taifa. Kamati ilipopata taarifa hii mwezi Machi, 2016 fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu hazikuwa zimetolewa. Katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 Serikali imetenga **shilingi bilioni 3 (3,000,000,000.00)** kwa ajili ya uendelezaji wa mradi katika mji wa Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza na Mbeya.

Shirika la Posta Tanzania

Mheshimiwa spika, shirika hili linahitaji mtaji ili liweze kujidesha kibiashara na kukabiliana na ushindani uliopo na changamoto ya soko katika sekta ya posta. Kamati imejulishwa kuwa Serikali imeendelea kufanya kazi Shirika hili ili liweze kujidesha ikiwa ni pamoja na kulipa madeni mbalimbali. Aidha, shirika lililipa kiasi cha **shilingi billion 5** kwa ajili ya kulipa pension za wastaafu wa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki kwa niaba ya Serikali kwa makubaliano ya kurejeshewa fedha husika na Serikali.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake na hatimae kuanza kulipa deni hili ambapo mpaka sasa Serikali imelipa kiasi cha **shilingi bilioni 1.7**.

Mheshimiwa spika, kufuatia hali mbaya ya kifedha Shirika limeshindwa kulipa madeni ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania -TRA ilikamata akaunti za shirika mara tatu kati ya Desemba 2015 na Februari 2016 kwa wakati tofauti kwa limbikizo la **takribani bilioni 15**. Aidha, Shirika kuwekwa kwenye orodha ya mashirika yanayokusudiwa kurekebishwa kumesababisha Shirika kushindwa kupata kibali cha kukopa fedha kwa taasisi za fedha kwa ajili yakuongeza mtaji na kuendeleza rasilimali za Shirika na kutoa huduma zake.

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

Mheshimiwa spika, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote Kamati imejulishwa kuwa mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kupeleka huduma ya mawasiliano maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara. Changamoto kubwa ni watoa huduma wengi wa simu kutokishiriki kikamilifu katika zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa, kumekuwepo na mafanikio mbalimbali kuitia utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano vijiji ambapo katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka 2016/2017, Mfuko wa Mawasiliano ulifikisha huduma za mawasiliano katika kata 138 zenye jumla ya vijiji 557 na kata 443 zinafikishiwa huduma ya mawasiliano kwa kutumia ruzuku ya Serikali ambapo kata 122 bado hazijakamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia sekta ya Mawasiliano iliingia mkataba na Kampuni ya simu ya Viettel ili kufikisha mawasiliano vijiji ambapo Kampuni hiyo ilitakiwa kufikisha mawasiliano kwenye vijiji 4,000 ndanii ya miaka mitatu. Hadi kufika Desemba 2016 Kampuni ya Viattel ilifikisha mawasiliano katika vijiji 2,889 kati ya vijiji 3,000 vilivyo takiwa kufikiwa. Kuchelewa kukamilisha kumechangiwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa vibali vya ujenzi katika maeneo ya minara. Awamu ya tatu ya mradi huu inatarajiwa kukamilika Oktoba, 2017. Kampuni ya Viettel imebakiza vijiji 1,178 ambavyo vinapaswa kukamilika hadi kufikia mwezi Novemba 2017.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukubwa wa nchi yetu na muda ambaa mfuko huu umekuwepo toka kuanzishwa kwake, Kamati bado hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara hasa vijiji. Kamati imebaini kuwa Makampuni makubwa ya simu bado hayajaimizwa vya kutosha kupanua huduma zao katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara kama mojawapo ya uwajibikaji wao kwa jamii (*corporate social responsibility*). Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kutoa ruzuku kuyafikia maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara ili kuyafikia yote kwa haraka zaidi utaratibu wa kuzitaka Kampuni kubwa kuonekana zinasaidia ni jambo sahihi.

SEHEMU YA TATU

MAONI, MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI

Bajeti ya Miundombinu

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuendeleza miundombinu nchini ambapo kwa mara ya kwanza Sekta ya Miundombinu katika Bajeti ya Mwaka 2016/2017 imetengewa **asilimia 16.7** ya bajeti yote ya Serikali. Hata hivyo, Kamati inasisitiza Serikali kutoa fedha kwa wakati ili kurahisisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuepuka limbikizo la madeni

Sekta ya Uchukuzi

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Bandari Tanzania, Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) Kwa kuwa Bandari ya Dar es Salaam ni kiungo muhimu kati ya nchi yetu na nchi jirani ambazo hazina bahari (*land lock countries*); na kwa kuwa bandari hii ikiimarishwa itaweza itaweza kuingizia nchi yetu mapato mengi zaidi na hata kukuza uchumi; Kamati inashauri Serikali kuboresha mazingira ya Bandari ya Dar es Salaam kwa kuongeza kina katika gati namba 1-7, upanuzi wa lango la kuingilia meli, kujenga gati namba 13 & 14 pamoja na kuimarisha usafiri wa njia ya reli kutoka bandarini. Vilevile Mamlaka ya Bandari Tanzania iwe na mkakati wa kutangaza maboresho hayo na huduma zake kuliko ilivyo sasa.
- b) Aidha, Kamati inashauri changamoto zifuatazo zifanyiwe kazi kwa kina ili kuongeza ufanisi wa Bandari nchini:-
 - i. Hofu ya wateja kutohana na kuanzishwa kwa Sheria ya (Value Added Tax-VAT) kwa huduma zitolewazo na mawakala kwenye mizigo ya nchi jirani (*VAT on transit goods*) ambayo ni kinyume na Sheria za Kimataifa. Uwepo wa Sheria hii unawafanya wateja kutotumia bandari za Tanzania kwa sababu ya gharama;
 - ii. Mgongano wa tozo za hifadhi za mizigo "Customs Warehouse Rent" inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA na "Storage Charges" zinazotozwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA. Malipo haya yanafanana isipokuwa

yametofautiana majina tu, hivyo wafanyabiashara kuona kuwa wanalipa mara mbili igharama ya hifadhi za mizigo;

- iii. Tozo za barabara (*Road Tolls*) ambapo hutozwa **Dola za Kimarekani 16** kwa Kilomita ukililinganisha na **Dola za Kimarekani 8** kwa Kilomita zinazotozwa katika nchi zenye bandari shindani;
- iv. Tozo ya **Dola za Kimarekani 23** kwa tani kwa mizigo wa shaba ambapo bandari nyingine shindani kama Durban hutoza Dola za **Kimarekani 17.86**;
- v. Kwa mujibu wa makubaliano ya mwanzo, tozo kubwa kwa mizigo yote inayotoka ama kwenda Zambia tofauti na tozo za nchi nyingine kama Rwanda na Burundi. Mfano, kasha la urefu wa futi 40 linatozwa **Dola za Kimarekani 530** kwa mizigo wa Zambia badala ya **Dola za Kimarekani 320** ambazo hutozwa kwa kasha hilo hilo linalokwenda Rwanda ama Burundi;
- vi. Himaya ya forodha kwa pamoja (*Single Customs Territory*) kwa mizigo wa Congo umeleta utata na kupunguza motisha kwa wafanyabishara wa nchi hiyo kwa kutumia Bandari ya Dar es Salaam. Hii inatokana na kuwa mfumo wa ukusanyaji kodi ndani ya DRC unatoa mwanya kwa baadhi ya wafanyabishara katika nchi hiyo kutolipa kodi kwa asilimia mia moja (100%) tofauti na mizigo inayopatikana kwenye mfumo wa "*Single Customs Territory*" ambayo hutozwa kodi kwa asilimia mia moja (100%) jambo linalosababisha baadhi ya wafanyabishara wa Congo kuona gharama kubwa kuitisha mizigo yao Tanzania;
- vii. Muda mfupi (*Short grace period of Transit Bulk liquid*) kwa mizigo wa mafuta wa nchi za jirani (Siku 30) bila kujali mazingira ya usafirisha wa barabara katika nchi yetu tofauti na nchi nyingine shindani ambazo ni siku 60 hadi 90 na utaratibu duni;
- viii. Mfumo wa TANCIS wa TRA kutokurushu kugawanya "*Bill of Lading*" ili kuruhusu kutoa mizigo ambayo haina tatizo panapokuwa na tatizo la Mzigo Moja badala ya mizigo wote kuzuiwa na kusababisha gharama za tozo za hifadhi kwa mteja ambazo sio za lazima;
- ix. Kuongezeka kwa Tozo kutokana na "Government Chemical Agencies" kutoza USD 1.00 Kwa Tani badala ya USD100 Kwa "*Bill of lading*" kwa bidhaa ambazo wanazikagua kama vile mbolea na hivyo kuongeza kutoka wastani wa USD 500 hadi USD 20,000 au zaidi kutokana na ukubwa wa mizigo;
- x. Idara za Serikali (OGD's) na Mabenki kutokufanya kazi masaa 24 /7. Utendaji wa bandari unategemea upatikanaji wa vibali kutoka idara za mbalimbali za serikali pamoja na huduma za kibenki;
- xi. Usalama mdogo wa mizigo inayosafirishwa kwenda nchi za jirani (wizi wa mizigo na madereva kuvamiwa) na hivyo wenye mizigo kulazimika kuingia gharama ya kuweka walinzi wa kusindikiza mizigo; na
- xii. Gharama kubwa za usafirishaji kwa njia ya barabara inayochangiwa na wingi wa vituo vyta ukaguzi "*Check Points*" na malipo yanayodaiwa na watendaji wasio waaminifu.

- c) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu bandari kavu- ICD's, Kamati inapongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri wa kujenga bandari kavu itakayomilikiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) katika eneo la Kwala-Wilayani Kisarawe kwani kwa kiasi ICD's zinazomilikiwa na watu binafsi uchelewashaji na upotevu wa mizigo pamoja na ukwepajji wa kodi.
- d) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwapo kwa udanganyifu unaofanywa na mawakala (*freight forward*) kwa kuongeza gharama kwenye hati za madai zinazotumwa kwa wateja. Kamati inashauri adhabu kali zitolewe kwa mawakala wanaobainika kuongeza gharama hizo ikiwezekana wafutiwe leseni zao;
- e) Kwa kuwa mionganoni mwa kero za wafanyakishara wanaautumia Bandari ya Dar es Salaam ni kutokuwepo kwa maegesho ya magari yanayoingiza na kutoa mizigo bandarini; Kamati inashauri Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa kushirikiana na Halamshauri ya Wilaya ya Temeke kushirikiana na kuhakikisha eneo liliokuwa limetengwa kwa ajili ya maegesho linapatikana.;
- f) **Mheshimiwa Spika**, licha ya kuwa mchakato wa ununuzi wa *flow meter* mpya unaendelea; Kamati inasisisitiza kuwa suala hili lipewe kipaumbele ili mchakato huo uweze kukamilika haraka kwani ni muhimu kufahamu kiasi cha mafuta kinachoingia na kutoka ili kuweza kutoza kodi stahiki;

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha standard gauge;

Kwa kuwa sasa Serikali imeonesha nia ya kutaka kuifufua reli ya kati na kujenga katika kiwango cha kisasa kwa kutenga katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2016/2017 **shilingi trillioni 1**; na kwa kuwa wakati nchi yetu inajianadaa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*, nchi zingine wanachama wa Afrika Mashariki zinaendelea kujenga kwa kasi kubwa sana reli kwa kiwango cha *Standard gauge* kutoka Mombasa- Nairobi- Kampala hadi Kigali.; Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

- a) Serikali kuharakisha ujenzi wa reli ya kati na matawi yake ambayo ni kutoka Dar es Salaam – Kigoma, Uvinza - Msongati kwa ajili ya mizigo wa Burundi; tawi la Tabora- Kalemi kwa ajili ya mizigo ya DRC; na Tabora- Shinyanga- Mwanza kwa ajili ya ukanda wa ziwa. Aidha, Kamati inashauri Serikali pia kuanza kufanya utafiti wa kupanua matawi (*spurs*) ya reli ya kati kutoka Bandari kavu ya Isaka (Shinyanga) hadi Rusumo Mkoani Kagera, hivyo kuwezesha mradi wa kuchimba madini ya Nickel huko Kabanga kutekelezeka.
- b) Ni vyema mradi huu wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*, Serikali uipe Kampuni moja ili yenyele iijigawe kadri inavyoweza badala ya kujenga vipande vidogo vidogo na Kampuni tofauti. Ikiwa reli hii itajengwa na Kampuni moja itasaidia katika viwango vya reli itakayojengwa. Vilevile, Serikali itangaze rasmi muda wa kuanza na kukamilisha kazi ya ujenzi wa reli hii na matawi yake.
- c) Uimarishwaji wa reli uende sambamba na kutafuta suluhisho madhubuti katika maeneo korofi kama vile stesheni ya Kilosa- Gulwe Morogoro kwani tatizo la kuharibika eneo hili kwa reli kusombwa na maji limekuwa lingirudia mara kwa mara na kugharimu fedha nydingi bila kupata suluhisho la kudumu.
- d) Serikali iimarishe karakana za treni nchini ili kutoa wataalam watakaoweza kuhudumia reli zetu kwa ufanisi na kwa namna endelevu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuunganisha Mashirika ya Serikali RAHCO na TRL, TPA na MSCL;

Kwa kuwa lengo zuri la Serikali kutenganisha mashirika yake ya RAHCO na TRL pamoja na TPA na MSCL limeshindwa kufanikiwa kwa sababu ushindani uliotegemewa haukupatikana (*Market Failure*). Kamati inashauri Mashirika haya yaunganishwe ili Mashirika yake mama yasaidiane na mashirika ya huduma ambayo mpaka sasa yanatengeneza hasara (cross-subsidization) na yanahitaji kusaidiwa na shirika mama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia- TAZARA

Kwa kuwa utendaji wa TAZARA umekuwa ukishuka siku hadi siku; na kwa kuwa moja ya sababu ya TAZARA kushuka ni mapungufu yaliyopo katika Sheria Na.4 ya Mwaka 1975; Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

- a) Serikali ihakikishe inakamilisha utaratibu mpya waliokubalina kati yake na Zambia juu ya uendehaji wa Shirika la TAZARA. Vilevile, Serikali iendelee kusaidia kulipa wafanyakazi wa TAZARA mishahara kwa mwaka wa fedha wa 2016/17 mpaka hapo itakapowekeza mtaji wa kutosha kwenye Shirika hili; Aidha, Serikali ilipe madeni ya wafanyakazi pamoja na kuhakikisha makato ya wafanyakazi yanayopelekwa katika mifuko ya hifadhi jamii ili kuepuka usumbufu kwa wafanyakazi wanaostaifu;
- b) TAZARA kubuni mbinu za kujarendesa kibiashara ikiwemo kuangalia upya bei zake kwani wafanyabiashara wengi wamehamia kwenye usafiri wa barabara kwa kuwa ni nafuu zaidi ukilinganishwa na usafiri wa treni. Mfano, gharama za kusafirisha mbao kutoka mbeya kwa gari ni shilingi 2,000,000 mzigo unafika mpaka sehemu ya biashara ukilinganishwa na behewa moja linalokodiwa kwa kiasi cha shilling 3,600,000 na bado kuna gharama za kupeleka mzigo kupakia na baadae kushusha kupeleka sehemu ya biashara;
- c) Serikali kutoa fedha kwa ajili ya matengenezo ya vichwa sita (6) ambavyo vinasubiri matengenezo kwa gharama ya inayokadiriwa kuwa shilingi billion 6;
- d) Serikali kujenga kipande cha reli chenye urefu wa kilometra 18 kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafishaji wa makaa ya mawe kwani mzigo unaotoka ni mkubwa hivyo unaweza kupatia TAZARA mapato ya kutosha kujarendesa;
- e) Serikali kuimarisha manajimenti ya kiwanda cha kokoto cha kongoro ili kiweze kujitegemea kwani sahivi zaidi ya asilimia 60 ya kokoto zinazozalishwa hapo hutumiwa na TAZARA na kiasi kidogo kinauzwa kwa watu binafsi na hata ikiwezekana kijitegemee ili Tazara wawe wanakwenda kununua kununua kokoto hizo kwani wameshindwa kuweka mtaji kwa ajili ya kukiendeleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA

Kwa kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inatoa mchango mkubwa katika mapato yatokanayo na viwanja vya ndege nchini, na kwa kuwa bado kuna changamoto kubwa ya uboreshaji na ujenzi wa viwanja vya ndege, Kamati inashauri yafuatayo;-

- a) Serikali kuipatia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege angalau **asilimia 50** ya maduhuli (*retention*) yatokanayo na viwanja vya ndege ili kusaidia kuongeza kasi ya shughuli za Mamlaka zikiwemo ukarabati na upanuzi wa viwanja vikiwemo Kiwanja cha

Ndege cha Mtwara, Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga, Kiwanja cha Ndege cha Arusha, Kiwanja cha Ndege cha Moshi, Kiwanja cha Ndege cha Bukoba, Kiwanja cha Ndege Musoma, Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga Kiwanja cha Ndege cha Mpanda na Kiwanja cha Ndege cha Nduli-ringa. Vile vile, kuweza kulipa fidia kwa viwanja vya ndege vya Julius Nyerere International Airport- JNIA, Mwanza, Bukoba, Omukajunguti, Msalato, Kigoma, Shinyanga, Songwe, Sumbawanga, n.k

- b) Serikali ihakikishe inamaliza kwa wakati malipo ya fedha yaliyoidhinishwa kwa kuendeleza viwanja vya ndege nchini hususan Kiwanja cha ndege cha Mwanza, Songwe na Mtwara;
- c) Kamati inashauri Serikali kuharakisha kutekeleza awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la tatu (*Termin III*) la abiria katika kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere ili mradi huu uweze kukamilika katika muda uliopangwa yaani Disemba 2017. Aidha, Kamati inashauri wakati ujenzi wa jengo la tatu unaendelea, ni vyema kuendelea kuboresha mifumo ya jengo la pili la abiria linalotumika sasa ili kuwa na muonekano mzuri na kuleta taswira nzuri ya nchi;
- d) Pamoja na kwamba Serikali imeanza kutekeleza ushauri wa Kamati wa kubadilisha umiliki wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro kutoka KADCO kwenda TAA ambapo hatua iliyofikiwa ni kuweka kumbukumbu sahihi za taarifa na mizania zilizopo BRELA na taratibu za kisheria za kuondoa mikataba miwili iliyobaki (*Concession Agreement na Lease Agreement*). Kamati inasitiza kuharakishwa kwa mchakato huu ili Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro kirejeshwe kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA na kiweze kuongeza ufanisi, tija na mapato;
- e) Pamoja na kwamba Serikali kwa kiasi imezingatia utekelezaji wa maaagizo ya Kamati kuhusu kupima viwanja vyake, ambapo hadi sasa Kamati imejulishwa kuwa viwanja vya ndege vinane (8) vimeshapatiwa hati miliki, bado kuna haja ya kuhakikisha kuwa viwanja vingine viliviyobakia vinapimwa na kupatiwa hati miliki pamoja na kuwekwa uzio ili ili kujiepusha na uvamizi wa maeneo jambo ambalo huleta migogoro na wananchi na kusababisha Serikali kuingia gharama kubwa kwa ajili ya fidia; na
- f) Kuhusu viwanja vya ndege kujengwa na TANROADS, Kamati inashauri Serikali kuzingatia Sheria na Mamlaka ya uanzishwaji wa vyombo hivyo viwili. Kwamba kwa mujibu wa uanzishwaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege-TAA ndiyo Taasisi ya Serikali ya kusimamia na kuendeleza Viwanja vya Ndege. TANROADS majukumu yake ni kusimamia barabara zilizo chini yake kwa mujimu wa sheria. Hivyo, Serikali iimarishe uwezo wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA na si kuyahamisha majukumu ya Mamlaka ya viwanja vya ndege Tanzania kwa Mamlaka nyingine. Kamati inaona wazi kuwa ueledi wa barabara uko TANROADS na ueledi wa ujenzi wa viwanja vya ndege uko kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege-TAA.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kampuni ya Ndege ya Tanzania-ATCL

Kwa kuwa Serikali imechukua hatua ya kufufua Shirika la ndege la Tanzania kwa kununua ndege mbili mpya aina ya Dash 8-Q400 na kwa kuwa kuna mpango wa kuongeza ndege nyingine mpya mbili (2) zenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya watu 155; na kwa kuwa ndege hizo kwa vyovyyote vile zitakuwa kichocheo cha Uchumi wa Tanzania katika kuwawezesha watanzania kupata usafiri wa haraka na hivyo kutimiza malengo katika nyanja mbalimbali za uchumi.Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) Mafunzo ya menejimenti ya biashara ya ndege (kwa kwenda nchi zilizofanikiwa hasa China), hasa kwa viongozi wa bodi na viongozi wakuu wa Kampuni ya Ndege-ATCL ili waje na mawazo ya kisasa yatakayowawezesha kuingia katika ushindani wa kibashara. Ikumbukwe kuwa mikakati ya ATCL pia inafanywa na washindani wake;
- b) Mifumo ya uendeshaji wa shirika iwe yenyne malengo chanya yenyne kupelekea kuleta mabadiliko katika sekta ya usafiri wa anga;
- c) ATCL sasa ijitangaze kwenye vyombo rasmi vyya kimataifa ambavyo huonyesha safari za ndege dunia nzima ya GDS kama Galileo na Amidius ili kutoa huduma bora za usafiri wa anga ndani na hata kimataifa, Kamati inashauri ; na
- d) Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) ijpange kuingia katika soko la usafiri wa anga na kuhakikisha abiria wengi zaidi wanatumia usafiri wa ndege zake hii ikiwa pamoja na kuendelea kujitangaza katika vyombo vya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali, kujali wateja (costomer care) na kuwa gharama nafuu za nauji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Udhiliti wa Usafiri wa Anga Tanzania -TCAA

Kwa kuwa Mamlaka ya Udhiliti wa Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) ni Mamlaka yenyne jukumu la udhibiti katika sekta ya usafiri wa anga nchini (kama inavyosimamiwa na sheria ya usafiri wa Anga CAP 80 (R.E 2006)), na kwa kuwa kumekuwa kukiokoa changamoto mbalimbali katika usafiri wa anga hasa pale ndege zinapohairisha ama kufuta safari ghafla, Kamati inashauri kuwa Mamlaka ya Udhiliti wa Usafiri wa Anga ifanye kazi zake vyema kwa kuhakikisha kuwa inatoa elimu kwa umma na inakuwa na dawati la kufuatilia malalamiko kutoka kwa abiria pamoja na kutangaza namba za simu na hata kuzionesha kwenye tiketi za ndege za abiria;

Vilevile, Kamati inashauri Mamlaka ya Udhiliti wa Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) itengeneza Kanuni zenyne kuakisi Sheria na Kanuni za Kimataifa za usafiri wa anga ili kuwatendea haki abiria hasa pale ndege zinapohairisha au kufutwa safari;

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania-TMA Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) Serikali itenge fedha ili Mamlaka hii iweze kuimarishe miundombinu yake ya utendaji kazi kama kujenga jengo lake, kuwa na vifaa vya kutosha sambamba na ukarabati na kuongeza idadi ya vituo vya kupimia hali ya;
- b) Serikali kutoa ruzuku kwa ajili ya kusomesha wataalam wa hali ya hewa (meteorologist) ili kuweza kukabiliana na uhaba wa wataalam wa hali ya hewa

wenye wenye shahada ya kwanza ambayo ndicho kigezo ama matakwa ya Shirika la Hali ya Hewa Duniani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (Surface and Marine Transport Regulatory Authority-(SUMATRA)

Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) Kwa kuwa kumekuwepo tatizo la upandishaji nauli kiholela na kwa kuwa tatizo hili limekuwa likiathiri wananchi hasa wa pembezoni, Kamati inashauri SUMATRA ihakikishe kuwa inafatilia nauli za maeneo mbali mbali nchini ili wananchi wapate auheni ya usafiri hususani maeneo yaliyo pembezoni mwa nchi kama Mpanda, Tabora, Kigoma na Mtwara;
- b) Kwa kuwa SUMATRA kisheria ndio wamepewa jukumu la kuhakikisha magari yanayobeba abiria yanakidhi ubora wa kusafirisha abiria, na kwa kuwa teknolojia imekuwa ikibadilika mara kwa mara, Kamati inashauri Serikali kuitia SUMATRA ianze kuona uwezekano wa kuwa na vituo vya kisasa vya ukaguzi wa magari kwa kila kanda kwani itasaidia kuongeza Pato la Serikali na kuondoa usumbufu kwa wananchi; na
- c) Kwa kuwa kumekuwepo na ongezeko kubwa la ajali za pikipiki, na kwa kuwa ajali hizi zimekuwa zikiathiri sana wananchi kwani wengi wamekuwa wakipoteza viungo vya mwili na hata kubaki kuwa watu wenye ulemavu, Kamati inashauri SUMATRA itoe mafunzo ikiwezekana nchi nzima ukianzia maeneo yale ambayo ajali za pikipiki ni nyingi ili kusaidia kupunguza madhara yatokanayo na ajali hasa za pikipiki; na
- d) Kamati inashauri SUMATRA iangalie uwezekano wa kuruhusu aina ya vyombo vingine vya usafiri kama Noah katika utoaji wa huduma ya usafiri hasa katika maeneo yaliyoko vijiji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Usafirishaji Tanzania –NIT

Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) Kwa kuwa Chuo cha Usafirishaji Tanzania ni Chuo cha Serikali na kwa kuwa kinatoa elimu ya kipekee hapa nchini, Kamati inashauri Serikali kupeleka nguvu Chuo cha Usafirishaji Tanzania (NIT) ili kuboresha miundombinu ya Chuo hasa majengo na magari ya kufundishia. Vile vile, Serikali iharakishe kulifanya kazi andiko lenye lengo la msaada wa kupanua Chuo toka Serikali ya China; na
- b) Kwa kuwa Chuo cha Usafirishaji – NIT kinatoa mafunzo muhimu na ya kipekee kama mafunzo ya uhandisi wa ndege, na kwa kuwa gharama ya ada kwa ajili ya mafunzo haya ni kubwa, Kamati inashauri Serikali itoe ruzuku kwa kozi ambazo ni za kipekee na ambazo ada zake ni ghali ili kuweza kupata wanafunzi wengi na hatimae kuwa wataalam wengi; Aidha, Serikali sasa iboreshe Miundombinu ya Vyuo hivi ili viweze kuvutia watu wengi toka ndani na nje ya nchi kuijunga na kupata elimu katika vyuo hivi;

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Bahari Dar es salaam (DMI)

Kwa kuwa Vyuo vinavyofundisha elimu ya bahari Afrika viro vinne tu pamoja na Chuo cha Bahari Dar es Salaam, na kwa kuwa mafunzo haya yanaongeza tija na ufanisi; hivyo basi Kamati inaishauri Serikali iongeze ruzuku kwenye Chuo cha Bahari Dar es Salaam ili kukarabati karakana ya kufundishia ili iweze kufanya kazi na Chuo kiweze kujitegemea na kutoa mafunzo kwa wanafunzi wengi na kuwapa ajira watanzania wengi.

Sekta ya Ujenzi

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Barabara Tanzania-TANROAD

- a) Kwa kuwa malengo ya Sekta ya Ujenzi ni pamoja na kujenga barabara kuu ili kufungua fursa za maendeleo na kuhakikisha miji yote mikuu na mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami ifikapo 2017/18; na kwa kuwa lengo hili bado halijakamilika kutohana na Mikoa mingine ambayo hajjaweza kuunganishwa kwa barabara ya lami; Kamati inashauri Mikoa iliyosalia kama vile Mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera, Njombe-Makete-Mbeya nayo iunganishwe ili kufungua fursa za kiuchumi katika maeneo hayo. Vilevile, Serikali ikarabati baadhi ya barabara za Mikoa zilizo katika hali isiyoridhisha na kutopitika hasa wakati wa mvua na kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii;
- b) Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi isimamie Sheria za barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vya habari kama runinga, magazeti na radio. Pia kufanya mikutano na kuweka alama zitakazoonesa mwisho wa eneo la barabara;
- c) Serikali kuendelea na ujenzi wa barabara hasa kwa barabara zile zinazounganisha nchi yetu na nchi za jirani, mikoa, wilaya na maeneo ya uzalishaji kama vile kilimo, madini na viwanda;
- d) Serikali iendelee kuzingatia kuoanisha uendelezaji wa miundombinu na mipango miji;
- e) Matuta madogo madogo ya barabarani maarufu kwa jina la rasta na matuta makubwa yasiyo na kiwango yaondolewe kwa kuwa zinasababisha ajali na uharibifu wa magari. Aidha matuta yabaki sehemu zenye umuhimu tu na yawe na kiwango maalumu;
- f) Ili kuilinda miundombinu yetu hasa alama za barabara na reli; upo umuhimu mkubwa wa kutungwa kwa Sheria ya kudhibiti uuzaji wa chuma chakavu ili kunusuru miundombinu yetu iliyogharimu fedha nyingi na kwa usalama wa watumiaji wa barabara zetu; na
- g) Serikali inunue mizani ya kisasa ambazo zinauwezo wa kupima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo (*Weight in Motion*). Kamati inaendelea kushauri mizani hizi za kisasa zifungwe pia katika maeneo mengine yanye kusababisha msongamano mkubwa wa kupima magari Mfano, Himo-Moshi, Mizani ya Mikese-Morogoro, Kihonda-Morogoro, makambako, kwa mpemba n.k. Kamati inashauri adhabu kali zitolewe kwa wanaozidisha uzito wa mizigo ili iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam;

- a) Kwa kuwa Serikali imeonesha nia ya kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam kwa kuweka barabara za juu (flyovers) eneo la TAZARA na Ubungo, na kwa kuwa msongamano katika jiji la Dar es Salaam hautaweza kupunguzwa kwa barabara za juu katika maeneo hayo mawili tu; Kamati inashauri barabara za juu maarufu kama (flyovers) zijengwe hasa katika makutano ya barabara kuu zenyne msongamano mkubwa kama vile, Magomeni, Morocco, Mwenge, Kilwa Road, Makutano ya Kenyata, Kinondoni na Ali Hassan Mwinyi Road na Kamata. Kamati inaona ni vyema ikiwa Serikali itahusisha Sekta binafsi na Mifuko ya Pension katika ujenzi wa barabara hizi za juu (flyovers) ili iweze kukamilika kwa haraka. Aidha, kamati inasitiza umuhimu wa upanuzi wa daraja la Salenda na daraja la gerezani;
- b) Ili kupunguza msongamano katika jiji la Dar es salaam, ni muhimu kukamilisha ujenzi wa barabara zinazosaidia wananchi kufika maeneo yao bila kupita katikati ya Jiji la Dar es salaam, ikiwa ni pamoja kukamilisha barabara kutoka Goba-Madale-WazoHill, Goba -Kimara, Ardhi-Makongo-Goba n.k. Pia barabara za mitaani (ring roads) nazo zifunguliwe kwa kuwekwa lami kwani zitapunguza msongamano kwa kiasi kikubwa; pia
- c) Katika juhudhi za kupunguza msongamano wa magari katika vituo vya mizani, ni vyema Serikali kuamua sasa kuwa na vituo vitatu katika kila barabara kuu kama vile, kutoka Dar Es Salaam kwenda Rusumo, Dar Es Salaam kwenda Namangana Dar Es Salaam kwenda Tunduma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Majengo Tanzania-TBA;

Kamati inashauri Serikali kuimarisha uwezo wa TBA ili iweze kuzalisha fedha na kuchangia Pato la Serikali. Vilevile Kamati inashauri Wakala wa Majengo Tanzania-TBA, pamoja na kujenga nyumba za gharama nafuu, kuhakikisha zinakuwa katika hali ya ubora na viwango vinavyostaili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Ujenzi Morogoro na Chuo cha matumizi stahiki ya nguvu kazi Mbeya (Appropriate Technology Training Institute-ATTI);

Kamati inashauri Serikali iviunganishe vyuo hivi na kuvijilili ili mafunzo yanayotolewa katika vyuo hivi yaweze kutambulika. Aidha, Serikali ivitengee bajeti ya kutosha vyuo hivi ili viweze kuwa na mvuto kwa watu wengi kuijunga na kupata elimu kwani bado kuna uhitaji mkubwa wa wataalam hasa wa barabara katika Halamashauri nchini ambapo wataalam hao wanategemewa kutoka katika vyuo hivi;

Sekta ya Mawasiliano

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA;

Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuharakisha kutafuta ufumbuzi wa namna bora ya kupata taarifa za makusanyo ya simu za ndani kwa kutumia mtambo wa TTMS ili Serikali iweze kutoza kodi stahiki kutokana na miamala ya fedha inayofanyika kuititia simu za mkononi. Kuendelea kuchelewa kulitekeleza suala hili kunazidi kuikosesha nchi kodi stahiki kutokana na Makampuni haya kutotozwa kodi stahiki;

- b) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai na hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao na ili kuimarisha usalama wa watu na mali zao; na
- c) Serikali kupitia TCRA ikabiliane na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano na changamoto zake kama vile uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA iendelee kusaidia Jeshi la Polisi katika kutekeleza sheria ya Cyber Crime na kuwabana wahalifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF;

Kwa kuwa mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kupeleka mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibashara; na kwa kuwa Kamati bado hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa mawasiliano sehemu hizo; Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) Katika Bajeti ijayo ya mwaka 2017/2018, Serikali kuzingatia kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF, kwani ruzuku inayotolewa na Serikali ikitumika vizuri inaweza kusaidia zaidi kuliko kupewa Makampuni ambapo mwisho wa siku hawapeleki mawasiliano;
- b) Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA kuweka masharti ya kutoa leseni kwa Makampuni ya Simu pamoja na masharti mengine iwe kupeleka mawasiliano katika maeneo ya pembezoni kama mchango wa kijamii (Corporate Social Responsibility);
- c) Serikali kuja na mpango wa uwiano wa mawasiliano nchi nzima hasa maeneo ya mipakani ambapo mara nyingi watu katika maeneo hayo hupata mawasiliano ya nchi jirani jambo linalohatarisha usalama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta;

Kwa kuwa mradi huu unamanufaa makubwa kwani utawezesha kuwepo kwa utambulisho wa makazi ya watu na makampuni na hatimae kurahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa; na kwa kuwa kwa kuwa utekelezaji wa mradi huu umekuwa ukisuasua; hivyo basi, Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi mkubwa; na
- b) Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu zitolewe mapema kwani hadi kufikia mwezi Januari 2017 zimetolewa **asilimia 3.17** tu ya Fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kampuni ya Simu Tanzania- TTCL;

Kwa kuwa Serikali imekamilishaa malipo ya hisa ya **asilimia 35** zilizokuwa zinamilikiwa na Bharti Airtel katika TTCL; na kwa kuwa sasa Kampuni hii inamiliikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja (100%); Kamati inashauri TTCL kuhakikisha inaboresha makusanyo ya mapato na madeni yanayotokana na huduma za simu ambayo kwa kiasi kikubwa wateja wanaodaiwa ni Serikali na taasisi zake;

Aidha, Kamati inashauri Kampuni hii ipate dhamana ya mikopo na kuweza kujijimarisha na kuongeza ufanisi

SEHEMU YA NNE

HITIMISHO

Mh.Spika, Miundombinu ikiwa ni pamoja na Reli, Barabara, Viwanja vya Ndege, Bandari na Mawasiliano ni nguzo ya Taifa lolote na kwa kweli ndiyo vichochezi vya maendeleo ya sekta zingine. Hivyo, ni lazima tutambue kuwa maendeleo ni vita na lazima tupange mipango yetu kama tungapavyo vita yoyote ile. Kosa moja lawezi kugharimu uchumi wan chi yetu. Lazima tuamue kwa usahihi na kwa muda muafaka ili kupata maendeleo.

Shukrani

Mheshimiwa spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe. Eng. Prof. Makame Mbarawa Mnyaa (Mb) akishirikiana na Naibu Waziri Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani (Mb), pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara hii Eng. Joseph Nyamuanga (Sekta ya Ujenzi); Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Sekta ya Uchukuzi), Eng. Dkt. Maria Sasabo (Sekta ya Mawasiliano); pamoja na Naibu Katibu Mkuu Ndg. Angelina Madete. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. Ni kwa ushauri na utadalim wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, vile vile nachukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashillilah kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani ziwaendee makatibu wa Kamati hii Ndugu Hosiana John na Ndugu Richard Masuke pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Catherine Kitutu kwa kuihudumia Kamati muda wote. Nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao wa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza Shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo, sasa naomba kutoa Hoja kwamba Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017 pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja.

.....
Prof. Norman Adamson Sigalla King, Mb

Mwenyekiti

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu

07 Februari, 2017

KIAMBATISHO NAMBA 1:

SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 2016 HADI JANUARI 2017

	Kipindi cha Utekelezaji	Shughuli zilizofanyika	Dhumuni
1.	08-12, Februari 2016	Mafunzo (<i>Training</i>) kwa Wajumbe wa Kamati	Kuwajenglea uwezo wajumbe (<i>Capacity Building</i>) katika maeneo wanayoyafanyia kazi hasa kuhusu Muundo, Majukumu, Sera na Sheria za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano
2.	13 Machi - 24 Aprili 2016	<p>a) Vikao na Taasisi/Mashirika yaliyo chini ya Wizara;</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Wakala wa Barabara Tanzania – TANROADS; ii. Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA; iii. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA; na iv. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA. <p>b) Ziara Taasisi/Mashirika yaliyochini ya Wizara</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Ziara eneo la Soga-Kibaha liliojengwa (1.5 km za reli ya standard gauge); ii. Karakana ya Vichwa vya Treni Morogoro na Ofisi za Railway Dodoma; iii. Kiwanja cha Ndege cha Dodoma, Shinyanga na Mwanza; iv. Barabara ya Nzega-Tabora, v. Bandari ya Mwanza 	Kupokea taaarifa ya utendaji wa baadhi ya Taasisi/Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano
3.	29 Machi-05 Aprili 2016	Ziara za ukaguzi wa miradi ya Maendeleo:-	Kwa mujibu wa Kanuni ya {Kanuni ya 98 (1)}. Kutembelea miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka 2015/2016 ili kujiridhisha na utekelezaji uliofikiwa.
	08-15 Aprili 2016	Kupokea na kujadili taaarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2016/2017 <ul style="list-style-type: none"> i. Sekta ya Mawasiliano Fungu 68; ii. Sekta ya Ujenzi Fungu 98; na iii. Sekta ya Uchukuzi Fungu 62. 	Kupokea na kujadili taaarifa ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

	22 Agosti- 02 Septemba 2016	Vikao na Mashirika/Taasisi zifuatazo:- i. Shirika la Ndege la Tanzania-ATCL; ii. Tanzania Electrical Machechnical and Electronics Service Agency- TEMESA; iii. Kutembelea Kiwanja cha Ndege cha Dodoma; iv. Wakala wa Majengo Tanzania-TBA, Railway Holding Company (RAHCO); v. Tanzania Railway Limited (TRL); vi. Tanzania and Zambia Railway (TAZARA); vii. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA; viii. Kampuni ya Simu Tanzania- TTCL; na ix. Kilimanjaro Airport Development Company Limited- KADCO	Kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Mashirika/Taasisi ili kushauri ipasavyo
	17-30 Oktoba, 2016	Vikao na Mashirika/Taasisi zifuatazo:- i. Wakala wa Barabara (TANROADS); ii. Chuo cha Ujenzi Morogoro; iii. Chuo cha Matumizi Stahiki ya Nguvu Kazi Mbeya (Appropriate Technology Training Institute-ATTI); iv. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); v. Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (Universal Communication Service Access Fund - UCSAF); vi. Mamlaka ya Bandari Tanzania(TPA); vii. Marine Services Company Limited (MSCL); viii. Kampuni ya Meli ya Tanzania na China (SINOTASHIP); ix. Chuo cha Usafirishaji Tanzania(NIT); x. Chuo cha Bahari Dar es salaam (DMI); xi. Kampuni ya Ndege Tanzania-ATCL; xii. Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA); xiii. Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA); na xiv. Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (Surface and Marine Transport Regulatory Authority-(SUMATRA)	Kupokea na kujadili Taarifa ya Utendaji wa Mashirika/Taasisi ili kushauri ipasavyo
	10-14 Januari 2017	Ziara ya kutembelea Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia-Mbeya	Wajumbe kuona, kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa TAZARA
	17- 29 Januari 2017	Ziara kutembea Mashirika/ Taasisi zifuatazo:- i. Kiwanja cha Ndege cha Arusha , Moshi na Kilimanjaro (KIA); ii. Bandari ya Tanga iii. Eneo lilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mwambani-Tanga; iv. Eneo lilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mbegani- Bagamoyo; c) Vikao i. Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA (Bandari ya Dar es Salaam); ii. Kupokea taarifa ya utendaji wa Sekta ya Ujenzi na Sekta ya Mawasiliano; iii. Kupokea taarifa ya utendaji wa sekta ya Uchukuzi; iv. RAHCO- Railway Holding	Wajumbe kuona, kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Mashirika/Taasisi ili kushauri ipasavyo

		Company; v. Wakala wa Ndege za Serikali	
--	--	--------------------------------------------	--

**KIAMBATISHO NAMBA 2:
JEDWALI LA VIFUPISHO (ABBREVIATIONS)**

TAZARA	- Tanzania and Zambia Railway
SUMATRA	- Surface and Marine Transport Regulators Authority
TPA	- Tanzania Ports Authority
TMA	- Tanzania Meteorology Agency
TEMESA	- Tanzania Electrical Mechanical and Electronics Services Agency
TTCL	- Tanzania Telecommunication Company Limited
TCC	- Tanzania Communication Commission
UCSAF	- Universal Communication Services Access Fund
TBA	- Tanzania Building Agency
MSCL	- Marine Services Company Limited
DMI	- Dar es Salaam Maritime Institute
NIT	- National Institute of Transport
ATCL	- Air Tanzania Company Limited
TCAA	- Tanzania Civil Aviation Authority
IATA	- International Air Transport Association
SITA	- Societe Internationale Telecommunication Aeronautique
IOSA	- IATA Operation safety Audit
RAHCO	- Railway Assets Holding Company
TAAC	- Tanzania Airport Authority
KOJ	- Kurasini Oil Jet
TANROAD	- Tanzania Roads Agency
WIM	- Weigh in Motion Weighbridge
TCRA	- Tanzania Communication Regulatory Authority
TTMS	- Telecommunication Traffic Monitoring Systems
TRA	- Tanzania Revenue Authority
VAT	- Value added tax
GCLA	- Government Chemistry Laboratory Agency
TAMISEMI	- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na utaratibu mwingine unaofuata. Sasa tumsikie Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. (Makofi)

MHE. DOTO M. BITEKO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ni moja ya Kamati za Kisikta yenye majukumu mbalimbali yaliyoainishwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni ya 117.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, sitaweza kusoma taarifa yote. Hivyo naomba taarifa yote, pamoja na sehemu mbalimbali ambazo sitazisoma zichukuliwe na kuingizwa kwenye Hansard.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2016, Kamati imetekeleza majukumu mbalimbali ya kikanuni kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 7(1), Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo 2016 la Januari. Pamoja na majukumu mengine, Kamati imetekeleza majukumu ya msingi yafuatayo:-

Kwanza, kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini; pili, kushughulikia taarifa za mwaka za utendaji wa Wizara ya Nishati na Madini; kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia mbalimbali zimetumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Katika kutekeleza majukumu ya Kamati, Kamati yako ilitumia njia mbalimbali ili kufanikisha majukumu yake ya ukaguzi wa miradi, kupokea taarifa mbalimbali, majadiliano na Wizara pamoja na taasisi zake. Mafunzo na semina zilifanikisha Kamati hii kufikia malengo yake kama ilivyokuwa imepangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitekeleza matakwa ya Kanuni ya 98 ya Kanuni za kudumu za Bunge kwa kufanya ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali iliyotekelawa na Wizara ya Nishati na Madini. Ziara hizo zilifanywa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Manyara, Njombe na Mbeya kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo chini ya Wizara ya Nishati na Madini na miradi hiyo ambayo ilikuwa imetengewa fedha kwenye Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi iliyokaguliwa na Kamati yako ni pamoja na Mradi wa Uzalishaji Umeme wa Kinyerezi One (I) wenye kuzalisha umeme wa Megawatt 150; mradi wa bomba la gesi wa Mtwara; Mradi wa Makambako/Songea Transmission Line ya Kilovoti 220; miradi ya umeme vijiji (REA) katika Mkoa wa Njombe; mgodi wa makaa ya mawe wa Kiwira na mgodi wa Tanzanite One ulioko Mererani huko Mkoani Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukaguzi uliofanywa na Kamati yako, zilibainika changamoto mbalimbali zinazochangia kuzorota kwa utekelezaji wa miradi katika maeneo mbalimbali hasa yaliyokaguliwa na Kamati. Pamoja na Wizara ya Nishati na Madini kutengewa fedha za kutosha kila mwaka kwenye miradi ya maendeleo, Kamati imekuwa ikisikitishwa na upelekaji hafifu wa fedha hizo, hasa kwenye miradi ya REA ambayo fedha zake ni rahisi kukusanya na zina wigo wa kisheria (*Ring fenced*).

Mheshimiwa Naibu Spika, toka kuanzishwa kwa Mfuko wa Umeme Vijiji mwaka 2013 hadi Desemba, 2016 Mfuko ulikuwa umepaswa kupokea shilingi bilioni 749 ambazo ni makusanyo ya tozo za mafuta yaliyoingia nchini, lakini katika kipindi hicho cha kuanzia 2013 mpaka 2016 Mfuko wa REA umepokea shilingi bilioni 630.99. Bakaa ya jumla ya shilingi bilioni 105.67 hazijapelekwa kwenye Mfuko wa REA hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo hiki cha kutokupeleka fedha za REA zinazotokana na tozo mbalimbali za mafuta kwa wananchi, kinaleta hisia kwa Kamati na Bunge lako kwamba, Serikali hajaona umuhimu wa kutosha wa kupeleka fedha hizi kwa wakati ili kuisaidia miradi hii iweze kutekelezwa kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miradi iliyokaguliwa na Kamati yako, Kamati ilikutana na changamoto kubwa ya usimamizi mbovu na usioridhisha katika Miradi ya REA na kusababisha miradi hiyo kutekelezwa chini ya kiwango. Mifano iko mingi katika Mkoa wa Njombe ambako Kamati ilienda na kukuta baadhi ya transformer nyingi zilizokuwa zimelewewa zimeshaharibika tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasikitishwa na usimamizi mdogo wa Mgodi wa Tanzanite One, mgodi ambao umekuwa hauna tija iliyokusudiwa na Taifa kupitia madini haya adhimu yanayopatikana Tanzania pekee. Miogoni mwa mambo yaliyochangia usimamizi usioridhisha ni pamoja na mgogoro wa muda mrefu wa wachimbaji wadogo na Mwekezaji wa

Tanzanite One, utoroshwaji wa madini ya Tanzanite nje ya nchi pamoja na usimamizi mbovu wa mgodi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali zilizofanywa kwenye Mgodi wa Tanzanite kama vile ukaguzi maalum na kuanzishwa kwa mnada wa madini ya vito, Kamati imebaini kuwa madini haya yanayouzwa kwenye mnada huo na kusafirishwa nje ya nchi yanakuwa ni ghafi kinyume na matakwa ya Sheria ya Madini ya 2010. Hivyo Kamati yako inaitaka Wizara kuhakikisha Sheria, Kanuni zinazingatiwa katika uendeshaji wa minada hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Januari, 2017, Kamati iliweza kutembelea Mgodi wa Stamigold kwa nia ya kujionea uendeshaji wa mgodi huo unaomilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Katika ziara hiyo, Kamati imebaini changamoto kubwa zinazokwamisha utendaji na uzalishaji katika mgodi huo. Moja ya changamoto hizo ni mgodi kukosa fedha na mtaji wa kuendeshea shughuli zake. Pili, ukosefu wa mitambo ya kufanya kazi na hivyo kusababisha mgodi huu kukodi mitambo ya kufanya kazi.

Tatu, kukosekana kwa msamaha wa kodi kwenye vifaa na hasa mafuta yanayotumika kama ilivyo kwenye migodi mingine. Nne, kutokuwa na Mining Development Agreement(MDA) kama migodi mingi hapa nchini. Mgodi kushindwa kukopesheka kwa sababu ya kutokuwa na mali (Assets) za Mgodi na tano, Sheria ya Manunuzi inakwamisha ununuvi wa vipuri na hivyo kufanya ununuaji wa mitambo kuchukua muda mrefu zaidi. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kwamba changamoto hizo zinapatiwa ufumbuzi wa haraka ili kusaidia mgodi huo uweze kuijendesha vizuri na kutengeneza faida iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini ya Kamati kuwa, mashapo yaliyopo katika mgodi huo yakisimamiwa vizuri na Serikali yataongeza mapato ya nchi pamoja na sifa kwa nchi yetu kuwa Watanzania wanaweza kuendesha migodi yao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati ilitembelea mgodi wa Buzwagi unaomilikiwa na kampuni ya ACACIA kwa lengo la kujionea utekelezaji na usimamizi wa shughuli zake katika mpango wa maandalizi ya kufunga shughuli za uchimbaji katika mgodi huo. Mgodi huo unatarajia kufunga shughuli za uchimbaji ifikapo Desemba, 2017 kutokana na kiwango kidogo cha upatikanaji wa dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na mgodi katika maandalizi hayo ya ufungaji wa shughuli zake, Kamati haikuridhishwa na maandalizi hayo kwa kuwa hayakubainisha ni lini hasa mgodi huo utakamilisha taratibu mbalimbali zinazotakiwa kufuatwa ili kuhitimisha shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio ya Kamati kuwa Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, itahakikisha kuwa mgodi huu unakamilisha shughuli zake na taratibu zote za Kisheria na za Kikanuni, kama vile kulipa kodi mbalimbali za Serikali na za Halmashauri husika ili kuepusha usumbu uliojitekeza katika Mgodi wa Resolute uliofunga shughuli zake za uchimbaji huko Nzega, Mkoani Tabora na kuacha madeni mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati vilevile ilipata semina mbalimbali katika kuendelea kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati. Ofisi ya Bunge iliandaa mafunzo ya siku moja kupitia Mradi wa UNDP kuhusu masuala ya Kutunga Sheria na Kanuni mbalimbali. Pia, Wizara ya Nishati na Madini iliomba kuwapatia Wajumbe wa Kamati Semina ya siku moja kuhusu miradi kabambe inayotekeliza na inayoendelea kutekeliza kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Lengo la mafunzo hayo ya Wizara ilikuwa ni kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati kuifahamu vema miradi kabambe pamoja na ile ya kimkakati inayotekeliza na Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi isiyokuwa ya Kiserikali ya Natural Resource Government Institute(NRGII) imekuwa msaada mkubwa kwa Kamati kwa kuandaa semina mbalimbali za kuwajengeta uwezo Wajumbe wa Kamati katika sekta hizi muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Nishati na Madini katika kipindi cha mwaka mzima imetekeleza majukumu yafuatayo:-

Kwanza, kupokea taarifa ya nusu ya mwaka ya upatikanaji wa fedha; pili, kupokea na kujadili taarifa za utendaji wa taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Madini; tatu, ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2015/2017 na kupokea na kuchambua utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya 2015/2016 pamoja na uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kurejea Hati Ihini ya Serikali Namba 144 ya tarehe 22 Aprili, 2016. Lengo lilikuwa ni kuoanisha bajeti iliyotengwa, iliyopelekwa na matokeo ya utekelezaji wa bajeti na matarajio ya wananchi kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujiridhisha na utekelezaji wa Bajeti, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Wizara kwa nusu ya mwaka hadi Desemba, 2016 na kubaini kuwa hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2016, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 291.3 sawa na 25.95% ya bajeti yote iliyotengwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka 2016/2017. Shilingi bilioni 267.53 sawa na 36.9% ni fedha za miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 11 sawa na 28.3% ni fedha za matumizi mengine. Tafsiri ya upatikanaji wa fedha hizi kwa kiwango hiki unatishia kwa hali ya juu utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia utendaji wa Wizara, Kamati iliweza kupokea taarifa mbalimbali zinazohusu Sekta ya Nishati na Madini pamoja na sekta ndogo ya mafuta. Katika kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Kamati ilikutana na wadau mbalimbali wa sekta ndogo ya mafuta na kupokea taarifa kutoka Wizara ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, taasisi zifuatazo ziliwasilisha taarifa kwa Kamati na kujadiliwa:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Nishati Vijiji /Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wakala wa Umeme Vijiji REA), kuhusu utekelezaji wa miradi ya Awamu ya Pili na kuanzishwa kwa mradi wa Awamu ya Tatu kwa kubaini changamoto kadhaa ambazo zimekuwa kikwazo katika utendaji wa kazi wa Wakala huu. Changamoto hizo ni pamoja na ucheleweshwaji wa upelekaji wa fedha usioridhisha wa miradi, kwa REA umekuwa kikwazo kikubwa katika utendaji kazi.

Pili, kuongezeka kwa ghamama za utekelezaji wa miradi na kushindwa kulipa wakandarasi kwa wakati. Tatu, usimamizi usioridhisha wa wakandarasi wanaotekeleza miradi hiyo katika maeneo mbalimbali nchini. Nne, ushirikishwaji mdogo wa viongozi katika maeneo ya miradi hasa wakati wa uainishaji wa vijiji na vitongoji umesababisha vijiji vingi kurukwa na zoezi la uunganishaji wa umeme vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utendaji wa Shirika la Umeme (TANESCO), lenye jukumu la kuzalisha, kufua na kusafirisha na kusambaza umeme. Katika taarifa hiyo Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

(a) Shirika linadaiwa jumla ya shilingi bilioni 822. Deni hili linasababisha kuzorota kwa utendaji wa shirika;

(b) Wateja wengi wa TANESCO zikiwemo Wizara na Taasisi nyingi za Serikali kutokulipa ankara zao kwa wakati. Kwa mfano, Serikali peke yake, inadaiwa na TANESCO jumla ya shilingi bilioni 269 ambazo zimekuwa zikilipwa kidogo kidogo na hivyo kukwamisha shughuli za TANESCO;

(c) Uharibifu wa Mitambo ya Kufua Umeme inayosababisha mitambo hiyo kuzimwa kwa muda mrefu, kunaleta gharama kubwa kwa shirika katika uzalishaji wa umeme;

(d) Ukosefu wa umeme wa kutosha unaotokana na kushindwa kuwekeza katika mitambo ya kuzalisha umeme kwa muda mrefu licha ya ukuaji wa mahitaji ya umeme nchini; na

(e) Uchakavu wa miundombinu unaosababisha umeme mwangi kupotea njiani na hivyo kupunguza kiwango cha umeme kinachowafikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC); Kamati pia ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa shirika hili. Pamoja na mafanikio yaliyopo hasa kutosha na kugundulika kwa gesi nchini, bado manufaa yake kwa wananchi hayajaonekana kwa kiasi cha kuridhisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- (i) Ukosefu wa soko la uhakika na la kuaminika la gesi inayozalishwa nchini;
- (ii) Bajeti ndogo inayotengwa kwa Shirika inapelekea shirika kushindwa kutekeleza majukumu yake muhimu kwa Taifa hasa ya uwekezaji na utafiti wa gesi na mafuta nchini; na
- (iii) Serikali kutokupeleka fedha za miradi kwa wakati, kunasababisha miradi hiyo kutotekelezeka. Kwa mfano, mradi wa kusambaza gesi katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika hili linawadai wateja wake wakubwa jumla ya shilingi bilioni 307.47 ambazo mpaka sasa hazijalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Chuo cha Madini Dodoma na kubaini changamoto mbalimbali zikiwemo bajeti ndogo ambayo imetengwa, vile vile idadi ndogo ya madarasa ya kufundishia, uhaba wa wakufunzi katika fani ya Jiolojia, Uhandisi wa Migodi, Fizikia na Kompyuta. Hakuna sehemu ya kutosha wanafunzi wao kupata maeneo ya kufanya mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa majukumu yanayotekelawa na Wakala wa Jiolojia ambayo ni kukusanya, kuchambua, kutafsiri, kutunza takwimu na taarifa mbalimbali za kijiolojia, kutengeneza na kusambaza ramani, takwimu na taarifa mbalimbali zinazoainisha kuwepo kwa aina mbalimbali za miamba nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala hufanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli mbalimbali za miamba, madini, maji, mimea na udongo kwa ajili ya tafiti mbalimbali nchini na kuratibu utokeaji wa majanga kama vile matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano, maporomoko ya ardhi, mionzi ya asili na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majukumu haya mazito waliyonayo GST, changamoto zifuatazo ni kikwazo katika utekelezaji wa majukumu yao:-

- (i) Ukosefu wa watumishi wa kutosha;
- (ii) Uhaba wa vifaa maalum vyta kisayansi vyta kufanya kazi; na
- (iii) Ufinyu wa bajeti wanayotengewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Madini la STAMICO nalo kama yalivyo mashirika mengine linakabiliwa na changamoto mbalimbali. Pamoja na kazi nzuri inazofanya, shirika limetengewa na kuidhinishiwa na Bunge lako jumla ya shilingi bilioni 6.8. Hadi kufika Desemba, 2016 shirika lilipokea jumla ya shilingi bilioni 1.34 sawa na asilimia 20 ya bajeti iliyoidhinishwa, ambapo mishahara ni asilimia 16 na matumizi mengineyo ni 4% ya bajeti hiyo. Kamati haioni dhamira ya dhati ya Serikali ya kuendeleza Shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika limekwama kwa kiasi kikubwa kutekeleza majukumu ya msingi kuendeleza Sekta ya Madini kutokana na changamoto zifuatavyo:-

- (ii) Miradi mingi walijowekeza hadi sasa hawajaanza kupata faida ya mgodi. Kwa mfano, Mgodi wa Tanzanite One, Stamigold/Tulawaka, Kiwira na migodi mingine;
- (iii) Shirika limekabidhiwa majukumu mengi pamoja na bajeti ndogo inayoidhinishwa kwake; na
- (iv) Ukosefu wa Mikataba katika migodi ya Stamigold na Kiwira kunapelekea migodi hii kushindwa kukopesheka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na Wizara pamoja na wadau wa Sekta Ndogo ya Mafuta nchini, katika mfumo mzima wa uingizaji wa mafuta pamoja na maendeleo ya sekta hiyo. Katika taarifa hizo Kamati ilipata uelewa wa hali ya upatikanaji wa mafuta nchini pamoja na changamoto zinazoikibili sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio ya Serikali ya kuanzisha Wakala wa Uingizaji wa Mafuta kwa Pamoja nchini, Sekta hii ndogo inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- (i) Ukosefu wa matanki makubwa ya kuhifadhia mafuta (*Farm Tanks*). Baada ya kupakuliwa kutoka melini kunasababisha hasara kwa Makampuni yanayoingiza mafuta pamoja na kuikosesha Serikali mapato;
- (ii) Usalama mdogo wa mabomba yanayotumika kupakulia na kusambazia mafuta hasa yale ya KOJ-1 na hivyo kusababisha Makampuni yanayoagiza mafuta yatumie gharama kubwa kwa ajili ya ulinzi;
- (iii) Gharama kubwa ya uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta na yenye ni changamoto kubwa inayolalamikiwa na wadau wa mafuta;
- (iv) Tozo za Taasisi mbalimbali za Serikali kwenye bei ya mafuta zimekuwa nyngi mno na kuwa mzigo kwa wafanyabiashara wa sekta ya mafuta; na

(v) Bei elekezi ya mafuta haizingatii maeneo yaliyo mbali na Miji/Makao Makuu ya Wilaya na hivyo kusababisha wananchi waliopo katika maeneo hayo kupata bei ya nishati ikiwa juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa matanki ya kuhifadhiha mafuta (*Farm Tanks*) ni changamoto kubwa ambapo Serikali inatakiwa kuchukua hatua madhubuti ili kuokoa mapato ya Serikali yanayopotea kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sekta hii imekuwa ikilalamikiwa sana na wananchi wengi hasa wanaoishi maeneo ya migodi kuwa ni sekta ambayo haitoi mchango mkubwa katika pato la Taifa kama ilivyo katika nchi nyingine zenyne rasilimali hii; na kwa kuwa madini ni rasilimali inayokwisha, ni vyema Serikali ikaweka mkazo katika kusimamia sekta hii kwa kuziwezesha taasisi zinazosimamia upatikanaji na udhibiti wa mapato yatokanayo na madini kwa kuzitengea bajeti ya kutosha na kuzipelekea fedha hizo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji ruzuku kwa wachimbaji wadogo ni jambo zuri sana, lakini kuisaidia sekta hii, hasa kuwasaidia wachimbaji wadogo, Kamati haijaona manufaa ya moja kwa moja ya ruzuku hii kwa wachimbaji wadogo, kwa sababu ni hofu ya Kamati kuwa fedha hizi za ruzuku zisiposimamiwa vyema, hazitaweza kuleta tija na kukidhi lengo la kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe kuwa wachimbaji wadogo wadogo pamoja na wananchi waliopisha wawekezaji wanalipwa fidia stahiki na kutengewa maeneo mengine ya kuendeleza shughuli zao za uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa jitihada zake za makusudi ilizochukua kuokoa wachimbaji wadogo 15 waliokuwa wamefukiwa na kifusi katika mgodi mdogo wa Nyarugusu. Kamati inaomba ipongeze sana uongozi wa Mkoa wa Geita, Naibu Waziri wa Nishati na Madini na Mbunge wa Jimbo la Busanda, Mheshimiwa Bukwimba kwa juhudui zao walizozitoa wakati wa kuokoa ndugu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji umeme nchini imeendelea kuimarika katika maeneo mengi hususan Vijiijini. Mafanikio haya yametokana na ukamilishwaji wa miradi mingi ya REA ya Awamu ya Pili. Kwa sasa nchi yetu ina uwezo wa kuzalisha Megawatt 1,300 na matumizi ya juu kabisa ya umeme kwa nchi yetu yanafikia Megawatt 1,041. Matumizi haya yakadiriwa kuongezeka siku hadi siku kutokana na mahitaji ya nishati hii kukua kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji haya ya umeme yanapaswa kabisa kuendana na kasi ya ukamilishaji wa miradi mingi ya umeme inayotekelizwa hapa nchini. Kamati inaishauri na kuitaka Serikali kupeleka fedha za miradi yote ya umeme ili iweze kukamilika kwa wakati ili tuweze kufikia lengo tulilojiwekea la kufikia Megawatt 5000 ifikapo 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ili iweze kuwa nchi ya viwanda na baadaye kuwa nchi ya uchumi wa kati, ni lazima kuwe na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata fursa ya kuchambua utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2015/2016 pamoja na kuichambua bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2015/2016, miradi mingi ya umeme hasa ya REA imeshindwa kukamilika kwa wakati kwa sababu ya ukosefu wa fedha na usimamizi usioridhisha wa miradi hiyo iliyosababisha kutekelezwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa kwenye taarifa ya Kamati Bungeni hapa, mnamo tarehe 19 Mei, 2016, tunaipongeza Serikali kwa kutenga bajeti ya kutosha katika miradi ya maendeleo hususan miradi ya umeme itakayosaidia wananchi kupata umeme wa uhakika katika maeneo mengi ya nchi na kupelekea uchumi wa viwanda kutekelezeka kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, ni ushauri wa Kamati kuwa bajeti iliyotengwa ya miradi ya maendeleo itolewe yote na kwa wakati na kwa muda na usimamizi wa fedha hizo uwe mzuri ili uweze kuleta tija. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kufanya kazi maoni ya Kamati na ushauri kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea taarifa mbalimbali za Wizara na kukagua miradi mbalimbali, Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

- (i) Kutokupatikana kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na Kamati kuitisha bajeti ya kutosha kila mwaka;
- (ii) Kukosekana kwa bei elekezi ya mafuta kwenye maeneo yaliyo mbali na miji na hasa Makao Makuu ya Wilaya, kunasababisha changamoto ya kuwa na bei kubwa kwa wananchi wa maeneo hayo;
- (iii) Kuwepo kwa tozo nyingi za taasisi za Serikali kwenye bei ya mafuta, kunamwongezea mzigo mwananchi;
- (iv) Kutopatikana kwa fedha za miradi ya REA kwa wakati, kunasababisha kuongezeka kwa gharama na muda wa ukamilishaji wa miradi hiyo;
- (v) Upungufu wa gati za kupakulia mafuta kunasababisha msongamano wa meli wakati wa kupakua mafuta, hivyo kufanya nchi jirani zishindwe kuitisha mafuta katika bandari zetu;
- (vi) Ukosefu wa matenki ya kuhifadhia mafuta (*Central Storage Facility*), baada ya kupokea na kabla ya kusambaza kwenye depot za waagizaji wengine, kunasababisha hasara kwa Serikali kwani inakosa takwimu sahihi za mafuta yanayoingia nchini;
- (vii) Utaratibu wa kununua na kufungwa kwa *Flow Meters* kwenye meli badala ya kwenye matanki ya kuhifadhia mafuta siyo sahihi kwa ajili ya kupata takwimu sahihi za mafuta yanayoingia nchini;
- (viii) Ukosefu wa fedha na bajeti ndogo inayotengwa na Serikali kwa taasisi ya TMAA, inaathiri utekelezaji wa majukumu ya kukagua madini nchini;
- (ix) Serikali haina budi kuwekeza kwa wachimbaji wa kati na wadogo ili waweze kuendeleza sekta hii kwa uchumi wa Taifa letu;
- (x) Ili kuwa na uwazi katika tasnia ya uzinduaji, ni vyema Serikali ikaiwezesha taasisi ya *TEITI* iweze kutekeleza majukumu yake kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapendekeza kwamba kutokupatikana kwa fedha za REA, jambo hili Serikali iliangular kwa uharaka zaidi kwa sababu miradi mingi inasimama mpaka tunaingia awamu nyingine wakati fedha nyingi hazijatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, KWA KUWA TPDC inao uwezo wa kuzalisha gesi nyingi zaidi ya soko lililopo sasa na kwamba haina uwezo wa kujenga miundombinu ya kusambazia gesi ili kuwafikia watumiaji wengi sokoni;

NA KWA KUWA, hali hiyo inasababisha TPDC kuendelea kuwa na gesi isiyonunuliwa na kukosa pesa ambazo ingezipata kwa kuuza gesi ya ziada, jambo linalochangia kuifanya TPDC kushindwa kuijendesha kibiashara kama ilivyo;

HIVYO BASI, Bunge liishauri Serikali kuwezesha utekelezaji wa mradi wa kusambaza gesi katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwekeza katika miundombinu ya kusambazia gesi kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, KWA KUWA Chuo cha Madini Dodoma ndiyo Chuo pekee kinachotoa mafunzo ya mafundi mchundo na mafundi sanifu katika Sekta ya Madini, nchini lakini kinakabiliwa na ufinyu wa bajeti na kuchelewa kupata fedha;

NA KWA KUWA, hali hiyo inasababisha chuo hicho kushindwa kudahili wanafunzi wa kutosha kutokana na kushindwa kuajiri Walimu wa kutosha;

HIVYO BASI, Bunge liliishauri Serikali kukiwezesha chuo hiki kiweze kupatiwa fedha za kutosha. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, KWA KUWA Wakala wa Jiolojia wanapewa jukumu muhimu la kukusanya, kuchambua, kutafsiri na kutunza taarifa mbalimbali za kijiolojia, kwa lengo la kuliwezesha Taifa kufanya maamuzi sahihi kuhusu matumizi ya nishati,

NA KWA KUWA, kutokuwezeshwa kibajeti kwa taasisi hiyo kunachangia utekelezaji hafifu wa majukumu yake;

HIVYO BASI, Bunge liishauri Serikali kuwezesha Wakala wa Jiolojia nchini kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake ikiwemo kufanya tafiti mbalimbali kuhusu majanga na mitetemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, KWA KUWA, matenki ya kuhifadhiya mafuta (*FarmTanks*) ni muhimu kwa ajili ya kuiwezesha Serikali kudhibiti hujuma za wafanyabiashara ya mafuta nchini;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa matenki hayo kunasababisha upotevu wa kitakwimu na mapato kwa Serikali;

HIVYO BASI, Bunge liishauri Serikali kuiwezesha TPDC kuwekeza katika ujenzi wa matenki hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Spika wa Bunge, Mheshimiwa Job Ndugai Spika, Naibu Spika, Dkt. Tulia Ackson na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wenu kwa Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao walioutoa katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile niipongeze Wizara ya Nishati na Madini chini ya uongozi wa Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake

Dkt. Medard Matogolo Kalemani na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao walioutoa katika kipindi hiki ambao umeiwezesha Kamati yako kutekeleza majukumu yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashilillah kwa ushirikiano wake kwa Kamati yetu na pia kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Mwanahamisi Mkunda na Ndugu Felister Mgonja pamoja na Msaidizi wa Kamati, Ndugu Kokuwaisa Gondwe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana.

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI
ZILIZOTEKELEZWA KATIKA KIPINDI CHA KUANZIAJANUARI, 2016 HADI JANUARI, 2017
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ni moja ya Kamati ya kiseka yenye majukumu mbalimbali yaliyoanishwa kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Bunge. Kwa mujibu wa kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Nishati na Madini inawajibu wa kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Mwaka kuhusu utekelezaji wamajukumu yake katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, sitoweza kusoma taarifa yote. Hivyo naomba taarifa yote, pamoja na sehemu ambazo sitozisoma ichukuliwe kwenye Hansard.

1.1 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Disemba, 2016, Kamati imetekeleza majukumu mbalimbali ya kikanunikama ilivyoanishwa katika Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Pamoja na majukumu mengine Kamati imetekeleza majukumu ya msingi yafuatayo:-

- a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini;
- b) Kushughulikia Taarifa za Mwaka za Utendaji wa Wizara ya Nishati na Madini pamoja; na
- c) Kufuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hiyo.

1.2 Njia zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yakekama yalivyoanishwa kwenye Kanuni hapo juu, Kamati ilitumia njia mbalimbali ili kufanikisha majukumu yake. Ukaguzi wa miradi, kupokea taarifa mbalimbali, majadiliano na Wizara pamoja na taasisi zake, mafunzo na semina zilifanikisha Kamati kufikia malengo yake ya utekelezaji wa majukumu yake ya Kikanuni.

1.2.1 Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2015/2016

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitekeleza matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016 kwa kufanya ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali inayotekelizwa na Wizara ya Nishati na Madini.

Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Manyara, Njombe na Mbeya kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo chini ya Wizara ya Nishati na Madini iliyotengewa fedha na kupelekewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Miradi iliyokaguliwana Kamati yako kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni kama ifuatavyo;

- i) Mradi wa Kuzalisha umeme wa Kinyerezi I MW 150,
- ii) Mradi wa Bomba la Gesi Mtwara,
- iii) Mradi wa Makambako/Songea Transmission line 220kv na
- iv) Miradi ya umeme vijiji (REA) katika mkoa wa Njombe.
- v) Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira
- vi) Mgodi wa Tanzanite One

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi uliofanywa na Kamati yako, zilibainika changamoto mbalimbali zinazochangia kuzorota kwa utekelezaji wa Miradi katika maeneo mbalimbali hasa yaliyokaguliwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na Wizara ya Nishati na Madini kutengewa Bajeti ya kutosha kila mwaka kwenye miradi ya maendeleo, Kamati imekuwa ikisikitishwa na upelekaji hafifu wa fedha hizo, hasa kwenye miradi ya REA ambayo fedha zake ni rahisi kukusanywa na zina wigo wa Kisheria yaani (Ring fenced).

Mheshimiwa Spika, Toka kuanza kwa Mfuko wa Umeme vijiji mwaka 2013 hadi Disemba, 2016 Mfuko ulipaswa kuwa umepokea jumla ya shilingi Bilioni 749 ambazo ni makusanyo ya tozo za Mafuta yaliyoingia nchini katika kipindi hicho pamoja na makusanyo yatokanayo na Customs processing Fee.

Aidha, katika kipindi hicho cha kuanzia mwaka 2013 hadi Disemba, 2016 Mfuko wa REA umepokea jumla ya Shilingi Bilioni 630. 99 na Bakaa ya jumla ya Shilingi Bilioni 105.67 hazijawapelekwa katika Mfuko hadi sasa, Hali hii inasababisha kurudisha nyuma kasi ya utekelezaji wa Miradi.

Mheshimiwa Spika, kitendo hiki cha Serikali kutopeleka fedha za REA zinazotokana natozo mbalimbali za Mafuta kwa Wananchi kinaleta hisia mbaya kwa Kamati na Bunge lako kwa jumla kuwa Serikali inashindwa kuheshimu utaratibu uliowekwa kisheria wa kuzilinda fedha hizi.

Mhesimiwa Spika, Upelekeaji wa fedha za Miradi ya REA usiyoridhisha kumesababisha miradi mingi kushindwa kukamilika kwa wakati.Pia kuchelewesha malipo kwa wakandarasi kuna sababisha kuongezeka kwa gharama za miradi hiyo kwa mwaka husika. Kielelezo namba moja na namba mbili kinatoa ufanuzi kuhusu mchanganuo wa upatikanaji wa fedha za Miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa kwa mwaka husika pamoja na ufanuzi wa upatikanaji huo kwa asilimia.

Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika kipindi cha miaka mitanokuanzia 2012/2013 hadi 2016/2017

Mhesimiwa Spika, Katika miradi mingi iliyokaguliwa na Kamati yako, Kamati ilikutana na changamoto kubwa ya usimamizi mbovu na usiyo ridhisha hasa katika miradi ya REA nakupelekea miradi hiyo kutekelezwa chini ya kiwango katika maeneo mengi. Mfano miradi mingi ya REA katika mkoa wa njombe.

Aidha, mradi mingi ya sekta ya Madini iliyokaguliwa na Kamati yako ilikuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha za kuendeleza miradi hiyo kama vile Mgodi wa Makaa ya Mawe kiwira.

Mhesimiwa Spika, Kamati inasikitishwa nausimamizi mdogo na usiyoridhisha katika Mgodi wa Tanzanite One, mgodi ambaa umekuwa hauna tija iliyokusudiwa na Taifa kupitia madini haya adhimu yanayopatikana Tanzania peke yake. Miiongoni mwa mambo yanayochangia usimamizi usiyoridhisha ni pamoja na Migogoro ya muda mrefu ya wachimbaji wadogo wadogo na Mwekezaji wa Tanzanite One, Utoroshwaji wa Madini ya Tanzanite nje ya nchi pamoja na usimamizi mbovu wa Mgodi huo.

Mhesimiwa Spika, Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali kwenye Mgodi wa Tanzanite One kama vile ukaguzi maalumu na kuanzishwa kwa Mnada wa madini ya Vito, Kamati imebaini kuwa Madini haya yaliyouzwa kwenye mnada huo na kusafirishwa nje ya nchi yalikuwa ni ghafi kinyume na matakwa Sheria ya Madini 2010 pamoja nauamuzi wa Serikali wa kutokusafirisha madini hayo yakiwa ghafi.

Hivyo Kamati yako inaitaka Wizara kuhakikisha Sheria na kanuni zinazingatiwa katika uendeshaji wa Minada hiyo.

- Ziara ya Kamati katika Migodi ya Buzwagi na Stamigold/ Tulawaka katika kipindi cha Januari,2017

Mhesimiwa Spika, Katika kipindi cha Januari, 2017 Kamati iliweza kutembelea Mgodi wa Stamigold kwa nia ya kujionea uendeshaji wa Mgodi huo unaomilikiwa na Serikali kwa asilimia moja. Katika ziara hiyo Kamati imebaini changamoto kubwa zinazokwamisha utendaji na uzalishaji katika mgodi huo kama vile;

- a) Mgodi kukosafedha ya Mtaji wa kuendeshea shughuli za Mgodi;
- b) Ukosefu wa Mitambo ya kufanya kazi na hivyo kulazimika kukodisha kwa gharama ya juu;
- c) Kukosekana kwa misamaha ya kodi kwenye vifaa hasa mafuta yanayotumika kuendeshea shughuli za mgodi huo;

d) Mgodi kutokuwa na Mining Development Agreement MDA kama Migodi mingi hapa nchini;

e) Mgodi kushindwa kukopesheka kwa sababu ya kukosa umiliki halali wa Mali (Assets) za Mgodi; na

f) Sheria ya Manunuzi inakwamisha ununuzi wa vipuri kwa haraka kwa ajili ya matengenezo.

Aidha, kamati inaitaka Wizara kuhakikisha changamoto hizo zinapatiwa ufumbuzi wa haraka ili kusaidia mgodi huo kuweza kujiendesha vizuri na kutengeneza faida inayokusudiwa.

Mhesimiwa Spika, Ni matumaini ya Kamati kuwa, kwa mashapo yaliyopo katika Mgodi huo ukisimamiwa vizuri na Serikali itaongeza mapato ya nchi pamoja na sifa kwa nchi yetu kwa kuweza kuendesha mgodi wetu wenyewe bila kutegemea Wawekezaji kutoka nje.

Mhesimiwa Spika, Pia Kamati ilitembelea mgodi wa Buzwagi unaomilikiwa na kampuni ya ACACIA kwa lengo la kujionea utekelezaji na usimamizi wa sheria na kanuni katika Mpango wa maandalizi ya Kufunga Mgodi inavyotekelawa katika Mgodi huo.

Mhesimiwa Spika, Mgodi huo unatarajia ifikapo Disemba, 2017 itafunga shughuli za uchimbaji kutokana na kiwango kidogo cha upatikanaji wa dhahabu katika eneo hilo.

Mhesimiwa Spika, pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Mgodi katika maandalizi hayo ya ufungaji wa shughuli zake, Kamati haikuridhishwa na maandalizi hayo kwa kuwa hayakubainisha ni lini hasa Mgodi huo utakamilisha taratibu mbalimbali zinazotakiwa kufuatwa ili kuhitimisha shughuli zake.

Mhesimiwa Spika, ni matarajio ya kamati kuwa Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, itahakikisha kuwa Mgodi huu unakamilisha taratibu zote za Kisheria na za kikanuni, kama vile kulipa kodi mbalimbali za Serikali pamoja na za Halmashauri husika ili kuepuka usumbufu kama ulojitokeza katika Mgodi wa Resolute ulipofunga shughuli zake za uchimbaji huko Nzega mkoani Tabora.

1.3.1 Ziara za mafunzo

Mhesimiwa Spika, baadhi ya Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kusafiri kwenda nchini Bangladesh kwa ajili ya kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu sekta za Nishati Jadidifu (Renewable Energy). Lengo la ziara hii ilikuwa ni kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati katika masuala ya uzalishaji umeme unaotokana na vyanzo vingine ambavyo ni rahisi na vinapatikana katika mazingira yetu.

Mafunzo hayo yamekuza uelewa kwa Wajumbe kuhusu masuala ya Nishati Jadidifu na hivyo kuwasaidia kutoa ushauri kwa Wizara ya Nishati na Madini kuhusu uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo vingine kama upepo, jua pamoja na Tungamo Taka.

Mhesimiwa Spika, katika ziara hiyo Wajumbe walipata wasaa wa kukutana na viongozi mbalimbali wa Serikali kama Mshauri wa Waziri Mkuu katika masuala ya Nishati, ambaye aliwaeleza wajumbe kuwa kutokana na kuendelea kuharibika kwa mazingira, Bangladesh imejipanga kuhakikisha inatumia vyanzo vyta nishati ya umeme ambavyo ni rafiki kwa mazingira kama vile kuzalisha jua, tungamotaka na upepo.

1.3.2 Semina kwa Wajumbe wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Katika kuendelea kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati yako, Ofisi ya Bunge iliandaa mafunzo ya siku moja kupitia mradi wa UNDP (**Legislative Support Program**) kuhusu masuala ya kutunga Sheria pamoja na Kanuni mbalimbali.

Pia Wizara ya Nishati na Madini iliomba kuwapatia wajumbe wa Kamati Semina ya siku moja kuhusu Miradi kabambe itakayotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/17.

Lengo la mafunzo haya ya Wizara lilikuwa nikuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati kuifahamu vyema miradi Kabambe pamoja na ile ya kimkakati inayotekelawa na Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, Taasisi isiyo ya kiserikali ya *Natural Resource Government Institute* (NRGI) imekuwa msaada sana kwa Kamati hii kwa kuandaa Seminambalimbali za kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati katika sekta hizi muhimu za madini, mafuta na gesi.

Semina hizozimekuwa zikilenga kuwajengea uwezo wajumbe kuhusu Sheria mbalimbali zinazohusu udhibiti na ukusanyaji wa Mapato kutoka kwenye Sekta hizi kwa maendeleo ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kupitia mafunzo haya Kamati yako ya Nishati na Madini imekuwa na uelewa wa kuhusu sekta hizi muhimu inazosimamia kwa kuelewa vyema mambo muhimu ya kuzingatia kama Kamati wakati wa kutekeleza majukumu yake ya kushauri na kuisimamia Wizara ya Nishati na Madini.

2.0 KAZI MAHSUSI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Nishati na Madini katika kipindi cha mwaka mzimaimetekeliza majukumu yafuatavyo:-

i) Kupokea Taarifa ya nusu Mwaka ya upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016;

ii) Kupokea na kujadili taarifa za utendaji wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Madini

iii) Ukagazi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016; na

iv) Kupokea na Kuchambua utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 pamoja na uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017.

2.1 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Ujumla

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kurejea hati idhini ya Serikali namba 144 ya tarehe 22 Aprili, 2016 (Government instrument). Lengo lilikuwa ni kuoanisha bajeti inayotengwa, iliyopokelewa, matokeo ya utekelezaji wa bajeti na matarajio ya wananchi kwa Serikali yao.

Mhesimiwa Spika, ili kujiridhisha na utekelezaji wa Bajeti kamati ilipokea na kujadili taarifa ya upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha nusu mwaka (kuanzia Julai hadi Disemba 2016) na kubaini kuwa hadi kufikiatarehe 31 Desemba, 2016 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya bilioni 291.30, sawa na asilimia 25.95 ya Bajeti yote iliyotengwa na kuidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Mhesimiwa Spika, Shilingi bilioni 267.53 sawa na asilimia 36.90 ni fedha za miradi ya maendeleo na Shilingi Bilioni 11.0 sawa na asilimia 28.30 ni fedha za matumizi mengineyo. Tafsiri ya upatikanaji wa fedha kwa kiwango hiki unatishia utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi husika.

SEHEMU YA PILI

3.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI YA NISHATI NA MADINI

Mhesimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia utendaji wa Wizara, Kamati iliweza kupokea taarifa mbalimbali zinazohusu sekta ya Nishati, Madini pamoja na sekta ndogo ya Mafuta nchini.

Mhesimiwa Spika, Katika kufanya uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Kamati ilikutana na wadau mbalimbali wa sekta ndogo ya mafuta pamoja na kupokea taarifa kutoka Wizara ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, taasisi zifuatazo zilizowasilisha taarifa kwenya Kamati na kujadiliwa.

3.1 Wakala wa Nishati Vijijini (REA)

Mhesimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wakala wa Umeme vijijini kuhusu utekelezaji wa miradi ya umeme kwa awamu ya pili na uanzishwaji wa mradi wa awamu ya tatu na kubaini changamoto kadhaa ambazo zimekuwa kikwazo katika utendaji kazi wa Wakala huu. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

- a) Ucheleweshwaji na upelekaji wa fedha usioridhisha kwenye miradi ya REA umekuwa kikwazo kikubwa katika utekelezaji wa miradi hii muhimu kwa maendeleo ya taifa letu pamoja na fedha hizo kuwa nawigo wa kisheria;
- b) Kuongezeka kwa garama za utekelezaji wa Miradi kwa kushindwa kulipa Wakandarasi kwa wakati;
- c) Usimamizi usiyoridhisha kwa Wakandarasi wanaotekeleza Miradi hiyo katika maeneo mbalimbali nchini; na
- d) Ushirikishwaji mdogo wa Viongozi katika maeneo ya miradi hasa wakati wa uainishaji wa vijiji/vitongoji umesababisha vijiji vingi kurukwa katika zoezi hili la uunganishaji wa umeme.

3.2 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

Mhesimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utendaji kazi wa Shirika la umeme TANESCOlenye jukumu la kuzalisha /kufua, kusafirisha, kusambaza na kuuza umeme. Katika taarifa hiyo Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

- a) Shirika linadaiwa jumla ya Shilingi Bilioni 822, deni hili linasababisha kuzorota kwa utendaji wa Shirika;
- b) Wateja wengi zikiwemo Wizara na Taasisi nyingi za Serikali kutolipa ankara zao kwa wakati.Kwa mfano Serikali peke yake, inadaiwa na TANESCO zaidi ya shilingi bilioni 269 ambazo imekuwa ikilipa kidogo kidogo na hivyo kukwamisha shughuli za TANESCO kutekelezeka kwa wakati;
- c) Uharibifu wa Mitambo ya kufua umeme inayopelekea mitambo hiyo kuzimwa kwa muda mrefu, kuna ligharimu shirika na Taifa kwa ujumla kwa kukosekana kwa umeme wa uhakikatika maeneo mengi hapa nchini;
- d) Ukosefu wa umeme wa kutosha kunakotokana na Serikali kushindwa kuwekeza kwenye mitambo ya kuzalisha umeme kwa muda mrefu licha ya ukuaji wa mahitaji ya umeme nchini; na
- e) Uchakavu wa miundombinu unaosababisha umeme mwangi kupotea njiani na hivyo kupunguza kiwango cha umeme kinachowafikia wananchi.

3.3 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

Mhesimiwa Spika, Kamati pia ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini. Pamoja na mafanikio yaliyopo hasa kutokana na kugundulika kwa gesi nchini bado manufaa yake kwa wananchi hayajaonekana kwa kiasi cha kuridhisha.

Mhesimiwa Spika, katika kipindi hiki cha nusu mwaka hakuna fedha ye yeyote ya miradi ya maendeleo iliyotolewa na Serikali. Hivyo, miradi na tafiti nyingi zilizopangwa kufanyika katika kipindi hiki cha nusu mwaka hazijaweza kutekelezeka. Kamati inasikitishwa na hali hiyo kwa kuwa nia ya Shirika/ Kampuni hii kujienda kibaashara itashindikana.

Aidha, shirika linawadai wateja wake wakubwa jumla ya shilingi bilioni 307.47 kutolipwa kwa fedha hizi kwa wakati na kulifanya shirika kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na shirika hili katika ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vingine, bado linakabiliwa na changamoto zifuatazo;

- a) Ukosefu wa soko la uhakika na lakuaminika la gesi inayozalishwa nchini;
- b) Bajeti ndogo inayotengwa kwa Shirika inapelekea shirika kushindwa kutekeleza majukumu yake muhimu kwa Taifa hasa ya uwekezaji na utafiti wa gesi na mafuta nchini;
- c) Serikali kutokupeleka fedha za miradi kwa wakati kunasababisha miradi hiyokutokutekelezeka. Kwa mfano mradi wa kusambaza Gesi katika mkoa wa Dar Es Salaam.

3.4 Chuo cha Madini Dodoma

Sikazi wa Chuo cha Madini Dodoma ambacho kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo ya ufundi sanifu, ushauri na utafiti katika sekta ya madini.

Mhesimiwa Spika, Chuo hiki kimeendeleo kukabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha , hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2016 Chuo kilikuwa kimepokea jumla ya Shilingi Milioni 324.4 sawa ma asilimia 24.6 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2016/17. Utalawaji huu wa fedha hauridhishi kwani unakwamisha maendeleo ya chuo hiki muhimu kinachotusaidia Taifa kupata Mafundi sanifu na Mafundi Mchundo ambao ni muhimu sana kwa maendeleo ya sekta hii ya Madini.

Pamoja na mafanikio mbalimbali ambayo Kamati ilielezwa, changamoto kubwa zifuatazo zilibainika:-

- a) Bajeti ndogo inayotengewa inakwamisha utekelezaji wa majukumu;
- b) Idadi ndogo ya madarasa ya kufundishia;
- c) Uhaba wa wakufunzi hasa katika fani za jiolojia, uhandisi migodi, fizikia na kompyuta; na
- d) Hakuna sehemu za kutosha za wanafunzi wao kufanya mafunzo kwa vitendo.

3.5 Wakala wa Jiolojia nchini (GST)

Mhesimiwa Spika, Kamati ilielezwa majukumu yanayotekelawa na Wakala wa Jilolojia ambayo ni kukusanya, kuchambua, kutafsiri, kutunza takwimu na taarifa mbalimbali za kijiosayansi (jiolojia, Jiomeria na jiofizikia), kutengeneza na kusambaza ramani, takwimu na taarifa mbalimbali zinazoainisha kuweipo kwa aina mbalimba za miamba nchini.

Mhesimiwa Spika, Wakala hufanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli mbalimbali za miamba, madini, maji, mimea na udongo kwa ajili ya tafiti mbalimali nchini na kuratibu utokeaji wa majanga kama vile matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano, maporomoko ya ardhi, mionzi asili n.k.

Mhesimiwa Spika, pamoja na majukumu hayamazito waliyonayo GST changamoto zifuatazo zimekuwa kikwazo katika utekelezaji bora wa majukumu yake:-

- (i) Bajeti inayotengewa ni ndogo na haitolewi yote hususan ya miradi ya maendeleo, hivyo kushindwa kutekeleza Miradi kwa wakati;
- (ii) Uhaba wa Vifaa maalum vya kisayansi vya kufanya kazi; na
- (iii) Ukosefu wa watumishi wa kutosha.

3.6 Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

Mhesimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Stamico. Shirika hili la madini limepewa jukumu la kusimamia sekta ya madini kwa kufanya tafiti na uwekezaji katika migodi ya madini kama zilivyo kampuni zingine kwaniaba ya serikali.

Mhesimiwa Spika, Shirika hili lilitengewa na kuidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya Shilingi Bilioni 6.8, hadi kufikia Disemba, 2016 shirika ilipokea jumla ya shilingi Bilioni 1.34 sawa na asilimia 20 ya Bajeti iliyoidhinishwa, ambapo mishahara ni asilimia 16 na matumizi mengineyo ni asilimia 4 ya bajeti hiyo, Kamati haioni dhamira ya dhati ya Serikali ya kuendeleza Shirika hili.

Mhesimiwa Spika, Shirika limekwama kwa kiasi kikubwa kutekeleza majukumu ya msingi ya kuendeleza Sekta ya Madini kutokana na changamoto zifuatavyo:-

- a) Ukosefu wa Fedha unaosababisha kukwama kwa shughuli nyingi za shirika hilo. Aidha, ukosefu wa mtaji wa kuanzisha/ kuwekeza katika miradi mingine,
- b) Miradi mingi waliyowekeza hadi sasa hawajaanza kupata faida, kwa mfano Mgodi wa Tanzanite one, Stamigold/Tulawaka, Kiwira n.k;
- c) Pia shirika limekabidhiwa majukumu mengi pamoja na bajeti ndogo wanayopewa kwa mwaka.
- d) Ukosefu wa Mikataba katika migodi ya Stamigold na Kiwira kuna pelekea migodi hii kushindwa kukopesheka.

4.0 Sekta Ndogo ya Mafuta na hali ya upatikanaji wa Mafuta nchini

Mhesimiwa Spika, Kamati pia ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na Wizara pamoja na wadau wa Sekta ndogo ya mafuta nchini kuhusu mfumo mzima wa uingizaji wa mafuta pamoja na maendeleo ya sekta hiyo. Katika taarifa hizo Kamati ilipata uelewa wa hali ya upatikanaji wa mafuta nchini pamoja na changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

Mhesimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya Serikali ya kuanzisha Wakala wa uingizaji wa mafuta kwa Pamoja nchini, Sekta hii bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo;

- (i) Ukosefu wa Matanki makubwa ya kuhifadhia mafuta(FarmTanks) baada ya kupakuliwa kutoka Melinikunasababisha hasara kwa Makampuni yanayoingiza mafuta pamoja na kuikosesha Serikali mapato;
- (ii) Usalama mdogo wa mabomba yanayotumika kupakulia na kusambazia mafuta hasa ya KOJ-1, na hivyo kusababisha Makampuni yanayoagiza mafuta yatumie gharama kubwa kwa ajili ya ulinzi;
- (iii) Gharama kubwa ya uwekaji wa Vinasaba (Tsh. 12 kwa lita) ikilinganishwa na nchi jirani kama Kenya gharama ni Tsh. 1 kwa lita na Uganda Tsh. 2 kuna muongozea mzigo mwananchi.
- (iv) Tozo za Taasisi mbalimbali za Serikali kwenye bei ya Mafuta ni mzigokwa Wafanyabiashara wa Sekta ya mafuta;
- (v) Bei elekezi ya Mafuta haizingatii maeneo yaliyo mbali na Miji/Makao Makuu ya Wilaya na hivyo kusababisha wananchi waliopo katika maeneo hayo kupata nishati hii kwa bei ya juu sana.

Mhesimiwa Spika, Ukosefu wa Matanki ya kuhifadhia Mafuta yaani (Farm Tanks) ni changamoto kubwa ambayo Serikali inatakiwa kuchukua hatua za madhubuti ili kuokoa mapato ya Serikali yanayopotea kila siku kutoka katika Sekta hii. Aidha, kwa kuwa TPDC ina maeneo ambayo mradi huu unaweza kutekelezwa, ni vyema Serikaliikaiwezesha TPDC kuititia Kampuni tanzu ya COPEC kuwekeza katika ujenzi wa Matanki hayo.

4.1 Sekta ya Madini

Mhesimiwa Spika, Kwa kuwa sekta hii imekuwa ikilalamikiwa sana na Wananchi wengi hasa wanaishi maeneo ya migodi kuwa ni sekta ambayo haitoi mchango mkubwa katika pato la Taifa kama ilivyo katika nchi nyingine zenyenye Rasilimali hii.

Mhesimiwa Spika, Na kwa kuwa, Madini ni Rasilimali inayokwisha ni vyema Serikali ikaweka mkazo katika kusimamia sekta hii kwa kuziwezesha Taasisi zinazosimamia upatikanaji na udhibiti wa mapato yanatokanayo na madini kwa kuzitengea bajeti ya kutosha na kuzipelekea fedha hizo kwa wakati.

Mhesimiwa Spika, Utoaji ruzuku kwa wachimbaji wadogo ni jambo zuri sana katika kuisaidia Sekta hii, hasa kuwasaidia na kuwaendeleza wachimbaji wadogo hapa nchini. Aidha, ni hofu ya Kamati kuwa fedha hizi za ruzuku zisiposimamiwa vyema hazitaweza kuleta tija na kukidhi lengo la kuwasaidia wachimbaji wadogo nchini.

Mhesimiwa Spika, Serikali ihakikishe kuwa Wachimbaji wadogo wadogo pamoja na Wananchi waliopisha Wawekezaji wanalipwa fidia stahiki, na kutengewa maeneo mengine ya kuendeleza shughuli zao za uchimbaji.

Mhesimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa jitihada zake za maksudi walizochukua ili kuokoa maisha ya Wachimbaji wadogo wadogo 15 waliokuwa wamefukiwa na kifusi katika Mgodi mdogo wa Nyarugusu. Ni rai ya Kamti kuwa Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini waongeze jitihada ya kutoa Elimu kuhusu mbinu bora za uchimbaji wa Madini hasa kwa Wachimbaji wadogo wadogo katika nchi yetu. Aidha, elimu hii itasaidia kupunguza matukio ya aina hii kwa Wachimbaji wadogo wadogo.

4.2 Hali ya Upatikanaji wa Umeme nchini

Mhesimiwa Spika, Hali ya upatikanaji umeme nchini imeendelea kuimarika katika maeneo mengi hususani vijijini, mafanikio haya yametokana na ukamilishwaji wa miradi mingi ya REA awamu ya kwanza na awamu ya pili.

Kwa sasa nchi yetu inawezo wa kuzalisha MW 1300 na matumizi ya juu kabisa ya nchi yetu yameweza kufikia hadi MW 1041, matumizi haya yakadiriwa kuongezeka siku hadi siku kutokana mahitaji ya nishati hii kukua kwa kasi nchini.

Mhesimiwa Spika, mahitaji haya ya umeme yanapaswa kabisa kuendana na kasi ya ukamilishaji wa miradi mingi ya Umeme inayotekelawa hapa nchini, Kamati inaishauri na kuitaka Serikali kupeleka fedha katika miradi yote ya umeme ili iweze kukamilika kwa wakati na kufikia malengo ya wizara iliyojiwekea ya kufika MW 5000 ifikapo 2021.

Mhesimiwa Spika, iliNchi yetu iweze kuwa nchi ya Viwanda ni lazima miradi mingi ya umeme ipelekewe fedha kama ilivypangwa hasa kwa miradi ya REA inayotekelawa nchi nzima. Aidha, ukarabati na matengenezo ya Mitambo ya kufua umeme ni jambo la muhimu katika kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini.

4.3 Kuchambua utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na mchakato wa bajeti wa wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kuchambua utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka Fedha 2015/2016 pamoja na kuchambua Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 miradi mingi ya umeme hasa ya REA imeshindwa kukamilika kwa wakati kwa sababu ya ukosefu wa fedha na usimamizi mbovu wa miradi hiyo iliyosabisha miradi mingi kutekelezwa chini ya kiwango katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoelezwa kwenye taarifa ya Kamati ilivyowasilishwa Bungeni mnamo tarehe 19 Mei, 2016 tunaipongeza Serikali kwa kutenga bajeti ya kutosha katika miradi ya maendeleo hususani miradi ya umeme itakayosaidia wananchi kupata umeme wa uhakika katika maeneo mengi ya nchi na kupelekea uchumi wa viwanda kutekelezeka kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, Hivyo basi, ni ushauri wa kamati kuwa bajeti iliyotengwa ya miradi ya maendeleo itolewe yote na kwa wakati na kuwe na usimamizi mzuri wa fedha hizo ili ziweze kuleta tija.

Kamati inaendelea kusitiza Serikali kufanya kazi maoni na ushauri wa Kamati kwa manufaa ya Taifa.

SEHEMU YA TATU

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

5.1 Maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Baada ya kupokea taarifa mbalimbali za Wizara ya Nishati na Madini, ziara za ukaguzi wa miradi pamoja na kukutana na Wadau wa sekta zote mbili za Nishati na Madini, Kamati ina maoni yafuatayo;

- a) Kutopatikana kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na Kamati kuitisha bajeti ya kutosha kila mwaka;
- b) Kukosekana kwa bei elekezi ya Mafuta kwenye maeneo yaliyo mbali na Miji/Makao Makuu ya Wilaya kunasababisha changamoto kubwa kwa wananchi wa maeneo hayo;
- c) Kuwepo kwa tozo nyingi za taasisiza Serikali kwenye bei ya Mafuta ni kumuongezea mzigo mwananchi;
- d) Kutopatikana kwa fedha za miradi ya REA kwa wakati, kuna sababisha kuongezeka kwa gharama na muda wa ukamilishaji wa miradi hiyo;
- e) Upungufu wa Gati za kupakulia Mafuta kunasababisha msongamano wa Meli wakati wa kupakua mafuta, hivyo kufanya nchi jirani zishindwe kuitisha Mafuta katika Bandari zetu. Mfano; Meli moja inaweza kuchukua katika siku 4 – 8 kupakua mafuta;
- f) Ukosefuwa matanki ya kuhifadhia mafuta (Central Storage Facility) baada ya kupokea na kabla ya kusambaza kwenye depot za waagizaji wengine kunasababisha hasara kwa Serikali kwani inakosa takwimu sahihi za Mafuta yaliyoingia nchini;

g) Utaratibu unaotumika wa kufunga *Flow Meters* kwenye meli badala ya kwenye Matanki ya kuhifadhi mafuta siyo sahihi kwa ajili ya kupata takwimu sahihi za mafuta yanayoingia nchini;

h) Ukosefu wa fedha na bajeti ndogo inayotengwa na Serikali kwa taasisi ya TMAA, inaathiriutekelezaji wa majukumu muhimu ya taasisi hii;

i) Serikali haina budi kuwaendeleza Wachimbaji wa Kati na Wadogo wadogo ili waweze kuendeleza sekta hii kwa uchumi wa Taifa letu;

j) Ili kuwa na uwazi katika tasnia ya Uzinduaji ni vyema Serikali ikaiwezesha taasisi ya TEITI iweze kutekeleza majukumu yake ya msingi;

k) Serikali ifanye haraka kulipa Madeni ya Tanesco, ili kuipunguzia Shirika mzigo wa madeni hayo;

l) Bunge liongezewe Bajeti ya kutosha ili kuliwezesha kutekeleza makujuku yake ya kikatiba, hasa ya kufanya ukaguzi katika miradi mingi inayotekelawa na Serikali ili liweze kushauri ipasavyo.

5.2 Mapendekezo

Mhesimiwa Spika, baada kutekeleza shughuli zilizotekelawa na Kamati, naomba kutoa mapendekezo kama ifuatavyo:-

5.2.1 Wakala wa Nishati vijiji (REA)

a) Kutokupatikana kwa fedha za Miradi ya REA kwa wakati

Kwa kuwa, fedha za miradi ya REA zimekuwa zikichelewa kupelekwa na hupelekwa chini ya kiwango kilichokusanywa kutoka kwenye Tozo za Mafuta na hata zile zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu na kusababisha miradi mingi kushindwa kukamilika kwa wakati;

Na kwa kuwa, kuchelewa kukamilika kwa miradi hupelekwa Kuongezeka kwa gharama za Miradi husika kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo fidia kwa wakandarasi na kupanda kwa thamani ya dola hapa nchini;

Hivyo basi, Bunge lako liazimie kuwa fedha za miradi ya REA zipelekwe kwa wakati katika kutekeleza miradi hiyo kwa mwaka husika, ili kuipunguzia Serikali gharama ya kulipa fidia wakandarasi wanaocheleweshewa malipo yao.

b) Usimamizi wa Miradi ya REA

Kwa kuwa imebainika kuwa Miradi mingi ya REA iliyotekelawa katika awamu ya kwanza na ya pili haikuwa na usimamizi mzuri,

Na kwa kuwa, usimamizi duni wa miradi hiyo ulisababisha kushindwa kutimiza malengo ya miradi ikiwemo kutokuwa na mashine humba (Transformer) zinazofanya kazi vizuri kwa muda mrefu,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri serikali kuhakikisha kuwa iweke utaratibu madhubuti unaotekelozeka kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa miradi ya REA kwa namna inayowezesha ufanisi na tija.

c) Ushirkishwaji mdogo wa viongozi katika maeneo ya Miradi

Kwa kuwa, vijiji na vitongoji vingi katika maeneo ya utekelezaji wa Miradi ya REA awamu ya kwanza nay a pili, kutokana na kutokuwashirikisha viongozi wa maeneo husika,

Na kwa kuwa, hali hiyo inasababisha kutokufikiwa kwa malengo ya mradi na kusababisha kero kwa wananchi hasa kwenye maeneo yaliyorukwa,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liishauri Serikali kuhakikisha kuwa viongozi wa maeneo ambapo miradi ya REA inatekelezwa wanahusishwa ipasavyo, na hasa wakati wa kuainisha vijiji na vitongoji vitakavyohusika.

5.2.2 Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)

Mhesimiwa Spika, Kutokana na uchambuzi wa Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kuhusu TANESCO, Kamati ina mapendekezo matatu:

a) Wateja wengi kutolipa Ankara za umeme kwa wakati

Kwa kuwa, Taarifa za Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) zinaonesha kuwepo kwa wateja wengi wasiolipa Ankara za umeme inavyostahili na kukwamisha shughuli za Shirika hilo,

Na kwa kuwa, kutokufanyika kwa shughuli za TANESCO kutokana na kuchelewa kupata malipo ya wateja wake, kunazorotesha utendaji na uendeshaji wa TANESCO,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza kwamba Bunge, liitake TANESCO kuwachukulia hatuaza kisheria wateja wote wasiolipa Ankara kama inavyostahili.

b) Uharibifu wa Mitambo ya kufua umeme

Kwa kuwa, Mitambo mingi ya kufua umeme imekuwa ikiharibika na kushindwa kufanya kazi kutokana na kutokufanyiwa matengenezo kwa wakati,

Na kwa kuwa, kuharibika kwa mitambo hiyo mara kwa mara husababisha kukosekana kwa umeme wa uhakika nchini jambo linaloigharimu TANESCO na Taifa kwa ujumla,

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri kuwa Bunge liitake Serikali kuliwezesha Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania kumudu kufanya matengenezo ya mitambo ya kufua umeme ili kuliepusha Taifa na tatizo la kukosekana kwa Umeme wa uhakika.

c) Uchakavu wa miundombinu ya kusafirishia umeme

Kwa kuwa, imebainika kuwa uchakavu wa miundombinu ya kusafirishia umeme inasababisha kupotea kwa umeme mwingi njiani, jambo linaloathiri kiasi cha umeme kinachowafikia watumiaji,

Na kwa kuwa, upotevu huo unasababisha hasara kwa shirika na upungufu katika ugavi wa meme, hali inayoweza kuathiri uzalishaji na uchumi nchini,

Kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kuiwezesha TANESCO kumudu matengenezo Rekebishi (Rehabilitation) katika vituo na miundombinu ya kusafirishia umeme nchini.

5.2.3 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

Mheshimwa Spika, kuhusu Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Kamati ina mapendekezo makuu mawili:

a) Uzalishaji wa Gesi nyingi kuliko inavyonunuliwa

Kwa kuwa, TPDC inao uwezo wa kuzalisha gesi nyingi zaidi ya soko lililopo kwa sasa na kwamba haina uwezo wa kujenga miundombinu ya kusambazia gesi ili kuwafikia watumiaji wengi sokoni,

Na kwa kuwa, hali hiyo inasababisha TPDC kuendelea kuwa na gesi isiyonunuliwa na kukosa pesa ambazo ingezipata kwa kuuza gesi ya ziada, jambo linalochangia kuifanya TPDC kushindwa kujidoresha kibiashara kama ilivyo kusudiwa,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri Serikali kuwezesha utekelezaji wa mradi wa kusambaza gesi katika mkoa wa Dar es salaam kwa kuwekeza katika miundombinu ya kusambazia gesi kwa watumiaji.

b) Ufinyu wa bajeti kwa shughuli za TPDC

Kwa kuwa, Taarifa zinaonesha kuwa mapato yote yanayopatikana kwa shughuli za TPDC yanapelekwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali na kwamba bajeti yake hutegemea kiasi kinachotengwa na Serikali,

Na kwa kuwa, uatartabiu huo husababisha TPDC kutengewa bajeti ndogo kuliko kiasi inachopeleka kwenye mfuko mkuu, hali inayokwamisha utekelezaji wa shughuli zake kutokana na ufinyu wa bajeti,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri Serikali kuipatia TPDC bajeti ya kutosha na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ya msingi kama inavyotakiwa.

5.2.4 Chuo cha Madini Dodoma (MRI)

Kwa kuwa, Chuo cha Madini Dodoma ndio chuo pekee kinachotoa mafundi mchundo na mafundi sanifu katika sekta ya Madini nchini lakini kinakabiliwa na ufinyu wa bajeti na kuchelewa kupata fedha kwa wakati,

Na kwa kuwa, hali hiyo inasababisha chuo kushindwa kudahili wanafunzi wa kutosha kutokana na kushindwa kuajiri walimu wa kutosha pamoja na kujenga miundombinu ya mafunzo, jambo linaloongeza upungufu wa mafundi mchundo na mafundi sanifu wanaohitajika,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri Serikali kukiwezesha chuo hiki kifedha kwa kikitengea bajeti ya kutosha.

5.2.5 Wakala wa Jiolojia nchini (GST)

Kwa kuwa, Wakala wa Jiolojia nchini amepewa jukumu muhimu la kukusanya, kuchambua, kutafsiri na kutunza taarifa mbalimbali za kijiosayansi, kwa lengo la kuliwezesha Taifa kufanya maamuzi sahihi kuhusu matumizi ya ardhi (Earth),

Na kwa kuwa, kutokuwezesha kibajeti kwa TAASISI hiyokunachangia utekelezaji hafifu wa majukumu hayo muhimu na kusababisha Taifa kukosa taarifa za msingi kuhusiana na jiolojia ya nchi,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri serikali kuwezesha Wakala wa Jiolojia nchini kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake ikiwemo kufanya tafiti mbalimbali kuhusu majanga kama vile, matetemeko ya Ardhi, Milipuko ya Volkano na maporomoko ya ardhi, kwa lengo la kuiliwezesha Taifa kukabiliana na majanga hayo.

5.2.6 Sekta Ndogo ya Mafuta

Mheshimwa Spika, kwenye Sekta ya Mafuta nchini, Kamati ina mapendekezo makuu mawili:

a) Umuhimu wa Matenki ya Kuhifadhiya Mafuta

Kwa kuwa, matenki ya kuhifadhiya mafuta (Farm Tanks) ni muhimu kwa ajili ya kuiwezesha serikali kudhitbiti hujuma za Wafanya biashara ya mafuta nchini pamoja na kuinongeza Serikali mapato,

Na kwa kuwa, kukosekana kwa Metnki hayo kunasabaisha hatari ya kushindwa kudhibiti itakapotokea hujuma za makampuni ya mafuta nchini hali ambayo awali ilikuwa ikidhibitiwa na TPDC,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri Serikali kuiwezesha TPDC kuwekeza katika Ujenzi wa matenki hayo.

b) Bei elekezi kutokuzingatia umbali kutoka makao makuu ya miji/wilaya

Kwa kuwa, uuzaji wa mafuta nchini huongozwa na bei elekezi ambayo kwa mujibu wa uchambuzi wa Kamati, haizingatii tofauti iliyopo ya umbali kutoka makao makuu ya miji/ wilaya,

Na kwa kuwa, Kutokuzingatiwa kwa tofauti hiyo ya umbali kunasababisha wauzaji wa mafuta kuuza kwa bei ambayo inawaumiza wananchi, jamba linalohitaji kuwekewa utaratibu bora,

Kwa hiyo basi, Bunge liishauri Serikali kuhakikisha kuwa bei zote elekezi za mafuta zinazingatia umbali uliopo kutoka makao makuu ya miji/wilaya.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Job Ndugai Spika, Dr. Tulia Akson Naibu Spikana Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano wenu kwa Kamati yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati yako.Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

	Mwenyekiti
	M/Mwenyekiti
1. Mhe. Doto Mashaka Biteko, Mb	Mjumbe
2. Mhe. Deogratius Ngalawa, Mb	"
3. Mhe. Joyce Bitta Sokombi, Mb	"
4. Mhe. Mohamed Juma Khatibu, Mb	"
5. Mhe. Bahati Ali Abeid,Mb	"
6. Mhe. Susan limbweni Kiwanga, Mb	"
7. Mhe. Maulid Said Abdallah Mtulia, Mb	"
8. Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb	"
9. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb	"
10. Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb	"
11. Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb	"
12. Mhe. Zainabu Mussa Bakar, Mb	"
13. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb	"
14. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb	"
15. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb	"
16. Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb	"
17. Mhe. Desderius John Mipata, Mb	"
18. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb	"
19. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb	"
20. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb	"
21. Mhe. Stella Ikupa Alex, Mb	"
22. Mhe. Dustan Luka Kitandula, Mb	"
23. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb	"
24. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb	"
25. Mhe. John Wegesa Heche, Mb	"

Pia Kamati inaipongeza Wizara ya Nishati na Madini chini ya uongozi wa Mhe. Prof. Sospeter Muhongo(Mb) Waziri wa Nishati na Madini, Naibu wake Dr. Medard Matogolo Kalemani na watendaji wote wa wizara kwa ushirikiano waliooutoa katika kipindi hiki ambao umeiwezesha Kamati yako kutekeleza majukumu yake kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika,kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah, kwa ushirikiano wake na Kamati yetu. Pia namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Michael Chikokoto pamoja na Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Mwanahamisi Munkunda na Ndg. Felister Mgonja pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Kokuwaisa Gondo kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Doto Mashaka Biteko, Mb
Mwenyekiti
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini
Januari, 2017

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na utaratibu mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina kadhaa hapa ya wachangiaji tutakaoanza nao asubuhi hii. Tutaanza na Mheshimiwa Richard Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Maselle na Mheshimiwa Jesca Kishoa ajiandae.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijadili taarifa hizi mbili lakini nitajikita sana kwenye Taarifa ya Nishati na Madini. La kwanza, kwa sababu Kamati zetu hizi zinatoa mapendekezo na maoni mbalimbali; tunatumia karibu siku tano, sita kutoa mapendekezo; tulishawahi kufanya hivyo siku za nyuma, lakini tukijuliza: Je, haya mapendekezo mwisho wa siku nani anakuja kuyajadili?

Taarifa hizi tunazopendekeza, zinaletwa Bungeni lini na kujua kwamba kweli haya tuliyopendekeza yametekelezwa? Kama yametekelezwa, ni kwa kiasi gani? Nani anajua? Au kazi yetu sisi ni kutoa mapendekezo, yanakwenda Serikalini halafu basi yanaishia hapo hapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba ule utaratibu wa zamani kweli kwenye enzi za akina Mheshimiwa Shelukindo, taarifa ziliwa zinasomwa, mapendekezo yanatolewa, baadaye Serikali inakuja inajibu pale ambapo imetekeliza; kwa nini imeshindwa na kwa nini imefanikiwa, ili kusudi kuweza kujua haya yote ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge tunakaa siku mbili tatu humu ndani tunayasema. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, hili wala siyo la Serikali hata kidogo, ni letu sisi Waheshimiwa Wabunge. Kwa sababu tukisema kwamba tunataka kufanya jambo hili, lakini lazima tujue kwamba mambo haya yanatekelezwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naomba unikubalie niipongeze Serikali kupitia Shirika la Umeme (TANESCO); sijui wamefanya miujiza gani. Siku hizi sijasikia kukatika katika kwa umeme, lakini mgao wa umeme; hata kama unakatika labda ni bahati mbaya. Lazima niseme ukweli, ni tofauti na siku za nyuma. Sasa hivi kukatika kwa umeme kumepungua sana, lakini hata mgao wa umeme nchini sasa hivi hakuna. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaiomba Serikali kupitia TANESCO waongeze ile kasi ya kulismamia Shirika hili la TANESCO, kwa sababu yapo mambo mengi. Jambo la kwanza ambalo naionba Serikali, tulikubaliana katika kutekeleza kwamba ipunguze gharama za pale tunaponunua huu umeme. Kwa mfano, Symbion, Aggreko na Songas ambayo kwa taarifa ya

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, mpaka sasa TANESCO inadaiwa shilingi bilioni 63. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, hapa kuna mkanganyiko wa madeni ya TANESCO. TANESCO inadaiwa kiasi gani na TANESCO inadai kiasi gani? Mfano, kwa mujibu wa taarifa ambayo imesomwa sasa hivi na Mwenyekiti wa Kamati, wanasema kwamba TANESCO inadaiwa shilingi bilioni 822, lakini kwa mujibu wa taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, wanasema TANESCO inadai shilingi bilioni 796. Sasa ipi ni ipi? TANESCO inadaiwa au TANESCO inadai?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri tukapata mchanganuo vizuri ili sisi Waheshimiwa Wabunge tuweze kujua, kwa sababu hii inachanganya. Kwa mujibu wa taarifa ambayo imesomwa sasa hivi hapa, wanasemwa Serikali na taasisi inaidai TANESCO shilingi milioni 269. Sasa hii inachanganya. Tunaomba Serikali, itakapokuja kujibu au Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati mtusaidie kujua hasa. Mtupe mchanganuo halisi TANESCO inadai kiasi gani na TANESCO inadaiwa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naomba tusaidiwe tu, ni haya katika utekelezaji. Lipo suala la Sera ya Gesi na Mafuta kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Tulikubaliana kwenye Kamati na tukaleta mapendekezo ndani ya Bunge, ndio maana nikasema mambo haya kama hatufuatilii utekelezaji wake, inaweza ikawa ni tatizo. Jambo hili tumelisema humu ndani lakini imekuwa halieleweki.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, mpango maalum kuhusu mageuzi katika Sekta ya Madini; tulikubaliana na hili nafikiri hata Mheshimiwa Rais alilisemea siku moja, kuhusu kuweka uzio. Hili lilikuwa ni pendekezo la Kamati ya Nishati na Madini, ndani ya Bunge na tukaazimia kwamba uwekwe utaratibu sasa wa kulinda madini yetu ya Tanzanite huko Mererani; na bahati nzuri na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati amelisema hili kwamba hatuoni tija ya uzalishaji katika eneo hilo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako tulikubaliana kwamba iangaliwe namna nzuri zaidi ya kuweka uzio, tanzanite inapatikana Tanzania peke yake, hakuna sehemu nyingine. Sasa kama hatuweki utaratibu mzuri wa kuweka uzio kwenye eneo hilo, itasaidia mambo mawili; wale walangazi; kutorosha madini; lakini na kutokujua uhalisia wa madini yenyewe. Kwa hiyo, bado Serikali ituletee majibu. Je, suala zima la uzio, ni lini litakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kabla kengele hajjalia, Waheshimiwa Wabunge, suala zima la ruzuku kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo; wiki mbili au tatu zilizopita, baadhi ya Wajumbe wa Kamati walikwenda Nkasi ili wachimbaji hawa wadogo wadogo waende kupata hela yao ya ruzuku. Inasikitisha kwamba walikwenda Mpanda, kwamba hawa wachimbaji wadogo wapate hela ya ruzuku. Wamefika kule, hela ya ruzuku haipo. Kwa hiyo, hawa waliokwenda kule wakatumia hela za Serikali bila manufaa yoyote yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala hili la ruzuku ya Serikali lisitumike kisiasa kwa sababu hawa wachimbaji wadogo wadogo wangependa zaidi wanufaikia kama tuliviyokubaliana. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, mnapozungumzia kwamba mnakwenda kutoa ruzuku kwa ajili ya wachimbaji wadogo, basi iwe kwenda kutoa ruzuku kweli kweli, lakini siyo kuwabeba kutoka maeneo ya huku na huko, halafu wanakwenda kwenye eneo husika wasikute chochote kile. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iyatekeleze haya, lakini tunapenda zaidi tuwe tunapata mrisho nyuma kwa yale ambayo Bunge linapitisha ndani ya Bunge, kwamba hili limetekelzeza, hili halijatekelezeza; ili tuweze kuishauri vizuri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Naunga mkono taarifa zote mbili. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Augustino Masele, atafuatiwa na Mheshimiwa Jessica Kishoa na Mheshimiwa Bhagwanji Meisuria ajiandae.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii adhimu ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hotuba za Kamati zetu mbili za kudumu za Bunge; Kamati ya Nishati na Madini na Kamati ya Bunge ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii ili kwa namna moja au nyingine, niweze kwanza kuipongeza Serikali yetu kuititia Wizara hizi mbili pia. Wizara ya Nishati na Madini imefanya kazi kubwa, nzuri na ya kutukuka kwa Taifa letu hili la Tanzania; tumeona juhudhi zilivyo nzuri katika kuhakikisha kwamba umeme unapatiwana katika Taifa letu na umeme wa uhakika. Kwa hiyo, naomba tu kwa kweli Serikali kuititia Hazina, itoe pesa kwa wakati katika miradi mbalimbali ambayo imeletwa na Wizara hii ndani ya Bunge lako na kuidhinishwa ili ikapate kutekelezwa katika mwaka unaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Wizara hii pia ambayo imeonesha kwa mfano kabisa, kuwachukua Watanzania wenzetu na kuwapa *full scholarship* katika Mataifa mbalimbali kuweza kujelimisha na kupata taaluma muhimu katika Sekta mbalimbali za Nishati na Madini katika Taifa letu. Nina imani baada ya muda siyo mrefu, Tanzania itakuwa na wataalam waliobobe wa hali ya juu na Taifa letu litapata manufaa makubwa katika sekta hizi zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Nishati na Madini iijitahidi sana kuisimamia Sekta ya Umeme nchini, maana hii ndiyo injini ya mapinduzi ya viwanda kule ambako tunatarajia kwenda. Kwa sababu umeme unapokuwa unapatiwana katika bei ambayo ni ndogo, tunaamini kwamba tunaweza tukavutia wawekezaji wa ndani na nje kwa urahisi zaidi. Hata katika Wakala wa Umeme Vijijiini, napendekeza Serikali iendelee kutoa pesa kwa wakati ili hata hii REA Phase III iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwa macho yetu wote kwamba Tanzania imepiga hatua katika usambazaji wa umeme katika maeneo mbalimbali vijijiini na naomba tu kwamba ule mtandao wa umeme vijijiini uendelezwae zaidi. Pale ambapo tumefika, kasi iongezwe zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miundombinu, napo tuongeze jitihada katika kuhakikisha kwamba Reli ya Kati inaendelezwae. Naipongeza kwanza Serikali kwa kuingia mkataba na Waturuki kutaka kujenga hii Reli ya Kati kwa kiwango cha standard gauge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Serikali yetu kwa dhamira ya dhati ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Joseph Pombe Magufuli tutafika kule ambako tunatarajia ili tuweze kuwa na treni ambazo zinaweza kwenda mwendo kasi; *bullet train*, tuweze kuzipata katika Tanzania hii, watu na vitu viweze kufika mahali panapostahili kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kabisa kwamba Taifa la Tanzania tumejaliwa kuwa katika eneo ambalo kijigrafia linatupa nafasi nzuri ya kuweza kuwa tegemeo katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki na Afrika ya Kati. Kwa maana hiyo, upanuzi wa bandari zote; ya Tanga, Dar es Salaam, Bagamoyo pamoja na kule Mtwara ni bandari ambazo ni za muhimu sana. Ni muhimu kabisa Tanzania ikawa na kipaumbele cha peke yake katika hizi bandari, kwa sababu zote zinategemewa. Bandari ya Mtwara, Mataifa ya Msingi, Malawi hata Zimbabwe wanaweza wakaitumia bandari hii. Kwa maana hiyo, ile reli ya kutoka Mtwara mpaka Mbambabay ni ya muhimu sana kwa sababu itakuwa na matokeo mazuri sana katika ukuzaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Reli ya Kati inaunganisha Bandari ya Dar es Salaam na nchi hizi za Zaire kwa maana ya DRC, Rwanda na Burundi pamoja na Nchi ya Uganda. Bandari ya Tanga imeteuliwa kabisa na nchi ya Uganda na kwa maana hiyo, ujenzi wa reli ya kutoka Tanga - Arusha mpaka Musoma na yenyewe ni muhimu ikapewa kiaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, niseme kabisa kwamba Taifa letu la Tanzania katika mchango wake wa kuleta uhuru katika Mataifa mbalimbali ya Afrika, bado inayo nafasi nzuri tena katika kuchangia ukuzaji wa uchumi katika Mataifa yote haya ya Afrika ambayo Tanzania yenyewe ilishiriki katika kuyaletea uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme dhahiri tu kwamba kwetu huko Geita ni sehemu ambayo tunayo madini ya dhahabu. Naishauri Serikali ifanye kila linalowezekana kuharakisha kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo ya Wilaya yetu ya Mbogwe na wachimbaji waliotapakaa katika Mkoa wa Geita, wapate kutengewa maeneo ya kufanya shughuli zao za uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno haya, nakushukuru kwa mara nyiningine kwa kunipatia nafasi hii. Ahsante sana. (Makofisi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jesca Kishoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Bhagwanji Meisuria. Muda wetu ukituruhusu, atamalizia Mheshimiwa Ally Keissy.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi kwa Kamati ambayo imewasilisha muda siyo mrefu, kwa sababu kuna mambo ya msingi wameweza kuyaweka bayana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianza na suala la Serikali kuchelewa kupeleka fedha za miradi katika maeneo husika, hasa katika eneo la umeme; mimi ni mionganini mwa wahanga katika tatizo hili. Umeme wa upepo Singida, kwa muda mrefu, toka miaka ya 1990 mpaka Bunge lililopita, Serikali imekuwa ikipiga danadana kuhusiana na suala hili. Majibu ni yale yale! Kila siku Mheshimiwa Waziri husika anapokuja kuzungumzia suala hili, analeta majibu yale yale ambayo anayazungumza toka Bunge lililopita na bahati nzuri ni Waziri yule yule kutoka Bunge lililopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali, kama wameshindwa kupata fedha kutoka nje ambazo wanazitegemea, basi ni heri watumie fedha za ndani kutekeleza mradi huu, kwa sababu ni muda mrefu sana. Tumepewa majibu haya haya kila siku, wananchi wa Mkoa wa Singida wamechoka na Wabunge wa Singida naamini hapa wataniunga mkono katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika suala hili la umeme wa upepo wa Singida, Serikali, kama kuna uwezekano wa kuchukua fedha kutoka ndani, ichukue na itekeleze mradi ule kwa sababu kiukweli tumechoka. Upopo wenye labda tungekuwa tumepewa na mtu; tumepewa na Mwenyezi Mungu, ilikuwa ni suala la Serikali kutekeleza mradi huu na kuweza kutimiza ahadi ambazo wanazitoa kwa wananchi wa Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Singida ninyi Chama cha Mapinduzi mnajua ni champion wa kutoa kura kwa Chama cha Mapinduzi mfululizo miaka yote, lakini ni mionganini mwa watu ambaao kwenye miradi mmewasahau. Naomba suala la umeme wa upepo wa Singida, Serikali ilichukulie kwa uzito wa kipekee, kwa sababu ni ahadi za muda mrefu sana ambazo zimekuwa hazitekelezeki. (Makofisi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuachana na hayo, naomba pia nizungumzie suala ambalo limekuwa likizungumzwa miaka nenda miaka rudi karibu Mabunge yote; ni suala la mikataba kuwekwa wazi. Namaanisha mikataba ya gesi pamoa na mikataba ya madini specific. Suala hili la mikataba kuwekwa wazi limeshazungumzwa kwa muda mrefu sana. Wamezungumza

Awamu ya Nne, wamezungumza Awamu ya Tatu na Awamu ya Tano tena tunalizungumza suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Serikali yoyote ambayo inajipambanua kwamba yenewe ni ya uwajibikaji, uwazi na ya kutumbua majipu, suala la mikataba kuwekwa wazi lilikuwa siyo suala la kuanza kuihoji, lilikuwa ni suala ambalo lilipaswa kutekelezeka tu. Mionganoni mwa vitu ambavyo tulipaswa tuvizingatie ni pamoja na sisi kuwa Wajumbe kwenye organizations ambazo zinazungumzia masuala ya mikataba kuwa wazi. Mfano, sisi ni member kwenye OGP (Open Governance Partnership), lakini toka mwaka 2011 tumekuwa member katika organization hii, bado vitu vyetu tunafanya kwa mazingira ya usiku usiku; Bunge usiku, mikataba usiku. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado sisi toka mwaka 2009 ni member kwenye Shirika la EITI (Extractive Industry Transparency Initiative). Hii ni aibu. Ukiachana na sisi kuwa member katika hizi taasisi, lakini bado Awamu ya Nne Bunge hili lilipitisha sheria ya kutaka mikataba kuwa wazi na Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete akasaini, lakini danadana zikaanza kupigwa baada ya kufika kwa Waziri husika kwa maana ya kutunga kanuni ambazo zinaweza zikasababisha sheria hiyo kutekelezeka. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu ni kutofahamu, linapokuja suala la sheria ambazo zina maslahi kwa umma, kwa mfano, mwaka 2016 tulipitisha sheria ambazo zinafunga vyombo vya habari, zinafunga demokrasia, zimepitishwa Rais akasaini immediately na Waziri husika akatunga kanuni na zikaanza kutekelezwa, lakini zinapokuja sheria kama hizi ambazo zina maslahi kwa umma, kwamba mikataba iwe wazi, sheria hizi zinakaa muda mrefu sana. Mfano, toka Awamu ya Nne mpaka sasa, bado Mheshimiwa Waziri hajatunga kanuni na mpaka dakika hii hajasema sababu ni nini. Labda ni kutofahamu, au ni kufahamu lakini ni kiburi tu kwamba mikataba ikiwa wazi kuna faida gani? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba inapokuwa wazi, kwanza wananchi wanakuwa na confidence na Serikali yao. Pia mikataba inapokuwa wazi, wale wawekezaji katika eneo husika wanakuwa na mahusiano mazuri na watu wa eneo lilo ambalo linawazunguka kwa kuamini kwamba wanayoyafanya ni mambo ambayo wanayajua kwa maana yako wazi. Lingine, mikataba kuwa wazi inasaidia sana zile organisations na NGOs ambazo zinafanya tafiti mbalimbali kuwa na correct details, figures ambazo ni sahihi kuhusiana na mkataba husika au investment husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi mbalimbali ambazo unaweza ukafikiri labda ni Tanzania tu tutakuwa wa ajabu sana, lakini zipo nchi nyengi sana ambazo zimeweka mikataba wazi; na kwa sababu ya muda nashindwa kuzitaja lakini nitazitaja chache, ninazo hapa zote. Nchi ya Liberia, Ghana, Congo, USA, Colombia, Canada; nchi karibu zote zimeweka mikataba wazi. Kwa nini Tanzania tunaendelea kuweka mikataba hii katika hali ya usiku? Naomba kama Bunge, ikiwezekana tutunge sheria ambayo itambana Waziri, kwamba ndani ya miezi sita atunge kanuni ambazo sheria itaanza kutekelezeka, lakini siyo afanye anavyotaka yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine ambalo limenishtua kidogo na napenda kushare na Wabunge wenzangu humu ndani. Naomba Waziri atakapokuja kuhitimisha ailelezee kwa ufasaha kabisa, kwa sababu siyo vyema kuliona linaandikwa kwenye majadala ya Kimataifa halafu kama Wabunge humu ndani hatuna information sahihi. Kuna kampuni inaitwa BG Group ya Uingereza ambayo inamiliki vitalu vya gesi Tanzania. Ilifanya transfer share kwenda Kampuni ya Shell ambayo ni kampuni kutoka Uhlanzi. Kisheria na kiutaratibu wakati kampuni inafanya transfer shares, ni lazima kama Serikali tupate kitu kinaitwa Capital Gain Tax, lakini ni aibu kwa Serikali hii, transfer share imefanyika lakini Serikali haijapewa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha hapa aseme kama kodi hii imelipwa au kama suala hili lina ukweli kiasi gani? Siyo vyema kuona linazungumzwa na kama Wabunge hatulifahamu lakini pia kama Serikali hajji kutoa maelezo yoyote kwa maana ya Wizara. FCC hawana majibu, nimewauliza na wakasema watatao kwa maandishi, mpaka leo hawajanipa; TRA hawana majibu, lakini pia Wizara tunaomba majibu leo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine la uwekezaji katika gesi asilia. Unapozungumzia... (Makofi)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Bhagwanji Meisuria, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Keissy.

MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru nimepata nafasi hii mara ya kwanza. Namshukuru Mwenyezi Mungu, tumejaliwa sote tuko pamoja na *Insha Allah* Mungu ataleta neema yake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge pamoja nawe Naibu Spika kwa kazi yako nzuri. Katika Bunge hili mimi ni *Baniani* peke yangu. Kama nimekosea, mtanisamehe, lakini nitajitahidi. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napongeza Kamati yangu ya Miundombinu, imefanya kazi nzuri kabisa, pamoja nami, nimetembelea bandari, uwanja wa ndege, reli na barabara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Rais wangu wa Muungano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ye ye amefanya kazi nzuri kabisa katika Tanzania yetu na nchi yetu. Ameboresha miundombinu, barabara na mambo mengine ya reli na bandari. Nasi Wabunge tunamsaidia kufanya kazi apate sifa, kazi tu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nampongeza Mheshimiwa Rais wangu wa Zanzibar, amefanya kazi nzuri na kuiboresha Zanzibar kwa miundombinu ya barabara, taa za solar Michenzani, Amani na sehemu nydingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza vile vile Waziri Mkuu. Waziri Mkuu anafanya kazi nzuri pamoja nasi na anakwenda kila mahali anafanya kazi yake nzuri, nasi tuko pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja katika mada yetu ya Kamati yetu ya Miundombinu. Kamati yetu tumetembelea barabara zote na hivi juzi tumekwenda kuanzia Dar es Salaam, tumetoka Dodoma kwenda Arusha, tumeona barabara inajengwa na madaraja. Naipongeza Tanzania yetu na Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri na kuweka uchumi bora. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nataka kuzungumza kuhusu Uwanja wa Ndege. Nimetembea viwanja vya ndege mbalimbali. Tumetoka kwenda Arusha, tumeona mambo mazuri, lakini yanatakiwa kuboreshwa. Mnara wa uwanja wa ndege ni mdogo sana, unatakiwa ufanywe mkubwa upate kuonekana. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati yetu na mimi nimefaidika kumsaidia Mheshimiwa Rais, uwanja wa ndege wa Kilimanjaro wa *International* ni mzuri kabisa; lakini uwanja wa ndege wa Moshi, tunatakiwa tutie mkazo katika Serikali. Yaani uwanja wa ndege wa Moshi ile ndege inatua katika barabara mbovu kabisa. Tokea enzi ya *British* ipo pale. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali pamoja na Mheshimiwa Waziri, tuboreshe uwanja wetu ule, kwa sababu katika uwanja wa ndege wanakuja watalii. Watu wanakuja kwa utalii wanashuka Arusha wanateremka Kilimanjaro, lakini pale uwanja wa ndege wa Moshi upo karibu na mlima wetu wa Kilimanjaro na Mount Meru. Uwanja wa ndege wa Arusha ndege nyingi zinatua pamoja na ATC, kwa hiyo, kwa nini usiboreshw pale Moshi? Kwa sababu pale Moshi ni centre, wanakuja watalii wapate kwenda moja kwa moja katika mambo ya kutazama wanyama pamoja na Mlima wetu wa Kilimanjaro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetembelea bandari nyingi sana. Bandari hii inahitaji kuboreshwa hasa. Tumekwenda Tanga, Mwanza, tumeona Bandari ya Mwanza ni nzuri, lakini inatakiwa kutiwa nguvu kabisa kuboreshwa ili kukuza uchumi, kusafirisha mizigo nchi za jirani. Bandari ya Tanga ipo jirani na Zanzibar na Mombasa. Tumeona kuna uzito na ipo haja kubwa sana ya kuboresha, kupanua na kuleta meli kubwa za makontena makubwa kuliko Dar es Salaam ambapo tunateremsha kontena zetu. Ni bora kufika Tanga kwenda kwa nchi za jirani. Vilevile tuboreshe bandari yetu ya Bagamoyo. Tumetembezwa, tumeridhika na tunesema Tanzania yetu naomba Mheshimiwa Rais aboreshe ile Bandari ya Bagamoyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye sekta ya reli. *Standard gauge* ya reli sisi Kamati tulikwenda kutembea, nampongeza Mwenyekiti na Kamati yangu. Mara ya kwanza nimekwenda Tanzania nimeona reli. *Standard gauge* imekwama sehemu fulani, haikuweza kuboreshwa, lakini nashukuru Mheshimiwa Rais wetu amepata ufadhili mpya, tutaboresha tufanye kazi; reli yetu kwa upande wa Congo tupate kupeleka mali yetu Burundi na Rwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutakuwa tunaongeza uchumi wa nchi na hiyo ndiyo sekta muhimu. Wenzetu wa Kenya kutoka Mombasa wamefika Nairobi, wataunganisha na jirani pale Congo na wapi, sisi tutakosa soko. Naiomba Serikali tufanye kazi na namshukuru Mwenyezi Mungu na naishukuru Serikali ya Awamu ya Tano, Mungu ampe uzima na afya Mheshimiwa Rais wetu afanye kazi ya ziada...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda wangu umekwisha, naunga mkono Kamati hii na Bunge letu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme jambo moja, kama nimekosea, ulimi hauna mfupa. Ahsante. (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Baniani mmoja, naona umechangia vizuri. Naona Bunge zima linakupigia makofi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Ally Keissy atakuwa mchangiaji wa mwisho kwa siku hii.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, naipongeza Wizara ya Nishati na Madini hasa Mkurugenzi Mkuu wa REA na Mkurugenzi wa

TANESCO kwa kusaidia mradi wa kupeleka umeme kwenye Bwawa la Mfii, tegemeo kubwa la maji Namanyere kupunguza kutoka shilingi bilioni 59 mpaka shilingi bilioni 23.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa ya deni ni kulipa. TANESCO inadaiwa shilingi bilioni 820 na TANESCO yenye inadai pesa. Kuna Mashirika maalum yanadaiwa pesa. DAWASA, Idara ya Maji, inadaiwa; yenye inauza maji, kwa nini isilipe hela za TANESCO? Wakala wa Umeme Zanzibar (ZECO) wanadaiwa pesa shilingi bilioni 123. Wakala tofauti na kitu chochote, ni sawa na mimi na duka langu, wewe unaleta mali yako nakuuzia kwa bei unayonipa mimi nakurudishia zile hela. Cha ajabu ZECO hairudishi hela TANESCO, ni aibu! Serikali nzima ya Bara inadaiwa shilingi bilioni 40, ZECO inadaiwa shilingi bilioni 123, tutafika wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba TANESCO wawe na mtindo wa kukatia umeme popote wanapodai. Haiwezekani kuleana namna hii! Kuna Wizara zote za Serikali ya Bara zinadaiwa. Hakuna Wizara hata moja isiyodaiwa na TANESCO, ni ajabu. Mtu binafsi, mwanakijji ambaye hana mbele wala nyuma, ananunua umeme kwa LUKU. Mwisho wa mwezi hana hela, hapati umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wizara za Serikali hapa pamoja na Mashirika ya Serikali makubwa, hayalipi deni la TANESCO. Haji kwenye akili ya binadamu kabisa! Dawa ya deni ni kulipa. Mwanakijji hana mbele, hana nyuma, hana chochote analipa deni la TANESCO, anawekewa LUKU. TANESCO lazima ifanye operation nchi nzima hasa miji mikubwa. Kuna wizi wa ajabu wa umeme katika nchi hii. Kuanzia Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Sumbawanga, popote pale kwenye mji mkubwa, kuna wizi mkubwa wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Nishati na Madini, kama haina wafanyakazi wa kutosha wakaazime JKT. Wachukue kwenda nyumba kwa nyumba, kijiji kwa kijiji; haiwezekani Shirika kupata hasara namna hii! Kuna wizi mkubwa wa umeme! (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naiomba Serikali, msongo wa umeme kutoka Mbeya kwenda Kigoma kuitia Sumbawanga na Mpanda, hii mikoa mitatu au minne hii, inaleta hasara kubwa sana kwa Shirika hili la Umeme. Tunatumia majenereta, mafuta yanalika kwa kiasi kikubwa, hakuna faida TANESCO inapata kwenye Mikoa hii ya Kigoma, Katavi na Rukwa, Shirika hili linapata hasara, ndiyo maana Shirika hili linaingiza hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haiwezekani tusipate umeme wa gridi ya Taifa kutoka Mbeya kwenda Kigoma mpaka Nyakanazi ili kuondoa mzigo kwa TANESCO. Haiwezekani mchakato kila siku; tupate umeme wa uhakika. Kwingine wanapata umeme wa uhakika, lakini mikoa hii mitatu, ni majenereta tu yananguruma. Kwanza yanaharibu mazingira kwa kusababisha moshi mijini. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu REA. Tatizo la REA ndugu zangu ni kutokupata hela za Serikali. Tuliamua hapa mafuta shilingi 150 iende REA, lakini hela haziendi. Asilimia 40 ndiyo hela zinakwenda, zikiingia Hazina hela zile, hazitoki kwa wakati. Wakandarasi hawafanyi kazi kwa sababu hawapati pesa. Mradi wa shilingi milioni 200 utafika milioni 300 kwa riba kwa sababu pesa hazipecleksi kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, hela tunazoamua hapa Bungeni za 150 kila lita ziende moja kwa moja REA. Haiwezekani zikifika Hazina zinakwama zinatoka kwa masharti au zinabadiishwa njiani, haiwezekani. Kwa hiyo, naiomba Hazina ipeleke hela za REA ili wananchi wafaidike na umeme. Hatuwezi kumaliza vijiji hivyo 7,000 kama pesa haziendi, tunadanganya hapa. REA wanapata kiwango cha chini cha pesa, hawawezi kuendelea

kuweka umeme vijiji kama hawapati pesa. Tumeamua hapa na mafuta ni *hot cake*, mafuta yanauzika. Tunauza mafuta, hela zinaingia, lakini hazijulikani zinakokwenda. Haiwezekani, lazima wapewe pesa zinazohitajika ili Wakandarasi waanze kazi yao. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naishauri TANESCO, sehemu za mapori makubwa, REA wapeleke nguzo za zege kuondoa hujuma ya kuchoma mapori na nguzo kuungua. Kuna mapori mazito na watu wetu hata ukiwapigia mbiu, useme mpaka uchoke, lakini kila msimu lazima wachome mapori. Hawa watu ni hatari sana! Kwa hiyo, nawaomba, sehemu ambazo ni misitu minene, waangalie kutafuta nguzo za zege ili kuepuka kuitia hasara TANESCO. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimefurahi na *REA III*. Waziri ametuhakikishia kwamba transformer zote na waya zote watanunua katika viwanda vyetu. Hiyo itasaidia kabisa kwanza kuharibu hela zetu za Kigeni kwenda kununua transformer mboru nje au China wakati Arusha kuna transformer imara na zinatosha miradi yetu kuzalisha umeme. Tuna viwanda vingi pamoja na TANESCO ina-share katika *East Africa Cable*, wanunue waya pale. Haiwezekani kwenda kununua waya nje wakati tuna waya zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wajiepushe kupitia Wakandarasi amba o ukienda, inapitia kwa watu wanazidisha bei ajabu! Miradi ya ajabu; unakuta mtu unayechukua tenda kuagiza waya nje, haijulikani ananunua bei gani kule anakuja kutubamiza bei wakati tuna viwanda vyetu wenyewe hapa nchini. Huu ni ubadhirifu na ufisadi wa hali ya juu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bandari. Ndugu zangu hii nchi ina bandari Mungu kaibariki. Nilikwenda Bandari ya Mtwara hata Afrika Kusini hakuna bandari kama ya Mtwara. Bandari ya Tanga ambayo ingesaidia Mkoa wa Kilimanjaro, Mkoa wa Arusha, Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Mara na Tanga yenyewe, ni ajabu watu wa Tanga na Kilimanjaro wanatumia Bandari ya Mombasa. Ni aibu kubwa kwa Serikali, wakati tuna bandari yetu wenyewe. Mungu katupa bandari katika mwambao wa bahari, lakini ni ajabu tunatumia Bandari ya Mombasa kuliko kutumia Bandari ya Tanga. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mpaka watu wa Dar es Salaam, wafanyabiashara wa Dar es Salaam wanatumia Bandari ya Mombasa, ni aibu kubwa kwa Serikali. Ni aibu, tumekuwa kama Burundi au Rwanda amba o hatuna bandari! Tujiulize mara mbili mbili, kuna nini hapa? Kuna mdudu gani? Lazima tuimarishe bandari zetu ili wananchi wafaidike na bandari zetu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kwenda hovyo hovyo, tunafanya kazi hovyo hovyo. Serikali iwe kali kidogo kwa kiongozi yoyote anayeingia tenda, manunuzi ya ajabu ajabu yanayotuumiza sisi, mdudu wa manunuzi huyu; lazima achukuliwe hatua kali. Haiwezekani wewe kitu unajua, hata mimi ambaye sikusoma na wala sio Mkandarasi, unajua kabisa hiki kitu sh. 10/= unakwenda kuandika sh. 500/= na unatia saini *cheque* inatoka! Kusema ukweli hao ndio maadui wa nchi. Hawa nilikuwa nazungumza siku zote! Huyu mdudu manunuzi, tungewakamata hawa tukawapiga risasi siku ya Ijumaa au Jumapili watatu au wanne, wangeshika adabu. (Kicheko/Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani hii Serikali ni tajiri kuliko Ubelgiji, kuliko Ureno, leo unashangaa hapa wanasema Ureno inajenga reli ya kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro. Ni aibu, wakati sisi ni matajiri kuliko Ureno. Ureno maskini wa Mungu wale leo hata chakula hawana. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali ifuatilie. Naishukuru sana *REA* lakini wapewe hela kwa wakati ili wafanye miradi yetu na vilevile wafikirie vijiji ambavyo viko nyuma

sana, kuna mikoa iko nyuma sana, ndiyo waelekeze REA III. Kuna mikoa mingine kuna umeme mpaka chooni. Sasa watufikirie na sisi kule Rukwa ambaa tumekuwa nyuma kabisa, tumepata umeme miaka miwili iliyopita. Ni ajabu kabisa katika nchi hii! Ndiyo tufikirie zaidi kutupelekea huu mradi wa tatu na wananchi wetu wapate mwanga. Wananchi wa kule siyo wezi kama hawa wa Dar es Salaam au Dodoma. Huku kuna wizi; tukipita leo hapa hapa Dodoma, tutakamata wezi siyo chini ya 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani Shirika lipate hasara, ni wizi mkubwa! Pamoja na mashule haya, viwanda hivi, wanasaga usiku, wote ni wezi. Kwa hiyo, nawaomba sana Wizara ya Nishati na Madini wanisikilize. Operation maalum ifanyike, pamoja na Waheshimiwa Wabunge humu tumo, haiwezekani. Ndiyo nimesikia juzi juzi wanalaumu sana Ma-DC. Leo kuna Wabunge walikuwa Ma-DC humu, walikuwa wanakemea mpaka bangi, Mheshimiwa Mwamoto ni shahidi kule Kibondo, lakini leo ni Mbunge, akiona bangi,...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Anaogopa kura zake zitapotea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Keissy muda wako umekwisha, ahsante sana.

MHE. ALLY M. KEISSY: (Hapa Aliongea Nje ya Microphone)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Keissy muda wako umekwisha. (Kicheko/Makofii)

MHE. ALLY M. KEISSY: ...wote sisi ni wanafiki, Waheshimiwa Wabunge ni wanafiki! (Kicheko/Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Keissy, ahsante sana . Ni kweli.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza kwa siku ya leo. Nitasoma majina machache tutakayoanza nayo mchana:-

Tutakuwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Joyce Sokombi, Mheshimiwa Mussa Mbarouk na Mheshimiwa Maftah Nachuma, ndio tutakaoanza nao mchana.

Baada ya kusema hayo, kabla sijasitisha shughuli, naambiwa kuna taarifa ndogo ya kuongeza tangazo tulilotoa asubuhi kuhusu semina itakayofanyika hapa kwenye ukumbi wa Bunge. Wale mtakaohudhuria semina mnakaribishwa kwa ajili ya chakula Canteen ya Bunge halafu baada ya chakula, mtarudi hapa ili mwendelee na semina.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 mchana leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Wakati tukisitisha shughuli za Bunge asubuhi, nilikuwa nimesoma majina kadhaa ya Waheshimiwa Wabunge watakaochangia kuhusu hoja ya Kamati ya Nishati na Madini na hoja ya Kamati ya Miundombinu.

Waheshimiwa Wabunge, pia kabla sijasitisha Bunge saa 7.00 mchana nilipata taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Zitto Kabwe akitoa maelezo kwenye hii taarifa alioitoa kwamba anataka kueleza Bunge kwamba kuna jambo la Haki za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 51. Kanuni ya 51 kimsingi inamtaka Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye anaona kuna jambo la Haki za Bunge kuweza kutumia Kanuni ya 60 kusimama au kumtaarifu Spika juu ya jambo hilo analotaka kulizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ujumbe huu wa Mheshimiwa Zitto, ameeleza kuhusu Haki za Bunge na kwamba kwa mujibu wa notisi hii aliyotupa, kwa mujibu wa Sheria ya Kinga na Haki za Bunge, Sheria Na. 3 ya mwaka 1988 Sehemu ya 12, 13. Kwa hiyo nitampa nafasi Mheshimiwa Zitto kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni zetu zinataka jambo kama hilo likiwepo, lazima mtu apewe nafasi. Kwa hiyo, nitampa nafasi ya kueleza jambo hilo halafu Kanuni ya 51 itatuongoza. Mheshimiwa Zitto.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuleta na kuwasilisha Bungeni jambo linalohusu Haki za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 51(1) mpaka 51(4).

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hilo linahusu Mamlaka ya Jeshi la Polisi kukamata Waheshimiwa Wabunge wakati Mikutano ya Bunge inaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, unafahamu kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sheria hiyo imezia Mbunge yeyote kukamatwa ndani ya viunga vya Bunge, isipokuwa tu kwa ruhusa ambayo imetolewa na Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hivyo tu, leo mchana nimekwenda Maktaba ya Bunge kuangalia *practice* ya Mabunge mengine ya Jumuiya ya Madola. Kama unavyofahamu ya kwamba licha ya kuongozwa na Katiba, Sheria, Kanuni za Bunge na Maamuzi ya Maspika, pia Bunge letu kama sehemu ya Jumuiya ya Madola inaongozwa kwa taratibu za Jumuiya ya Madola na maamuzi ambayo yamefanywa na Mabunge mengine ya Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mezani kwangu ninacho kitabu cha Erskine ambacho ndiyo msahafu wa taratibu za Mabunge na imeeleza katika sehemu yake ya 14 kuhusiana na *Criminal Law and Statutory Detention, House to be Informed of Arrest*. Kitabu hiki kinafafanua na kimetoa mifano dhahiri ya Mabunge mbalimbali ya Jumuiya ya Madola taratibu gani ambazo zinatumika pale ambapo Mbunge anatakiwa na mamlaka nyingine kwa ajili ya kukamatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna matukio kadhaa ambayo yametokea. Tukio la kwanza ni la Mbunge wa Arusha Mjini. Alikuja Bungeni, akashiriki kwenye shughuli za Bunge, lakini alivyotoka, akakamatwa akaenda kushtakiwa kwa taratibu za Sheria kabisa, lakini mpaka leo hivi tunavyozungumza Bunge lako halina taarifa yoyote kama ukamatwaji wake ulifuata taratibu ambazo zimeelezwa na Sheria yetu ya Kinga na Madaraka ya Bunge na desturi za Mabunge ya Jumuiya ya Madola. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, taratibu za Mabunge zinaeleza kwamba hata kama Mbunge amekamatwa kokote kule kwa kosa lolote lile, baada ya kuwa amekamatwa, mamlaka zilizomkamata ama Hakimu au Jeshi la Polisi, wanapaswa kutoa taarifa ya maandishi kwa Bunge na taarifa ile Spika wa Bunge aisome ndani ya Bunge kuwataarifu Wabunge ni kwa nini Mbunge mwenzao hayupo kwenye shughuli za Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo tunavyozungumza, hakuna taarifa yoyote ambayo imetolewa kwa ajili ya Mbunge wa Arusha Mjini, Ndugu Godbless Lema ambaye mpaka sasa bado yupo mahabusu akiendelea na kesi yake ambayo inaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuna Mbunge ambaye amefungwa. Amehukumiwa kifungo cha miezi sita jela. Kwa taratibu na desturi za Mabunge ya Jumuia ya Madola ilipaswa Hakimu atoe taarifa rasmi kwa Spika wa Bunge kumjulisha Spika wa Bunge sababu za kufungwa kwa Mbunge yule na Spika wa Bunge kutoa taarifa zile ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwataarifu Wabunge kwa nini mwenzao hayuko pamoja nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka tunapozungumza sasa, huu ndiyo Mkutano wa Kwanza wa Bunge, wiki ya pili hii toka Mbunge huyo wa Jimbo la Kilombero, Ndugu Peter Lijualikali akamatwe na hakuna taarifa yoyote ambayo imetolewa ndani ya Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu matukio hayo yote ya nyuma hakuna hatua zozote ambazo Bunge lako limechukua kuhakikisha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge imetekelezwa, Jeshi la Polisi sasa limeona hiyo ni kawaida. Jana Mbunge wa Singida Mashariki akitoka nje ya geti la Bunge, amekamatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami personally nilimpigia simu Mheshimiwa Spika kumuuliza, umepata taarifa za Mheshimiwa Tundu Lissu kukamatwa? Akasema wewe ndiye unaniambia. Kwa maana hiyo ni kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu alikamatwa bila, siyo tu approval ya Spika wa Bunge, angalau hata kumwandikia sms Spika wa Bunge kwamba tunamkamata Mbunge wako. Ni dharau kubwa sana kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mhimili yote ya dola inalinda hadhi yake kwa vivu wa hali ya juu. Mhimili wetu wa Bunge umechezewa mno na haulindwi, hauchukui hatua zozote za kulinda hadhi yake.

MBUNGE FULANI: Kweli!

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninavyozungumza hapa, mimi Polisi wanani subiri hapo nje. (Kicheko/Makofi)

MBUNGE FULANI: Kweli!

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Nimetumia tu privilege ya Bunge, sijatoka nje ya geti kwa sababu hawawezi kuingia kwenye precinct ya Bunge, lakini najua nitakapotoka watanikamata na niko tayari wanikamate, lakini taarifa hii iweze kufahamika kwamba angalau basi wewe kwenye Kiti hicho upate taarifa ili kuweza kuhakikisha kwamba taratibu zote zinaweza zikafuatwa. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Tutoke Wabunge wote, tutamlinda wenyewe.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yote haya ya awali, jambo hili kwa sababu linahusu haki za Bunge, ni jambo ambalo linapaswa kujadiliwa na kutolewa resolution ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kama jana nilivyosema, huu ni mtego wa panya; leo watakamatwa Wabunge wa upande huu wa kushoto kwako, kesho watakamatwa wa upande huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba haya ni mambo mapya. Huko nyuma tumeshawahi kuwa na Mbunge wa Mbarali, alikamatwa. Bahati nzuri Spika, Mheshimiwa Anna Makinda alikuwa analinda hadhi ya Bunge kwa namna yoyote ile. Aliondolewa polisi. Alikamatwa Mbunge wa Nzega kipindi kile, kabla Nzega hajagawanywa, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla, ilifanyika intervention na hakulala Polisi aliondolewa; na alikuwa Jimboni wala hakuwa Dodoma. Hii ya sasa ni kwamba Wabunge wanakuja kunyakuliwa Dodoma, Bunge likiwa linaendelea. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Uingereza mwaka 2011 kulitokea jambo kama hili. Ikaenda hoja kama hii ndani ya Bunge, Bunge likapitisha resolution kwamba linawekea nguvu Sheria yake ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge kwamba Mbunge yeyote atakapokuwa anataka kukamatwa kwa makosa yoyote ni lazima mamlaka za ukamataji zipate baraka ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hili jambo linatuhusu sisi wote hapa bila kujali vyama. Kwa hiyo, naomba nitoe hoja kwamba Bunge hili liazimie kutilia nguvu Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zitto, kabla hujamalizia, maana naona unasema unataka kutoa hoja. Kanuni ya 51(3) ni mpaka mimi nikishaongea ndiyo utaruhusiwa aidha utoe hoja ama tutaendelea na utaratibu mwingine. Malizia maelezo yako.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 51(3) naomba sasa utoe maelezo yako. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotoa maelezo kuhusu taarifa ya Mheshimiwa Zitto na kwamba alikuwa amesema angetaka kueleza kuhusu Haki za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 51, sitayarudia yote isipokuwa kwa ufupi ili kuweza kuyaweka vizuri maelezo nitakayoyatoa.

Mheshimiwa Zitto ameeleza kuhusu Mamlaka ya Jeshi la Polisi kukamata Wabunge wakati wakiwa kwenye shughuli za Bunge ama wakati wakifanya shughuli za Bunge ama wakati shughuli za Bunge zikiendelea; na ametoa maelezo kwamba ukiangalia kwa ujumla uendeshaji wa Bunge katika Jumuiya ya Madola ni kwamba Spika lazima apate taarifa ama Spika ndiye ambaye anatakiwa kutoa ruhusa kabla Mbunge hajakamatwa. Ameeleza pia japokuwa wakati wa maelezo yake hajatueleza ni kifungu gani lakini ametupeleka kwenye Sheria ya Haki na Madaraka ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, wakati akieleza hayo, ametoa mifano ya Wabunge mbalimbali ambao wamepata tabu. Amemwelezea Mheshimiwa Godbless Lema, akamwelezea Mheshimiwa Peter Lijualikali.

Mheshimiwa Godbless Lema kwa mujibu wa taarifa aliyoitoa ni kwamba alikamatwa akiwa anatoka Bungeni na mpaka leo hajaweza kutoka kifungoni, lakini pia ametoa maelezo kuhusu Mheshimiwa Peter Lijualikali akisema kwamba amefungwa kifungo cha miezi sita lakini kwa mujibu wa taarifa alizozisoma kuhusu uendeshaji wa Mabunge katika Jumuiya ya Madola ni kwamba Hakimu alipaswa atoe taarifa kwa Spika na Spika aje atoe taarifa Bungeni kuhusu Mheshimiwa Godbless Lema, lakini pia kuhusu Mheshimiwa Lijualikali.

Waheshimiwa Wabunge, katika maelezo yake Mheshimiwa Zitto, ameeleza kwamba kwa kuwa hayo matukio mawili yalipotokea Bunge halikuchukua hatua yoyote na hivyo Polisi wameendelea na vitendo hivyo ikiwa ni pamoja na kumkamata Mheshimiwa Tundu Lissu jana tarehe 6 Februari. Ameeleza pia wakati akimalizia maelezo yake kwamba hata yeye anazo

taarifa kwamba naye atakapotoka leo atakamatwa, maana yake atakapotoka nje ya maeneo ya Bunge. (Makofij)

Waheshimiwa Wabunge, Sheria tuliyonayo sisi ili tuweze kupata mwelekeo wa pamoja, Kanuni ya (5) inaeleza hivi, nitasoma fasili ya (1). "Katika kutekeleza majukumu yake yaliyotajwa katika Ibara ya 84 ya Katiba, Spika ataongozwa na Kanuni hizi na pale ambapo Kanuni hazikutoa mwongozo, basi Spika atafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyngine za nchi, Kanuni nyngine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge pamoja na mila na desturi za Mabunge mengine yenyе utaratibu wa Kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania."

Waheshimiwa Wabunge, pale ambapo Kanuni zinatoa maelekezo ya nini cha kufanya, tutazitumia Kanuni. Pale ambapo Kanuni hazina jambo la moja kwa moja namna ya kufanya, basi tutatumia utaratibu aliota maelezo Mheshimiwa Zitto.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, Sheria yetu ya Haki na Madaraka ya Bunge Kifungu cha 12 na 13 lakini pia kuna Kifungu cha (6), (7) na cha (8) ukivisoma hivi vyote kwa pamoja vitakupa maelezo ni katika maeneo gani ambayo Mbunge hataweza kukamatwa wala Mheshimiwa Spika hata wangemtaarifu hawataweza kumkamata.

Sasa maelezo kwa ujumla kwa sababu Sheria hii pamoja na kwamba iko kwa Kiingereza, sina haja ya kuisoma, iko wazi na wote naamini tunazo. Ukisoma Kifungu cha 12 kinaongelea kuhusu mambo ya madai ama kesi za madai, siyo kesi nynginezo.

Sasa katika maelezo yote aliyoyatoa Mheshimiwa Zitto, niseme wazi, Kiti kimemwelewa na kwa ujumla wote, siyo kwamba Kiti kwa namna yoyote kinafurahia Mbunge akipata tabu, lakini Mbunge atakapokuwa amekamatwa kwa kosa ambalo siyo la madai, Spika kupewa taarifa kwa mujibu wa namna Mabunge mengine yanavyoendesha taratibu zao, za kwetu sisi kwa kuwa tunayo sheria inayosema hivyo, basi tutafuata utaratibu ulioko kwenye sheria.

Makosa ambayo siyo ya madai Spika kupewa taarifa, sawa ni utaratibu mzuri, lakini asipopewa haimaanishi Mbunge hatakamatwa kwa kosa ambalo siyo la madai. Makosa ya madai ndiyo ambayo sheria hii inayaongelea na kwamba lazima Spika kwa namna moja ama nyngine itolewe taarifa...

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima, naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo, Kanuni ya 51 inayoeleza kuhusu masuala yanayohusu Haki za Bunge na ukisoma fasili ya (3) inasema hivi: "endapo Spika ataamua kwamba jambo hilo linahusu Haki za Bunge, basi atampa nafasi Mbunge husika kutoa hoja yake kisha hoja hiyo itapewa kipaumbele katika kupanga shughuli nyngine zote za kikao kinachofuata." Sawa.

Katika utaratibu, unaendelea sasa fasili inayofuata ya (4). Fasili ya tatu inanipa mimi maelekezo kwamba nikishajiridhisha kama hoja iliyotolewa ni ya kuhusu Haki za Bunge, basi ningempa nafasi sasa Mheshimiwa Zitto atoe hoja ili Bunge lijadili.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo niliyotoa, kwa mujibu wa sheria yetu tuliyonayo kwamba inahusu makosa...

MHE. HALIMA J. MDEE: Taarifa!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima, tafadhali, nimesimama. naomba ukae. Mheshimiwa Halima naomba ukae. Naomba ukae Mheshimiwa Halima, nimesimama.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, baada ya maelezo hayo na kwa kutumia hii Kanuni ya 51, sitaitoa hiyo hoja ili iamuliwe wala kujadiliwa na Bunge kwa sababu suala lenyewe linalotaka kujadiliwa halihusu mambo ya makosa ya madai.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Baada ya kusema hayo, tutaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea. Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu
na
Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini**

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Dkt. Christine Ishengoma atajiandaa Mheshimiwa Mendrad Kigola.

MHE. HALIMA J. MDEE: Huwezi kutuburuzaburuza hapa!

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kunipatia nafasi hii. Napenda sana kujadili taarifa hizi mbili ya Nishati na Madini pamoja na taarifa ya Miundombinu. Nitaanza kwa kujadili...

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaishukuru Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya kwa upande wa Nishati na Madini. Naomba kuendelea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ryoba naomba utoke nje, Mheshimiwa Ryoba naomba utoke nje.

MHE. MARWA R. CHACHA: Sitoki.

NAIBU SPIKA: Sergeant-At-Arms mtoeni Ryoba nje.

MHE. HALIMA J. MDEE: Unapeleka peleka mambo hovyo hovyo tu!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mollel zima microphone yako.

MHE. HALIMA J. MDEE: Bunge linakuwa kama...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima tafadhali kama unatoka nje, toka kwa heshima tafadhali.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mambo ya kipuuzi...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima, toka nje kwa heshima umeamua mwenyewe ondoka.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya tafadhali toka nje kwa heshima.

WABUNGE FULANI: Hooo! Huuu!

(*Hapa Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani walitoka nje ya ukumbi wa Bunge isipokuwa Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma aliyebakia ndani ya ukumbi wa Bunge*)

NAIBU SPIKA: Ester Bulaya, toka nje kwa heshima. Mheshimiwa Christine naomba uendeleee.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naomba kuwapa pongezi Wizara ya Nishati na Madini na hasa kwa upande wa umeme. Kwa umeme wa REA wamefanya mambo mazuri sana, wamesambaza umeme vijiji na nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vijiji ambavyo bado hawajasambaza waweze kuvisambaza, Wizara inasema kuwa kuwa Awamu ya Tatu watasambaza vijiji vyote. Kwa hiyo, naomba kweli waweze kusamba vijiji vyote kwa Awamu hiyo ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme wa TANESCO, na wenyewe wanafanya vizuri ila kuna sehemu ambazo bado umeme haujafikiwa vizuri. Kwa hiyo, sehemu ambazo bado hazijafikiwa vizuri kwa mfano Mkoa wangu wa Morogoro, kuna kata pale Manispaa hazijafikiwa na umeme. Kwa mfano Mindu, pamoja na Kihonda na kata zingine, Kigegeya naomba sana waangalie waweze kuipatia umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme wa TANESCO, kwa upande wa TANESCO imeonekana kuwa wanadai, na kweli wanadai mashirika mbalimbali kwa mfano magereza, mashule na vitu vingine, kudai sio vizuri. Nilikuwa naomba sana Serikali yetu angalau iweze kupunguza hayo madeni kwa wakati na ifikie kuwa hayo madeni yamekwisha kabisa. (Makofifi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wachimbaji wadogo wale wa madini, uwekezaji tunaupenda na tunaupenda sana kusudi tuweze kuendelea nchi yetu. Ila nilikuwa naomba kwa wale wachimbaji wadogo wadogo waweze kupewa mahali na wenyewe waweze kuchimba, waweze kuijendeleza wenyewe. Pale wanapowatoa pale abapo wawekezaji waweze kuwekeza, waweze kupata mahali pa kuchimba na waweze kupewa ruzuku na hiyo ruzuka iweze kupewa kwa wakati. (Makofifi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa bajeti, bajeti inatolewa, bajeti ya Wizara zote tunapanga vizuri, bajeti ya Wizara hii ya Nishati na Madini tumelezwu kuwa imeandaliwa vizuri, lakini inapokuja kutolewa haitolewi kwa wakati. Kwa hiyo, naomba kuwa mtiririko wa wa fedha wa Wizara hii uweze kutoka kwa mpangilio kusudi wananchi waweze kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kuwa Tanzania ya viwanda ndio tunayokwenda nayo. Bila ya nishati ya umeme hatuwezi kuwa na viwanda, kwa hiyo, naomba sana hasa huko vijiji ni umeme uweze kuwepo hata mjini tuwe na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miundombinu na yenye natoa pongezi sana kwa Wizara hii kwa sababu wameweza kutengeneza barabara nyingi za lami, nawapa pongezi, wameweza kuunganisha mikoa mbalimbali kwa barabara za lami, nawapa pongezi. Ila nawaomba sana kwenye barabara zile ambazo miji ya mikoa haijaunganishwa kwa mfano Kigoma na Kagera na mikoa mingine, naomba sana lami iweze kutumika kusudi watu tuweze kupata usafiri kwa urahisi pamoja na kusafirisha mizigo kwa urahisi na hayo ndio maendeleo. Serikali yetu inafanya vizuri lakini naomba iweze kufikia na mikoa hiyo ambayo bado haijafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa bajeti pia na yenye iweze kutolewa kwa wakati. Kwa upande wa makandarasi nafikiri wakiweza kulipwa kwa wakati wataweza kufanya mambo mazuri sana. Kwa hiyo, na wenyewe tuwaangalie kudai madeni ambayo hawalipwi huwezi kuwa na moyo wa kuendelea na kazi kama hujalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuongelea reli ya kati. Wananchi wengi wanasaafiri na reli ya kati, wananchi wengi wanasaafirisha mizigo yao na reli ya kati. Kutoharibu barabara inapendekeza hasa kusafiri na reli ya kati, kwa hiyo kujenga reli ya kati kwa standardsgauge Serikali naipa pongezi sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipa pongezi sana kwa kusaini mkataba amba o umesainiwa juzi juzi kusudi Uturuki waanzu kujenga ile reli ya kati kwa standardgauge kwa kuanzia Dar es Salaam kuja mpaka Morogoro ikiwa wamu ya kwanza. Na naamini wananchi wengi watasaafiri kwa reli kwa sababu itatumia muda mfupi kama mlivyo sikkia kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma ni masaa mawili tutamia. Waheshimiwa Wabunge ikiisha naomba wote mtumie hii reli tuweze kuunga mkono Serikali yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano, minara ya simu ni muhimu sana. Kuna vijiji vingi hasa Mkoo wangu wa Morogoro amba o bado hawajapata matumizi ya simu kwa sababu hakuna mawasiliano. Kwa hiyo, huo ni mfano tu, ni mikoa mingi, vijiji vingi ambayo minara hakuna kwa hiyo mawasiliano yanakuwa hafifu. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali, iweze kutimiza ahadi hiyo ya kupeleka mawasiliano hasa vijiji ni. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ujenzi Morogoro. Chuo cha Ujenzi Morogoro ni kizuri sana na kinatoa wanafunzi wengi lakini hakijasajiliwa. Naomba kisajiliwe kusudi wahitimu waweze kujulikana vizuri sana naungana na Kamati na waweze kuajiriwa kwa sababu bado tunawahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ya Tanga, Bagamoyo na bandari zinginezo kusudi tuende na maendeleo naomba sana tuweze kutimiza na bajeti iweze kutoka ya kumaliza hizi bandari ambazo nimezitaja kwa mfano bandari ya Tanga itasaidia kusafirisha mizigo ya Mikoa ya Kaskazini pamoja na nchi jirani za huko Kenya, Uganda na nchi zinginezo. (Makofii)

Mheshimiwa Niabu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia hii nafasi ya kutoa machache na kuchangia kwenye Kamati hizi nawapa pongezi sana mmefanya kazi nzuri sana, nashukuru na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Amina Makilagi ajiandae.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache.

Kwanza kabisa nianze na pongezi, natoa pongezi kwa Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na Naibu Waziri wamefanya kazi nzuri sana. Naibu Waziri alikuja mpaka kwenye jimbo langu akieleza mpango mzima wa Serikali wa umeme vijijiji. Ukweli katika ziara yake ilikuwa nzuri sana na wanachi wanakupongeza sana walikuelewa vizuri. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nkinukuu speech za Naibu Waziri ambazo zilielewaka kwa kila mtu. Nilipenda sana usemi wake, alisema masuala ya umeme sio kwamba unapelekwa umeme halafu wananchi wanaanza kuangalia nguzo, kwa sababu tumeona kuna vijiji vingi sana vinakuwa umeme umepita hasa huu umeme wa Gridi ya Taifa, vijiji vingi sana vinakuwa havijapewa umeme umepita tu pale. Lakini akasema kwamba Serikali itaangalia kwamba vijiji vinapewa umeme, umeme unaenda kwenye nyumba za watu, hiyo nilipemda sana na akasema kwamba, vitongoji vyote vinapewa umeme, akasema kata zote zitapewa umeme, bahati nzuri sana alisema tarehe 15 Desemba, makandarasi wanaanza kusaini mikataba halafu wanaanza kazi ya Awamu ya III, umeme wa REA vijijini unaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi speech ni nzuri sana, naifurahia sana Serikali kwa mpango mzuri na bahati nzuri katika quotation yake ni kwamba zahanati zote zitapewa umeme, shule za msingi zote zitapewa umeme, vituo vya afya, pamoja na hospitali, hilo ni jambo zuri sana. Sasa niiombe tu Serikali kwa ushauri wangu kama tumeponga mpango umekamilika na tumeshawaambia wananchi, kwa mwaka huu wa fedha ambao tunaingia mwaka 2017/2018 basi tufanye utekelezaji ambao unaonekana kwa wananchi, isionekane tumeponga speech nzuri halafu hazitekelezeki. Hii itatusaidia sana na wapiga kura wetu watatusaidia sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kwenye jimbo langu nina kata 16, katika kata 16 ni kata sita tu zina umeme, ina maana kata 10 hazina umeme. Nina vijiji vingi sana, nikianza kuorodhesha hapa naweza nikachukua muda wote kwa kutaja vijiji tu. Sasa kwa sababu Naibu Waziri alikuja kule aliahidi wananchi, naendelea kuiomba Serikali kwamba vile vijiji vyote vya Jimbo la Mufindi Kusini, ambavyo havijapatiwa umeme kwenye mwaka huu wa fedha angalau katika kata 10 tufikie hata nusu. Wakipata kama kata tano kwa mwaka 2017/2018 kwa kweli nitaishukuru sana Serikali. Hiyo naomba sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile leo tulikuwa tunajadili kwenye semina vifo vya mama na mtoto, na ni kweli sababu kubwa inaonekana kwenye zahanati na vituo vya afya hakuna umeme. Na unaweza ukaona mtoto amezaliwa labda hajafikia umri wake, mtoto anatakiwa aongezewe labda oxygen kijijini hauweze kuongezewa oxygen kama hakuna umeme. Imekuwa ni tatizo kubwa sana. Kuna zahanati nyingine wanatumia kule zile taa tunaita koroboi, sasa hilo Serikali lazima iangalie vizuri sana ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili nakuja kwenye masuala ya miundombinu. Kwenye Jimbo la Mufindi Kusini kila siku huwa ninasema, sisi maeneo yetu ni maeneo ya mvua sana, bahati nzuri sana namuomba Waziri wa Ujenzi aangalie sana ahadi ambazo zilitolewa na Rais na aangalie zile ahadi ambazo ziko kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi. Kuna barabara ambazo, upembusi yakinifu ulishakamilika tayari. Hazihitaji kwamba tunaanza kuandaa upembusi yakinifu, upembusi yakinifu ulishakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mfano kuna barabara hii ya Nyororo mpaka Mtwango pale kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini, kuna barabara kutoka Mafinga mpaka Mgololo, kuna barabara ya kutoka Kasanga mpaka Mtambula. Hizi barabara zimeandikwa mpaka kwenya llani ya Chama cha Mapinduzi kwamba watatengeneza kwa kiwango cha lami, na

kuna sababu sio suala la kutengeneza kiwango cha lami lazima kuwe na sababu kwa nini upeleke barabara kule? Kwenye Jimbo langu la Wilaya ya Mufindi kuna viwanda vingi sana, na vile viwanda siku zote nasema, Pato la Taifa tunategemea katika viwanda vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Tanzania tumesema Tanzania ya viwanda, kuna viwanda vingine inabidi vifufuliwe au vijengwe vipyta. Sisi kule hatufufui viwanda, viwanda viko tayari lakini tuna matatizo ya barabara. Na ninavyoongea saa hizi, mvua kule inanyesha sana, sisi hatuna uhaba wa mvua. Tumepewa neema na Mwenyezi Mungu, lakini zile barabara pamoja kwamba; tumeimarisha kwa kiwango cha kokoto inatakiwa tuweke kiwango cha lami. Bahati nzuri, kwenye Mpango wa Mwaka 2014/2015 upembuzi yakinifu mimi walishakamilisha barabara ya Nyororo kilometra 40. Sasa naomba kwenye mwaka huu wa fedha amba ni 2017 tunaounza kesho kutwa, kwenye bajeti ninaposoma nione kwamba tayari Wizara imejipanga kwa ajili ya kujenga ile barabara kiwango cha lami kama ilivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nije kwenye masuala ya mawasiliano. Mawasiliano ndio yanayounganisha nchi, mawasiliano ndio inayounganisha vijiji, kata, na vitongoji. Nakumbuka mwaka 2013/2014 kipindi kile Waziri wa Mawasiliano alitoa taarifa alitupatia na barua kwamba minara ya simu itajengwa kwenye vijiji vile ambavyo hakuna minara ya simu, bahati nzuri na mimi nilipewa. Kuna kata moja ya Idete, ile kata kutoka Mafinga Mjini mpaka uikute hiyo kata ni kilometra 160. Kata ile ina vijiji vikubwa tatu, kuna Idete, Holo na Itika, ni vijiji vikubwa, yaani kijiji hadi kijiji sio chini ya kilometra 40 lakini hakuna mnara hata mmoja, hakuna mawasiliano.

Naomba vijiji vile vipewe mawasiliano kama waziri alivyoahidi wa nyuma; kwa sababu Waziri hata ukibadilishwa wizara, ofisi inakuwepo naomba vijiji vile vya Idete, Holo na Itika viweze kujengewa minara. Na kuna kata nyingine, hii kata ya Ihoanza ambayo hiyo kata tunapakana na Mkoa wa Mbeya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuna vijiji vingine kule kwa mfano kijiji cha Katangwa, lyai hawana mawasiliano kabisa na makao makuu ya wilaya kwa sababu hakuna minara ya simu. Naomba na ile sehemu yote ambayo Waziri niliwahi kumpa majina basi apelike huduma hii ya mawasiliano kama alivyoahidi. Hii itatusaidia sana kuhakikisha kwamba huduma kwa wananchi tunafikia kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wanaweza kuugua kijiji kule hakuna mawasiliano hata ya hospitali, wakinamama wengine, wanajifungulia porini au wanajifungulia nyumbani kwa sababu hakuna mawasiliano hata wakipiga simu tukajua kwamba kuna gari inabidi ipelekwe kule *ambulance* kutoka Mjini Mafinga ni kilometra karibu 120 na kama hakuna mawasiliano basi tunampoteza mama huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iwekee mkakati kuhakikisha kwamba sehemu zote nilizotaja zinaweza kujengewa minara ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono ila naomba Serikali ifanye utekelezaji, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Desderius Mipata atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Makilagi, Mheshimiwa Maftaha Nachuma ajiandae.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii namshukuru pia Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima, naungana na wenzangu kuchangia

katika taarifa za Kamati hizi mbili. Mimi ni mmoja kati ya Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini. Nianze na taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpungeze Waziri na watendaji wake wote pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa hakika inaonekana kwa Watanzania, isipokuwa kitu kinachokwamisha ni pesa zinazotolewa zinawafanya majukumu yaliyopangwa yasifikasiwe kwa wakati, lakini juhudhi tunaiona. Kwa hiyo, niishauri Serikali kuhakikisha kwamba katika eneo la usambazaji umeme na kwa vile tumejitangazia kila mahali umeme ufike pawepo nidhamu ya utoaji wa fedha kuendana na utaratibu wa kibajeti kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wananchi tulishakubaliana kwamba tunatoa tozo kwenye mafuta, pesa ambayo ingeenda kwa mwananchi, tunamkama ili pesa iende kwenye usambazaji wa umeme. Kwa hiyo, hatuna sababu ya kukosa pesa kwa jukumu hili. Lakini nisifie kwamba katika usambazaji wa umeme sisi Wilayani Nkasi tumepata umeme katika vijiji vya Kundi, Kibande, vijiji vyote mpaka kufika Namanyere kwa barabara hiyo, lakini bado tatizo la usambazaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifika pale Nkundi, Kipande, Katawa, Milundikwa, Chala, Kasu, Kacheche na Kanondokazi, wapo wananchi wengi wanahitaji umeme na wanagombana leo haujawafikia. Umefika kijijini, lakini haujafika *angle* ile pale na ile pale. Pawepo utaratibu maalum wa usambazaji, ili wote wanaohitaji umeme waweze kupata, hilo la kwanza. Na wengine hapa wanaingiza siasa, yupo Mwenyekiti wangu mmoja wa Nkundi pale anasema aliyezuwia tusipate umeme upande huu hapa ni Mheshimiwa Mipata, lakini ana sababu zake. Naomba tugawane, ni sungura mdogo lakini tugawane wote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo pia ya kupeleka umeme ambayo bado katika eneo langu, kama Kata ya Sintali, Kata ya Ntuchi, Wampembe, Ninde, Kizumbi, Kala na vijiji ambavyo vilisahauluka katika Awamu ya Pili, vijiji hivyo ni Katani, Malongwe, Komolo Ilipamoja na Kisura. Ni vijiji ambavyo viko jirani sana na maeneo umeme unapita kwa hiyo, wanauangalia tu hivi. Jambo hili si jema sana, linawatia simanzi na wanaona wakati mwingine ni kama tumewafanya jambo ambalo sio lenyewe, kumbe sio kwa nia mbaya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipotutembelea niliweza kumfikisha kijiji cha Wampembe na njiani kote huko aliona jinsi watu wanavyohitaji umeme. Na wamebaki na matumaini na kila mara tukiwaambia Awamu ya Tatu inafuta machozi yenu wote, wote wamekuwa hawaamini. Kwa hiyo, naomba awamu hii ianze mara moja ili maeneo haya niliyoyataja yote yaweze kupata umeme, hasa njia ndefu ya kupeleka mwambao wa Ziwa Tanganyika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipo Kitengo cha Utafutaji wa Madini, mimi kama Mjumbe wa Kamati hii tumekuwa tukizunguka huku na kule tunaangalia jinsi wananchi wanavyopata ajira katika uchimbaji wa madini mdogo mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo wadogo inaonekana ni ajira ambayo kwa kweli, fursa hiyo sehemu nyingine hatuna, naomba kitengo hiki kije kitafute Mkoani Rukwa, tuna madini yakutosha, lakini hawajatafuta. Tumemuomba Waziri kwenye Kamati kwamba watupe *potentials* zilizopo ili wananchi wenyewe waangalie na kama kuna mashirika mengine ambayo yanaweza yaka-chip in waweze kuangalia katika maeneo haya kwa sababu tumeona ni muhimu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni barabara. Naungana na wote wanaosema kuna kazi nzuri ya barabara inayofanyika na sisi tuna barabara ya lami kutoka Sumbawanga

kwenda Kibaoni inajengwa vizuri sana kwa kiwango cha lami na kasi imeongezeka. Sasa hivi barabara inasogea pale Kichala na nyingine inatoka Kibaoni, imeshafika Namanyere tayari kwa hiyo, bado kipande kidogo sana. Naomba wasisimame, kasi hii iliyopo sasa iendelee ili wakamilishe hiyo barabara tuweze kunufaika na wananchi waweze kunufaika na matunda ya Chama cha Mapinduzi, wasisimame, watusaidie. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hizi pia zipo za Halmashauri ambazo zinatusumbua. Kuna barabara ya Kitosi - Wampembe, ambayo Mheshimiwa Rais kabla hajawa Rais aliweza kunipa shilingi milioni 500, nayo inaanza kususua na wataalam wameanza kuitengea hela kidogo kidogo, naomba waendelee kuitengea. Alipokuwa kwenye Wizara walitenga hela ya kutosha, sasa hivi hawatengi, nitawashitaki kwake. Hakikisheni kwamba mnatenga ya kutosha. Iko Barabara ya Ninde - Namanyere na Barabara ya kutoka Kasu kwenda Myula, bado inasuasua sana hii, mtusaidie bila kuacha ile ya kupeleka Chamiku pamoja na maeneo mengine. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la mtandao wa simu. Suala la mtandao wa simu kwa kweli limekuwa ni huduma muhimu. Kata yangu moja ya Kala imekuwa haina kwa kipindi kirefu na sasa hivi wanaonekana kama wametengwa na wanajimbo wengine na Watanzania kwa ujumla.

Naomba nitumie nafasi hii kumuomba Waziri, amekuwa akitoa ahadi kila wakati, lakini wananchi hawajapata eneo la Kala, hata wale wa eneo la Wampembe na Ninde wamekuwa wakipata on and off; on and off! Wakati mwingine unasimama wakati mwingine unapatikana! Sasa haitusaidii sana, tunaomba huduma hii imekuwa muhimu kibiashara, katika huduma za jamii, katika kuhimiza mambo ya kiafya kwa hiyo, ni muhimu iende kila mahali sawia itatusaidia sana. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nimalizie kwa kusema kero moja, kijiji changu, kijiji cha Kasapa wananchi wake wamelima mashamba, yale mashamba yamefyekwa na wahifadhi wa Msitu wa TFS. Jambo hili limekuwa kero sana na nilipojaribu kufuatilia sana wale jamaa ni wakatili sana, wameshindwa hata kuwaruhusu wananchi wakatunze mazao zaidi ya hekta 2000 ambazo wameshalima. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wanakijiji wote wanashinda kijijini hawaendi kutunza mazao yao, jambo ambalo ni kero kubwa sana na kwetu kwa kweli mvua zinanyesha vizuri, naomba sauti hii ifike kwa wahusika wote, waruhusiwe tu wakatunze saa hizi mazao yao ili wasife njaa, hawana kimbilio lingine lolote zaidi ya kilimo ambacho wanatumia jasho lao. Zaidi ya kaya 395 na watu 2,500 wanakaa hawaendi shamba kwa sababu msitu umezunguka. Na sababu ni kwamba, msitu wenyewe walikuwa hawajaweka vibao. Juzi ndio wanatuwekea vibao mpaka mlangoni, jambo ambalo wananchi hawapati nafasi hata ya kutoka mlangoni kwenda kulima. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii ni kero na kijiji hiki kwa kweli kilifanya vizuri hata kwenye uchaguzi. Mimi nilipata kura zote, Mheshimiwa Rais alipata kura zote. Leo hii wanapoona matendo kama haya yanayofanywa na watendaji wao wanakuwa wanasema kwa kweli, labda Serikali imetuchukia, kumbe Serikali hii ni ya wanyonge, inasikia sauti, nafikiri sauti hii ataisikia Mheshimiwa Rais na atatoa maelekezo. Nimeenda kumuona Mkuu wa Mkoa hajanisaidia katika hili. Naomba maelekezo yatolewe ili waweze kusaidiwa angalau wakavune mazao yao. Sisemi wakae siku zote, hii ni masika na ajira yao ni hiyo, kwa hiyo, mashamba zaidi ya hekta 2000 yamekaa bila kutunzwa tutegemeetutakuwa na njaa ya ajabu Mkoa wa Rukwa ambayo sio stahili yake. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kunipa nafasi hii, Mungu akujalie sana. Ahsante sana. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Amina Makilagi atafuatiwa na Mheshimiwa Maftaha Nachuma, Mheshimiwa Ignas Malocha ajiandae.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Lakini vilevile nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama na kuweza kuchangia katika hoja hii muhimu iliyo mbele yetu katika sekta hizi muhimu za miundombinu na nishati. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kutimiza miaka 40 kwa kuzaliwa kwake kwa mafanikio makubwa sana katika kuwaletea wananchi maendeleo, ikiwemo miundombinu ya barabara, reli, mawasiliano ya simu na bandari na kadhalika. Maana ni ukweli usiopingika kwamba kabla ya miaka 40 ya Chama cha Mapinduzi, hali yetu haikuwa namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukishukuru Chama cha Mapinduzi na ninaomba kikitakia kila la heri katika miaka mingine 40, kiendelee kutekeleza llani yake na miaka mingine 40 tuwe tumefika mbele zaidi kuliko ilivyo sasa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wote wa Tanzania walioshiriki katika uchaguzi wa kata 19 katika chaguzi ndogo za Madiwani na uchaguzi mdogo wa Jimbo la Dimani ambako Chama cha Mapinduzi kiliibuka mshindi wa kishindo kwa kupata kata 18 na Jimbo la Dimani Chama cha Mapinduzi kilipata 75%. Kipekee nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Tanzania na ninaomba niwaambie kwamba imani huzaa imani na leo tunazungumzia suala la miundombinu ya barabara, tunazungumzia mawasiliano ya simu, tunazungumzia suala la nishati vijijini, waendelee kuwa na imani na CCM, yote tuliyowaahidi kuititia llani ya Chama cha Mapinduzi tutayatekeleza. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya utangulizi huo naomba sasa njielekeze kwenye mambo machache niliyoyachagua kuyatilia mkazo. Jambo la kwanza naomba niwakumbushe Wabunge kwamba katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2016/2017 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha fedha nyingi sana kwa ajili ya maendeleo ya miradi ya barabara, reli, nishati na kadhalika. Lakini kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa hali inaonekana kwamba fedha hazipelekwi kwenye miradi kama ilivyokusudiwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuishauri Serikali, kwa sababu inabana matumizi katika kuendesha shughuli zake, inakusanya mapato, imebuni vyanzo mipya. Ninachoiomba Serikali fedha hizo zilizotengwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo ninaomba ipelekwe ili miradi iweze kutekelezwa kama ilivyokusudiwa kwa sababu, nimepitia ripoti za Kamati mbalimbali zilizowasilishwa, Kamati ya Miundombinu kabisa inaonekana hata 30% bado hawajafikia. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kutazama Kamati ya Nishati na Madini kiwango kilichopelekwa ni zaidi ya 25% tu. Ninaiomba Serikali na kwa kweli na Waziri wa Fedha yuko hapa, hebu tujipange vizuri kupeleka fedha za maendeleo katika miradi iliyokusudiwa kwa sababu kama haikupelekwa fedha hata kama Mawaziri ni hodari namna gani, hata kama watendaji ni hodari namna gani hatutafikia lengo lilitokusudiwa.

Naomba Serikali ibuni mipango mipya ya kuhakikisha fedha za miradi ya maendeleo zinapelekwa ili miradi yote iliyokusudiwa iweze kutekelezwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali kuna miradi mingi ya maendeleo ya miundombinu ya barabara, miundombinu ya reli na miundombinu mingine, na hasa hapa nizungumzie ya barabara. Kuna miradi mingi iliyoanzishwa mwaka 2010 haikukamilika, 2011 haikukamilika na sasa hivi tuko mwaka 2017 miradi ya baadhi ya barabara haijakamilika na alipomalizia Mheshimiwa Mipata na hapa nitoe mifano ya barabara za Mkoa wa Mara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafurahi sana Waziri wa Miundombinu juzi amekwenda na amejionea mwenyewe zile barabara hali yake ilivyo, inasikitisha. Barabara ya kutoka Makutano, Butiama kwa Baba wa Taifa, barabara ya kutoka Butiama kuelekea Mugumu mpaka Loliondo, mpaka Mto wa Mbu, kwa kweli ni hatari. Ile barabara tangu imeanza kujengwa hakuna kinachoendelea, Mheshimiwa Waziri amekwenda amejionea kuna wakandarasi wazalendo zaidi ya 10 wanajenga ile barabara, mimi nimekata tamaa kwa sababu ninachokiona sasa hivi ni kuchimba tu udongo wanaleta barabarani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ile ni barabara ya kihistoria, ni barabara aliopita Baba wa Taifa kudai uhuru wa nchi hii, ni barabara ambayo hatupaswi kupiga kelele namna hiyo, Mwalimu Nyerere aliangalia Watanzania wote bila kujijali yeye mwenyewe, leo barabara ya kutoka Butiama kuelekea nyumbani kwake, kwenda Mugumu, kwenda mpaka Loliondo, kwenda mpaka Arusha ili kufungua barabara wananchi wa Mkoa wa Mara na hasa ukizingatia kuna mbuga ya wanyama ya Serengeti, kuna ziwa, kuna uchumi uliotukuka, lakini barabara hii kwa kweli sasa inatuchonganisha kwa wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejaribu kuzungumza, wananchi wa Mkoa wa Mara wana imani na CCM, wamechagua CCM, lakini barabara hii sasa inawafanya wanaanza kujenga wasiwasi.

Ninaomba hatua zichukuliwe, kama Serikali imekuwa ikichukua hatua kwa makandarasi wabovu, makandarasi ambao wako tayari naomba na hatua zinazostahili huyu mkandarasi anayejenga hii barabara atazamwe upya, je, anao uwezo? Kwa sababu nimefuatilia fedha ameshalipwa, ni kwa nini hajengi hii barabara? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sio barabara hii peke yake, barabara zote za ule mkoa haziko sawasawa. Barabara ya Kisorya - Bunda mpaka hapo Mugumu kupita Nyamuswa mpaka Serengeti haiendele! Barabara zote ambazo kwa kweli zimetengewa fedha na zilipitishwa kuanzia mwaka 2010 hakuna kinachoendelea.

Naomba Serikali hebu ichukue hatua za haraka ili Mkoa wa Mara na wenyewe ufunguke kwa sababu, ni mkoa wa kiuchumi. Na ukifunguka kuanzia kule Ukerewe mpaka Mara uchumi wa samaki, uchumi wa madini, uchumi wa mbuga za wanyama na kadhalika. Hata Kaburi la Baba wa Taifa ni uchumi, maana watalii wanakuja kuangalia kaburi, lakini hawana pa kupita kwa ajili ya uchumi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie suala zima la fedha za Mfuko wa Barabara (*Road Fund*). Nimefuatilia kitabu hiki kunaelekea kuna tatizo, hizi fedha pia hazitoki. Sasa ningependa tutakapokuwa tuna *wind up*, hebu Waziri atuambie tatizo ni nini? Maana hii fedha iko kwenye *ringfence*, hazitakiwi zitoke. Kwa nini haiendi kuhudumia Mifuko ya Barabara Vijiji, kumetokea kitu gani? Barabara hazipelekewi fedha, barabara zimeharibika tena ni za vumbi zinazounganisha vijiji na vijiji, kata na kata, lakini hazijengwi kwa Mfuko wa Barabara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nitoe ushauri, kwa sababu zimekuwa zikitengwa fedha nyingi na Watanzania wanakatwa kodi kwa ajili ya kuimarisha hizi barabara za vijiji, barabara zinajengwa na baada ya muda mfupi mvua ikinyesha barabara zinabomoka. Ushauri ninaoutoa hebu tuangalie sasa mbinu mpya, badala ya kuwa tunajenga barabara za vumbi za changarawe na kila baada ya mwaka barabara inaondoka na fedha inapotea hebu twende na mpango mpya sasa wa kujenga hata lami kwa kilometra hata tano, tano. Tunajenga kitu cha kudumu, kuliko mabilioni ya fedha yanateketea na baada ya muda barabara inaondoka, halafu sasa tunatenga nyingine kila mwaka. Hebu naomba tubadilike tujaribu kutumia wataalam wetu wa barabara, hebu watushauri at least tujenge kila kata kilometra tano, tano ili tuweze kupata matokeo ya haraka na ya mapema. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala zima la upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam. Nimefurahishwa na maoni ya Kamati yaliyo kwenye ukurasa wa 35 mpaka ukurasa wa 40. Nayaunga mkono kabisa, na hapa naishauri Serikali na Mamlaka inayohusika, hebu chukueni ushauri walioutoa Kamati ya Miundombinu muufanyie kazi. Ile gati ya kwanza mpaka ya saba zipanuliwe, lakini na ile gati ya 13 na yenewe ijengwe ili Dar es Salaam ipanuke na meli ziweze kuja za mizigo, zinashusha mzigo kwa haraka na uchumi uweze kukua kwa haraka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hapa nishauri, hebu tuangalie na Bandari ya Bagamoyo, ilikuwa kwenye mpango mzuri na maendeleo yalishafikia hatua nzuri, lakini mimi sioni kama inazungumzwa na sioni kinachoendelea. Bandari ya Bagamoyo ingejengwa kama ambavyo tulikusudia na kama ambavyo tuliweka kwenye mpango, nina imani uchumi wa haraka katika nchi yetu ungeweza kupatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nishauri tujenge na bandari ya Tanga kwa sababu, Bandari ya Tanga itatuimrisha zaidi maana itawezesha nchi mbalimbali na ikiwemo na Bandari ya Musoma. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kengele ya kwanza eeh! Ya kwanza ya pili?

MBUNGE FULANI: Ya kwanza!

MHE. AMINA MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni ya kwanza, naomba niendelee kwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa Amina!

MHE. AMINA MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maftaha Nachuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Elias Kwandikwa ajiandae. (Makofi)

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia taarifa hizi mbili za Kamati ya Nishati na Kamati ya Miundombinu. Lakini kabla ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kunipa afya njema na leo hii nimesimama hapa katika upande huu nikiwa peke yangu kabisa na afya njema kuawakilisha wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini ambao wamenituma nije nieleze haya ambayo nakusudia kuyaeleza hivi sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Wenyeviti wote wa Kamati zote mbili kwa mawasilisho yao mazuri kabisa. Niungane na wenzangu kutoa vipengele kadhaa ambavyo wameweza kuvionesha katika taarifa zao zote mbili.

Nianze na Wizara hii ama taarifa hii ya Miundombinu, moja kwa moja sehemu moja wamezungumza kwamba, Serikali imeweka ama imeanza mkakati wa kupanua viwanja vya ndege na mimi ni-declare *interest* ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, tuliweza kutembelea pale Dar es Salaam, *Terminal III* kuangalia upanuzi wa ule uwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo ambalo naweza kulizingumza kwamba, tulipata maelezo pale kwa yule mkandarasi kuna suala hili ambalo Mwenyekiti wa Kamati kaeleza kwamba ucheleweshwaji wa kupewa pesa ili waweze kuendelea na ule ujenzi na ule ujenzi uweze kukamilika kwa wakati. Hili suala kwa kweli, Serikali inatakiwa iliangalie kwa jicho la kipekee kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka hivi sasa tunavyozungumza ni kwamba ujenzi wa utanazi ule unasuasua kwa sababu yule mkandarasi hajamaliziwa pesa zake. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja atueleze kwa nini anachelewesha kumpa mkandarasi pesa ili utanazi wa ile *Terminal III* uweze kwisha kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nizungumzie utanazi huu uendane sambamba na utanazi wa viwanja vile tunaita viwanja vya kanda, kwa mfano Kanda ya Kusini kiwanja kikuu kiko Mtwara Mjini na pale Mtwara Mjini tulizingumza wakati wa bajeti mwaka uliopita kwamba ule uwanja hauna taa, ule uwanja unatakiwa utanuliwe! Ule uwanja safari moja tulishindwa kutua pale tukalazimika kurudi Dar es Salaam kwa sababu ya ukosefu wa taa na taa ziliuwepo huko miaka ya nyuma, lakini ziliweza kuondolewa hatujui zilipelekwa wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hoja hii atueleze ya kwamba mkakati upoje wa kutanua ule uwanja wa Mtwara ikiwemo sambamba na kuweka taa za ule uwanja. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine nizungumzie suala hili la utanazi wa bandari, wenzangu wamezungumza sana hapa kwamba kuna mkakati huu kwa mujibu wa Kamati wa kutanua Bandari za Mtwara na Tanga. Lakini katika utanazi wa bandari hizi, Mtwara haikutajwa kinaga ubaga kama ilivyotajwa bandari zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri atakavyokuja kuhitimisha hoja atueleze kwa sababu mwaka jana tulipitisha bajeti hapa kwamba kuna utanazi wa gati moja Mtwara Mjini ambapo Bandari ya Mtwara tunasema ni bandari yenye kina kirefu kuliko bandari zote Afrika Mashariki na kati lakini bado nimezungumza na Meneja wa ile bandari pale Mtwara anasema bado mkataba ule haujasainiwa; pesa zilitengwa sasa tunataka kujua kwamba tatizo ni nini mpaka leo hawajasaini ule mkataba wa kutanua gati la Mtwara. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nizungumze suala hili la meli ambalo limetajwa katika Kamati kwamba inaipongeza Serikali kununua meli na wanataka kukarabati meli za Ziwa Victoria lakini niombe kwamba isiwe tu katika Ziwa Victoria; tuna Bahari ya Hindi kwa mfano Mtwara miaka ya nyuma tulikuwa tunasafiri kwa usafiri wa meli kwa kiasi kikubwa na niseme tu kwamba sasa hivi pale kuna kiwanda ambacho kinazalisha cement kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dangote anasafirisha anasafirisha cement yake kwa barabara na barabara inaharibika sana wakati Mtwara tuna bandari yenye kina kirefu angeweza kununua meli mzigo wake ukawa unapitia katika Bandari ya Mtwara kuelekea Dar es

Salaam na kwingineko duniani. Lakini tunaacha hatuboreshi, hatununui meli kwa ajili ya usafirishaji wa mizigo kwa kupitia Bandari ya Mtwara - Dar es Salaam na kipindi kile tulikuwa tunaafiri kutoka Mtwara mpaka Zanzibar kwa kupitia Bahari ya Hindi; sasa hivi haya mambo hayapo kabisa na wala hayatajwi kabisa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana kwamba Serikali ihakikishe ya kwamba inavyoboresha ununuzi wa meli katika Ziwa Victoria wahakikishe na Bahari ya Hindi pia kuwe na ununuzi wa hizi meli, lakini hata kule Ziwa Victoria, ukienda kule Ziwa Tanganyika pia kule Kigoma wana shida sana ya usafiri wa meli kuelekea nchi zile za jirani. Nilikuwa naomba kuwe na uunganishaji wa aina hii. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hili la barabara ambalo Kamati imezungumza kwa kiasi kikubwa kwamba kuna ucheleweshwaji wa pesa za ujenzi wa barabara na niseme tu hata barabara ile ya kutoka Mtwara Mjini kwenda Mivata ambayo inaunganisha Wilaya zote za Mtwara Mjini na Mheshimiwa Ghasia juzi aliliza swali hapa ndani kwamba mkataba ule unashubiri nini kusainiwa? Na ukimuuiliza Meneja wa TANROADS anasema tayari umesainiwa lakini Waziri anasema bado haujasainiwa kuna mambo wanayashughulikia; sasa sijui imekwama wapi kusaini ujenzi ule wa kilometra 50 kutoka Mtwara Mjini mpaka Mivata; tunaomba tupate taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika nishati na madini; hivi sasa ninavyozungumza Mtwara na Lindi takribani miezi zaidi ya mitatu hivi sasa umeme unakatika sana; kila sekunde umeme unakata. Tunashukuru sana Serikali kwamba imeweza kutanua wigo wa umeme kutoka Mtwara Mjini kuelekea Lindi na Wilaya zake zote. Sasa tunashangaa kwamba utanuzi huu hauendani sambamba na kuhakikisha kwamba nishati ile inapatikana na ufanisi. Mtwara Mjini, Lindi na Wilaya zake zote umeme unakatika sana, tunaomba maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri hapa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizungumze kidogo ambalo Kamati pia imegusia suala la madini Tanzanite One. Hili suala mimi nikiwa chuoni mwaka 2008 alitembelea Rais wa Afrika Kusini wakati ule Mheshimiwa Thabo Mbeki alikuwa na *article* yake aliandika inaitwa "African Renaissance" yaani kwamba Waafrika tunatakiwa tufufuke tena upya na alikuwa ametueleza sana kwamba watanzania nyie sisi tuna madini haya ya Tanzanite ambayo yanapatikana Tanzania tu; dunia nzima wanategemea Tanzania lakini wanufaikaji wa kwanza ni Wamarekani, wanufaika namba mbili ni Wahindi, watatu ni Waafrika Kusini, wanne ni Wakenya na watano ni sisi wenyewe Watanzania; yaani sisi wenyewe ni wa mwisho. Alitueleza haya Mheshimiwa Rais Thabo Mbeki pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Nkurumah Hall. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tangu mwaka 2008 yule ametufungua masikio lakini mpaka leo bado tuaambiwa kwamba kampuni ama taasisi hii ya madini ya Serikali (STAMICO) inajиendesha kihasara; tunashangaa hasara hizi zinatoka wapi? Wakati madini tunayo yamejaa kweli kweli na haya yapo Tanzania tu hata tungeamua wenyewe kuuza bei yoyote tunayohitaji. Kwa nini tusiende kujifunza kwa wenzetu ambao wameendelea kupitia sekta hii ya madini kwa mfano Botswana kanchi kidogo tu, tunashindwa nini na Wizara ipo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nieleze kwamba hii STAMICO kampuni ama taasisi hii ya madini imeshindwa kufanya kazi zake, wakati tunahoji kwenye Kamati ya PIC juzi tu hapa hawana hata mtaji, wanadaiwa kwelikweli wakati tuna madini yamejaa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana kama Serikali imeshindwa kuziwezesha hizi taasisi zake ikiwemo STAMICO basi ni vyema ingeifuta kwamba kusiwe na hii taasisi kwasababu tunaendelea kutumia resources nyingi za Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimalizie suala hili la kusambaza gesi ambalo Kamati imezungumza pia kwamba kuna ucheleweshwaji wa kusambaza gesi ambayo tulipitisha kwenye bajeti hapa katika Bunge lako hili Tukufu lakini nieleze na niombe sana kwamba usambazaji huu uanzie kule inakotoka gesi Mtwara na Lindi ili iweze kutunufaisha sisi na baadaye kunufaisha Watanzania wote kama ilivyokuwa kwenye korosho. Ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ignas Malocha atafuatiwa na Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Mheshimiwa Joseph Musukuma ajiandae.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakuru sana kwa kunipa nafasi niungane na wenzangu katika kuchangia taarifa hizi zote mbili, Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza naomba nianze na Kamati ya Miundombinu, kwanza naipongeza Kamati kwa taarifa nzuri, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii kwa utendaji mzuri. Kwa kweli kiuwajibikaji wanawajibika vizuri na nadhani tatizo kubwa litakuwa ni pesa. Sasa labda nizungumzie suala moja ambalo naona kwangu kama linanitesa, ni vipaumbele vyta Serikali katika suala la barabara za lami, tunafahamu kwamba sisi wote kwamba kuunganisha Mikoa na baadae itakuja Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nazungumzia Mkoa wa Rukwa unasemekana tumeunganisha barabara ya lami ni sawa, ni katika ukanda wa upande wa juu. Mkoa wa Rukwa umegawanyika katika pande mbili; ukija ukanda wa Bonde la Ziwa Rukwa barabara kuanzia kibaoni unakuja, Kiliamatundu, unakuja Kamsamba, unakuja Mlowo; ni ukanda mwingine tofauti kabisa ambaao hauwezi kufaidika kabisa na barabara ya lami ya kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu imekingwa na mlima ambaao gari haiwezi kubeba mzigo wa zaidi ya tani tatu, lazima iwe inabeba nusunusu na barabara hii bahati nzuri inaunganisha Mikoa mitatu; Katavi, Rukwa na Songwe. Barabara hii ina kilometra karibu 200 na ni barabara ya siku nyingi hata wakati wa ukoloni ilikuwepo ndio maana sababu ya kuwepo wakati wa ukoloni ni umuhimu wake; potential zilizopo katika maeneo yale, kilimo ni bonde la ufa linakubali mazao karibu mengi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sijaua ni kwanini Serikali hajjatilia umuhimu wa kuweka lami katika barabara hii, na juzi wakati wamekuja watu wa MCC II waliuona umuhimu wa kuweka lami barabara hiyo kulingana na vigezo vilivyokuwa vimewekwa, ni bahati mbaya tu waliweza kujiondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kuiambia Serikali kwa nini haitaki kuona umuhimu huo ambaao hata watu wa MCC wamekuja kuiona na wakoloni waliona; kwa nini haitaki kuona umuhimu wa kutengeza barabara hii katika kiwango cha lami? Ni barabara ambayo ina eneo la bonde la ufa na ina rutuba, inakubali mazao yote, inalima mpunga, matunda; ina mito isiyokakuka karibu kipindi chote cha mwaka na mvua za kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri atakapokuwa anakuja kutoa maelezo atueleze ni kwa nini Serikali haitaki kuangalia barabara hii na ninajua sababu yake ni viongozi kutokupita katika maeneo yale na bahati mbaya sana Mawaziri karibu walio

wote ni wageni. Nawaomba safari hii mjaribu kutembelea ile barabara mtaona umuhimu, itawagusa mpaka kwenye mioyo yenu, naombeni sana mtusaidie katika eneo hilo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nishukuru kwa ujenzi ambao mnatarajia kuanza wa daraja la Mto Momba, niwashukuru sana. Lakini faida ya ujenzi wa daraja lile ni kuunganisha sasa ile barabara kwa lami; lakini kama mtalijenga mkaacha barabara ya vumbi itakuwa haina maana yoyote. Kwa hiyo, na mimi nashauri kabisa jitihada za kujenga hilo daraja tunapongeza lakini ziende sambamba na kufanya barabara ile iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwa upande wa Kamati ya Nishati na Madini; kwanza nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote na Kamati kwa taarifa yao nzuri. Lakini nataka kusema ni muhanga wa REA katika Jimbo langu. Jimbo langu nimeeleza mara kadhaa kwamba ni jimbo ambalo limeachwa kabisa halina miundombinu ya umeme; na kwa jinsi liliwyokaa kijiografia sijajua ni kwa sababu gani linaendelea kuchelewa. Ninafahamu wazi kwamba tumpangwa kuletewa umeme katika REA III. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini sisi tunakuwa nyuma kiasi hicho, kila jambo tunakuwa nyuma na tunakaa gizani? Na bahati nzuri yapo maeneo mnapeleka umeme mnapeleke watu hawataki kuutumia, umeme umeenda watu hawataki kuutumia, lakini lie eneo ni eneo ambalo ukipeleka umeme watu watautumia kwa sababu viro viashiria vya uchumi vingi sana na ndio maana utakuta karibu eneo lote watu wamefunga solar; sasa watu wanaojimudu kununua solar ukipeleka umeme utakuwa umewasaidia sana.

Ninamuomba Mheshimiwa Waziri ulione hili, nataka kipaumbele katika suala la umeme katika maeneo yale yote; nikiungana na Mheshimiwa Kikwembe kule hatuna umeme kabisa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu cha ajabu mmekuja kupitisha nguzo mkapitisha Muze, mkapitisha kwenye Kata zangu mkapeleka Mpanda sijui mlipeleka wapi huko; kwa hiyo wananchi wangu wanazonia nguzo tu. Juzi niliongea na Meneja wa TANESCO kwamba naomba basi utele hata umeme wa TANESCO potelea mbali wananchi watalipa; wamewasha kijji kimoja cha Muze wananchi wamelipa karibu shilingi laki moja na kitu; wanajitoa wamalipa. Sasa wanalipa kwa gharama hiyo je, ukipeleka umeme wa REA si wananchi wengi watafaidika na umeme huu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo lingine ambalo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri unisaidie umeme ambao mnapeleka REA III kwangu upande wa Kusini Mashariki, mmefikisha nguzo katika Wilaya ya Mbozi kwa kijji cha Kamsamba; kijji cha Kamsamba kinacho tutenganisha ni mto. Mmeshapeleka nguzo mmefunga na transforma kwa maana REA II watapata umeme wale watu, nina vijiji zaidi ya nane ambavyo vimepangana vinauangalia umeme utawashwa Kamsamba halafu huku hakuna umeme, zaidi ya vijiji nane na vyenye uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri uliangalie hilo, kuwasha umeme Kamsamba halafu kinachotutenganisha ni mto haizidi hata mita 500; kwa nini umeme usivuke ukaja kuvisaidia vijiji vyangu zaidi ya nane ambavyo vina uhitaji huo umeme na kupunguza gharama?

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu tukubaliane vile vile hata kisiasa mnakuwa mmeniweka mahali pabaya; wananchi wanashangaa kijji kimoja kimepata umeme ng'ambo ile, vijiji zaidi ya nane viko huku vinachelewa kwa Mheshimiwa Silinde ni mambo ya ajabu sana. Kwa hiyo,

Mheshimiwa utakapokuwa unakuja ueleze ni kwa nini usitumie ule ule umeme kuvusha huku. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ukanda ule una mito mingi sana isiyokauka na nilishaeleza hapa kuna mto mmoja unaitwa Mto Nzovwe ulishafanyiwa utafiti kwamba unaweza kutoa megawati kumi; nashangaa kwanini Serikali haitaki kutumia chanzo hiki kuongeza umeme katika Mkoa wa Rukwa na umeme ambaao una unafuu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka Waziri utakapokuja kama ukipata nafasi unipe maelezo juu ya jambo hili. Nilikuwa na jirani yangu Mheshimiwa Mipata anasema kwake umeme unakatika katika kwa hiyo, mliangalie na suala la kukatika katika umeme kwenye baaadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja lakini naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Elias Kwandikwa atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Musukuma, Mheshimiwa Richard Mbogo ajiandae.

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye taarifa za Kamati ya Nishati na Madini na ile ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii nipongeze sana kamati zote hizi mbili kwa kuja na ripoti nzuri; ripoti ambazo ukizisoma zimesheheni mapendekezo mazuri sana na maazimio mazuri kwenye ripoti hizi na imani yangu kwamba Serikali itafanyia kazi na kuyatekeleza vema mapendekezo ambayo yapo kwenye ripoti ya Kamati hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya ya miundombinu pamoja na nishati na madini ni muhimu sana katika kuchochaea ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Stadi zinaonesha asilimia 80 ya uwezeshaji wa uwekezaji inatokana na nishati hizi pamoja na miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mkazo mkubwa ukiwekwa kwenye sekta hizi utachochaea kiasi kikubwa sana cha maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimboni kwangu Ushetu hatuna umeme, tumebahatika kuwa na vijiji vitatu tu ambavyo vimepata umeme, imekuwa ni vigumu sana kushawishi wawekezaji kuja kuweka uwekezaji wa aina mbalimbali. Kwa hiyo, ninaamini kabisa katika hii REA III kwa vile vijiji vyangu vimeonekana kwenye ule mpango basi nafikiri Mheshimiwa Waziri hapa atanihakikisha kwamba tutapata umeme ili ile kasi ya kuvutia wawekezaji katika maeneo ya kwetu tuweze na sisi kuweza kusukuma katika maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ninasema ni muhimu katika ukuaji wa uchumi; hivi majuzi tulikuwa tunazungumza juu parameter mbalimbali za ukuaji wa uchumi ikiwemo mfumuko wa bei; nilitaka nijikite hapa kidogo nizungumze na namna ambavyo hata wakati mwингine bei hii ya nishati ya umeme na mafuta inavyoweza kuathiri; kuna muda wa kutafsiri hili suala la mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu utakuja kuona mfumuko wa bei umekuwa mkubwa sana katika hizi nishati za petroli, mafuta ya taa pamoja na vitu vinavyoambatana na petroli. Kwa mfano kwa ripoti za BOT zinaonyesha kwamba kwa mwezi ule wa Oktoba na Novemba mfumuko wa bei umepanda sana kwenye nishati hii ya mafuta na umeme kutoka asilimia 6.2 kwenye asilimia 11.7. Sasa utakuja kuona kwamba hii ndio maana wakati mwингine

inaleteleza tukitafsiri mfumuko wa bei inakuwa haieleweki kwa watumiaji hasa kule vijijiini kwa sababu utaona kwamba maeneo mengine kumekuwa na mfumuko katika rate ndogo, lakini hii ukija kuchanganya kwa ujumla wake utakuja kuona unapata wastani wa nne nukta tano mpaka nne nukta nane katika mwezi ule tu wa kutoka mwezi wa kumi kwenda mwezi wa kumi na moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukizungumza juu ya hali ilivyo vijijiini saa nyingine inaweza isieleweke sasa nataka niseme kwamba upo umuhimu sasa wa Serikali kutazama eneo hili la nishati ili kuweza kuudhibiti huu mfumuko katika maeneo haya ya nishati ili ule uwiano wa ujumla ulete maana halisi. Kwa hiyo, nilikuwa naona hii ni sehemu muhimu sana kwamba Serikali iweze kuiangalia. Kwa sababu ukiona upandaji wa gharama hizi za nishati za mafuta na umeme zinasababisha ukuaji ambao uko shaghala bagala katika maeneo mbalimbali ya utumiaji kama kwenye chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nilikuwa najaribu kuangalia ripoti hii utaona kabisa kwamba wakati mfumuko wa bei unapanda kwenye nishati hii, bei ya chakula inakuwa ni shida. Nilikuwa najaribu kuona katika kipindi kirefu kwa mfano, nimeangalia kipindi cha mwezi Mei mpaka Oktoba, 2016 hii ilikuwa imeshuka *inflation* katika eneo hili. Lakini kipindi kilichoefuata baada ya Oktoba kume-shoot sana katika nishati. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali naishauri ijaribu kuangalia kwa sababu nishati hii inavyopanda, bei ya chakula inapanda ukizingatia kwamba wananchi wetu sasa kwasababu ya miundombinu iliyopo mjini sehemu ambayo kuna umeme kumekuwa na uzalishaji wa vyakula na bidhaa nyingine zimekuwa bora zaidi. Kwa hiyo, wananchi wanauza mazao yao yanakuja mjini halafu baadae yanarudi kwa ajili ya utumiaji kule; kwa hiyo kunakuwa kuna athari kubwa ndio maana tunaona kwamba bei ya chakula inakuwa ni shida. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nizungumze eneo lingine kwa sababu natoka maeneo ya uzalishaji wa chakula, umuhimu wa matumizi ya nishati yetu katika kutengeneza mbolea, niishauri tu Serikali kwamba ilitazame eneo hili ili uzalishaji wa mbolea uwe kwa wingi ndani ya nchi lakini pia wananchi tuweze kupata mbolea kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka pia nijue kwamba ule mradi wa kutengeneza mbolea ya Urea ambao kulikuwa kuna majadiliano kati ya TPDC na wale Wajerumani umefikia wapi kwa sababu sisi ndiyo matumaini yetu. Katika msimu huu hatukupata kabisa mbolea, tulipata mbolea kwa ajili ya kilimo cha tumbaku, wakulima wa mahindi hawajapata mbolea sasa na wananchi wameitika vizuri sana kutumia hizi pembejeo. Na kwa kweli inatia matumaini kwa sababu sasa wananchi wanaweza kuzalisha hadi gunia 30 kwa eka kama watawezeshe. Kwa hiyo, nilitaka niisemee Serikali itazame uzalishaji wa mbolea kwa kutumia hizi nishati zetu za gesi asili ili mbolea ipatikane kwa wingi wananchi waweze kupata mbolea na kuweza kufanya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kusaidia wachimbaji wadogo, maeneo ninayotoka tuna maeneo ambayo wachimbaji wadogo wanachimba. Sasa ni ombi langu tu kwa Serikali kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni isaidie kuweka mazingira mazuri kwa wachimbaji wetu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kusema naunga mkono hoja hizi, Serikali iweze kutusaidia tuweze kusonga mbele. Ahsante. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Joseph Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kutoa mchango wangu.

Kwanza nianze kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kwa kazi nzuri waliyofanya katika kuandaa taarifa yao. Pia nimpongeze Waziri na Wizara yake, wamekuwa wakifanya vizuri sana kwenye barabara zetu za Geita kwa ujumla, tunaona kazi za TANROADS zinavyofanyika vizuri, hatuna mashaka. Lakini zipo changamoto ndogo ndogo ambazo tunaiomba Wizara iweze kuzipa kipaumbele barabara ambazo tayari Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano akiwa Waziri alianzisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Geita kwenda Kahama, lakini na barabara ya kutoka Bwanga kwenda Bihamulo na kwenda Runzewe, yakikamilishwa haya ataongeza tija sana kwenye Mkoa wetu wa Geita. Pia nimuombe Waziri aendelee kuona huruma zile kilometra 57 tulizoahidiwa kwenye Jimbo la Geita Vijiji, sisi wenzenu huko tulikozaliwa vijiji hatujawahi kuona lami kabisa, tunaiona mjini tu kwa wale amba wanapata bahati ya kusafiri. Sasa angalau kwa mwaka huu ukianza hata kilometra moja/mbili na sisi tukapata kuzungumza kwamba tunaanza kuingia kwenye dunia ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri ya kuandaa taarifa pamoja na changamoto mbalimbali mlizokumbana nazo. Niiombe Wizara pamoja na kwamba wametuwekea umeme kwenye Jimbo la Geita Vijiji, tumepata umeme mijini tu, kwenye vijiji vingi ambavyo vinazalisha hasa vya wakulima, umeme haukingia, lakini tumeahidiwa kwenye REA Awamu ya Tatu mtatukumbuka. Nimuombe Waziri kwa huruma yako uwaangalie wananchi wa Jimbo la Geita Vijiji katika vijiji ambavyo tumeviomba viingizwe kwenye REA Awamu ya Tatu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kushauri, nimekuwa nikzungumza hapa mara nyingi kuhusiana na suala la wachimbaji wadogo kwenye Mkoa wangu wa Geita na kwenye Jimbo langu la Geita. Wananchi wa Geita wamekuwa na kilio cha muda mrefu sana na awamu zote tumekuwa tukiahidiwa, Awamu ya Tano ilipofika tulipomuomba Mheshimiwa Rais aliona huruma na akaturuhusu tupewe magwangala. Sasa nimuombe ndugu yangu Mheshimiwa Profesa, ni kweli ulivyotuahidi kwamba mnang'ang'ania kuomba magwangala mtakiona cha moto, sio mchezo tuliona cha moto kweli kweli maana badala ya kupewa magwangala tulipewa mawe ya kujengea nyumba. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikawaambia ndicho ulichokiahidi kwenye mkutano kwamba tutakiona cha moto, tulivumilia tu, tumekula hasara na wananchi wangu sasa hawana tena shida na magwangala kama ulivyosema. Wamenituma nikuombe kwa kuwa eneo la GGM ni kubwa na wewe ni mtaalam wa miamba ninaamini hutarudia tena kuwapa kwa sababu sisi na wananchi wangu wote ni darasa la saba kule, hawana utaaliam wa miamba kule sisi tuna utaaliam moko tu kuchimba. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe kwa kuwa wewe ni Profesa, term hii basi usirudie kuwapa na wewe ule mwamba wa mbali kama uliowapa mwaka 2012, uwaangalizie Nyamatagata na Samina walipokuomba. Ni sheria, sasa imeshapita miaka mitano, wamege lile eneo ambalo wachimbaji wangu wakienda na la saba lao wakichimba tu wakifika kwenye magoti angalau wawezi kupata hata dhahabu kidogo kidogo kufidia yale machungu ya SACCO\$ zile ulizoiunda wewe. Kwa kweli cha moto tumekiona, na tumeamini Profesa wewe ni bingwa kwa sababu wa darasa la saba tumefeli kwenye hilo. (Kicheko/Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe tu Mheshimiwa Waziri, kumekuwa na kilio cha muda mrefu sana kwa wananchi wa Wilaya ya Geita kwenye eneo la STAMICO, na eneo linalopiganiwa ni dogo sana na wewe ulivyokuja kule *term* hii ultuahidi leseni zile zinaisha mwezi wa tisa, tunazisubiria, ama uwape wazungu au uturudishie, hapo hatutajali cha Profesa tunaanguka la saba kwa nguvu mule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nikuombe sana usi-renew hiyo leseni bila kumega eneo ukatupa la saba na sisi tukapate riziki pale, tumelia mara nyngi Rais ametuahidi, umetuambia kuna kesi ya Sinclair lakini Sinclair, wewe unazo message kwenye mtandao wake anamtukana mpaka Mkuu wa nchi, kwamba anaendesha nchi kibabe na unajua hiyo email, lakini bado unasema tukimnyang'anya ile atatupeleka mahakamani.

Sasa kama muda wake unaisha mwezi wa tisa *wallah* nakwambia la saba tutakaa pale, yaani ikifika tarehe 27,28 tunaanguka porini. Na ultuahidi ukajisahau ukatamka na tarehe, bahati nzuri la saba huwa hatushau tarehe, tunasahau kila kitu tarehe 28 tuko kwenye lile eneo, tutalichukua kwa nguvu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona mchakato wa EWURA wakati anatumbuliwa Mkurugenzi wa EWURA nikawa najaribu kujiuliza, hivi kweli kwa nini Mkurugenzi wa TANESCO anatumbuliwa peke yake na Wakurugenzi wale wengine, ni kwa sababu kweli walifanya vikao mpaka wakakubaliana na EWURA bila Profesa kupita kuona documents zile? Nikawa nashindwa kuelewa, nikasema ipo siku ntapata nafasi, ninayo document ya Mheshimiwa Profesa Muhongo ambayo yeye mwenyewe anamwandikia Mheshimiwa Dkt. Mpango tarehe 30, Septemba akimpelekea mpango kazi wa TANESCO, na wameweka mapendekezo yao humu ndani ukihitaji nitakupa kama unahitaji wanamuomba EWURA kufikia mwezi wa 12 awe amepandisha umeme, na yeye ameisaini hii document, iko saini yako hapa usitikise kichwa ntakukabidhi Mheshimiwa.

Baada ya mwezi wa 12 amevua koti tena akawasakizia wenzie, na saini yake iko humu. Naomba sana hebu tuangalie tusiwe tunatumbua tu watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, lile la wachimbaji wadogo...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, naomba umalizie, muda wako umekwisha usianzishe hoja nyngine.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, lile la wachimbaji wadogo kupelekwa kupewa ruzuku ya Katavi...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma muda wako umekwisha. Ahsante.

Mheshimiwa Richard Mbogo, Lakini kabla Mheshimiwa Richard Mbogo hajaanza kuzungumza Waheshimiwa Wabunge, yako maombi mengi sana hapa mezani ya Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kuchangia, kwa sababu hizo na kwa kuzingatia muda wetu ambavyo hautatosha, atakapomaliza Mheshimiwa Mbogo wachangiaji wengine wote watakaofuata itabidi tupunguza dakika ili wengi wapate nafasi ya kuongea moja ama mawili yaliopo katika majimbo yao.

Mheshimiwa Richard Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, kuanzia kwa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo tutakuwa tumeshaanza kupunguza dakika, Katibu tafadhalii uzingatie hilo, Mheshimiwa Richard Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja za Kamati zote mbili, Kamati ya Mindombinu na Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwa haraka, hoja yangu ya kwanza ni kutoa msisitizo kwa Serikali juhudhi ambazo wameonyesha katika vipande vingine upande wa reli kwenda kwenye *standard gauge* basi wasisahau na reli yetu ya Mpanda ambapo inaanza kuchepuka kutokea Kaliua kwenda mpaka Mpanda na vilevile reli kufanyiwa usanifu kutokea Mpanda mpaka Karema, upande wa Karema tunatarajia kuwa na bandari ambapo pana upana mdogo katika Ziwa Tanganyika na upande wa pili wa nchi yetu ya jirani ya DRC.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa hizi reli pamoja na bandari kule Karema ni kupitisha mizigo, sasa na tunaona nchi nyingi ambazo hazina bandari (*landlocked countries*), tutumie hiyo fursa ili tuweze kuongeza mapato katika bandari yetu. Taarifa ya Kamati imeonyesha jinsi gani mizigo kwenye bandari imeweza kushuka kwa asilimia 0.1 na sehemu nyingine asilimia 5.2, kwa hiyo tuombe sana Serikali iangalie reli upande wa Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwanja wetu wa ndege wa Mpanda, uwanja wa ndege wa Mpanda hauna gari la zimamoto, hamna mkandarasi wa mafuta, kwa hiyo tunahitaji Serikali iweze kushawishi hivyo vitu. Tuna Mbuga ya Katavi ambapo ni moja ya maeneo ya mbuga ambayo wanasema ni *very virgin*, wanyama wana asili sana, ukienda Mbuga ya Katavi utaona asili yao ukishuka kwenye gari samba anakimbia, tofauti na maeneo mengine kama Serengeti. Kwa hiyo, uwanja wa ndege huu ni muhimu sana kwa ajili ya utalii kwenye Mbuga yetu ya Katavi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la mawasiliano tunahitaji kampuni za simu ziendelee kuimarisha mawasiliano, na hasa Kampuni ya Halotel ambayo ilianzia vijijini, maeneo yetu mengi tuna matatizo ya mawasiliano. Ukiwa unasafiri kutoka Mpanda kuja Tabora kuna maeneo ya katikati unatembea kilometra karibu 90 hakuna mawasiliano, sasa inapotokea dharura yoyote na dunia sasa hivi iko kwenye kiganja, kwa hiyo, tunaomba Serikali iendeleee.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la SUMATRA, mamlaka hii ipo lakini usimamizi wa bei bado ni hafifu sana. Tumepata kero nyingi kwenye ziara tulizozifanya, kwa mfano watu wetu wanaotoka Mpanda kwenda Ugala wote wanachajiwa shilingi 5,000 lakini katikati hapa kuna sehemu wanatakiwa walipe shilingi 2,000, shilingi 3,000 na shilingi 4,000 lakini wote wanalipa bei moja. Kwa hiyo, SUMATRA wasiwe wanasubiri malalamiko ya wananchi, wawe wanafanya *testing* ya hizi *control* zao zinafanyaje kazi na wachukulie hatua watu wenye vyombo hivi vya usafiri. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapohapo kwenye mawasiliano, TCRA watusaidie Halmashauri zetu, na ningombwa mwongozo wa Serikali, hii minara inakuwa na rekodi ya mawasiliano yamefanyika katika lile eneo na yale mapato ambayo yametokana na kampuni za simu kwenye mnara husika.

Sasa ile service levy haya makampuni wanalipa wapi? Kwa hiyo, unakuta Halmashauri zetu hazipati mapato toka kwenye makampuni ya mawasiliano kwa sababu ya mawasiliano au muunganiko katika ya TCRA na Halmashauri kidogo uko tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye madini, tumekuwa na changamoto kwa wachimbaji, wamekuwa na migogoro na watu ambao wamepewa leseni. Kwa mfano kwenye Jimbo langu la Nsimbo, eneo la *Kijani Investment* imekuwa ni mgogoro, Kampuni ya Sambaru imekuwa ni mgogoro wanasema hakuna muhtasari, sasa shida iliyopo ni nini, tungeomba Serikali itenye maeneo kwa ajili ya watu ambao hawana leseni, watu leo anaamua akachimbe anunue unga au aliye ada na yawe chini ya uongozi wa kijiji ndiyo uweze kusimamia. Tukifanya hivyo tutaondoa migogoro kwenye haya maeneo ya watu ambao wanakuwa na leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile upatikanaji wa service levy toka kwenye makampuni haya yanayochimba yenye leseni ndogo (*PML*) na leseni kubwa, rekodi zao haziko sahihi kwa hiyo, Halmashauri zetu hazipati service levy. Kwa hiyo, nashauri Serikali iangalie *fixed amount* kulingana na aina ya leseni na sehemu nydingine iwe ya kiasilimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe upande wa nishati, *REA III*, kwa Mkoa wetu wa Katavi vijiji 74 haviko kwenye huu mpango wa sasa hivi, kati ya vijiji 191 tumepeewa vijiji 117 na ni mkoa wa pembezoni ambao ulisahaulika sana kimaendeleo. Kwa hiyo, tunaomba vijiji 74 viongezwe na wakandarasi waongezewe mikataba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tunaomba Serikali iendelee kutoa ushirikiano kwa kampuni inayofanya utafiti wa mafuta Ziwa Tanganyika na pia gesi na maeneo mengine ya madini katika Mkoa wa Katavi na mikoa jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja za Kamati hizi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa ajiandae. Mheshimiwa Balozi Adadi.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii kuweza kuchangia hoja hii ya Kamati. Kwanza kabisa ningependa kupongeza sana Wizara hii ya miundombinu, kwa kiwango kikubwa katika miezi sita hii ambayo tumekuwa nayo imeonyesha dalala kweli kwamba kuna mambo ambayo yanaonekana kabisa na ni dhahiri kabisa kwamba wamejitalidi kwa kadri ya uwezo wao. Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Profesa ametembea nafikiri nchi nzima hii nilikuwa kila nikiangalia television naangalia anapumzika wakati gani lakini naamini kabisa amefika mikoa yote kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona tu ni dhahiri kabisa ametuletea ndege zimeletwa hapa bombardier mbili na nydingine zinakuja, mkataba wa reli umetiwa saini juzijuzi hapa, barabara wametengeneza karibu kilometra 400 za lami, kuna flyovers ambazo zimeanza kuonekana pale TAZARA, madaraja ya Coco Beach yameanza kushughulikiwa na magati mengi kule bandarini. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba Wizara hii ya Miundombinu kwa kiasi fulani imejitalidi na imetoa nuru ya Awamu ya Tano ni kitu gani ambayo inataka katika hiki kipindi cha miezi sita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengi ambayo imeyafanya especially mambo ya reli, lakini utaona kwamba reli yetu ya Tanga kidogo imesahaulika na sijui ni kwa nini, katika taarifa ya Kamati kwa kweli ingebidi na reli hii ya Tanga iangaliwe, hatuwezi kusubiri mpaka reli ya kati imalizike ndiyo mipango wa kuanza kushughulikia reli ya Tanga ianzishwe. Kwa hiyo, ningeomba vitu hivi viende kwa pamoja, simultaneously, huku inafanyika na huku inafanyika kidogo. (*Makofi*)

Kuna suala la bandari pia, bandari Tanga sijaona kitu chochote ambacho kimefanyika uktilia maanani kwamba kuna bomba la mafuta ambalo linafanyika lakini mipango ya kupanua ile bandari ya Tanga ili kuweza kukidhi mahitaji ya hili bomba ambalo linakuja bado sijaiona. Kwa hiyo, ningeshauri Kamati iitake Serikali maandalizi hayo yaanze mapema ili n watu wa Tanga waanze kufaidika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la barabara ambazo Wizara hii imejitahidi sana kwenye kilometra 400 lakini barabara hasa jimboni kwangu, sijaiona na ninaomba Mheshimiwa Waziri usisahau kuingiza kwenye bajeti inayokuja barabara kilometra 40 ya Amani mpaka Muheza, ni barabara muhimu sana na ambayo sasa hivi ina matatizo sana ya kuipitika. Kwa hiyo, wananchi wa Muheza wanaamini kwamba safari hii barabara hiyo basi itawekwa kwenye bajeti hii.

Vilevile kutokana na ukame ambaeo upo sasa hivi tunategemea kwamba ahadi zile za Mheshimiwa Rais za kilometra tatu ambazo alituahidi pale Muheza basi zitatekelezwa kwa sababu vumbi limekuwa kbwa na ukame umeongeza vumbi, basi tunategemea hizo kilometra tatu tukipata lami kidogo tutapata ahueni ya lami. (Makofi)

Kuhusu mawasiliano, kuna tatizo kubwa, hasa kwenye Mlima wa Amani kule, ambapo redio hazisikiki, simu hazisikiki na nilikwishamuomba Mheshimiwa Waziri ili aweze kuliangalia tupate minara maana yake hatupati mawasiliano kabisa maeneo ya Amani, tarafa yote nzima, vijiji vya Ngomole, vijiji vya Zirai, Vijiji vya Kwezitu, inakuwa mawasiliano ni matatizo makubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nije kwenye Wizara ya Nishati na Madini; ishu ya bomba la mafuta kutoka kule Hoima, Uganda mpaka Bandari yetu ya Tanga linasisimua sana pale Mkoani Tanga na linasisimua sana hata Muheza. Lakini sijaona fukutofukuto lolote ambalo wananchi wanaweza kusema kwamba sasa hivi hii kitu inafanyika, tunaona mkataba umetiwa saini, lakini hatuoni...

Mheshimiwa Naibu Spika, REA Awamu ya Tat...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha Mheshimiwa.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa atafuatiwa na Mheshimiwa Costantine Kanyasu. Mheshimiwa Peter Serukamba ajiandae.

MHE. DKT. SHUKURU KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja ya Kamati hizi mbili, Miundombinu na Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuipa pongezi sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuthubutu kutenga fedha jumla ya shilingi trilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kwa standard gauge. Ni jambo kubwa, jambo la uthubutu na hilo ndilo ambalo limewezesha wahisani kuweza kuunga mkono juhudhi hizo na sasa hivi ujenzi karibu utaanza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zote duniani ambazo zina mtandao mzuri wa reli, zenye uwezo mkubwa wa kuhudumia shehena kubwa na nyingi zimeunganisha usafiri huo wa reli pamoja na bandari kwa maana ili tunapojenga reli yenye uwezo mkubwa, inayoweza

kuhudumia shehena kubwa ya makontena na shehena mchanganyiko maana yake lazima uwe na bandari kubwa ambayo inaweza kupokea mzigo huo na kuweza kuingiza kwenye reli. Mwaka 2009 TPA wamefanyastadi na wakaibua mpango wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane mkono na maoni ya Kamati ukurasa wa 41 ambapo wameitaka Serikali iharakishe ujenzi wa reli hii ya kati, lakini uharakishaji wa ujenzi huu wa reli ya kati lazima uungane sasa na uharakishaji wa ujenzi wa Bandari kubwa ya Bagamoyo ambayo itakuwa na uwezo sasa wa kuzalisha shehena hiyo ambayo inahitajika kwa miundombinu mikubwa hii. Bila kufanya hivyo tutakuwa tumetwanga maji katika kinu. Hatuwezi kupata mafanikio yale ambayo tulikuwa tunayatarajia kwa uchumi wetu ambaa unakua na ambaa tunategemea tufike katika uchumi wa kati mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi huu wa Bandari ni muhimu tuupe kipaumbele na katika kuupa Kipaumbele maana yake kwanza tumalize kadhia ile ya fidia kwa wale wananchi ambaa wanapisha ujenzi wa Bandari hii. Hivi sasa nisemapo baadhi ya wananchi wachache bado hawajalipwa fidia zao. Nadhani ni muhimu zaidi wakati tunaamua kujenga Bandari tuhakikishe kwamba hakuna mwananchi ambae hajalipwa fidia lakini wapo wananchi wale ambaa walipunjwa na Mkuu wa Wilaya au Kamati ya Mkuu wa Wilaya ilibainisha kwamba wananchi 687 walipunjwa fidia katika mradi huu wa ujenzi wa bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wanahakikiwa. Naiomba Serikali iweze kutenga fedha mapema ili mara uhakiki utakapomalizika hawa ambaa walibainishwa kwamba wamepunjwa, basi waweze kulipwa fedha zao kwa wakati na waweze kupisha ujenzi wa bandari. (Makof)

Mhehimiwa Naibu Spika, pamoja na suala hili la fidia lakini kuna suala kubwa zaidi ya kwamba ujenzi wa Bandari hii kubwa, unamaanisha kwamba tutaondosha katika ramani ya Tanzania kijiji kinachoitwa Pande.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji chote cha pande na Vitongoji viwili vya kijiji cha Mlingotini vitaondoka kabisa katika ramani kwa maana vitamezwa na bandari hii, sasa hivi hao ndiyo wapo katika mchakato wa kulipwa fidia. Sasa hawa wapewe maeneo ya kuhamia, kaya zaidi ya 2,200 hawawezi wakaambiwa tu tokeni bila ya kuwa na sehemu ya kwenda. Muda umeniishia naomba kuunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Daimu Mpakate ajiandae.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru. Kwanza naomba kupongeza Kamati zote mbili kwa taarifa zao nzuri, lakini naomba nianze na tatizo la umeme kwenye Mji wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku umeme Geita unakatika kila siku zaidi ya mara nne. Nimezungumza mara nyingi sana na Waziri, nimezungumza na Naibu Waziri na tatizo hili kwa zaidi ya miezi nane halipatiwi majibu. Nafahamu kuna mradi ambaa unaendelea lakini nadhani speed ya mradi huo ni ndogo sana, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Waheshimiwa Mawaziri wanisikie kwamba kuna tatizo kubwa sana la umeme katika Mji wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, mji wenywewe wa Geita ule, ni nusu peke yake ndiyo unaowaka umeme, sehemu zingine umeme hakuna. Tunaambiwa tunasubiri umeme wa REA na niliongea na Naibu Waziri nikamuomba basi atupe ratiba ya mradi wa REA wa nchi nzima tuje kwamba Geita unakuja lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, linguine pamekuwepo na malalamiko mengi sana kwamba watu wanalamika kwanini Geita uwanja wa ndege umejengwa Chato? Sisi watu wa Geita ndiyo tunajua. Mheshimiwa Rais akitokea Geita kwenda Chato ni kilometra 160. Ili afike Chato, magari yanayotangulia mbele yanasmamisha watu matokeo yake kwa saa sita watu wamesimama Barabarani. Kwa hiyo, solution ni kumjengea uwanja karibu na nyumbani kuondoa ule usumbufu. Kutoka Geita kwanda Chato ni kilometra 160 kwa hiyo, watu wanaolalamika kujengwa uwanja Chato ni kwa sababu hawafahamu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili, nilikuwa naiomba tu Wizara ya Mawasiliano isiondoe sasa nafasi ya kutujengea uwanja wa Mkoa wa Geita kwa sababu hatuwezi kuzuia Mheshimiwa Rais ule uwanja usijengwe kule. Hata usipojengwa kero yake ni kubwa sana kwa wananchi pale barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la tatu, Mheshimiwa Rais Mgodi ule wa Geita karibu miaka kumi ijayo utakuwa umeshachimba dhahabu. Geita hii tunayoizungumza ambayo kwa Mgodi ule ndiyo *the leading gold producer* hapa Tanzania na karibu ya pili Afrika, wananchi bado ni maskini. Na ukitazama, sioni dalili za namna ambavyo huu mgodi utabadilisha maisha ya Wananchi sasa hivi kwa muda mfupi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali, wangeanzisha mfuko wa *natural resources rent extraction* ambao unafanyika katika nchi nyingi sana. Kwa mfano, mfuko kama huu upo Norway, mfuko kama huu upo Marekani. Wakati kazi za madini zinapokuwa zinaendelea, mfuko maalum kwa ajili ya kuwafanya wananchi wa maeneo yale baada ya shughuli za madini kuisha waweze kuendelea na mambo mengine unakuwa umeandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyokwenda sasa hivi, kesho kutwa dhahabu zitakwisha kama zinavyoisha Kahama, wananchi watabaki maskini, Geita hatuna hospitali, Geita hatuna barabara, Geita hatuna maji, Geita hatuna kila kitu lakini dhahabu zipo nyingi. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba kuna tatizo hapa, siyo suala la kwanza duniani ni tatizo ambalo watu wengi wameshindwa kulisemea hili. Tukianzisha mfuko huu ambao utatusaidia watu wataweza kusoma, utaweza ku-deal na *humanitarian crisis* lakini utaweza kushughulika pia na mambo mengine ya *development* kwenye maeneo yale. Sasa hivi tunapata 0.7 CSR kwa miaka 17, mgodi umejenga shule moja ya wasichana. Kila siku wanaonesha kwenye television, miaka 17 0.8 percent ya CSR wangeweza kuifanya Geita kuwa Ulaya, lakini kwa sababu wanaamua wenyewe wafanye nini hakuna kinachooneka kimefanyika pale. Maisha ya wananchi wa Geita inaendelea kuonekana kama vile hawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nashukuru kwa kunipa nafasi. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Peter Serukamba atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Mpakate, Mheshimiwa Daniel Mtuka ajiandae.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Niwapongeze kwa speech nzuri, nina mambo matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, nililisema na nazidi kulisema ili angalau wenzangu wa Serikali huko walielewe. Sisi tuna madini mengi sana, lakini nchi hii katika wanaotuzunguka sisi hatuna soko la madini. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, leo Tanzania tukiweka soko la madini kwamba mtu yoyote anayekuja pale sokoni hatumuulizi madini ameyatao wapi lakini yule anayekuja kununua anapoondoka tunaweka export levy, tutapata fedha nyingi sana

kama Taifa. Fedha zile zitaingia kama kodi ni nyingi sana na tutapunguza kodi nyingi hizi za kero. Lakini kila tukisema suala la madini, kwa sababu leo tunawachimbaji wadogo wadogo, hivi wanaiza dhahabu wapi? Nani anajua wanaiza wapi? Kwa hiyo, inawezekana wanachimba kwetu wanaenda kuuza kwingine kwa hiyo faida inaenda kwa wengine, lakini tuna uwezo wa kuanzisha soko la madini Tanzania na watu wote wakaja wanunuizi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naongea na mtu mmoja hapa anasema, ukienda leo Telaviv-Israel, moja ya biashara yao kubwa ni *diamond* na *diamond* wala haichimbwi Telaviv. Walichofanya wameweka soko la *diamond*, so everybody *in the world* anakwenda kuuza *diamond* pale Telaviv. Kwa hiyo, na sisi kama Tanzania tukiweka soko hapa, tuna hakika Wakongo wataleta dhahabu, nani ataleta dhahabu halafu watu wanaponunua wanapoondoka ndiyo tunaweka *export levy*, tutapata fedha nyingi sana na hawa wanunuizi watacaa kwenye hoteli zetu, watakula chakula chetu na wale Wauzaji wakishauza dhahabu watanunua bidhaa so *triple down effect* kwenye economics itakuwa kubwa sana kama Tanzania. (Makof)

Lakini tunalisema hakuna anayetaka kulielewa, naomba sasa Profesa Muhongo, fanya hili jambo liwe *legacy* yako. Anzisha soko la madini Tanzania watakukumbuka tu kwa sababu utakuwa umeanzisha jambo kubwa sana na itakuwa ni source ya fedha nyingi sana kwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la mafuta, tunesema hapa bei za mafuta duniani zinapanda na kushuka. Kama nchi lazima tuwe na *strategic reserve* ya mafuta ili tukishakuwa na *strategic reserve* ya mafuta tunaweza tuka-survive kwa miezi sita bei ya mafuta inayo *treat haitatu-affect* sisi kwa sababu tutakuwa tuna mafuta yetu ambayo tunatumia miezi sita ama mwaka mmoja. Na hii haihitaji fedha nyingi sana kwa sababu tunayo *TIPPER*, tunayo *PUMA* ambayo tuna asilimia 50, *TIPPER* tuna asilimia 50, ni suala la kuamua tu na hapa Serikali itapata faida maeneo matatu:-

- (i) Itapata faida kwenye *TIPA* kwa sababu tuna asilimia 50 kwenye *reserve*.
- (ii) Itapata faida kwenye *PUMA* kwa sababu tuna asilimia 50.
- (iii) Itapata faida ya mafuta tutaweza ku-control *inflation*, tuta-control bei ya mafuta ambayo ni kubwa sana kwa maana ya nchi. (Makof)

La mwisho ni suala la *PPP project* kwenye barabara, niombe sana, umefika wakati, tumeongea habari ya *PPP project* ya barabara. Huu mwaka wa kumi niko Bungeni, tunaifanya Dodoma kuwa Makao Makuu lazima tufanye Dodoma iwe accessible. Lazima Dodoma iwe karibu, hatuwezi kutegemea watu wote wapande ndege. Tutegemee kwamba wanaokuja Dodoma atakayekuja kwa treni awahi, atakayekuja kwa gari awahi, atakayekuja kwa ndege awahi, tunafanyaje? Lazima fedha zetu tuweke fedha ya watu binafsi wajenge super high way, wata-charge...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru huo ndiyo mchango wangu. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daimu Mpakate, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Mtuka, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu ajiandae. Mheshimiwa Daniel Mtuka.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante kwa nafasi hii nitoe mchango wangu. Kwanza niwapongeze Kamati ya Miundombinu pamoja na Kamati ya Nishati na Madini. Baada ya pongezi hizo niende moja kwa moja kwenye point.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu bado liko pale pale kwa REA II ambao ni mradi ulikuwa umeanza tarehe 25 Novemba, 2013 na ulikuwa uishe tarehe 25 Novemba, 2015. Mpaka hivi ninavyozungumza hata robo haijafikia mradi ule, mkandarasi yule ni mbabaishaji SPENCON na nilishasema hapa huyo mtu hatumtaki. Tunaomba tubadilishiwe mkandarasi aletwe mkandarasi mwingine ili aweze kukamilisha mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu umeme ni fursa, kuna mashine za kukoboa, saluni vijana wafungue za kiume na za kike, welding, carpentry, tufunge pump za maji za umeme pia, zahanati zetu, vituo vya afya, shule. Sasa mtu anacheza cheza na maisha ya watu, hatumtaki huyu mkandarasi tunataka mkandarasi mwingine. Naomba mlisikie hilo Mawaziri mtusaidie tunataka umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni REA III; tunaomba ianze. Tuliambiwa Desemba mwaka uliopita lakini haikuanza, Februari haikuanza, tunaomba hii tarehe 15 Machi ambayo mmeisema basi tunaomba ianze REA III. Kwangu kule Manyoni, vijiji ambavyo vina umeme ni vile ambavyo vimepitiwa tu na njia kubwa ambavyo ni REA II, lakini kuingia ndani vijiji huko ambako ni mbali na njia kuu hakuna umeme. Nikizungumzia Jimbo la Manyoni Mashariki, vijiji ambavyo vimepata umeme kwa maana ya vile 58 ni karibu robo tu ndiyo vimepata umeme vingine vyote havijapata umeme. Lakini pia REA III component ile ambayo mnasema kwa kijiji kimoja kwa mfano, sasa hivi kwenye REA II ambavyo vilipata umeme ni robo tu ya kijiji lakini robo tatu ya kijiji hakijawashwa umeme. Kwa hiyo, tunaomba ile 100 percent kijiji kiwashwe kwenye REA III.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, Mji wa Manyoni unapanuka, tumepima viwanja zaidi ya 2000. Tunahitaji miradi ya umeme kwenye mji wa manyoni ili upanuzi wa mji uende pamoja na huduma ya umeme. Nimeliongea hili, naomba tena nirudie mara ya pili, tafadhali sana mtusaidie kwa sababu bei ya nguzo zile ni gherama kubwa, hatuwezi kumuuzia mtu kiwanja, mnawaambia waungane wanunue nguzo wapeleke umeme haiwezekani hatuwezi kupanua mji kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa upande wa miundombinu tunawashukuru tumepata ile...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

Mheshimiwa naunga hoja mkono, ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Dunstan Kitandula ajiandae.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kidogo hoja hizi mbili mbele yetu; Taarifa ya Miundombinu na Taarifa ya Nishati na Madini.

Kwanza napenda kusema kwamba, sekta ya madini kwa kipindi hiki wawekezaji wamepata shida sana, wengi wanakimbia, wengi wanarudi na sababu kubwa ni kwamba wawekezaji wengi wana hofu kwamba security of tenure ya leseni zao ziko hatarini wanaweza kunyang'anywa leseni wakati wowote, kwa hiyo, nilikuwa naiomba Wizara na Kamati hebu tujaribu kuishauri Serikali irudishe mazingira mazuri ya kuhamasisha Wawekezaji waje.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni wachimbaji wadogo ambao kwa sasa hivi wamekuwa wachimbaji haramu kwa sababu tozo na kodi mbalimbali za uchimbaji mdogo zilipandishwa sana katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, kwa hiyo, wameshindwa kulipa na

wengi haramu bado wanaendelea kuchimba. Naiomba Wizara hebu fanyeni review ya wachimbaji wadogo wanavyolipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, ni kuhusu mradi wa magwangala. Mheshimiwa Musukuma amesema, wameweka mahali ambapo kwanza hata hawajapafanya environmental impact assessment na kwa sababu hawajui watatunzaje mazingira ya eneo lile, Mheshimiwa Waziri labda au mtu mwingine alikwenda akachangua tu akasema wekeni hapa, sasa hayachukuliwi. Maana yake ni nini? Eneo hilo litachafuka kimazingira. Kwa hiyo, sisi tulikuwa tunaomba, Kamati inayosimamia mazingira huo mradi muusitishe. Tafuteni maeneo ya kuwapa hawa Wachimbaji wadogo kama alivyosema Mheshimiwa Musukuma, ni vizuri kushirikiana na mgodi, kushirikiana na wananchi mpate maeneo mazuri zaidi badala ya kufikiria kuwapa magwangala ambayo hayana Madini. (Makofii)

Mwisho ni kuhusu bandari, Bandari ya Dar es salaam ilipata matatizo kidogo sasa hivi tunaishukuru Serikali imeanza ku-pick up kidogo lakini kuna tatizo moja kubwa na tutalisema sana kesho kwamba Mkuu wa Bandari ameamea kubadilisha watumishi pale, wale wasimamizi wote kawabdalisha wako saba. Kaleta watu wengine ambao hata taaluma ya mambo ya maritime hawana. Hii inaleta m dororo zaidi wa huduma katika bandari yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaiomba Kamati pamoja na Wizara mliangalie hili, watu waliopewa nafasi pale, Wakurugenzi wote wanaomsaidia Bwana Kakoko pale hawana taaluma wengi ni wahandisi kutoka TANROADS, tutaendeshaje mambo haya kwa urafiki? Nashukuru kwa kunipa nafasi. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso. Mheshimiwa Dunstan Kitandula

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kunipa nafasi hii. Kwanza awali ya yote niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia, lakini ninanyongeza ya mambo ambayo tunahitaji kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la fedha kwa Wizara husika ambayo imepewa dhamana ya miundombinu bado ni ndogo, tunaomba sana Serikali ihakikishe inapeleka fedha kwa wakati ili miundombinu iliyolengwa iweze kujengwa kwa wakati. Lakini tunaipongeza Serikali kwa kufikia maamuzi ya ujenzi wa reli hasa reli ya kati ambayo kwa kuanzia Serikali imesaini na Kampuni za Waturuki kuweza kujenga reli ambayo itakuwa na manufaa zaidi. Ombi langu kwa Serikali ihakikishe inatengeneza mazingira mazuri ili kushawishi na makampuni mengine yaweze kuomba tender ili iweze kujengwa reli ambayo itaenda kwa haraka, ipambane na mazingira ambayo ni ya ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kitendo cha kujenga reli ambayo itaanzia Dar es Salaam kuishia Morogoro bado tuna kilometra nyingi ambazo zinahitaji kujengwa kwa wakati. Ni vyema Serikali ikajipanga kuhakikisha maeneo hayo yanatengewa fedha ili tupate fedha zitakazojenga reli kuanzia Morogoro kuja Dodoma, Dodoma - Tabora, Tabora - Kigoma, Kaliua - Mpanda hadi kule Kalema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado kuna maeneo ya kuanzia Tabora kwenda Isaka mpaka maeneo ya Kezya kule Rwanda ili yaweze kuendana na mazingira halisi ambayo kimsingi tutakuwa tumeteka soko. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo tunahitaji kuishauri Serikali ni kufanya maboresho ya ujenzi wa bandari hasa zile gati ambazo zinahitajika ziwe kwenye maeneo

ambayo yataenda kibiashara zaidi. Kwa sasa bandari bado haina uwezo mkubwa sana wa kupokea meli nyingi, tunahitaji Serikali ielekeze nguvu kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado tunahitaji Serikali iboreshe bandari za mikoani hasa kwenye maziwa makuu. Bandari zile zitachangia uchumi kwenye maeneo husika. Tunazo bandari ambazo zimesemwa sana na Waheshimiwa Wabunge, Bandari ya Dar es Salaam inahitaji maboresho, Bandari ya Tanga ambayo kimsingi itategemea kuchukua mzigo mkubwa sana kutoka nchi ya Uganda inahitaji iboreshwe. Bandari ya Kigoma ikiboreshwia itasaidia sana kukuza uchumi wa nchi hii kwa sababu iko jirani na DRC. Bandari ile ikitumika sambamba na bandari ambayo inategemewa kujengwa Kalema itasaidia sana kukuza uchumi wa nchi na sehemu kubwa na mzigo wa Congo ambao tunautarajia sana kutumika kwenye reli na Bandari ya Dar es Salaam zitafanya kazi vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzajji)

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri kwamba barabara zitengewe fedha za kutosha kwa ajili ya kuunganisha mikoa yote ya nchi yetu. Ahsante. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Mariam Kisangi ajiandae.

MHE. LOLEIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Kamati ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja ya Kamati inayozungumzia habari ya wananchi kupewa maeneo ya uchimbaji, hasa katika eneo la STAMICO. STAMICO kulingana na maelezo, Serikali imeliteua Shirika la STAMICO kwa ajili ya kusimamia shughuli za madini kwa ujumla wake pamoja na kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo nchini kwa ujumla. Lakini kwa hali iliyopo sasa tunaona jinsi ambavyo STAMICO imeshindwa kufanya kazi yake vizuri. Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali iweze kuangalia namna bora ya kuweza kuiwezesha hii STAMICO ili iweze kutekeleza majukumu yake vizuri kwa ajili ya manufaa ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia eneo moja la STAMICO ambapo imechukua baadhi ya migodi; katika Mkoa wa Geita kuna mgodi ambao unaitwa Bacliff. Ni muda, tangu mwaka 2011 mgodi huu umechukuliwa, wameingia ubia na kampuni nyingine ya kutoka nje inaitwa royalty lakini tangu wamechukua 2011 mpaka sasa hatuoni ufanisi wowote, hatuoni kazi yoyote inayoendelea ingawaje kwa hali ya kawaida kabisa tunaona wananchi wa kawaida wanaona shughuli mbalimbali zinaendelea, uchimbaji ukiendelea. Kwa hiyo hatuelewi kitu chochote hatuoni faida yoyote ambayo kwa mkataba huu imeweza kulinufaisha taifa na wananchi kwa ujumla. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwasababu hiyo basi nilikuwa naomba Serikali kuitia STAMICO, iangalie namna ya kuiboresha hii taasisi ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi kwani kwa sasa hivi tunaona inafanya kazi zake tofauti yaani hatuoni tija katika shirika hili ambalo Serikali imewekeza. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine ya STAMICO ni kuangalia namna ya kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Lakini katika suala hili ninaona jinsi ambavyo STAMICO bado inahitaji kujipanga zaidi kwani wapo wachimbaji wadogo wadogo wengi sana ambao hawafanyi kazi kwa ufanisi zaidi kutohana na

kwamba STAMICO bado haijaingia zaidi katika kuwawezesha. Kwa sababu hiyo sasa naiunga mkono hoja ya Kamati kwa kuona kwamba STAMICO inabidi ijipange vizuri ili ione namna bora ya kuweza kuwasaidia wachimbaji wadogo ili waweze kuchangia katika Pato la Taifa...

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Ghasia, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Allan Kiula ajiandae.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kutoa pole kwa Wana-CCM wenzetu amba walipata ajali na kupoteza maisha kule Mkoa wa Kilimanjaro. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aweke roho zao mahali pema peponi na pia awape moyo wa subira familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda niende haraka haraka katika kuchangia hoja. Suala la kwanza nilitaka kumuuliza Waziri wa Miundombinu, hivi zile Bombadier Mtwara zitaenda lini? Mimi nimezipanda kwenda Tabora, nimepanda kuja Dodoma, kwa kweli ni ndege nzuri zinaenda kwa kasi, zinachukua muda mfupi sana. Mtwara ni miongoni mwa viwanja bora sana ambavyo vimejengwa muda mrefu, kwa nini na sisi tunyimwe hiyo haki ya kupelekewa Bombadier? Kwa hiyo, nilikuwa naomba atueleze lini hizo Bombadier zitaanza kwenda Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nililotaka kulizungumzia ni kuhusu barabara ya kutoka Mbwenkulu kwenda Nangurukuru. Kwa kweli ile barabara kile kipande kimechakaa, kinatitia na kinasababisha ajali nyingi sana. Ukitoka Somanga kwenda Daraja la Mkapa kile kipande ambacho kimejengwa na Caraf unaweza mpaka kuandika hata barua, yaani huwezi kujua kama uko kwenye gari. Tunaomba na eneo lile la kutoka Mbwenkulu kwenda Nangurukuru nalo lirezewe na liwe na ubora ule ule unaofanana kutoka Somanga kwenda Darajani. Huwezi kuamini kama uko ndani ya gari. Tunaomba kwa kweli lile eneo lirudiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni kuhusu umeme. Katika Mji wa Mtwara juzi nimepokea message kwamba wanaomba samahani kwamba siku hizi kuanzia saa moja mpaka saa nne usiku hakuna umeme. Sasa hivi anaeanza kupata umeme kuanzia saa tano huo kweli si afadhali hata tungekuwa tunapewa saa moja mpaka saa nne?

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosababisha ni kwamba zile megawati 18 zimeshakwisha sasa hivi, kwa hiyo ikitokea shoti kidogo kwenye jenereta moja ni tatizo. Tunaomba yaongezwe majenereta hali ni mbaya katika Miji ya Mtwara na Lindi. Tunaomba Wizara ya Nisahati ije na kauli inaongeza lini megawati lakini hata ile mitambo iliyopo wanaifanyia lini matengenezo ya uhakiki? Huwezi kuwa na mahitaji megawati 18 na zilizopo megawati 18. Kwa kweli hapana, tunaomba hilo waliangalie. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na suala lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni suala la barabara kutoka Mtwara kwenda Newala - Masasi ni kilometra 30, tunataka kujua mkataba unasainiwa lini Mheshimiwa Waziri? Mheshimiwa Rais alituambia akiingia madarakani kazi ya kutoka Mtwara Mnivate inaanza na eneo lililobaki ataweka wakandarasi wanne ili wajenge kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba vile viatu vya Mheshimiwa Rais, ambaye alikuwa Waziri wa Ujenzi aliyeutangulia ujitalidhi ili viweze kukuenea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Mariam Kisangi atafuatiwa na Mheshimiwa Allan Kiula, Mheshimiwa Martha Mlata ajilande. Mheshimiwa Allan Kiula.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nishukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara hizi mbili. Nizipongeze Wizara zote hizi mbili na Kamati kwa kazi kubwa zilizofanyika kwa ujumla wake na tunaweza kuchangia hapa kwa sababu kuna kazi ambayo imefanyika na tunaiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala la REA. Suala la REA kazi kubwa imefanyika, lakini bado tunaomba Wizara ifuatilie kwa karibu. Nasema ifuatilie kwa karibu kwa sababu REA II ambako umepita, umeme umepita barabarani tu. Nguzo zimeingia kidogo sana na jambo hili tumekuwa tukilizungumza kwa nyakati zote. Kwa hiyo, hao wakandarasi wanapofanya kazi inabidi wafuataliwe. Ukienda sehemu kama za Kinyangiri na Ngalakala, maeneo yote yale umeme haujaingia sana ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine katika Wizara hiyo nzungumzie suala la madini. Sisi kule Mkalama tumepata madini ya gypsum na madini mengine ya shaba yapo, lakini kinachotokea ni kwamba watu wanakuja na leseni wanaanza kuchimba madini bila kuwa na utaratibu. Tunaposema utaratibu, maana yake waje, waonane na vijiji husika, wakionana na vijiji husika basi kunakuwa na utaratibu wa kuanza kufanya kazi hiyo bila manung'uniko. Sasa hao watu wanaopata leseni wanakuja huku wanatuletea migogoro na Maafisa Madini wa Mkoa wao wanawapa barua tu wale watu wanakuja lakini lazima uweke utaratibu mzuri kurekebisha jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikienda kwenye suala zima la barabara, kwanza kwenye ukurasa wa 53 wamesema kuna barabara mikoa ambayo haijaunganishwa kwa lami lakini sikusikia Simiyu wala Singida. Nafikiri ilikuwa ni mfano tu sasa tusiwe tunasahaulika Simiyu na Singida, ni jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine; suala la alama za barabarani. Sasa hivi kumekuwa na mgogoro mkubwa, alama nyngi zimepelekwa chuma chakavu. Mimi nafikiri kama Kamati ilivyopendekeza sheria itungwe, lakini pia hatua zichukuliwe, kuwa na nguzo za saruji labda inaweza ikasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spik ukienda Mlima Saranda pale kila siku wanafanya ukarabati kwenye Mlima Saranda, zile kingo zinagongwa kila siku, ukarabati huo una gharama kubwa. Sasa hakuna njia mbadala au kuna tatizo gani pale? Ziwekwe kamera tuone labda watu wanakuja kwa mwendokasi ndiyo maana ajali zinakuwa nyngi, ukarabati wa zile kingo naamini kabisa unaghari muhi muhi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya barabara inayogharimiwa na Serikali yakiwemo madaraja, pia likiwemo Daraja la Sibiti. Miradi hiyo imekuwa inachelewa kwasababu pesa za ndani haziji kwa wakati na jambo hilo limezungumzwa na Kamati. Serikali inabidi ione athari zake, kwamba gharama za mradi zinaongezeka ikiwepo gharama wakandarasi na wale washauri waelekezi, limekuwa ni jambo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wale wataalam washauri wamekuwa na tabia ya kuegemea upande wa mkandarasi Kamati zikienda. Kwa nini hawawi upande wa Serikali ili kuweza kuona ubora wa miradi? Jambo hilo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine la barabara TANROADS, watu wanajenga kwenye maeneo...

(*Hapa kengele illa kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Martha Mlata atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Masala, Mheshimiwa Joseph Kakunda ajiandae.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nipongeze Kamati zote kwa taarifa walizowasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina machache, kwanza ninapongeza kwa maendeleo yote ambayo yamepatikana tangu uhuru mpaka sasa, maana kwa kweli tumepiga hatua kubwa sana kwenye upande wa miundombinu ya barabara, lakini bado hata kwenye matumizi ya simu za mikononi. Sasa hivi watu wanapata redio, mawasiliano na taarifa kwenye simu za mikononi, yote ni maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mambo yafuatayo:-

Kwanza, nilikuwa naomba sana Wizara ihmize taasisi zinazohusika, kwamba kwenye kasi ya maendeleo na wenyewe wakimbie. Kwa mfano, mji unapokua, miundombinu ya umeme ambayo inakuwa imewekwa, TANESCO hawaendani na ile kasi. Utakuta maeneo watu wameshajenga, hakuna transforma hakuna nini, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana waendane na kasi ya maendeleo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna suala la hawa wakandarasi wa REA. Pale Mkalama, kuna vijana 40 ambao wanadai hela zao kwa muda mrefu, miezi mitatu sasa hawapewi. Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba tusaidie kuhusu mkandarasi yule, wale vijana walipwe maana anawakimbia mpaka sasa hivi hataki kuwaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimepata taarifa kutoka kwa wananchi wanaolima vitunguu kule Mkalama, kwamba kuna mtafiti mmoja amepewa leseni ili akatafiti madini yanayopatikana pale na awaondoe wale wakulima wanaolima vile vitunguu. Ninaomba suala hili lisitishwe mara moja, wananchi waachwe, waendelee kulima zao la vitunguu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jambo lingine, Mheshimiwa Waziri nakushukuru ulifika Singida ukaenda Tumuli ukakuta kuna wachimbaji wadogo wananyanyaswa na wanadhulumiwa, ukaagiza tatizo lile litatuliwe, lakini mpaka sasa hivi bado wale wachimbaji wadogo hawaelewi hatma yao. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba sana ufike pale ili uweze kuwasaidia wale vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo tu. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Hassan Masala atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa Deo Sanga ajiandae.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru sana kunipa nafasi niweze kuchangia. Naomba nitoe pongezi, lakini pia niwapongeze Mawaziri wote kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea katika uwasilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwangu mimi ni maeneo mawili makubwa. Jambo la kwanza ni suala la umeme. Wajumbe wenzangu waliotangulia wameshazungumza sana lakini kwa kuonesha msisitizo na kwa kuonesha tatizo ambalo mikoa yetu ya Lindi na Mtwara tunakabiliwa nalo naomba nilirudie pia kulizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme Mkao wa Lindi na Mtwara ni tatizo, kwa siku umeme unakatika si chini ya mara saba mpaka mara nane. Kila Mbunge anaesimama anaetoka Lindi na Mtwara jambo hili amekuwa analiulizia na kulitolea ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba pamoja na jitihada na kazi zote zinazoendelea kufanyika, suala la umeme, kile kituo ambacho tumeahidiwa kitajengwa pale Mnazi Mmoja kwa ajili ya kusambaza umeme katika maeneo ya Kanda nzima tunafikiri sasa ni wakati muafaka wa kuweza kulitekeleza jambo hili. Kwa kufanya hivyo tutaendana sambamba na kauli ya kujenga uchumi kupitia viwanda ambavyo tunaendelea kuvihamasisha. Nje ya hapo kwa kweli hali itaendelea kuwa mbaya na watu wetu kwa kweli wanaendelea kupata shida wakati hatuna sababu ya kupata shida ukizingatia gesi sasa hivi kwa sehemu kubwa inatoka katika ukanda wa kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili katika umeme ni suala la umeme vijiji. Naomba niishukuru Serikali, kwa awamu ya pili vijiji vingi vya Wilaya ya Nachingwea vimepata umeme, lakini nilikuwa naomba katika hii Awamu ya Tatu basi ni vizuri, kama ambavyo wenzangu wametangulia kusema msisitizo uweze kuanza ili vijiji vilivyobakia katika Tarafa tano za Wilaya ya Nachingwea viweze kupatiwa umeme wa uhakika ili wananchi waweze kupata huduma ambayo kimsingi inahitajika. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni suala la barabara. Mwaka jana tumezungumza habari ya barabara, lakini mwaka huu tunapokwenda kuanza kutekeleza mambo yetu ingawaje tuko ndani ya bajeti bado kuna umuhimu wa kujenga barabara kwa kiwango cha lami. Hapa naomba niitungumzie barabara ya Masasi - Nachingwea, Nachingwea - Nanganga, ni kilometra 91. Jambo hili wananchi wa Jimbo la Nachingwea, Masasi pamoja na maeneo ya jirani limekuwa linatunyima raha sana na limekuwa linatuchelewesha kwenye shughuli za maendeleo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri pamoja na watu wa Wizara katika utaratibu tunaoenda kuweka basi kwa sababu tayari feasibility study imefanyika, tunaomba barabara hii watu wa Mkao wa Lindi, watu wa Wilaya ya Nachingwea tuweze kupatiwa ili tuweze kujikwamua kiuchumi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la madini. Mheshimiwa Naibu Waziri, mwaka wa jana niliuliza swali hapa alinipa takwimu ya makampuni zaidi ya 240 yanayofanya utafiti katika Mkao wa Lindi, lakini baada ya kufuatilia mpaka sasa hivi makampuni haya yote ambayo yametajwa katika orodha yao sijaona kampuni hata moja inayoendelea na utafiti wa madini katika maeneo yetu. (Makof)

Kwa hiyo, nilikuwa naomba kutoa masisitizo, wananchi wanataka wapate fursa ya kuchimba madini katika maeneo yanayozunguka Nachingwea, lakini bado jitihada za utafiti hazijafanyika. Kwa hiyo, nitoe msisitizo, yale makampuni yaliyotajwa tunaomba yaje na tuyaone bayana ili tuweze kuwasaidia kuwaonesha maeneo gani tunaweza tukapata madini na hivyo tuweze kusaidia vijana wetu kupata ajira wajikwamue kupitia shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda naomba niseme hayo lakini pia naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga simuoni, Mheshimiwa Deo Ngalawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe, tutamalizia na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwenye Kamati ya Miundombinu naunga mkono hoja, taarifa yao ilikuwa nzuri sana. Nakubaliana nao hoja kwamba kuzorota kwa huduma za reli kumesababisha utegemezi kwenye barabara kwa usafirishaji wa abiria na mizigo. Na hiyo ina matokeo mabaya sana kwa upande wa uchumi wetu, kwa sababu barabara zetu zinaharibika kwa haraka, tunaongeza gharama za ukarabati, uhimilivu wa barabara unapungua kutoka miaka 20 hadi miaka mitano na gharama za usafiri na usafirishaji kwa ujumla zinaadhiri uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano lita moja ya petroli au dizeli kwa wastani inauzwa kama shilingi 2,000; lakini kama mafuta yale yangekuwa yanasaferishwa kwa njia ya reli isingefika bei hiyo ingekuwa labda shilingi 1000, shilingi 800 au shilingi 1200; na hiyo ingekuwa na matokeo mazuri kwa uchumi. Kwa hiyo naomba kutoa wito Serikali isilale, ifanye mbinu zozote zile hata kama gharama ni kubwa ijengwe reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa. Hiyo itakuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa Taifa letu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, wakati mbinu hizo za kujenga reli zinafanyika, wasiache kuendelea kujenga barabara za lami na barabara za changarawe hasa vijijini ili kusudi kuwezesha gharama zetu za usafiri na usafirishaji kupungua. Kwetu kule Sikonge kuna barabara muhimu ambazo nataka nizitaje hapa, barabara ya changarawe ya Tutuo - Izimbili - Usoke, barabara ya changarawe ya Sikonge - Mibono - Kipili naomba ziangaliwe kwa macho mawili. Barabara hizi tunadhani huwa kuna mchezo unafanyika. Kwa mfano barabara ya Sikonge - Mibono - Kipili kila mwaka hupangiwa fedha kwamba itatengenezwa kutoka Sikonge mpaka Kipili, lakini wakifika Mibono wanaacha, kila mwaka. Naomba mwaka huu imepangiwa milioni 862 ifike Kipili.

Naomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi aifikirie sana hiyo Wizara, na akubaliane na mimi kwamba barabara ile itobolewe mwaka huu ifike Kipili. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ambalo napenda kulizungumzia, suala la kusema Bandari ya Tanga na Mtwara zinajиndesha kwa hasara huo ni uongo uliopitiliza. Serikali ifanye uchunguzi kubaini sababu kwa nini bandari hizi zijiendeshe kwa hasara wakati potential ni kubwa? Kwa mfano wafanyakiaresha wa pale Tanga Mjini kwa nini wapitishie mizigo Mombasa? Ina maana kuna matatizo hapo kwenye bandari ya Tanga. Kwa hiyo, naomba sana uchunguzi ufanyike ili watakaobainika hatua zichukuliwe. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne suala la mawasiliano. Zinatumika fedha nydingi za mfuko wa mawasiliano vijijini, lakini kunakuwa na wababaishaji upande wa mitambo ambayo inawekwa. Inakuwa wananchi hawapati coverage ambayo tunaitaka kwenye mawasiliano, mtambo unawekwa lakini coverage inakuwa ndogo sana. Sasa mimi naomba Wizara inayohusika; kule kwetu kuna kata za Kipili, Kirumbi, Kilori, Kitunda, Ngoywa, Ipole, Kiloleli, Igigwa, Nyahuwa na Mole, hakuna mawasiliano ya uhakika licha ya kwamba kuna minara. Mimi naomba sana Wizara inayohusika ifuatilie matumizi ya fedha za mfuko wa mawasiliano vijijini, je, zilitumika kihalali au kulikuwa na ubabaishaji, ili kusudi hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa kwenye umeme...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha Mheshimiwa.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Deo Ngala wa atafatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe, mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi naomba moja kwa moja nijikite kwenye Wizara ya Miundombinu. Ikumbukwe kuwa Wilaya yetu ya Ludewa, eneo kubwa liko mpakani mwa Malawi. Tanzania imepakana na Malawi, lakini eneo kubwa la mpaka ni eneo la Wilaya ya Ludewa, ukilinganisha na Wilaya za Kyela na Nyasa. Lakini mpaka sasa ninavyozungumza, eneo lile halina mawasiliano ya barabara, katika eneo la tarafa ile ya mwambao ambayo ina kata tano na vijiji 15 vilivyoongozana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuna kipindi palitokea mgogoro, sasa mimi nikawa najiuliza maswali, hivi mgogoro ule ungeendelea wakati hatuna barabara ya uhakika hali ingekuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende tu kukwambia na niambie na Wizara wananchi wale kwa sababu ya kuchoshwa kwa kutokuwa na barabara wameamua kuanza kulima wenyewe kwa kutumia jembe la mkono. Wanalima kwa sururu, wanalima kwa jembe, wanalima kwa chepe na mitarimbo. Ile ni dhamira ya dhati kabisa kuonesha Serikali kwamba wale watu wana uhitaji wa hicho kitu. Vile vijiji vyote tume pangana, tunalima kwa jembe la mkono. Sasa niiombe Serikali iwa-support wale watu na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri niliwaonesha hata clips za watu wakiwa wanalima kwa jembe la mkono. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri mkubwa tunaoutegemea ni usafiri wa maboti, kwa sababu meli inaweza ikapita mara moja kwa mwezi na isitoshe lile Ziwa huwa linachafuka sana, kwa hiyo, inafikia kipindi usafiri unakosekana kabisa. Kwa hiyo, niiombe Serikali kwamba sasa ichukue hatua kwa sababu wenzetu wa Nyasa wanayo barabara inayopita kando kando ya Ziwa; wenzetu wa Kyela, wanayo barabara inayopita kando kando ya Ziwa. Kwa hiyo, tuwaombe sasa na sisi upande wa Ludewa tuwe na barabara ambayo inaunganisha, kwanza itakuza utalii, halafu pili italeta maendeleo kwa sababu kuna mazao kule ya uvuvi ambayo yanapatikana kwa wingi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia eneo lile halina mawasiliano ya simu kabisa. Mimi ninaamini katika nchi nane tulizopakana nazo, eneo ambalo halina mtandao wa mawasiliano ya simu inawezekana ikawa ni mwambao wa Ziwa Nyasa. Tuna kata tano, tuna vijiji 15 halafu viko mpakani. Sasa cha kushangaza tumekuwa tukifatilia hii kitu sijajua tatizo liko wapi lakini ningependa tu niseme watu wa Ludewa nao wangependa kuwa na maendeleo, wangependa kuwa na mawasiliano ya simu maeneo yale. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu bandari. Pamoja na kuwa wakati mwingine meli ile inatembea mara moja kwa mwezi, lakini bado bandari zake ziko kwenye umbali mrefu sana.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Deo Ngalawa. Mheshimiwa Hussein Bashe tutamalizia na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mimi nilitaka niseme kwanza niipongeze Kamati kwa taarifa walizoleta, lakini jambo moja nilitaka niseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nchi tumekuwa tukijadili suala la kuwa na viwanda. Mambo mawili ni muhimu sana, sekta ya miundombinu na sekta ya umeme. Nilitaka niishauri Serikali, imefika wakati wa ku-embrace private sector (PPP), energy sector mawazo ya kufikiri kwamba tutatumia fedha zetu za ndani kununua majenereta, kuzalisha umeme sisi, TANESCO izalishe umeme, ifanye nini, hatutopiga hatua ya kuwa na hizo megawati 10,000 tunazotaka. (Makofii)

Kwa hiyo, mimi ningeshauri, wizara mnafanya kazi kubwa sana kwenye rural energy, mnafanya jitihada kubwa sana lakini mfungue fursa kwa ajili ya uwekezaji wa sekta binafsi kwenye umeme, ili watu waweze ku-compete na kupatikana umeme wa bei rahisi ili Mwijage atuletee viwanda. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini umeme hauwezi kuja bila kuwa na proper incentive scheme kwenye sekta. Ningewashauri Wizara ya Nishati pamoja na Wizara ya Fedha, na Wizara ya Viwanda na Biashara, kaeni chini m-develop incentive scheme kwa ajili ya uwekezaji wa private sector mziweke wazi ili wawekezaji wajue tukienda Tanzania kuwekeza mtaji wetu, these are the benefits na Wizara ya Fedha iache mindset ya kuweka kodi kwenye inputs. Tarajieni kuvuna kwenye matokeo hilo ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niiombe Wizara ya Miundombinu, mmeanza jitihada kubwa sana ya kujenga reli ya kati, kupanua bandari, ni jambo jema. Lakini kule kwetu Nzega, kama Mkoa wa Tabora kuna barabara; mwaka 2014/2015 mliituwekea fedha kwa ajili ya visibility study hazikutosha, kwa hiyo ule mpango wa barabara ya kutoka Tabora kupita Mambali kwenda Bukene, kwenda Itobo, kwenda Kahama mpaka leo imesimama. Ni ahadi ya Rais Kikwete, ni ahadi ya Rais Magufuli, kwa hiyo, nakuomba kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, tukumbuke barabara hiyo ni muhimu sana kwa uchumi wa eneo lile. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kuna Daraja la Nhobola pale Nzega, Mheshimiwa Waziri unafahamu, tumegonga sana mlango ofisini kwako kuomba haka kadaraja. Sasa hivi wananchi wa jimbo la Nzega upande wa Nhobola hawavuki kwenda kupata mahitaji katika Mji wa Nzega, inabidi wazunguke kwenda Tinde kwenda kupata mahitaji Mkoa wa Shinyanga ambako ni mbali zaidi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye uwekezaji wa reli, Mheshimiwa Waziri hakuna clause muhimu ambayo mnatakiwa muiweke kama Serikali; mambo mawili, commitment ya nchi ya mapato yetu ya ndani ambayo tunatoa shilingi kulipa mkandarasi yatumike kama sehemu ya kulipa contract za ndani. Tukitumia zile fedha kumlipa mkandarasi wa nje maana yake tuta-transfer dola kupeleka nje, zitatuumiza.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bashe usianzishe hoja nyingine, muda wako umekwisha.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia. Transfer of knowledge... (Makofii)

NAIBU SPIKA: Haya tuaendelea na Mheshimiwa Fredy Atupele.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyio mbele yetu, ya Kamati ya Miundombinu. Kwanza niipongeze kamati kwa jinsi ambavyo wameleta taarifa ambayo iko vizuri na ipo very detailed pamoja na Mwenyekiti wa Kamati hii. Nina mambo machache ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni suala la viwanja vya ndege, nikisoma ukurasa wa 17 inaonesha kabisa viwanja vya ndege vingi katika nchi yetu vinaendelea kujengwa. Lakini kuna viwanja ambavyo vilikuwa vilikuwa vinaendela kwa muda mrefu hadi sasa hivi wanapoleta hii ripoti havijapelekewa pesa hata senti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na kiwanja cha ndege cha Songwe. Kiwanja cha ndege cha Songwe mwaka 2015/2016, kilitengewa shilingi bilioni tano lakini hawakuletewa fedha hizo, mwaka 2016/2017, tumetengewa bilioni saba hadi wanaandika ripoti hii hawajaletewa hata senti tano, maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanja hiki, ni mfano mzuri kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Mkoa wa Mbeya, Rukwa, Katavi, Njombe, Iringa mpaka Songea. Kwa maana nyine kwa wale wote ambao wanatumia ndege zinazokwenda Mbeya ni hivi karibuni ni majuzi tu fastjet imerudi kwa sababu ya kutweza kutua katika kiwanja kile. Imerudi kwa sababu ukungu ambao unatanda eneo lile, hakuna taa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nchi na kama Taifa tunataka tuwekeze zaidi katika masuala ya viwanda, na wawekezaji wengi wanataka watumie usafiri huu wa njia ya ndege kwa ajili ya kuja kuwekeza viwanda vyao hapa nchini. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwamba, kwa bajeti ambazo zimetengwa katika viwanja ndege mbalimbali katika nchi hii; ukizingatia Mheshimiwa Rais, nampongeza kwa sababu ameshanunua ndege nyngi katika nchi hii, na bado tunaendelea kununua kama Serikali. Kwa hiyo, viwanja hivi viweze kupelekewa fedha zao kwa wakati na viweze kutengenezwa kwa wakati. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine muhimu zaidi ni suala la barabara kwa za kuunganisha kwa kiwango cha lami. Nizipongeze Serikali ya Awamu ya Nne na ya Tano zote zinaendelea kuthubutu kuunganisha maeneo mbalimbali katika nchi yetu kwa ajili ya kuunganisha wananchi, lakini pia kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Nimuombe pia Mheshimiwa Waziri, kwamba kuna barabara ambayo imeahidiwa mara nyngi, na nimeisema hapa Bungeni kwa miaka mingi; barabara ya Katumba - Lwangwa - Mbwambwa - Tukuyu, kilomita 83, na wewe Mheshimiwa Naibu Waziri uliona jinsi ambavyo wananchi tulipokea kwa furaha na tupo tayari hata kutoa maeneo yetu kwa ajili barabara iweze kujengwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la mawasiliano. Mawasiliano katika nchi yetu yamekuwa kwa haraka sana, lakini jambo ambalo linasikitisha kidogo kwa wenzetu hawa wa TCRA kumekuwa na utapeli mkubwa sana kupitia mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara, lakini pia na wataalam, kuna wataalam wazuri katika nchi hii ambao wanaweza wakaishauri Serikali ni mechanism gani zitumike kwa ajili ya kuwabana wale wote ambao ni matapeli kwa njia ya mawasiliano na ninaamini kwa kuwa na mimi pia niko kwenye fani hiyo tunaweza tukasaidiana na watu wengi kuiwezesha Serikali ili wananchi wake wasitapeliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la umeme/nishati. Nakupongeza sana Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo pamoja na Naibu wako kwa kazi nzuri mnazozifanya. Suala la REA III na REA II imekuwa ni changamoto katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiw Naibu Spika, mara nyingi Mheshimiwa Waziri umekuwa ukisistiza kwamba wakandarasi wanapokuja katika maeneo yetu lazima wawasiliane na viongozi ambaao ama ni Waheshimiwa Wabunge ama Madiwani. Lakini kwa bahati mbaya sana wakandarasi wanakwenda eneo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge sasa tutanza kusikia upande wa Serikali halafu tutawaita watoa hoja. Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niunge mkono hoja, pia niungane na waliotoa pole kwa wenzetu wana-CCM ambaao walipata majeruhi huko Moshi, tuwaombee ndugu, jamaa na wengine wapate kupumzika salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajielekeza kwenye mambo ya msingi na niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, kwenye hoja za maandishi pamoja na zile za maneno. Kwa ujumla tuna hoja 30 za maneno na za maandishi nane, kwa hiyo, zilikuwa ni hoja nydingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge nianze tu na kuzungumza kidogo, kuhusiana na masuala ya kazi ya kusambaza umeme, hasa kwa Shirika letu la TANESCO. Nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge speed kulingana na uharaka wa utandazaji umeme kwa kweli haulingani na uwezo wa TANESCO kwa sasa, lakini tunachofanya ili kuendana na changamoto hizo sasa Serikali imeweka mikakati ya kufuata ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata umeme kwa haraka kutoka shirika letu la TANESCO.

La kwanza kabisa, tunawashukuru Bunge lililopita lilitupitishia bajeti ya kuanzisha ofisi 47 kwa ngazi za Wilaya, sasa tunaanza utaratibu wa kuimarisha ofisi na kujenga ofisi nydinge mpya katika maeneo ambako hakuna ofisi. Hii ni hatua madhubuti sana kuharakisha upatikanaji wa umeme katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo kwa sababu wakati mwininge ni ufinyu wa bajeti, ili kupambana na hatua hiyo, TANESCO sasa imeanza utaratibu ufuataao:-

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa tulishaagiza transfoma zote pamoja na nguzo yataanza sasa kununuliwa hapa nchini. Hii itarahisisha sana usambaziji wa umeme kwa kasi kubwa. Kwa hiyo, tuna imani kwamba kwa hatua hii itaharakisha sana usambazaji wa umeme mijini na vijijini. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili, wakati tunajipanga kujenga ofisi, tumeanza sasa kuanzisha madawati ya huduma kwa wateja mahala ambako kuna wateja wengi, badala ya kusubiri kujenga ofisi mpya. Hii ni hatua madhubuti itaturahisishia sana kusambaza umeme kwa wananchi wengi na kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine tumeagiza shirika letu, kuanzia Januari mwaka huu, litaanza sasa kufata wateje walipo badala ya lenyewe kufuatwa na wateja. Hii itasidia sana, kwa sababu maeneo mengine kwa wananchi hawawezi kufikia ofisi zetu na hata wakifika inakuwa kwa ghamama kubwa na wakati mwingine wanakata tamaa. Kwa hiyo, sasa wataalamu wa TANESCO wa shirika letu wataanza kufuata wateja walipo ili kuharakisha huduma hizi mahsus. Kwa hiyo, tunaamini kwamba utaratibu huu utachangia sana kuharakisha uzambazaji wa umeme ili kulingana na kasi ya ukuaji wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika sambamba na hilo nizungumzie kidogo kukatikakatika kwa umeme. Ni kweli, hasa maeneo ya Lindi na Mtwara hata kule Geita kwa Mheshimiwa Kanyasu na maeneo ya Dar es Salaam. Kazi inayofanyika sasa hivi ni pamoja na ukarabati wa miundombinu ambayo kwa kiasi kikubwa mingi imekuwa ya muda mrefu. Sasa katika kipindi hiki kifupi, maeneo mengi yataendelea kupata shida kidogo, lakini ni tatizo la muda mfupi, jithhada madhubuti zinafanyika ili kurekebisha hali hii. Ni matarajio yetu ndani ya miezi hii miwilii ukarabati wa maeneo mengi utakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la Lindi na Mtwara nielezee kidogo. Lindi na Mtwara wananchi wa Lindi wanatumia megawati 18. Kwa sasa mashine moja imeharibika, inafanyiwa ukarabati hasa kuhakikisha kwamba ile mashine iliyo haribika inafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo ujenzi wa kusafirisha umeme sasa kutoka Mtwara kwenda Lindi ambako kituo cha kupoza umeme pale Mnazi Mmoja kinajengwa na kinatarajiwa kukamilika ndani ya miezi miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa wananchi wa Mtwara baada ya kituo kile kukamilika, hasa kile kituo cha substation kutoka kilovolti 33 kwenda kilovolti 130 zitakapokamilika matatizo ya kukatika umeme kwa wananchi wa Lindi na Mtwara yatatataluka kwa mara moja. Kwa hiyo ni vizuri tuwaeleze wananchi wa Mtwara, ni kero hata kwetu sisi tunaliona lakini ni jambo ambalo linafanyiwa kazi kwa kina sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo lilizungumzwa, ni suala la sera ya mafuta kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Ni kweli kabisa suala la kutafsiri lugha za kigeni sasa ni muhimu sana kwa sababu watumiaji wengi ni Watanzania ambao ndio kwa kiasi kikubwa wanatumia lugha ya Kiswahili. Mkatati umeshaanza, timu ya wataalam imeshaundwa inayojumuisha wizara yetu pamoja na taasisi zinazojumuisha Wizara yetu; lakini kazi hii itafanyika kwa kushirikiana na TUKI ambao ni wataalam wa kutafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili kuepika kufanya kazi na TUKI peke yake, na kuna masuala mengine ya kiteknolojia na ya kitaalam zaidi, lazima timu mbili zifanye kazi kwa pamoja. Kwa hiyo, utaratibu unaofuata sasa ni kukaa pamoja ili kuanza kazi hiyo mara moja. Ni matarajio yetu ndani ya miezi miwili/mitatu timu hiyo itakuwa imeshaanza kazi, pamoja na TUKI. Kwa hiyo, suala la kutafsiri linafanyika na utaratibu tumeshauanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulinda Tanzanite. Kwanza niseme kwamba ni kweli kabisa madini ya Tanzanite hapa ulimwenguni yanapatikana Tanzania peke yake, hakuna sehemu nyingine, kwa maana ya yanakochimbwa. Lakini nikiri kwamba, yako matatizo na changamoto ambazo zimesababisha pia control yake kuwa kidogo. Hata hivyo hatua za Kiserikali ambazo zimefanyika, ni vizuri kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba hili neneo kuanzia mwaka 2001 lilianza kutengwa kama eneo tengefu ili kuhanakisha kwamba rasilimali ya Tanzanite haitoroshwi nje bila kuzingatia utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni changamoto kidogo, ilikuwa ngumu na ujenzi wa fence ulifanyika mwaka 2005, lakini kwa bahati mbaya sana wananchi wanaozunguka maeneo yale waling'oa fence pamoja na vyuma. Kwa hiyo, mkakati unaofanyika sasa ni kujenga fence ya mawe pamoja na tofali, tunatafuta fedha kwa ajili ya kujenga fence hiyo. Kwa hiyo, nikushukuru Mheshimiwa Ndassa ye ye alikuwa Mwenyekiti wa Nishati na Madini huko nyuma huko nyuma kwa kuliona hili, lakini jitihada zinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingi sana imefanyika katika eneo hili. Pamoja na kuanzisha Police Post, kimejengwa Kituo mahususi cha polisi pale Mererani ili kuhakikisha kwamba udhibiti unakuwa imara na ambao kwa kweli ni shirikishi. Tunaamini kwamba hatua hizi zimechangia kwa kiasi kikubwa kusaidia madini yetu yasiende nje sana. Lakini pia, kuna *joint committee* iliyyoundwa ikishirikisha taasisi mbalimbali ikiwemo Uhamiaji, TRA na nyininge ili kudhibiti utoroshaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hayo ili kupunguza utoroshaji wa madini ya Tanzanite, mwaka 2010 Sheria ya Madini Mpya ilivyotungwa ilipunguza kiasi cha mrabaha kutoka asilimia tano kwa madini yaliyokatwa kurudi asilimia moja ili kuvutia Watanzania wengi kukata madini ya Tanzanite hapa nchini. Kwa hiyo, hizo ni hatua ambazo Serikali imechukua, ambazo ni vizuri sana kuwaeleza wananchi, lakini pia, changamoto tunazichukua bado tutaendelea kuimarisha ulinzi zaidi katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu REA III nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge wengi, REA II iliyokamilika hivi sasa kwanza niseme imekamilika kwa asilimia 95.8 na asilimia 4.2 iliyobaki ni kwa ajili ya kuwaunganishia umeme wateja. Sasa kazi ya kuunganisha umeme inategemea mambo mawili, la kwanza utayari wa mwenye nyumba, mtaji.

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kalemani, naomba umalizie, muda wako umekwisha.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, basi nijielekeze la mwisho, nizungumzie kuhusiana na mikakati ya REA III. REA III imeshaanza maeneo ya mikoa sita kama nilivyotaja juzi, Mkoa wa Pwani, Mara, Arusha, Iringa, Njombe, Mbeya pamoja na Songwe, kwa hiyo, tumeshaanza na utaratibu utakwenda hivyo kwa nchi nzima, na mpaka kufikia tarehe 31 Machi nchi nzima sasa wakandarasi watakuwa wameingia kwenye mikoa yote kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa REA III.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zitakazofanyika, nisaidie kunipa dakika moja kwenye hili, ni pamoja na kufikisha umeme kwenye vijiji vyote vilivyosalia ambavyo ni 7,873 pamoja na vitongoji vyake. Lakini kazi ya pili ni kupeleka umeme kwenye taasisi zote za umma, hapa nina maana ya hospitali, zahanati, magereza, polisi, shule, masoko pamoja na pampu za maji. Kwa hiyo, huu ni mradi mkubwa, tunatarajia wananchi wote watapata umeme kwa kupitia mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia utapeleka umeme kwenye maeneo ambayo yako nje na gridi, hasa visiwani pamoja na yale ambayo yanapitiwa na Hifadhi za Taifa. Ni mradi wa miaka minne hadi mitano, kwa hiyo, mwaka wa 2020/2021 tuna matarajio kwamba vijiji vingi vitakuwa vimepata umeme kupitia mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kusema jambo hili ambalo nadhani ni tamu sana kwa Waheshimiwa Wabunge. Hatua tunayofanya kwa sasa ni utandazaji wa umeme shirikishi. Kabla mkandarasi hajaingia kwenye site yoyote ile ataanza kwanza kupiga hodi kwa Mbunge

husika. Hii itasaidia sana kupeleka umeme maeneo ambako wananchi mnajua vipaumbele, lakini pia ataenda hata kwa Mheshimiwa DC na Mkuu wa Mkoa ili kusaidia katika usimamizi wake. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu muda ni mfupi, ningependa niseme mengi sana kuhusu hili, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. (Makofij)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Engineer Ngonyani!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, na niseme mapema kabla sijagongewa kengele, nimefurahishwa sana na Taarifa ya Kamati ya Miundombinu na yote mliyoyaandika tutayazingatia kwa umakini kabisa. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mambo yote ambayo mmetuambia iwe kuhusu barabara, mawasiliano, tutayafatilia kama ambavyo mmetuelekeza. Najua hii ni taarifa ya Kamati, lakini mmetupa fursa na sisi tusikie yale ambayo mnahitaji kuyasikia. Na tumeyasikia, tutayachukua na tutayafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu niende kwa haraka sana katika maeneo machache. Kwanza naomba sana Waheshimiwa Wabunge wale wa upande wa Mtwara, walioongelea barabara ya Mtwara hadi Mnivata, naomba nitoe taarifa rasmi kwamba ni kweli mkataba umesainiwa tarehe 19 Januari. Taarifa ambayo tulikuwa tumetoa mwanzo ilikuwa inazingatia taarifa mpaka tarehe 31 Disemba, 2016, ambacho ndicho kipindi tulichokuwa tunakitolea taarifa. Naomba nitoe taarifa rasmi kwamba huo mkataba umesainiwa. Na ninamshukuru sana AG personally kwa namna alivyofatilia kuhakikisha kazi ya kukamilisha kile kipengele kidogo ambacho kilikuwa kinaleta matatizo amekishughulikia kwa haraka sana. Nakushukuru sana AG. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, ningependa vilevile kuongelea suala la ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mtwara nikianzia na cha Mtwara, kazi ya usanifu imeshakamilika hivi sasa taarifa ya mwisho inafanyiwa kazi na wataalam na mara watakapoikamilisha tutaenda kwenye hatua inayofuata ya kutafuta fedha kuanza ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa viwanja vya Tabora, Sumbawanga, Shinyanga na Kigoma, fedha tunazo kwa sababu tuna hela kutoka European Investment Bank na suala la mikataba hivi sasa tunavyoongeelea ndio tupo katika hatua ya mwisho ya kukamilisha uchambuzi, umeshafanyika, muda sio mrefu watatoa taarifa ya akina nani watakuwa wameshinda katika maeneo hayo na kazi ya ukarabati wa viwanja hivyo vinne ienze. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu kwa viwanja vya Musoma, Iringa na Songea, usanifu na ukarabati pamoja na usanifu kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa viwanja hivyo nao upo katika hatua ya mwisho. Taarifa itakapokamilika zabuni zitatangazwa kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa viwanja hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye kiwanja cha Mwanza, walismama muda mrefu. Nimshukuru Mheshimiwa Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, ametuwezesha tumelipa shilingi bilioni 7.6 na kazi ya ujenzi wa kiwanja kile cha Mwanza sasa imeanza kuchangamka zaidi. Tunashukuru sana kwa hilo na tunaomba wenzetu wa Fedha waendelee kutupa hela zaidi tuondoe maeneo yale yote ambayo tunadaiwa, ili kazi hii ya kujenga miundombinu kwa ajili ya Watanzania tuweze kuikamilisha kwa haraka kwa sababu tunataka tufanye hivyo, lakini

wenzetu wa Hazina ndio wanaotuwezesha. Nishukuru kwa kiwango hicho mlichotuwezesha hadi sasa na ninaamini mtaendelea kutuwezesha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na vivyo hivyo kwa Kiwanja cha Songwe tulichokamilisha, kwanza ni usimikaji wa Taa za kuongozea ndege, hiyo tumekamilisha. Kilichobakia ni ujenzi wa jengo la abiria na ambalo tulikuwa na ubishani kidogo au kuna mgogoro kidogo wa malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashukuru suala la mgogoro huo limekaribia kukamilika, tupo katika hatua ya mwisho ya kusainiana kwamba, ni kiasi gani tuliwalipa zaidi na hivyo waanze sasa kujenga kwa kiasi kile tulichowalipa zaidi, na bahati nzuri sasa tumeanza kuelewana. Mwanzo tulikuwa hatuelewani na ndio maana tumechelewa kidogo katika kuanza kujenga kiwanja hicho cha Songwe, sasa tumefikia mahali pazuri, naamini tutafika mahali sasa kiwanja hiki nacho kitakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kidogo kuhusu TCAA; labda kitu kimoja tu, kuhusu radar. Najua kuna wachangiaji wa maandishi wanatuletea, naomba tu nao niwathibitishie kuwa ujenzi wa radar au usimikaji wa radar katika sehemu kuu nne za Tanzania, kwa maana ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Songwe, mkataba wake tunatarajia muda si mrefu, sasa hivi zipo katika process za procurement, nina uhakika katika kipindi kisichozidi wiki mbili tutakuwa tumefika hatua nzuri na mwezi Machi mjenzi wa hizo radar itapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kuhakikisha Tanzania yetu inakuwa covered na radar. Si sahihi nchi yetu iwe inaangaliwa na Kenya, iwe inaangaliwa na Rwanda na sisi wenyewe tupo kwenye giza. Hatutakubali hilo, na tunahakikisha katika miaka miwili ijayo Tanzania yote tutakuwa tumei-cover kwa radar na tutakuwa tume-recover yale maeneo ambayo wenzetu walikuwa wajanja, waliwahi kuwekeza katika radar na wakaanza kupata mapato ambayo kwa kweli, yalistahili kuja katika nchi yetu; tutahakikisha mapato hayo tunayarudisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadugu zangu kwa upande wa mawasiliano; ninawashukuruni sana kwa mambo mengi mnayotusaidia. Kulikuwa na tatizo kubwa sana kwenye Kampuni ya Halotel, tumewapa mikataba ya kuweka mawasiliano katika vijiji mbalimbali karibu 4,000 lakini mmekuwa mkitupa taarifa (mrejesho) kwamba hapa wanasema wameweka na wakati mwingine ninyi Wabunge mnatuambia kwamba mawasiliano hayapo. Sasa nashukuru kuwaambia kwamba tuna mitambo imeagizwa na taasisi yetu ya TCRA sasa ina uwezo wa kupita kuhakiki katika kila maeneo ambayo wenzetu makampuni ya simu yamepewa kazi ya kuweka mitandao hiyo, hawawezi kutudanganya tena kwa kuwa tutakuwa na uwezo wa kuhakiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa hilo na tunawahakikisha hivi vijiji 4,000 lazima tukamilishe itakapofika mwezi Novemba, kama mkataba ambavyo tulikubaliana na watu wa Halotel. Vilevile niwambie tu kwamba hata Vodacom, Airtel na TiGo, mwanzo waliokuwa wanadai kwamba, vijijini hakuna fedha kwa hiyo, hawataki kwenda, sasa hivi wanavyoona jinsi Halotel wanavyochangamka maeneo ya vijijini na jinsi anavyo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kweli, naunga mkono sana na sasa naelewa kwa nini nina Maprofesa upande wa Kamati na upande wa Wizara. Nawashukuruni sana kwa kazi kubwa mnayoifanya. (Makofi)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Kwanza nianze kwa kusema kuna mengine yalikuwa ni ya utawala, mengine ni ya kibinagsi, mimi sitagusia mambo ya utawala kwa sababu tuna mihimili mitatu, siwezi kuja kujadili mambo ya utawala Bungeni, nadhani si utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha pili. Labda ifahamike vizuri sana hii ya bei, mimi ninawasiliana na Waziri, ninawasiliana na Mwenyekiti wa Bodi. Kwa hiyo, aliye na barua kutoka kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji au Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA hiyo ndio anapaswa kuileta hapa Bungeni, ndio mimi nawasiliana nao hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ninafanya vikao vingi sana na wafadhili, vingi sana. Ni vizuri ukiwa na barua moja uje na barua 20 maana vikao vyangu na wao ni vingi mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuje kwa mambo ya msingi. Kuhusu magwangala, niseme vilevile kwa kifupi, nina ripoti nimetoa ushauri kwenye kila tani kumi ya magwangala ndio natoa gramu nne! Kwenye kila tani kumi natoa gramu nne! Na yale magwangala katika kuchambua dhahabu, mgodini wametumia siodine na huyu anakuja kutumia mercury! Waheshimiwa Wabunge ninaacha mfanye tafsiri wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeulizwa swali la *capital gain* kati ya BG na Shell. Ukweli ni kwamba Shell hawajalipa *capital gain*, hata mchana huu nilimuita Vice President wa Shell ametoka London, kujadiliana nao. Msimamo wa Serikali ni kwamba lazima *capital gain* ilipwe kwa sababu iko kisheria. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwazi wa mikataba. Tulishasema mara mia hapa kwamba yeoyote anayehitaji mkataba wowote ataupata, tutauleta kwa Spika na pale atapata sehemu atasoma, atarudisha. Na niombe, labda kwa kuwa kwa Spika labda ni usumbufu sana, Mheshimiwa yule Mbunge Jumatatu, saa 2.00 asubuhi nimewaambia TPDC waweke mikataba yote wampe asome. Ndio uwazi huo, hakuna cha kuficha. Aende asomee pale TPDC. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ya kusema uzoefu wa nchi zingine kwamba mikataba inawekwa wazi, Waheshimiwa Wabunge na ninyi ni wazoefu, hakuna nchi ambayo unakuta mkataba umeandikwa kwenye gazeti. Na kama kweli mkataba unaandikwa kwenye gazeti, basi tuanze na mikataba yetu sisi wenyewe tuliyonayo tuchapishe kwenye magazeti. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria na kanuni. Ni kwei tunachelewa kutengeneza kanuni, sasa hivi kanuni mpya nzuri kabisa ni kwamba mgodi wowote unaoanzishwa mara moja unaenda kwenye Soko la Hisa. Sasa malalamiko kwamba hatufaidi yamekwisha, na ile iliyoanza zamanii imepewa miezi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndugu zangu wa Kahama, Tarime, nendeni soko la hisa sasa hakuna kisingizio kwamba, hatufaidiki. Narudia, Kanuni inasema lazima asilimia 60 zikamatwe na Watanzania, twendeni soko la hisa. Unajua huku sasa twende kwa vitendo Waheshimiwa Wabunge, kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ruzuku kwa wachimbaji wadogo. Ruzuku zipo, iko kwenye llani ya CCM na hizi ni fedha za mkopo wa World Bank. Wengine walisema ooh, nilijadiliana na World Bank kuhusu bei ya umeme! Nina mijadala mingi, mbona hii ya wachimbaji hawasemi? Fedha zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu TANESCO deni lake. TANESCO wanadaiwa, kama alivyosema Mwenyekiti, zimeshavuka shilingi bilioni 820. Na mimi bado msisitizo wangu sikubali

TANESCO ipandishe bei hata kama wengine wakizunguka na barua, msimamo wangu huo unafahamika, kwa sababu hili deni la shilingi bilioni 320 hatujalichambua, hatuwezi kuangalia tu wanasema uzalishaji wa umeme ni wa bei kubwa lakini hatujachambua. Mtu hajaniambia kwa nini bwana fedha wa kituo kimoja ana hoteli 4 wa TANESCO, huyo nae tumchangie, tupandishe bei, haiwezekani, haiwezekani! Au mtu ananunua lita 20 anaandika amenunua lita 50! Zimebekwa gari zote za TANESCO tracking system, hata maruti, hata zilizo kwenye mawe, eti tupandishe bei umeme! Narudia, haiwezekani. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwisho wa mwaka wanapeana bonus milioni 50, utapandishaje bei kwa ajili ya bonus zao? Haiwezekani. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, umeme haupandi hata mtu azunguke, kwanza wote wanafahamu, *World Bank, African Development Bank, European Union* kitu ambacho nilikuwa napambana nao, sikubali umeme upande. Lakini ukiangalia ile action plan wanasema tarrif...

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika tano tayari? *Tarrif review, nayo ni kiingereza. Review maana yake sio hacking, you can review and go down.* Hizi document ukizunguka nazo ni tafsiri vilevile. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado dakika ngapi?

MBUNGE FULANI: Dakika tano.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, haya, tano eeh! Okay, good! Thank you.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hivi ndugu zangu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa bado dakika tatu.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, tatu. Tuongee cha maana zaidi. Ni kwamba, tukitaka Taifa letu liendelee ni lazima *FDI (Foreign Direct Investment)* za kutoka nje tuzivutie kutoka za sasa hivi 2.5 mpaka zaidi ya 15 ifikapo mwaka 2025. Na kufanya hivyo kati ya mwaka huu na mwaka 2020 tunahitaji *investment* kwenye umeme; tunahitaji dola bilioni 12. Alichosema Bashe ni muhimu *12 billion* ikifika mwaka 2020 wakati tutakuwa na megawati zaidi ya 5000. Na ndiyo maana tunaibadilisha TANESCO iwe ya kisasa na itaumiza wenyewe biashara huko wanachukia lakini lazima ibadilike, iendane na haya matakwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema mengine ya muhimu sana kwamba hatujafaidika na gesi, umeme tunaoutumia hapa mwingi ni wa gesi na kitakachotupeleka nchi ya kipato cha kati ni uchumi wa gesi. Tuna mradi mkubwa wa *LNG*, tunaujadili, utachukua muda utakuja hapa Bungeni. Tuna bomba la Tanga litakuja hapa Bungeni, kote tupo kwenye matayarisho. *Investment* ya bomba la Uganda ni bilioni 3.5; lazima mtayarishie kabla hamjaanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *investment* ya *Liquefied Natural Gas (LNG)* ya Lindi ni *30 billion US Dollars*; wapo kwenye matayarisho. Juzi nimetoka Zambia tumeleta tena mradi mwingine mkubwa, bomba lingine tena; hii ndio maana inaitwa nchi ya mabomba mzee ambaa utakuwa karibu wa dola bilioni mbili. Sasa hii unaweza usione kitu kinafanyika, hii ni lazima ninyi

Waheshimiwa Wabunge mje hapa, miradi hii inataka sheria, watu wamejifungia huko sasa hivi hatulali mchana na usiku. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha mbolea Mheshimiwa aliesema tunajenga viwanda viwili, kimoja Kilwa na kingine Lindi. Cha Kilwa *investment* yake ni bilioni 1.9...

(*Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Kamati na Waheshimiwa Wabunge, naunga mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Profesa Mbarawa.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote na mimi napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajielekeza kwanza kwenye Reli ya Kati. Kama tunavyoju reli hii ya katiba imejengwa mwaka 1905 na imechoka sana kwa sasa; na ina uwezo a kuchukua tani milioni tano tu; na kutoka Dar es Salaam kwa mfano kwenda mwanzia unachukua takribani masaa 30. Serikali ya Awamu ya Tano chini ya kiongozi wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliamua sasa tujenge reli ya kisasa, reli ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua mizigo tani milioni 17. Pia itakuwa na uwezo wa kukimbia kwa speed ya kilometra 160 kwa saa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ina maana kuwa kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro tutatumia saa moja na dakika kumi na sita, kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma tutatumia masaa mawili na nusu na kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza tutatumia masaa saba na nusu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Afrika kuna nchi tatu zilizojenga *standard gauge*, ya kwanza Kenya, Ethiopia na Nigeria; lakini zote hizo treni zake zinakwenda speed ya 120 si 160 kama Tanzania. Na katika nchi hizo ni Ethiopia tu ndiyo inatumia umeme na sisi Tanzania. Katika Bara la Afrika ni treni moja tu sasa hivi inayokwenda kilometra 160 ambayo ni *Gautrain*, ni ile iliyopo pale Johannesburg na ile ni treni ya mjini inakwenda kilometra 80 tu; lakini ya Tanzania itakwenda kilometra takribani 1,600. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mlivyosikia tarehe tatu tulisaini mkataba kati ya RAHCO kwa niaba ya Serikali na kampuni ya Kituruki ambayo tunaita Yapi Merkezi na Kampuni ya Mota-Engil ya huko Ureno kwa gharama ya dola za Kimarekani bilioni 1.2 sawa na kila kilometra moja tutajenga kwa dola za Kimarekani milioni nne, hiyo ni pamoja na VAT. Ukiiondoa ushuru kwa kila kilometra moja tutajenga kwa dola milioni 3.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niwachukue Waheshimiwa Wabunge kwa wenzetu majirani. Kenya wanajenga reli yenye urefu wa kilometra 605, wao wanatumia dola za Kimarekani bilioni 3.1 sawa na kila kilometra dola za Kimarekani milioni 5.3 wakati Tanzania tunatumia dola za Kimarekani milioni 4. Ethiopia na wao wanajenga treni kama hii, wao wanatumia kila kilometra moja dola za Kimarekani milioni 4.5. Kwa hiyo, Tanzania tumeweza kufanya wajibu wetu vizuri na tumepata kwa bei nzuri kuliko wenzetu wote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kukawia kwingine ni kuzuri sana, unaweza kuwahi mwisho wake ukaenda ukaangukia pabaya. Tunaamini Tanzania na timu yetu iliyofanya kazi hii ilifanya

kwa uadilifu mkubwa na tumepata *good deal* tunasema. Na kazi hii ya ujenzi itaanza mwisho wa mwezi Machi na itachukua takribani miezi 30. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo tumetangaza tender kwa ajili ya Morogoro - Makutupora; tumetangaza tender nyngine kwa ajili ya Makutupora hadi Tabora, kutoka Tabora hadi Isaka na tender ya mwisho kutoka Isaka hadi Mwanza. Nia yetu ni kuwapata wakandarasi mbalimbali ili kazi hii iende haraka na Tabora - Kigoma inakuja. Lakini kama kazi hii tutampa mkandarasi mmoja anaweza kuchukua hata miaka minne ama mitano. Kwa vile Serikali tumeefanya uamuvi sahihi kwa watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijikite haraka haraka kwenye Mamlaka ya Bandari. Ni kweli Mamlaka ya Bandari katika robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha mizigo ilipungua wala hakuna mjadala kuhusu hilo. Lakini kuanzia mwezi Oktoba, Novemba na Disemba meli ziliongezeka na mizigo ulianza kuimarika. Ni kweli sasa hali ya bandari inaendelea vizuri kuhusu mizigo na tunategemea hali hiyo itaendelea vizuri kila tunapoendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ujenzi wa miundombinu, tayari tumemepata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi au ukarabati wa Bandari ya Dar es Salaam gati namba moja mpaka namba saba; na tunategemea baada ya mwezi mmoja na nusu kazi ya ujenzi itaanza. *World Bank* wanataka kutoa pesa, lakini kama watachelewa tayari tumejipanga, tunazo pesa bandari na tutaanza kufanya kazi hiyo mara moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Bandari ya Mtwara tayari vile vite tumeshampata mkandarasi na sasa hivi tunaanza kujipanga ili kazi ianze. Tumepeleka document Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya vetting na tunafanya due diligence ya mkandarasi huyo ili aweze kuanza kazi mara moja na gharama kwa ajili ya ujenzi wa gati hiyo italipwa na Mamlaka ya Bandari kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *flow meter*. Tulitangaza tender lakini kwa bahati mbaya sana tulipata wakandarasi wawili lakini wote hawakukidhi vigezo, kwa hiyo, tukaamua tuanze mchakato upya na mchakato unaendelea vizuri kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa scanner bandarini tayari tumetoa order ya scanner kama tano kwa ajili ya kuimarisha ulinzi kwenye bandari zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kidogo kwenye shirika la ndege. Kama mnavyojuu shirika letu la ndege linaimarika vizuri na Wabunge wengi sasa mmefaidi matunda ya Bombardier Q400, si kibajaji tena, sasa zimekuwa ndege. Serikali tunaamini tunaendelea kujipanga kuleta ndege nyngine mpya nne ambayo Bombardier moja itakuja mwezi wa tano; C series ambayo ni jet engine itakuja mwakani; kila moja itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 150. Mwakani vile tutaleta ndege nyngine Boeing Dreamliner yenye uwezo wa kubeba abiria 262. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mpango wa kuibadilisha au ku-trade in ndege yetu Bombardier Q300 ile ambayo ni mzee tuweze kupata ndege mpya Bombardier Q400. Itakapofika mwisho wa mwaka 2018 shirika la ndege la Air Tanzania litakuwa na ndege saba mpya. (*Makofii*)

Katika kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma wa Air Tanzania wamenunua programu mpya sasa kwa ajili ya kufanya reservation na booking kwa wateja wake. Sasa wateja wote wa

Air Tanzania wanaweza ku-book kupitia kwenye computer au hata kwenye smartphone. Tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba tunatoa huduma iliyotukuka. (Makof)

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marubani tunajipanga tulete marubani na kila sehemu ya Tanzania tunataka kuhakikisha kwamba Bombardier Q400 inatua. Mheshimiwa Hawa Ghasia tumekusikia na tutakuletea ndege hiyo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge tumesikia malalamiko yao kuhusu barabara, Serikali ya Awamu ya Tano tumejipanga sana na tunataka kuibadilisha nchi yetu kupitia miundombinu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa kuhusu sekta ya mawasiliano; tumebadilisha kanuni za Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kuhakikisha kwamba tunapeleka huduma ya mawasiliano kila eneo la Tanzania...

(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbarawa naomba umalize muda wetu umekwenda sana.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: ... hasa yale maeneo ya mpakani ambayo hayana mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa kuhusu TAZARA umepokelewa na mwisho kabisa kama nilivyoanza mwanzo ninaomba kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja, ahsanteni sana. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, sasa tutamsikia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu.

MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA KING – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kipekee kabisa kwanza kupongeza wachangiaji wote 15 ambao wamechangia kwa maandishi na 22 wamechangia hapa Bungeni. Mambo machache tu niangalize.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema shukrani hizo, Waheshimiwa Wabunge nichukue nafasi hii kipekee kabisa kumpongeza Waziri mwenye dhamana na wasaidizi wake wote kwa sababu kwa muda wote ambao Kamati imekuwa ikifanya kazi zake wamekuwa wakitupa ushirikiano mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo machache ambayo mmesitiza ni pamoja na ujenzi wa reli ya kati, barabara mbalimbali, bandari zote kwa maana ya Dar es Salaam ,Mtwara, Tanga na Bagamoyo; lakini pia mmesitiza upande wa ATCL. Pia Waheshimiwa Wabunge wamesitiza sana juu ya ajira pale bandarini na kwamba wako watu walioajiriwa ambao wamefukuzwa kama hivi; sisi kama Kamati tumepokea taarifa hiyo na Wizara imesikia na sisi wajibu wetu tutafuatilia kuona kwamba Serikali inafanya inavyopasa kama lilitofanyika halikupaswa kufanya hivyo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge nitumie nafasi hii kusema mambo machache tu, na hasa juu ya mradi huu wa reli ya kati. Ninaipongeza sana Serikali kwa sababu dhamira yake na haya maneno niliyasema Dar es Salaam wakati wa kusaini mkataba juzi wa

kutoka Dar es Salam kwenda Morogoro. Nikasema kwa sababu mipango yetu ya kwanza ya reli yetu haikuwa kilometra 160 kwa saa, kuchelewa huku ndiko kumetupelekea kwenye kilometra 160 kwa saa. Nikasema kama kuchelewa ni huku basi ni kuchelewa kuzuri, maana sasa tumeenda kwenye spidi kubwa zaidi yenye manufaa zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini muhimu kabisa ambalo Wizara ni vizuri ifahamu ni kwamba kukamilika kwa reli ya kati ni jambo moja, muda wa kukamilika reli ya kati ndio muhimu zaidi. Kwa sababu zilezile kwamba mzigo tunaotegemea ili uweze kurudisha mkopo wao wote wa reli ya kati ni ule ule ambao Kenya, Uganda, Rwanda, DRC na Zambia wanautegemea. Ndio maana nasisitiza tena na Kamati inasisitiza tena kwamba vyovyote itakavyokuwa tumieni mkandarasi yoyote mnayemjua kwa vipimo mnavyovijua, muhimu reli hii ikamilike haraka kabla wenzetu hawajakamilisha, hilo ni muhimu kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nisisitize tu kusema pia kwamba naunga mkono vizuri sana, Mheshimiwa Waziri amesema amegawa vipande vingi vingi kwa maana ya ujenzi wa reli ya kati na sisi Kamati hatuna tatizo na hilo lakini bado tunasisitiza kwamba standard ya reli na upatikanaji wa funding ndio unaotengeneza hot cake ya project yoyote. Narudia, project yoyote haiwi viable kama funding haipo; kwa hiyo ni funding inapokuwa available ndio inafanya mradi kila mkandarasi aone ni hot cake. Unayejua umuhimu wa kuchukua mizigo Kigoma au kuchukua Kalemi kule Mpanda ama Mwanza ni wewe Mtanzania; mjenzi anachoangalia ni funding. Ndiyo maana Serikali mijipange ili kufasili kwa usahihi kwamba funding iko vipi na kwahiyoo tunaelekea wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nichukue nafasi hii tena kuomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lilidhie taarifa ya Kamati ya Miundombinu iwe maelekezo rasmi kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MHE. HAWA H. GHASIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017 ilipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono kwa hiyo mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati ya Miundombinu yanachukuliwa kama ni Maazimio ya Bunge na kwa hiyo Serikali ikayafanyie kazi. (Makofi)

Sasa nitamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ili ahitimishe hoja yake. (Makofi)

MHE. DOTO M. BITEKO – MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nikushukuru sana wewe kwa kunipa fursa hii, lakini vilevile niwashukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Waziri wa Nishati na Madini na Wabunge wote waliochangia hoja hii. Kwa kweli michango yao imekuwa mizuri na imeboresha sana taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji kwenye hoja yetu walikuwa 32, hawa wote 32 wamechangia kwa kusema, lakini Waheshimiwa Wabunge tisa wamechangia kwa kuandika. Katika kujumuisha hoja yetu nitaelezea tu mambo machache ambayo yamejitokeza kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge na wachangiaji wengine kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamelichangia ni suala la umeme, na suala la umeme hili wamelijadili katika maeneo yote mawili – upande wa TANESCO na upande wa REA, hoja hii imechangiwa na Wabunge 27. Kwa upande wa TANESCO, Waheshimiwa Wabunge wengi wameeleza masikitiko yao, wameeleza msisitizo wao, wametoa maoni yao juu ya madeni ya TANESCO na kuomba kuwepo kwa namna ambayo TANESCO itaweza kutoka kwenye mkinzano huu wa madeni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye upande wa REA, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia juu ya usimamizi wa miradi ya REA, wamezungumzia vilevile upelekaji wa fedha za miradi ya REA na na wakandarasi kuwashirikisha viongozi wakati wakandarasi hao wanapokwenda site na kuongeza ule wigo (*scope*) kwenye maeneo ambako miradi hii inakwenda. Mambo haya yote kwenye taarifa yetu tuliyaleza na Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa madini jumla ya Wabunge 19 wamechangia hoja hii, na mambo yaliyojiteza kwenye michango yao ni pamoja na suala la wachimbaji wadogo wadogo. Kwanza wachimbaji wadogo wadogo kupatiwa maeneo ya kuchimba, lakini vilevile wachimbaji hawa wadogo wadogo kupatiwa ruzuku ili iweze kuwasaidia kuchimba kisasa. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia vilevile hili jambo la wachimbaji wadogo wadogo kuvamia leseni za wachimbaji, jambo hili kwenye Kamati pia na Serikali ilitupa ufanuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia wamezungumzia suala la Tanzanite. Tanzanite kupatikana Tanzania na Tanzania isiwe ya kwanza kwenye muuzaji wa Tanzanite linawakera Waheshimiwa Wabunge wengi kama ambavyo linawakera Watanzania wengi. Lakini naomba tu nitoe taarifa, Serikali jambo hili imelichukua kwa uzito wake na kwenye kamati tulipewa taarifa kwamba Serikali imepeleka ukaguzi maalum (*special audit*) na nilidhani tusizungumze sana hili kwa sababu baada ya taarifa ile kuja tutakuwa na mahali pa kuanzia kuishauri Serikali vizuri. Kwa hiyo, nadhani hili tuiachie Serikali kwa sababu imeshalichukua kwa uzito wa aina yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia STAMICO, Wabunge sita wamechangia juu ya STAMICO na wameelezea juu ya kuhodhi maeneo mengi ya STAMICO. Hili ni kweli, lakini hata kwenye kamati wajumbe walilizungumza kwa uchungu sana kwa sababu STAMICO ana maeneo mengi ambayo ameyashikilia lakini hachimbi, ameingia ubia na wawekezaji, wale wawekezaji kwa miaka karibu 12 hakuna wanachofanya. Tunaitaka na kuiomba Serikali kwamba sasa ifike mahali hawa wabia walioingia JV na STAMICO waanze kufanya kazi, vinginevyo itakuwa ni kupoteza muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaovamia yale maeneo ambayo yako dormant utakosa sababu ya kuwaondoa kwa sababu wewe hilo eneo umelishika. Kwa mfano Mheshimiwa Bukwimba amezungumzia suala la Baclif. Pale kuna leseni 12 ambazo STAMICO wameingia mkataba pamoja na TANZAM 2000; lakini toka wameingia makubaliano hayo hakuna kinachoendelea. Kwa hiyo, wananchi wale wanaweza kuvamia kwa sababu hawaoni jambo lolote linaloendelea, na Serikali imechukua hatua juu ya jambo hili, inaielekeza STAMICO.

Mheshimiwa Naibu Spika, na niwaombe Waheshimiwa Wabunge waliopendekeza kuifuta STAMICO, mimi nadhani tui-capacitate STAMICO. Itakuwa ni jambo la aibu sana sisi wenyewe, Serikali, Watanzania tunaanzisha shirika letu wenyewe tunaliua halafu tunaanzisha lingine, kwani Watanzania tutawatoa wapi? Si ni hawahawa tutakaowapata kuunda shirika lingine? Mimi nilikuwa naomba tuipe nguvu, tuisimamie vizuri STAMICO iweze ku-deliver kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachopungua pale STAMICO ni mambo mawili; jambo la kwanza ni upelekwaji wa fedha lakini jambo la pili ni usimamizi ulio madhubuti. Mimi naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wizara, kila mara wanapitishapitisha mikono yao pale STAMICO. Ninaamini baada ya muda fulani pengine tunaweza tukaona matokeo yanabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mgodo wa Serikali ambao ni wa Stamigold. Mgodi huu unasimamiwa vizuri sana na Watanzania, kuanzia mfagizi, mlinzi mpaka MD wa mgodi ule ni Mtanzania, mswahili mwenzetu. Nao wana changamoto ambazo wamezieleza. Changamoto ya kwanza wanayoizungumzia hawana MDA, ile *Mining Development Agreement*, tumewaoomba Serikali wahakiske wanafanya kazi ya kuwapatia hiyo MDA.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile mitambo walijonayo yote ni ya kukodi hawana mtambo hata mmoja wa kwao, jambo ambalo linasababisha gharama ya uendeshaji wa mgodi ule kuwa kubwa sana, zaidi ya asilimia 31.7 ya gharama za uendeshaji zote zinakwenda kwenye ukodishaji wa mitambo. Tumeiomba Serikali na katika hili nitumie nafasi hii kuiomba Wazara ya Fedha kama migodi mikubwa ya kigeni tunaipa exemption ya mafuta, kwa nini mgodi wetu wenyewe wa Stamigold ambao kwa asilimia mia moja ni wa Serikali, na wenyewe tusiupe exemption ili na wao wapunguze gharama za uendeshaji, tuapte faida haraka? Tunatoa fursa hii kwa wageni, migodi ya ndani tunaibinya, nilikuwa naomba jambo hili lichukuliwe kwa uzito wake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumza juu ya mafuta, ujenzi wa *farm tank* na hili tumelipata kutoka kwa wadau wote tuliotutana nao, wameeleza umuhimu wa kuwa na Central Storage System ya mafuta baada ya kuwa yamepakuliwa kabla ya kusafirishwa kwenda kwa watumiaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao na kwa kweli niseme toka nimekaa kusikiliza mchangiaji wa kwanza mpaka wa mwisho mimi binafsi nimejifunza vitu vingi. Wameona mambo haya kwa macho ya tofauti pengine na kamati tulivoona. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba sasa Bunge lako likubali kuipokea taarifa hii na kuwa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji, kulikuwa na jedwali la marekebisho la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum, katika hoja ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017, lakini kwa kuwa mwenye hoja hayupo nitawahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari 2017 ilipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Hoja ya Kamati imeungwa mkono na Wabunge wengi wamesema ndiyo. Kwa hiyo, mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati ya Nishati na Madini yanakuwa ni Maazimio ya Bunge na Serikali iende ikayafanyie kazi.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kuwapongeza Wajumbe wa Kamati hizi mbili, kwanza; Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa niaba ya Bunge na kutuletea hapa taarifa ya mambo waliyoyafanya katika mwaka uliopita na Wabunge wote kwa michango mizuri ambayo imeboresha utendaji wa Kamati kwa hapo baadaye ambayo ni mambo ambayo wataweza kuyafanya kazi. Lakini pia kwa nafasi mliyochukua kila mtu kwa eneo lake, watu wengi inaonekana wamesoma na walijandaa kuchangia, kwa hiyo mmeefanya vizuri sana na mimi nichukue nafasi hii kuwapongeza.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujamaliza, ninayo mambo matatu; la kwanza ni mambo ya jumla kuhusu kinga ya Mbunge. Kwa sababu ya yale yaliyotokea leo ni vizuri tukaweka sawasawa. Mambo haya yako kisheria na hayana namna ya kufanywa tofauti. Makosa ya madai, sheria inasema Mbunge anayo kinga na kinga yenyewe si kwamba anakingwa wakati wote, hata makosa ya madai ikiwa Bunge haliko kazini lakini pia ikiwa Mbunge hayuko maeneo ya Bunge anaweza kukamatwa. Kwa hiyo tuliweke vizuri tu, sheria ambayo tumetunga wenyewe Wabunge ndivyo inavyosema.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, makosa ya madai Mheshimiwa Mbunge akifanya kosa hilo akitaka kukamatwa wakati Bunge linaendelea ama katika viwanja vya Bunge kosa la madai hatakamatwa, taarifa atatakiwa kupewa Spika, lakini makosa mengine yote, kama ni hapa Bungeni mtu umempiga mwingine au umefanya kosa ambalo si la madai, hata hapa ndani litahesabiwa kuwa ni kosa. Kwa hiyo, hata nje ya viwanja vya Bunge litahesabiwa pia kwamba ni kosa.

Lakini sasa baada ya kusema hayo, nitoe ushauri Waheshimiwa Wabunge tuipitie ile sheria tuliytunga wenyewe, tusifanye makosa ya jinai kwa sababu tutakamatwa muda wowote, hilo ni la kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, hata makosa ya madai tujitahidi Waheshimiwa Wabunge tusifanye pia hata hayo kwa sababu hata hayo tuna uwezo wa kukamatwa kwa mujibu wa sheria tuliyojiwekea wenyewe, hakuna namna ya Bunge kuweza kutoa kinga ambayo sheria hajjasema, hilo lilikuwa ni jambo la kwanza ni vizuri tulielewe vizuri.

Jambo la pili, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na mambo mengi aliyoyleza, ametoa maelezo kuhusu uwazi wa mikataba.

Waheshimiwa Wabunge, sheria inaruhusu Mbunge mwenyewe kwenda kutafuta taarifa, lakini pia sheria inaruhusu Mbunge kutafuta taarifa kuitia Bunge. Ikiwa mikataba hii kama Mheshimiwa Waziri alivyosema; Mbunge atakwenda kuiona hiyo mikataba kwa utaratibu binafsi, itakapotokea vile vifungu vinavyohusu usiri wa mikataba vikaleta taabu hapo baadaye, Bunge halitahusika. Kwa sababu atakuwa ameenda binafsi kwa hiyo itakuwa ni kati ya Serikali au kati ya wale walioingia mkataba huo na yule aliyeenda kuuona, akitoa siri Bunge halitahusika moja kwa moja. Kwa hiyo Mbunge akiomba mkataba kuitia Ofisi ya Bunge ikitokea kile kifungu kimevunjwa Bunge litahusika lakini akienda yeye mwenyewe moja kwa

moja, kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, kwamba wengine wanaweza kwenda tu kuangalia, ni sawa, lakini Bunge halitahusika ikiwa vifungu hivyo vya kuhusu usiri vitakuwa vimevunjwa.

Jambo la mwisho ni kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Pamoja na mambo mengi yaliyozungumzwa, Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa maelezo mazuri kabisa kuhusu viwanja vya ndege na namna ambavyo watafanya bidii ili taa ziwekwe.

Waheshimiwa Wabunge, tunapoongelea mambo ya maendeleo ni pamoja na haya. Mimi niombe hii Wizara, kama ambavyo majibu yametolewa hapa mazuri sana, si jambo jema mtu ambaye amejipanga kwenda kulala sehemu nyingine akajikuta analala sehemu nyingine kwa sababu uwanja hauna taa. Kwa sababu Serikali inapojenga uwanja maeneo fulani ni kwamba inataraji maendeleo ya wale watu yaende haraka zaidi. Kwa hiyo niwaombe tumalizie yale maeneo ambayo hayana taa ili kuondoa usumbufu lakini pia kuwaharakishia maendeleo watu wa maeneo hayo na Mheshimiwa Waziri nadhani atakumbuka kuna siku tulilazimika kulala Dodoma badala ya kulala Dar es Salaam kwa sababu kiwanja hakina taa.

Sasa mambo kama hayo maana yake pia unaleta hasara kwa ndege nyingine lakini pia hata kwa bombardier zetu tunazoziongelea. Kwa hiyo tusingependa tujikute katika hali ambayo bombardier itatuambia inapata hasara kwa sababu imelala eneo ambalo haikutakiwa kwa hiyo inatakiwa kuwalipa abiria wake ambao walipaswa kusafiri. (Makofii)

Baada ya kuyasema mambo hayo matatu ya jumla, nimeletewa tangazo hapa, najaribu kulielewa Waheshimiwa Wabunge, hili ni tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka kuhusu michango iliyotolewa na Wabunge kwa kituo cha watoto ambao sijui kama nitakuwa nimetumia lugha sawasawa; lakini ni walemavu wa akili, Waheshimiwa Wabunge walijitolea kuchanga hapa.

Kwa hiyo anatoa taarifa kwamba kesho Wabunge watakaoweza wanakaribishwa kuambatana naye kwenda katika kituo hicho ambacho kipo barabara ya kuelekea Arusha ili waweze kwenda kukabidhi mchango huo. Ametaja hapa kwamba jumla ya michango ni shilingi 10,795,000, na magodoro yamenunuliwa kwa shilingi 4,672,000, fedha taslimu ni 6,123,000.

Kwa hiyo, fedha taslimu zitakabidhiwa kwa kituo kwa ajili ya mambo mbalimbali ambayo watakuwa nayo. (Makofii)

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, tarehe 8 Februari, saa tatu asubuhi.

(Saa 1.34 Jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 8 Februari, 2017, Saa Tatu Asubuhi)

